Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 9 Julai, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na kikao cha Kumi na Tisa cha Mkutano wetu wa Nane kinaanza, Katibu, endelea na ratiba.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI.

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. NEEMA H. MGAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2011/2012 na Maoni Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2012/2013.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAJI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maji Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 153

**Fidia kwa Wahanga wa Mabomu ya Mbagala.**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Baadhi ya Wahanga wa mlipuko wa mabomu ya Mbagala wanalalamikia kiwango kidogo cha fidia waliyopata na wengine bado hawajapata:-

(a) Je, ni vigezo gani vilitumika kukadiria viwango vya fidia?

(b) Je, wahanga waliobaki watafanyiwa lini tathimini na kulipwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vilivyotumika kukadiria viwango vya fidia kwa wahanga wa milipuko ya mabomu Mbagala ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa Majengo yaliyokamilika, kilitumika kigezo cha makadirio ya gharama ya mita ya mraba ya jengo husika. Kwa mfano jengo la ghorofa moja fidia ni kati ya shilingi 250,000/= hadi shilingi 400,000/= kwa mita moja ya mraba.

(ii) Kwa vifaa vya ujenzi, kilitumika kigezo cha bei za vifaa mbalimbali vya ujenzi katika soko.

(iii) Kwa majengo yaliyokuwa yanaendelea kujengwa yalikadiriwa kwa asilimia ya hatua ya ujenzi.

(iv) Kwa huduma za umeme kiwango cha bei ya TANESCO ya kuunganisha umeme kwa mteja kilitumika.

(v) Samani za ndani kilitumika kigezo cha bei ya samani hizo katika soko.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulipa fidia shilingi 7,756,956,482/= kwa wahanga 8,636 walioathirika kutokana na mlipuko wa mabomu

Mbagala, walijitokeza tena wahanga 2,575 wakilalamika kutofanyiwa tathmini na wengine kulipwa kiwango kidogo cha fidia.

Serikali iliyafanyia kazi malalamiko hayo yaliyoletwa na wananchi pia Mbunge wao Mheshimiwa Ndugulile, na jumla ya waathirika 1,696 walionekana wanastahili fidia ya jumla ya shilingi 2,200,000,000/=.

Tarehe 6 Juni, 2012 Ofisi ya Waziri Mkuu ilipeleka kiasi hicho cha fedha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ili wahusika wote waweze kulipwa. *(Makofi)*

**MHE. FAUSTINE E. NGUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Ni kweli kwamba malipo sasa hivi yameanza kulipwa lakini hii ni awamu ya nne ya tathmini ambayo imekuwa inafanyika, lakini bado kuna malalamiko makubwa sana kwa upande wa wananchi na mpaka sasa hivi wananchi kama kumi ambao wamekuja kwangu kama Mbunge wakilalamikia cheki za shilingi elfu moja, kwa sababu Waziri amesema hivyo vigezo. Sasa labda nipate ufafanuzi cheki ya shilingi elfu moja mwananchi anaipatataje na kwa kigezo gani kilichopo.

(b) Utaratibu wa malipo, kwa kweli wananchi wanalalamikia sana utaratibu ambao umewekwa wa malipo, Je kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba

wananchi hawa wanalipwa kwa wakati pamoja na kwamba fedha zote zimeshafika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE :** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema haya yalitokea wakati mimi nikiwa pale, nataka niwaambie kwamba zoezi kama hili ni gumu sana kwa upande wa waathirika lakini pia kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lina udanganyifu mkubwa, lina wizi mkubwa usipoliangalia, na ndiyo maana zoezi la kwanza la tathmini lilikuwa limetathminiwa kama shilingi bilioni kumi na mbili, lakini kutokana na raia wema wa Mbagala waliojitokeza kwangu wakasema kuna malipo hewa ambayo tunataka kulipwa sisi hatuna nyumba.

Kuna watu waliokuwa wanasimama kwenye nyumba wanapigwa picha lakini nyumba siyo zao. Kwa hiyo ndiyo uone kwamba mambo haya yanachukua muda kwa sababu yana uwongo mwingi lakini unaweza kulipa hela ya Serikali kwa watu wasiohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sambamba hivyo hivyo na waathirika nao vile vile, kuna watu walitoka Pemba kuja kuchukua nyumba pale wakati hawana nyumba pale. Kuna watu walitoka mikoani huko kuja Mbagala wakijua sasa ndiyo wakati wa mavuno. *(Makofi)*

Kwa hiyo wakati wowote Serikali ni lazima iwe makini katika kuhakikisha kwamba fedha za wananchi zinatumika vizuri na tathmini, kwa sababu wale *Valuers* na wenyewe wakati huu ndiyo wakati wa mavuno. Wapo Wathamini ambao siyo waaminifu wanaweza kutumia kigezo hiki kwa kujitajirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo makosa yote yanayofanyika si makosa ya maksudi, kama kuna matatizo yanatokea ni matatizo ambayo yanatokea kwa nia njema ya kujiridhisha ili kuhakikisha kwamba fedha za wananchi zinalipwa vizuri na ndiyo maana tumeenda awamu ya nne. Kila mara mtu yeyote ambaye ataona kwamba anatatizo na fidia yeyote ambayo imefanywa na Serikali ana wajibu wa kurudi tena Serikalini, Serikali tutafanya tena mpaka kila mtu apate haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba tu Mbunge kwa sababu wote tunakaa Dar es Salaam na ni rafiki yangu, hiyo cheki ya shilingi elfu moja, utaratibu unalipwaje njoo, tuzungumze huko nje nitakusaidia hayo yote yaishe.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi. Kwa kuwa suala la mlipuko wa mabomu lililotokea Mbagala linafanana na lile lilitokea katika Jimbo la Ukonga na kwa kuwa katika Jimbo la Ukonga wapo watu ambao walilipwa lakini pungufu, lakini wapo watu wengine ambao hawajalipwa kabisa fedha zao. Lakini kwa kuwa pia wapo wananchi watatu ambao mpaka sasa wanaishi kwenye mahema. *(Makofi)*

Je, Serikali sasa inasema nini kuhusu kuwalipa wahanga hawa ili waendelee sasa na maisha ya kiuchumi badala ya kuendelea kufuatilia malipo yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Mwaiposa amekuwa anafuatilia sana malipo haya ya Wahanga wa mabomu kule Gongo la Mboto.

Lakini tulifanya tathmini, tukakubaliana awamu ya kwanza kwamba wale waliobomolewa nyumba zao, Serikali iwajengee nyumba zenye thamani inayopendeza maisha yao ya sasa, badala ya kuwapa pesa. Tulifikiri hivyo kwa sababu tulifikiri ni ustaarabu, Jengo limebomolewa, mtu hakujiandaa, badala ya kumpa kazi ya kuanza kujenga upya na kutafuta fedha au unampa fedha halafu ikitokea vinginevyo zikatumika atakosa jengo. Kwa hiyo tuliamua hivyo.

Katika wote ambao tulikubaliana, nyumba tumejenga 36, lakini wengine sasa wamejitokeza wamesema hawataki nyumba wanataka walipwe, kwa hiyo tuko kwenye mjadala nao sasa ndiyo wameleta maombi yao. Hao wote ambao wanasema hawajalipwa maombi yao yameshafika ofisi ya Waziri Mkuu tunayatafakari, lakini lolote lile tutakubaliana tu, ni lazima haki yao ilipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mbunge kuwa, vyovyote itakavyokuwa tutakubaliana ili haki yao ilipwe.

Na. 154

## Umiliki wa Ziwa Kitangiri

**MHE. MESHACK J. OPOLUKWA** aliuliza:-

Ziwa Kitangiri linapakana Wilaya ya Meatu na Iramba lakini Serikali ilitoa ramani inayoonyesha kuwa Ziwa hilo liko Wilaya ya Iramba:-

Je, Serikali haioni kuwa, sasa kuna umuhimu wa kurejea ramani hiyo ili Wilaya zote mbili ziwe na umiliki wa Ziwa Kitangiri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opolukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza migogoro ya usimamizi wa Mamlaka za Mikoa na Wilaya, Serikali wakati wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala hutangaza mipaka ya maeneo hayo katika Gazeti la Serikali. Mkoa wa Singida ulianzishwa mwaka 1963 ukiwa na Wilaya za Iramba, Manyoni na Singida. Kwa upande wa Kaskazini Magharibi ndiko ilikuwa Wilaya ya Iramba ambayo inapatikana na Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kati ya Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Singida umefafanuliwa kwa

maelezo yaliyotolewa na tangazo la Serikali Na. 266 la tarehe 14 Desemba, 1973 lililoanzisha Wilaya ya Maswa na tangazo la Serikali Na. 137 la Tarehe 27 Mei, 1988 lililoanzisha Wilaya ya Meatu ambayo maelezo yake yanahusisha mpaka na Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya tangazo la Serikali Na. 266 la mwaka 1973 yanafafanua kuwa eneo la ziwa Kitangiri liko katika Wilaya ya Iramba. Aidha, maelezo hayo yanawiana na maelezo ya mpaka wa iliyokuwa *Central Province* kupitia ramani iliyochorwa kwa tangazo la Serikali Na. 471 la tarehe 16 Novemba, 1962 kuonyesha mipaka husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Opulukwa Ziwa Kitangiri lipo Iramba, swali la nyongeza.

**MHE. MESHACK J. OPOLUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza;

Kwa kuwa, kijiografia Ziwa Kitangiri lipo sehemu zote mbili Halmashauri ya Wilaya ya Iramba pamoja na Halmashauri ya Meatu; na kwa kuwa kulikuwa na *beacons* ambazo ziliwekwa na Mkoloni ambayo inaingia upande wa mto Manonga na inatokea upande wa Mto Sibiti, mto unapotoka, ambazo zilivunjwa.

(a) Je, Serikali sasa itakubaliana na wananchi wa Meatu kwamba ni wakati muafaka wa kukaa na kupitia upya ramani hiyo ili angalau hilo ziwa liweze kuwa *shared* na pande zote mbili?

(b) Kwa kuwa, mazingira ya kuanzisha Mkoa wa Singida mwaka 1963 yameshapitwa na wakati imekuwa ni zamani sana na mazingira ya sasa yamebadilika.

Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa imefikia wakati muafaka kama kuna uwezekano wa kukaa na Halmashauri zote mbili, Halmashauri ya Meatu pamoja na Halmashauri ya Iramba ili kuweza kutatua mgogoro huu ambao umekuwa ni wa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mnisikilize vizuri, na Mheshimiwa Opulukwa nakuomba unisikilize vizuri. Mimi ninachokizungumza hapa, ni kweli anasema hili ziwa linahama wakati mwingine unalikuta lipo Singida wakati mwingine unalikuta lipo Shinyanga. Lakini Wilaya inayozungumzwa hapa, sasa hivi wala haipo tena Shinyanga ipo Simiyu. *When you look these things in historical perspectively, you are trying to be scientific*.

Hapa nataka kusema tunaka niseme kwamba tunaleta habari ya sheria ya nchi inavyozungumza hapa. *Much as* na-*share* na Mheshimiwa Opulukwa, hiki anachokizungumza hapa, ninamwomba sana takapozungumza chochote ndani ya hapa na nje, kibebe wajibu kwa wananchi wote wa Tanzania na kibebe wajibu kwa wananchi wote wa Meatu na wale wa kule Iramba.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunachozungumza ni sheria iliyounda hizi Halmashauri. Halmashauri hii ya Wilaya ya Iramba tunayoizungumza hapa ilianza toka mwaka 1958 ilikuwepo. Mwaka 1963 ndipo Mkoa wa Singida ulipoanzishwa.

Halmashauri ya Wilaya ya Meatu haikutokana na Singida ilitokana na Shinyanga ilikuwa inatoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa. Mipaka ilipobadilika ya Wilaya ilikuwa ndani ya Mkoa wa Shinyanga wakati ule. Kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Maswa na Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.

Mheshimwia Naibu Spika, ukichukua GN. hii ninayoizungumza hapa hakuna mahali popote inaposema kwamba wakati ilipokuwa inaundwa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu mipaka ya Mkoa ule ilipanuka ikaenda mpaka Singida kwa maana ya Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba ili tusije tukaleta utata hapa niisome hiyo sheria inayozungumzwa hapa. Tafsiri ya tangazo Na. 266 la mwaka 1973 kwamba Ziwa Kitangiri lipo Wilaya ya Iramba ni hii ifuatayo:-

*Fence Westwards and Southwards along Northern and Western shores of lake to the boundary of Sibiti River, ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Opulukwa. (which marks the common boundaries of Shinyanga, Singida and Arusha Regions), Fence the Sibiti to the Northern shore of lake Kitangiri, fence along the*

*Northern shore of lake Kitangiri to the SRA of Sanga river*. Hii hapa ndiyo inazungumzwa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachozungumzwa hapa kama na *AG* upo hapo wewe unajua mambo ya sheria zaidi kuliko mimi. Tunazungumza habari ya utamaduni, tunazungumza habari ya desturi tunazungumza habari ya historia ambayo imeulizwa hapa kwamba imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, historia utamaduni ndiyo unaanza halafu inakuja sheria. Sheria kazi yake ni kulinda utamaduni, kazi yake ni kulinda sheria pamoja na historia ndicho ninachokielewa hapa. Tukitoka hapa tukaenda tukawaambia wale wananchi wa Singida pale Iramba kwamba leo Ziwa halipo kwenu hawatatuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini moja ambalo nataka Mheshimiwa Opulukwa aondoke nalo hapa amelielewa ni kwamba ni kweli kabisa kwamba kuna haja kama anavyosema ya wananchi wa pande zote mbili kukaa kwa pamoja na kuzungumza namna nzuri ya matumizi bora ya Ziwa Kitangiri pale.

Kama Waziri Mkuu unayekaimu sasa hivi, kama tunaweza tukazungumza namna ya kutumia Ziwa Tanganyika kati ya Rwanda na Burundi na Uganda na Kenya wote kwa pamoja tukawa na mamlaka moja ambayo inatuunganisha tunazungumza, iweje leo hapa kwetu nchini Tanzania sisi wenyewe kwa wenyewe hapa tushindwe kuwa na utaratibu mzuri wa

kukaa tukazungumza, tukaona jinsi ambavyo tunaweza tuka-*share* mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba Mbunge, nimewaagiza Ma-*RAS* wamekwenda wamekutana na juzi walikutana twende tukakae wote kwa pamoja tukaangalie vizuri hiki kinachozungumzwa hapa. Lakini narudia tena lolote tutakalolifanya libebe wajibu kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mwananchi anayezuiwa kukaa mahali popote katika nchi hii. Ukitaka leo kwenda Meatu, ukitaka kwenda Singida, ukitaka kwenda Mtwara, Kilimanjaro unaweza ukaenda. Ninataka nikuthibitishie katika hili niko tayari tukashirikiana na wewe kwa niaba ya Waziri Mkuu ili tusaidiane tuondokane na tatizo hili kwa maana ya kulinda maslahi ya wananchi wetu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Bado majibu ni kwamba Ziwa Kitangiri liko Iramba. Sasa anafuata Mheshimiwa Martha Mlata, usiendelee na mgogoro wa Iramba na Meatu.

Na. 155

### Kilimo cha Vitunguu-Mkalamu

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Katika Wilaya Mpya ya Mkalamu kuna ardhi nzuri inayostawisha zao la Vitunguu ambavyo ni bora Afrika Mashariki na Kati;

(a) Je, Serikali ina mkakati gani ya kuwasaidia wakulima wa vitunguu waweze kulima zao hilo na kuuza zaidi ya mara mbili kwa mwaka?

(b) Je, Serikali inatambua ubora wa Vitunguu hivyo na inatoa fursa gani ya kutangaza soko lake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge Viti maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Kuendeleza Mazao ya Bustani *(Horticulture Development Council of Tanzania)* na Wadau wengine imeaanda mkakati wa kuendeleza mazao ya Bustani *(National Horticulture Development Strategy)* likiwemo zao la vitunguu. Maeneo ya kimkakati yanayozingatiwa ni pamoja na kuongeza uwekezaji na ugharamiaji wa zao kuweka miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji uwe angalau mara mbili kwa mwaka, kwa maana ya kuongeza tija, usindikaji na kutafuta masoko ya uhakika ya nje na ndani kupitia Baraza la Kuendeleza Mazao ya Bustani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua fursa za kilimo cha vitunguu zilizopo katika Wilaya mpya ya

Mkalamu. Nachukua fursa hii na kumwahidi Mheshimiwa Martha Mlata na wakulima wa vitunguu wa Mkalamu kwamba nitawatuma watalaamu wa mazao ya Bustani kwenda kuwashauri wakulima juu ya kilimo bora cha vitunguu pamoja na usindikaji wa zao hilo. Aidha, naishauri Halmashauri ya Wilaya hiyo mpya kuanza kuweka kilimo cha vitunguu katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) hususan inayohusu kuweka miundombinu ya umwagiliaji.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Sasa kwa sababu Serikali inajipanga kwenda kutoa mafunzo kwa wakulima hawa wa vitunguu Mkalama. Lakini nilikuwa napenda pia nimweleze Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Mkoa wa Singida umekuwa ukizalisha vitunguu kwa mfano, mwaka 2009/2010 zaidi ya tani 15,000. Mwaka 2010/2011 zaidi ya tani 17,000.

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kutoa mafunzo haya kwa wakulima wote wa Mkoa wa Singida ili kuongeza uzalishaji wa zao hili?

(b) Pamoja na kwamba watakwenda kuweka miundombinu kwa ajili ya umwagiliaji. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa mikopo kwa vikundi kwa wakulima hawa wa zao la vitunguu ili waweze kununua mashine za kuvuta maji na kumwagilia kwenye maeneo yao? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niungane na Mheshimiwa Martha Mlata kwa sababu hata utafiti tu tuliofanya juzi kwenye soko la hapa hapa Dodoma linaonyesha kwamba vitunguu vya Mkalama kwa gunia bei yake ni kama 145,000 hadi 150,000 na vitunguu vya Ruaha – Iringa ni 120,000. Kwa hiyo, utaona hata sokoni tu *retail price* hapa hapa Dodoma *which is the first market* soko la awali kwa wakulima hawa *you can see the difference quality* baina ya vitunguu vya Mkalama na vitunguu vingine.

Kwa hiyo, naomba niseme kwa kuzingatia haya tumejipanga kwamba hili zao la kitunguu cha Mkalama, lakini kuna zao lingine la kitunguu cha Arusha ambacho nacho kina *fetch* bei kubwa zaidi kuliko hii vyote kwa pamoja tuvifanyie utafiti ambavyo pia vina-*respond* kwa *consumer demand* lazima utafiti huu uzingatie yale mahitaji ya watumiaji.

Kwa hiyo, naomba nimwahidi tu kwamba tumejipanga na kama kitunguu hiki kama zao hili pamoja na miundimbonu hii ya umwagiliaji yana-*respond* kwa Mkoa wa Singida yote, basi ni wazo zuri kwa sababu ni jambo ambalo tayari linaonekana kwamba litakuwa na maslahi makubwa ya kiuchumi kwa wananchi wa Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kuweka miundombinu ya *irrigation* ambayo tumesema

naomba nirejee tu kidogo nimesema ni jukumu la Serikali kuu na Halmashauri zake kwa maana hii miradi ya *Irrigation* inayokwenda kule tayari fedha zimekwenda kule lakini kuna usimamizi ambao unatakiwa wa sisi wenyewe Wabunge na Madiwani wenzetu ili kuhakikisha kwamba mipango hii ya umwagiliaji inafanya kazi vizuri.

Sasa hapo ambapo panaonekana kwamba kwenye vikundi pana *addition* au pana maombi ya ziada yanayohitaji mikopo.

Mimi nadhani kama kikundi kinakopesheka kwa jambo lolote lile la kilimo, liwe la madini, liwe la jambo lolote. Kama kikundi kinakopesheka na kinakidhi vigezo Serikali itaingilia kati ili vikundi hivyo viweze kukopesheka. (*Makofi*)

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna watalaam ambao kwamba watapita kwenda kuwafundisha maeneo ya Mkalama kilimo cha umwagiliaji. Katika Wilaya ya Kondoa kata ya Mnenia ni mojawapo wa wakulima wa vitunguu na kwa kuwa hawajatambulika kama jinsi walivyotambulika wengine.

Je, Serikali sasa inajipangaje sasa kuwatambua wananchi wa Wilaya ya Kondoa Kata ya Mnenia kuwa ni wakulima mojawapo wa vitunguu na ni kitunguu ambacho kina ubora ambacho kinatumika maeneo mengi, Serikali iko tayari kuwapatia utalaam zaidi wa

ukulima katika maeneo hayo pamoja na kuwatafutia soko?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Moza Abedi kama ifuatavyo:-

Naomba nikubaliane naye tu kwamba kama huko kwenye Kata ya Mnenia kuna vitunguu hivyo ambavyo vinaonekana vina maslahi makubwa kwa uchumi wa wananchi wa Kata ya Mnenia Wilaya ya Kondoa tutakwenda kuifanyia kazi. Lakini ninachosema ni kwamba kitunguu cha Mkalama tayari kitu kinaitwa *branding* kinatambulika, ukikipeleka sokoni, Dodoma, Dar es Salaam kinashindana na vitunguu vyote na kinawazidi bei.

Sasa twende tukaangalie kama kitunguu chako cha Kondoa kinaendana sambamba na hiki cha Mkalama basi hakuna tatizo kama hakiendani basi ni juu yetu sisi wenyewe kuhakikisha kwamba kitunguu hicho kipata ubora wa soko maana ndio njia pekee ya kuhakikisha kinauzika. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kutambua uwepo wa Mheshimiwa Samuel Sitta kama Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Ahsante sana karibu sana Mheshimiwa Sitta, tuendelee kushirikiana. (*Makofi*)

Na. 156

**Serikali Kununua Mtama na Uwele kwa Wakulima**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. SULEIMAN NCHAMBI SULEIMAN)** aliuliza:-

Kishapu ina tatizo kubwa la ukosefu wa mvua za kutosha na hivyo ni wakati muafaka kwa Serikali kuleta mbegu za kisasa kwa mazao yanayoweza kuhimili ukame kama vile Mtama, Uwele, Alizeti na hata Mahindi:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali isinunue mazao ya mtama na Uwele kutoka kwa wakulima kama inavyofanya kwenye mahindi ili kuwafanya wananchi wapate uhakika wa kuuza mazao yao na kujipatia fedha?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kununua mazao hayo kutoka kwa wakulima kwa bei nafuu yanaweza kuhifadhiwa na kutumika wakati wa njaa na majanga na hivyo Serikali kuokoa kupoteza fedha nyingi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa akiba ya chakula kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA).* Mazao ambayo wakala umekuwa ukiyanunua na mahindi na mtama. Hata hivyo

upatikanaji wa mazao aina ya mtama na uwele umekuwa si wa kuridhisha kutokana na uzalishaji wake kuwa mdogo hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kupanua wigo wa mazao ya hifadhi ikiwa ni pamoja na mtama na uwele. Hivyo Serikali itaendelea kununua zao la mtama na pia iko tayari kununua zao la uwele endapo mazao hayo yatapatikana kwa kiasi cha kutosha. Aidha, Serikali tayari imepanua wigo wa soko la mazao kwa kuanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo itanunua pia mtama, uwele na alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wanaotoka maeneo ya uzalishaji wa mazao haya kushirikiana na Wizara yangu katika kuhamasisha wakulima kwenye majimbo yao kuongeza uzalishaji wa mazao haya na wakala wa taifa wa hifadhi ya chakula utakuwa tayari kuyanunua. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hoja ya msingi hapa ya Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, ni suala zima la soko na suala zima la soko ndilo linaloleta hamasa ya kuongeza uzalishaji kwa wakulima. Kwa kuwa tayari Serikali ilishaanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko.

(a) Je, Serikali sasa iko tayari kuniahidi mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, kwamba mwaka huu wa fedha itatenga fedha ili kununua mazao hayo ya mtama na uwele kusaidia kuhamasisha kuongeza uzalishaji wa mazao haya katika maeneo yenye ukame ili kuongeza hifadhi ya chakula?

(b) Kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma na hasa jimbo la Peramiho kwa mwaka huu wa 2012/2013 uzalishaji wa mahindi umeongezeka kwa zaidi ya tani zaidi ya lakini na kwa kuwa Serikali imeagiza mwaka huu Serikali itanunua laki mbili tu kwa nchi nzima. Sasa Serikali iko tayari kuiruhusu na kuiongezea fedha Bodi ya mazao Mchanganyiko na nafaka ili na yenyewe isaidiane na *NFRA* kununua mahindi yaliyozidi katika Mkoa wa Ruvuma na hasa jimbo la Peramiho na kuondoa tatizo la njaa katika nchi ya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwenye suala la Mtama tusiseme ni kwamba tatizo la mtama mbali ya soko, tatizo la soko *actually* kwa tathimini iliyofanywa siyo kubwa sana. Tatizo la mtama ni uzalishaji kwamba hatujafikia kiwango kile cha uzalishaji ambacho kinaweza ku-*guarantee*. Sasa tulichofanya mwaka huu ni kwamba tumeongea na Wakuu wa Mikoa ya Singida, Iringa, Tabora, Shinyanga na maeneo hapa katikati kwa sababu inapotokea matatizo ya njaa

Mikoa hii inahudumiwa na zao la Mahindi kutoka Wilaya ya Sumbawanga na Mbozi ambayo ni gharama kuyaleta kwa kanda hii. Kwa hiyo, tumekubaliana kuwa watatusaidia hili zao la mtama liweze kusimama kama zao mbadala kwa sababu kwanza linahimili hali ya hewa na pili itatusaidia pia kupunguza gharama za usafirishaji wa mahindi na kadhalika kutoka huko. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba katika suala hili tayari Serikali imejipanga kwa maana ya kwamba ikibidi kuongeza ruzuku ya mbegu na mbolea ili kanda hii iweze kuzalisha mtama kwa wingi zaidi. Tumejipanga kwa hilo na tunaendelea kujadiliana na wakuu wa Mikoa na natarajia kwenye mwisho wa mwezi huu au katikati ya mwezi ujao tutakuwa tumeshafikia mkakati mzima wa kuongeza uzalishaji wa mtama na alizeti katika kanda hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili swali la pili la uzalishaji wa mahindi tani laki mbili za ziada nadhani amesema kwa Mkoa wa Songea peke yake tani laki mbili zimezidi. Naomba niseme kwamba uzalishaji huu wa ziada ni jambo zuri kwa sababu *at any stage* kama *NFRA* ilikuwa imejipanga kununua tani laki mbili tu za kuweka kwa ajili ya akiba na kwa maana sasa Songea peke yake ina tani za akiba laki mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwamba Bodi ya Mazao Mchanganyiko, *NFRA* yenyewe na mkakati mzima wa chakula utafanywa ili hizi tani laki mbili, ziweze kuondoka mikononi na ikiwezekana kupata soko kwenye maeneo mengine ambayo yanahitaji

mahindi kwa dharura zaidi hilo nalo litazingatiwa ili mahindi yasikwame mikononi mwa wakulima. *(Makofi)*

Na. 157

**Uhaba wa Dawa Katika Hospitali za Serikali**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Nchi yetu ina changamoto ya uhaba wa dawa katika hospitali mbalimbali za Serikali:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni asilimia ngapi ya mahitaji ya dawa za binadamu zinazozalishwa hapa nchini na asilimia ngapi zimeagizwa nje?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ujenzi wa viwanda wa dawa nchini ili upatikanaji wake uwe wa uhakika na bei nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa dawa, vifaa, vifaa Tiba na Vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na sababu nyingi ikiwemo ya uchache na uwezo mdogo wa viwanda vya ndani kuzalisha dawa.

Jumla ya viwanda sita (6) vinaendelea na uzalishaji wa dawa kwa sasa. Kufuatia uwezo mdogo wa viwango hivi kiasi cha dawa kinachozalishwa na viwanda hivi vya ndani kinatosheleza mahitaji ya nchi kwa takribani asilimia ishirini tu na hivyo basi kuilazimu Serikali kuagiza asilimia themani ya mahitaji yake kutoka nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeunda kamati maalum ya kitaifa ya kuboresha uzalishaji wa dawa nchini. Kamati hii inajumuisha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Ofisi ya Rais Utawala Bora.

Lengo la Kamati hii ni kuandaa mpango wa ukuzaji sekta ya viwanda vya dawa nchini unaolenga katika kuweka sera ya kuendeleza viwanda vya utengenezaji dawa nchini.

Mapendekezo ya mpango huu ni pamoja na kulegezwa kwa masharti ya uwekezaji wa viwanda vya dawa, uhamasishaji wa wahisani, mashirika na vyombo vya fedha ili waweze kuwekeza kwenye viwanda vya dawa nchini, pamoja na kutenga ardhi kwa ajili ya viwanda vya dawa nchini, kutoa mahitaji ya kiufundi na maeneo ya mafunzo kwa watalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kupitia Bunge lako Tukufu kuwa

Vikao vya Kamati hii vinaendelea na tayari Kamati imekamilisha maandalizi ya rasimu ya mkakati wa uboreshaji wa uzalishaji wa dawa nchini *(Strategy to Promote Domestic Pharmaceutical Production).*

Baada ya mkakati huu kupitiwa na wadau na kuridhiwa hatua stahili zitafuatwa ili kupata ridhaa ya Serikali ikiwa ni pamoja na kujadiliwa na Kikao cha Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Jibu la msingi linasema ndani ya nchi yetu Tanzania yenye wananchi wapatao 45,000,000 kuna viwanda sita (6) tu vya uzalishaji wa madawa ya binadamu ambavyo vinazalisha asilimia 20 ya mahitaji. Naomba kujua kati ya viwanda hivi sita (6) viwanda vingapi vya Serikali?

(b) Kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa madawa nchini. Je, Serikali haioni kuwa ni sababu mojawapo ya wahalifu kuitumia nafasi hii kuagiza madawa bandia? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Viwanda sita (6) ambavyo vinazalisha asilimia 20 ya mahitaji ya nchi kwa sasa ni *Shells Pharmaceutical, Keko Pharmaceutical, Mansoordaya Chemicals*

*Limited, Tanzania Pharmaceutical Industry, Zenufa Pharmaceutical* na *AA Pharmaceutical.*

Kuhusu suala la madawa bandia kusema ukweli hili ni eneo ambalo *TFDA* inawajibika na kwa kiwango fulani imekuwa ikiendelea kutushughulikia mpaka kugundua madawa siyo tu yanayotengenezwa nchini hata yale ambayo yanayotoka nje ya nchi. Lakini viwanda vyetu vyote vinapitiwa na *TFDA* na kudhibiti ubora wake. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na karibu nyumbani. Kwa kuwa madawa pia yanakwenda pamoja na vifaa tiba na vifaa tiba vimekuwa vinanung'unikiwa na watalaam wetu, madaktari wetu katika Hospitali.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulieleza Bunge hili ni asilimia pungufu kiasi gani ambacho kinapungua katika Hospitali kubwa kama vile ya Muhimbili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Viwango vya mapungufu vya vifaa tiba katika hospitali zetu sio kitu kinachobaki kama kilivyo, huwa kinabadilika kila wakati kutegemea na matumizi, hata kwa vitu amabvyo tayari vilishakuwepo kwenye kipindi f ulani utaambiwa kile kitu sasa hakipo au kile kile kitu mapungufu fulani.

Kwa hiyo, kusema kwamba sasa hospitali ya Muhimbili ina mapungufu kwa asilimia kadhaa, itakuwa ni kasoro kwa sababu kuna baadhi ya vitu ambavyo leo hii wanasema havifanyi kazi, lakini vilikuwepo jana na kwa namna hiyo tunachojaribu kukisema ni kwamba vile vifaa ambavyo vinahitaji labda *service* tu, inasemwa haifanyi kazi na mtu anasema kifaa hicho hakipo.

Sasa kwa tafsiri hiyo, itakuwa si rahisi kukwambia ni asilimia ngapi ya vifaa ambavyo havipo kwenye hospitali kama Muhimbili, lakini nilichosema kwamba ni asilimia kubwa ya vifaa ambavyo vinahitajika Muhimbili vipo hata hivyo ambavyo wanasema havifanyi kazi maana yake ni kwamba vipo vinahitaji *service* ili viweze kufanya kazi nikitolea mfano wa kitu kama *city scan.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

Na. 158

**Ahadi ya Kupeleka Madaktari Bingwa – Hospitali ya Mkoa wa Singida**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Hospitali ya Singida ni miongoni mwa Hospitali za Serikali zinazokabiliwa na uhaba mkubwa wa vitendea kazi na watumishi wakiwemo Madaktari Bingwa.

Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari Bingwa ili kutimiza ahadi yake iliyoitoa mwaka 2009?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mwaka 2009 Wizara iliahidi kupeleka madaktari bingwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida. Katika hatua za utekelezaji wa ahadi hiyo, mwaka 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilifanya uhamisho wa madaktari bingwa na kuwasambaza katika hospitali mbalimbali za Mikoa kwa madhumuni ya kupunguza tatizo la upungufu wa madaktari bingwa katika Hospitali mbalimbali za Mikoa kwa madhumuni ya kupunguza tatizo la upungufu wa madaktari bingwa katika hospitali hizo ikiwemo Hospitali ya Mkoa wa Singida. Hivi sasa hospitali hiyo ina madaktari bingwa wawili (2), Madaktari *(MD)* saba (7) na Madaktari Wasaidizi *(MO's)* tisa (9).

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mkoa wa Singida ilipangiwa Madaktari Bingwa watatu wa fani za magonjwa ya wanawake, magonjwa ya watoto na upasuaji. Kwa bahati mbaya madaktari hao kutokana na sababu mbalimbali hawakuweza kuripoti Singida. Mwaka 2011/2012 Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nilizozitaja hapo juu, iliwapeleka madaktari bingwa wengine wawili katika hospitali ya Mkoa wa Singida.

Mmoja wa fani ya magonjwa ya wanawake (*Gynaecololgist*) na mwingine wa fani ya afya ya kinywa (*maxillofacial specialist*). Taarifa tulizonazo ni kwamba madaktari hawa waliripoti kazini na mpaka sasa wanaendelea na kazi katika hospitali hiyo. Vile vile Wizara inaendelea na jitihada za kupata madaktari Bingwa wengine ili waende kuongeza nguvu katika Hospitali ya Mkoa wa Singida.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweka kumbukumbu sawa, kati ya Madkatari wote ambao waliwahi kupangwa kuanzia miaka hiyo iliyotajwa ni Daktari mmoja tu ambae aliripoti na hivyo Serikali kuamua kumpanga au kumwajiri Daktari Bingwa mstaafu kwa mkataba wa miaka miwili na hivyo ameshamaliza muda wake na ameshaondoka. Hivi ninavyoongea Hospitali ya Mkoa wa Singida ina Daktari Bingwa mmoja tu ambaye anahudumia wananchi wote. Swali langu:-

Bila maneno ya jitihada, mchakato wala mbinu ni lini kwa maana ya *specific time* Serikali itapeleka Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida ili kuweza kuhudumia, kutoa huduma bora kwa wananchi wa Mkoa huo ambao wanakadiriwa kuwa milioni moja na laki tatu na wala si kuongeza huduma kama alivyosema Naibu Waziri:-

(a) Nataka niambiwe ni muda gani Serikali itapeleka Madaktari Bingwa?

(b) Kwa kuwa kumekuwa na mawazo potofu au mawazo hasi kwa watumishi wengi wakiwemo Madaktari Bingwa kufanya kazi katika Mikoa iliyotelekezwa kimaendeleo na Seikali Singida ikiwemo. Je, Serikali imefanya utafiti na kugundua ni sababu gani ukiacha hii ambayo nimeitaja, zinazopelekea watumishi na hasa hawa Madaktari Bingwa kushindwa kuripoti katika Hospitali ya Mkoa wa Singida na kuweza kutoa huduma?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la lini Mdaktari watakuwa wamepelekwa, kwanza nitoe maelezo mafupi tu.

Kwanza Madaktari Bingwa wanachukua kwenye kipindi kisichopungua miaka mitatu baada ya kuwa wamekamilisha ile *Degree* yao ya kwanza na kufanya kazi ili waweze kumaliza na kuwa Daktari Bingwa. Kwa namna hiyo, sambamba na kutoa ufadhili wa kuwasomesha Madkatari Bingwa katika fani hiyo ya Udhamili (*Masters*), Serikali imekuwa ikijitahidi kuongeza idadi hiyo, mwaka hadi mwaka kutoka mwaka 2005 hadi sasa kutoka kiwango cha Madaktari Bingwa 140 kwa mwaka mpaka mwaka 2010/2011 wakati idadi ya wanaoingia kwa ajili ya *Masters Program* imefikia 300.

Kwa tafsiri hiyo, Madaktari hao wanapomaliza ndipo sasa Wizara yetu inapendekeza kwa TAMISEMI na TAMISEMI inawasilisha kwenye Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili hao Madaktari kupangiwa kwenye vituo mbalimbali.

Kutokana na ukweli kwamba hospitali zetu hivi karibuni zilipandishwa daraja kuwa Hospitali za Mikoa za Rufaa, mahitaji wa Madaktari Bingwa kwa mujibu wa ngazi hiyo ya huduma inakuwa kubwa kuliko ilivyokuwa mwanzo. Kwa sasa kiwango cha chini kabisa cha Hospitali ya Mkoa kinahitaji Madaktari wasiopungua 6 Madaktari Bingwa, lakini wanahitajika ili uweze kusema kwamba sasa wametimia unahitaji Madakatari Bingwa 30 katika Kituo kama hicho.

Kwa tafsiri hii, tunaposema kwamba tunawagawa, sasa kutakuwa na mbinu kama mbili, tatu za kuweza kufanya. Kwanza Wizara itasimamia ili kutoa ufadhili kwa Madaktari waliopo kwenye Mikoa na kupitia ufadhili wa Mikoa kuingia mkataba na Daktari anaehusika ili kumpa ufadhili yeye aende akachukue *Masters Program,* akimaliza arudi kwenye kufanya kazi katika Mkoa husika na kwa tafsiri hiyo tutaondoa upungufu huu ambao unaendelea kuwepo kwenye baadhi ya Madaktari kukataa kwenda kufanya kazi kwenye baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimjibu swali la pili Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Singida umetelekezwa na Serikali

kimaendeleo. Nataka kumhakikishia kwamba Serikali hii, haijawahi na haina mpango wa kutekeleza Mkoa wowote katika maendeleo na hasa Singida. Ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge ameingia kwenye siasa mwaka mmoja na nusu uliopita, ajifunze kidogo Singida ilivyokuwa na Singida ya sasa na hasa katika eneo la afya, katika miaka mitatu mfululizo ni Mkoa wa Singida tu ndiyo umepata fedha nyingi za kutosha kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa hospitali kubwa kabisa ya Mkoa na jitihada kubwa sana zimefanywa na Serikali katika kuboresha Mkoa wa Singida kimaendeleo. Kwa hiyo, nataka kukanusha hili kwamba hatuna mpango, hatujawahi kufanya na hatutafanya. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kwa kuwa mara nyingi sana hospitali ya Wilaya ya Kasulu imekuwa ikikabiliwa na tatizo la X-Ray hali ambayo inawafanya wananchi wa Mji wa Kasulu na Kasulu Vijijini kupata tatizo la huduma hiyo na kwenda kupata huduma katika hospitali ya Kabanga. Je, nilitaka kujua ni lini Serikali itamaliza tatizo hili ili wananchi wapate huduma na ikiwezekana huduma hiyo itolewe kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kuwa swali lililowasilishwa, tulikuwa tunazungumzia suala la Madakatari Bingwa katika hospitali ya Singida.

Swali linaloulizwa na suala la uwepo wa X-Ray katika hospitali ya Kasulu, nilikuwa naomba tu tunaweza tukazungumza hili wakati mwingine au awasilishe swali kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Na. 159

**Polisi Kuuwa Wananchi Katika Mji wa Mugumu**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Kumekuwa na matukio mengi ya uvunjifu wa haki za Binadamu zinazofanywa na Jeshi la Polisi. Kwa mfano mauaji ya wananchi katika Mji wa Mugumu ambapo tarehe 16/11/2010 kijana Machita James aliuawa kwa tuhuma ya wizi wa kuku na tarehe 2 Januari, 2011 Ndugu Chacha Marara, aliuwawa kwa tuhuma za kuuwa Faru.

(a) Je, thamani ya kuku ni sawa na uhai wa binadamu hadi kumlazimu Polisi kutumia risasi kuuwa watu wasio na silaha?

(b) Je, kwa nini Polisi waliosababisha mauaji hayo hawachukuliwi hatua?

(c) Je, kwa nini Tume zinazoundwa kufuatilia mauaji hayo huwa hazitoi majibu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Uhai wa binadamu hauwezi kulinganishwa na thamani ya kuku hata kidogo. Serikali inazo taarifa juu ya vifo vya raia aliowataja Mheshimiwa Mbunge na kwa kuzingatia kwamba ameondoa jina la Hamisi Nyasagari, nitaongelea Marehemu Machota James alifariki dunia t arehe 16 Novemba, 2010 kutokana na majeraha aliyopata kwa kushambuliwa na watu wasiojulikana baada ya kukurupushwa akiiba kuku katika kibanda cha Inspekta Temu wa Kituo cha Polisi Mgumu. Majeruhi aliokotwa na wasamaria wema na kufikishwa kituo cha Polisi Mugumu ambapo alifariki dunia baadaye akiwa njiani kupelekwa Hospitali. Serikali inakemea vikali tabia ya raia kuchukua Sheria mikononi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu Chacha Marara alifariki kwa majeraha aliyoyapata kichwani baada ya kuruka kutoka kwenye gari la wazi (*pickup*) akijaribu kutoroka chini ya ulinzi wa Polisi kufuatia kukamatwa kwa tuhuma za ujangili kwa kuua faru.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia matukio haya niliyoyaeleza hapo juu, Serikali ilifanya uchunguzi wa kina na kubaini kwamba hakuna Askari Polisi yeyote aliyehusika na mauaji haya. Kwa sababu hiyo, hakuna Askari Polisi yeyote aliyechukuliwa hatua za Kisheria.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, katika matukio yote matatu, taarifa za matokeo ya uchunguzi zilitolewa kwa ndugu wa Marehemu. Iwapo kuna mtu yeyote ambaye hajapata taarifa hizo ninamwomba awasiliane na Ofisi ya Kamanda wa Poli wa Mkoa wa Mara ili aweze kupatiwa taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa nasikitishwa na taarifa aliyotoa Waziri kwamba ni ya uwongo na sijui alienda kuwauliza watuhumiwa wenyewe. Ukweli ni kwamba na ushuhuda upo na mashuhuda wapo Inspeka Temu na Maaskari wengine watatu walimkamata Kijana James Machota, wakamshambulia kwa vyuma, wakaenda nae mpaka nyumbani kwao, wakaendelea kumpiga na hata Mama wakampiga kwa mkono wa bunduki.

Baada ya hapo Inspeka Temu alimchukua Marehemu akaenda nae mpaka soko kuu la Mgumu kwa muuza kuku kufuatilia kama kuna ushuhuda kweli amemwuzia yule kuku na wakachukua wale kuku kutoka kwa muuza kuku karibia 28, sasa nataka Waziri aniambie.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther swali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waziri aniambie kwamba taarifa amezipata wapi na kama yuko tayari kufanya uchunguzi wa kina na uhalali kwa sababu ushuhuda upo kwamba Maaskari ndiyo waliohusika kuuwa yule raia kijana kwa kuiba kuku na kulikuwa hamna wasamalia wema

waliomuokota na hadi walitoa kifuta jasho cha shilingi laki tatu. Ni kwa nini Askari watoe kifuta jasho kwa kibaka?

Swali la pili, kuhusu Chacha Marara, ukweli ni kwamba na taarifa zilizokuwepo ni kwamba Chacha Marara alikamatwa usiku wa saa tisa na watu wengine wanne na alipigwa kwenye chumba cha mahojiano wakikiita kama ni cha mauaji na alikufa katika kituo cha polisi.

Naomba Waziri aseme ukweli na awe tayari kuunda Tume iliyo huru ambayo haiwahusishi wauwaji wenyewe ili haki itendeke kwa raia. Vinginevyo Seriklai ya Chama cha Mapinduzi ituambie ni nini maana ya utawala bora maana yake Watanzania wanaendelea kufa na tunapewa taarifa za uwongo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, uliyoyauliza wala sio maswali, kinachoonekana ni kwamba wewe unataarifa bora zaidi kuliko alizonazo Serikali, kwa hiyo, tunakuomba ndani ya siku saba utupatie hizo taarifa kwa undani ili tuweze kujua ni nini hasa ambacho kinaendelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaziwasilisha maana yake zipo.

Na. 160

**Polisi wa Msafara wa Viongozi Kutumia Simu- Badala ya Radiocall- Zanzibar**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR** aliuliza:-

Kuna taarifa kwamba Polisi Zanzibar wanapokuwa kwenye msafara wa Viongozi hutumia simu badala ya Radiocall kwa ajili ya mawasiliani; jambo ambalo huchelewesha mawasiliano:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu jambo hilo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, magari na pikipiki zote zinazoongoza misafara ya Viongozi hutumia mawasiliano ya redio za poli. Hata hivyo wakati mwingine hujitokeza upungufu wa redio kwa baadhi ya Askari wanaosimama katika pointi mbalimbali barabarani na hivyo kuwalazimu kutumia simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kuwapatia Askari wetu vitendea kazi vya kutosha vikiwemo redio za mawasiliano.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa Waziri amekiri kuwa ana upungufu wa vifaa vya mawasiliano na wakati mwingine huwa wanatumia simu za mkononi na kwa kuwa wakati

mwingine simu za mkononi zinakosa mawasiliano. Je, panapotokea dharura, polisi hawa huwa wanafanya nini?

(b) Kwa kuwa ulinzi wa Viongozi una umuhimu wa pekee na unapotangaza kuwa una upungufu wa vifaa vya mawasiliano. Je, huoni unawapa nafasi wale waliokuwa hawana nia njema na nchi yetu kutumia nafasi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa najiuliza Mheshimiwa Amina anajuaje polisi wanafanyaje kazi. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mafunzo ya msingi sana wanaopewa Askari wetu wa Majeshi yote ni kujua namna ya kushughulika na jambo la dharura. Kwa hiyo, inapotokea jambo la dharura, wanashughulikia kwa udharura unaostahili. *(Makofi)*

Na. 161

**Mgodi wa Dhahabu wa GGM Kuzalisha Umeme**

**MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. MHE. DONALD K. MAX)** aliuliza:-

Mgodi wa dhahabu wa Geita *(GGM)* unazalusha MW.38 lakini matumizi yake ni MW 32.4 na kuna *Service* line iliyoachwa kwa ajili ya *TANESCO:-*

(a) Je, kwa nini *TANESCO* hainunui umeme wa ziada wa *MW 6.4* ili wananchi waweze kuutumia?

(b) Je, kwa nini mgodi huu haulipi *Service Levy* kwenye Halmashauri ya Geita?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa dhahabu wa *Geita Gold Mine (GGM)* hivi sasa unatumia umeme unaozalishwa na kampuni ya *Geita Power*. Kampuni hii ina jumla ya jenereta 7 zenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MV 5 kila moja. Umeme unaozalishwa na majenereta hayo 7 ni jumla ya MW 35. Aidha, matumizi ya umeme wa kila siku ni MW 24-25 kutoka katika majenereta 5 ambapo jenereta 2 ni kwa ajili ya dharura (*standby*). Hivyo, kampuni ya *GGM* haina umeme wa ziada kwa ajili ya kuiuzia *TANESCO. (Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *Service Levy* au *Local Levy,* hulipwa kwa mujibu wa Sheria ya *The Local*

*Government (Finance) Act, 1982,* ambayo inaelekeza kuwa, kila kampuni inayofanya biashara katika Halmashauri ya Wilaya husika, inatakiwa kulipa kodi *(Service Levy),* kwa kiwango kisichozidi 3%, 0.3% ya mapato ya *turn over.* Utekelezaji wa Sheria hii, unaitaka Halmashauri husika kutunga Sheria Ndogo *(By Law),* itakayoainisha kiwango kinachotakiwa kulipwa, ambapo Halmashauri hiyo ilitunga Sheria hiyo mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa *GGM,* uliingia Mkataba na Serikali, kwa ajili ya kuchimba madini ya dhahabu Wilayani Geita, ambapo mgodi huo hulipa dola za Marekani 200,000 kila mwaka kwa Halmashauri ya Geita, kuanzia mwaka 2007, kwa mujibu wa Mkubaliano ya Mkataba *(The Mining Development Agreement (MDA).* Mkataba huo, unabainisha kuwa, malipo yatakayofdanyika kwa Halmashauri kwa mwaka ikiwemo *service levy,* isizidi dola za Marekani 200,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Geita tangu mwaka 2004, iliishatunga *By Law* hiyo. Na kwa kuwa, Kampuni ya *GGM* ilianza kulipa *service levy* kwa mujibu wa Mkataba, Halmashauri ya Geita, inatakiwa kupeleka *invoice* kudai tofauti iliyopo ya miaka 2, kwa maana ya mwaka 2005 na mwaka 2006.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na kwamba, majibu hayajitoshelezi, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza; kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba Mgodi huu una uwezo wa kuzalisha *mega watt* 35 kwa siku kutokana na majenereta yake 7, lakini kwa makusudi Mgodi huu huwasha majenereta 5 kukidhi mahitaji yake ya *mega watt* 24 mpaka 25 na kuacha kuwasha yale 2, wakati ukijua kwamba, wananchi katika maeneo ya jirani wanaendelea kusota au kuburudika na kiza. Je, Serikali, inaona kwamba, ni halali kwa mgodi huo kuendelea kutowasha yale majenereta 2, yakisubiri dharura na wananchi wake waendelee ku-*enjoy* kiza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, mgodi wa Geita, unafanya shughuli zake hapa nchini kwa mujibu wa Sheria. Na kwa kuwa, ninaamini kwamba, kampuni hii inafahamu Sheria za Nchi. Je, ni kwa nini kwa miaka 6 imekaa kimya bila kulipa *service levy,* ya mwaka 2005 na 2006?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati nja Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lembeli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jenereta za *GGM* ambazo ziko *standby,* na kwamba, wao kwa madai yao ni kwamba, wanazitumia hizi pale itakapotokea kupata shida kwa haya majenereta mengine, ni haki yao kwa sababu, ni mali yao.

Lakini sote tunatambua kwamba, kuna wajibu wa kijamii wa makampuni haya, kwa ajili ya kujenga mahusiano mazuri na watu wanaozunguka maeneo ya

mgodi Serikali, inaona basi kwanza tutoe wito kwa *TANESCO* katika eneo lile kwenda kufanya mazungumzo ya kina ili, waone kama kuna uwezekano wa kampuni ile kuweza kuruhusu hata angalao jenereta moja hiyo, iweze kutumika kwa kusambaza umeme katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nitaomba niweze kufika mwenyewe niweze kuona na kuongea na uongozi wa *GGM,* kuona uwezekano huo. Kwa sababu, kwa kweli, hatuwezi kusema tunawalazimisha kama sisi hatujaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusiana na *Service Levy.* Ni kweli Sheria, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, Sheria ya Fedha za Halmashauri ya Mwaka 1982, inataka makampuni yote yanayofanya shughuli katika maeneo ya Halmashauri, yaweze kulipa *Service Levy* ya 0.3%, isioyozidi kiwango hicho. Sasa kama kuna tofauti hii ambayo nimeisema, ambayo Halmashauri wanapaswa kudai, wakifanya hivyo, mimi naamini hawa hawatakuwa na ugumu wowote wa kulipa, kwa sababu, Sheria ipo na wao wanaifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niweze kutoa wito tu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita; Kahama kulikuwa na tatizo kama hili, lakini leo hii Kahama wanalipwa vizuri tu na Mgodi wa Kahama. Kwa hiyo, niwaombe sana, waweze kuwasiliana na wenzao wa Kahama, waone ni namna gani walifanya

wakafanikiwa na sasa hivi wanalipana kwa sababu, walisimamia tu Sheria ile iliyopo.

Kwa hivyo, niwaombe sana waweze kufanya hivyo na pengine tunaweza tukalimaliza tatizo hili. Ahsante sana.

Na. 162

**Kupeleka Umeme Vijiji vya Jimbo la Chilonwa**

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE** aliuliza:-

Njia ya umeme itokayo Kiteto kupeleka umeme kwenye baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Kiteto na Kondoa, viko jirani sana na maeneo ya vijiji vya Jimbo la Chilonwa:-

Je, Serikali, haioni haja ya kufikisha umeme kwenye Vijiji vya Zajilwa, Izava, Segela na Itiso vya Jimbo la Chilonwa, kupitia njia hiyo ambayo, kwa sasa ina vikaribia sana vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hezekia Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na tathmini iliyofanywa na Shirika la Umeme *(TANESCO),* upelekaji wa umeme katika vijiji vya Zajilwa, Izava, Segala na Itiso, utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo

wa *Kv 33,* yenye urefu wa kilometa 68. Uwekaji wa *transformer* 11 na ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *volt 400* yenye urefu wa kilometa 40.

Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa *Kv 33,* itatokea katika Kijiji cha Matui, kilichopo Wilaya ya Kiteto, ambacho kitapata umeme kutoka mradi wa *MCC.* Mradi huu wa umeme utavinufaisha vijiji vya Osteti, Izava, Segala, Magungu, Zajilwa, Itiso na Solowu. Gharama za mradi huo, zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 3.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijijini wamekwisha kabidhiwa mradi huu kwa hatua zaidi.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, ambayo yanatia matumini kwa wananchi wa Itiso. Pamoja na hivyo vijiji vingine alivyovitaja. Sasa nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, l kwanza, pamoja na vijiji hivi vilivyotajwa katika swali la msingi, viko vijiji vingine viwili ambavyo viko karibu sana na njia ya umeme ambavyo vina ahadi ya Serikali, na kimojawapo, Mheshimiwa Naibu Waziri aliyemtangulia Mheshimiwa Malima, alishafika, Kijiji cha Msanga, ambacho kiko kilometa 4 tu kutoka Chamwino Ikulu. Wananchi waliahidiwa kuwekewa umeme pale. Pili ni Kijiji kingine ambacho kipo katika njia ya Dar-es-Salaam, Chinangali Mwegamile, nacho kina ahadi ya Serikali.

Je, leo Mheshimiwa Waziri, anatoa tamko gani kwa wananchi hawa wa Msanga na Mwegamile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa vile, Serikali, ina mpango wa kupeleka umeme Vijijini kupitia mradi wa *REA.* Je, Serikali, itapeleka lini umeme kupitia mradi huu, katika vijiji vya Kata za Ikowa na Msamale? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chibulunje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Serikali, iliyotolewa na Mheshimiwa Malima, kama ambavyo aliitoa, na kwa sababu hizohizo za kuitoa ni kwa kuwa, Serikali hii ni moja na mimi nimerithi mikoba yote ya Mheshimiwa Malima, napenda nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ahadi hii ya Serikali itaitekeleza.

Kwa harakaharaka tu ni kwamba, tutajaribu kuwasiliana na *TANESCO* kwa sababu, kilomita hizi ni nne (4) tu, kutoka Ikulu yetu ya Chamwino, basi nadhani tujaribu kujitahidi tuwasiliane na *TANESCO,* tuone namna tunavyoweza kufanya. Hii itaenda sambamba na Chinangali na Mwegamile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kata alizozisema hizo kwa swali la pili, Kata za Ikowa na hiyo nyingine

aliyoitaja, nitajaribu kuangalia kama hazipo kwenye miradi yetu ya *MCC* inayoendelea au ya *REA* inayoendelea kwa kipindi kijacho cha mwaka unaokuja. Tulikuwa tunajaribu kuwasiliana sisi Wizara yetu, kuweza kuwapa fursa Waheshimiwa Wabunge, kuwaita Wataalamu wetu waweze kuja kuonesha miradi ile na *planning* yake ilivyo katika Wilaya zetu na Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kwamba, hapa inaweza ikawa Ikowa haipo kwa sababu, Ikowa ninayoifahamu mimi ni mahali ambapo kweli, panastahili kuwa na umeme. Lakini Mheshimiwa Mbunge, tuwasiliane tuweze kuona kama kuna nini chakufanya katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali. Serikali, imekuwa ikizungumzia kupeleka umeme Vijijini kwa kuwa, nyumba za Vijijini nyingi ni za tembe na zimeezekwa kwa nyasi. Sasa Serikali, haioni kwamba, wakati sasa umefika, wawasaidie wananchi hawa kuboresha nyumba zao, badala ya kuendelea kuwakejeli kwa kuwapelekea umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa kujenga nyumba ni wajibu wa mwenye nyumba. Serikali, inachofanya ni kuweka mazingira mazuri, ili watu

waweze kuwa na uwezo wa kuweza kujenga nyumba zao na maisha yao mengine. Sasa kama Serikali, kupeleka umeme ambako wananchi wanauhitaji sana ni kuwakejeli, hiyo sio Sera ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Chama cha Mapinduzi ni kupeleka umeme vijijini, ili kuamsha uchumi wa maeneo ya Vijijini kwa ajili, ya kutoa ajira zaidi kwa wananchi.

Kwa kufanya hivyo, hatupeleki umeme kwa nia ya kuwakejeli wananchi wa Tanzania waelewe kwamba, tunapeleka umeme, ili waweze kuweka viwanda vidogovidogo, ili waweze kuzalisha na wajenge uchumi wao na kupitia hapo ndipo watakapoweza pia kujenga nyumba bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme tu kwamba, kama kupeleka umeme ni kuwakejeli, basi Chama chetu cha Mapinduzi (CCM), sio Sera yake. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na muda wetu wa kipindi cha maswali umeisha. Sasa niombe kutangaza wageni wetu wa siku ya leo kama ifuatavyo:-

Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Jumanne Mghembe. Ambao ni Kudra Maghembe, mke wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana mama; karibu sana. Nikuhakikishie Profesa Maghembe, anafanya kazi nzuri hapa Bungeni.

Mwingine ni Nldugu Mvumo Maghembe, mtoto wake na Minian Mbokoze, Shemeji yake; karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, ni Ndugu Helena Mahenge, mke wa Mheshimiwa Waziri, Ndugu Vladimir Nikitushikina, baba mkwe, karibu sana baba mkwe, natumaini unaweza kufuatilia Kiswahili. Ndugu Valentina, mama mkwe. Wengine ni Ndugu Diana Mahenge na Ndugu Anthony Mahenge wote wawsili ni watoto wa Naibu Waziri, Ahsanteni sana na karibuni sana. Familia ya Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Karibuni sabna Dodoma. *(Makofi)*

Naomba kumtambulisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Injinia Christopher Sai. Karibu sana Katibu Mkuu. Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Injinia Bashir Mrindoko, karibu sana Mhandisi Mrindoko. Wakurugenzi wa Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara na Watumishi wengine wote wa Wizara ya Maji, ahsanteni sana na karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Ndugu Sebastian Matondo, mgeni wa Mheshimiwa Meshack Opulukwa. Karibu sana Ndugu Matondo. *(Makofi)*

Wageni waliko kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 52 na walimu kutoka shule ya awali na msingi ya Ignitius ya Dodoma. Karibuni sana wanafunzi, karibuni sana Dodoma. Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa David Kafulila, Mwinjilisti Salvatory Moto na Kocha Baharani Sued. Mwinjilisti yuko wapi? Haya, karibu sana. Mheshimiwa, wewe umetuletea Mwinjilisti, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Vicent Nyerere, ni Baraka Majura na Juma Songo. Baraka na Juma? Karibuni pia.

Meneja wa Bodi ya Korosho Tawi la Tanga, Ndugu Juma Yussuf. Karibu sana.

Naomba niwatambulishe wageni wa Mheshimiwa John Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, ambaye ni Dkt. Stephen, *Resident Director* wa Shirika la *FES.* Karibu sana; lakini pia Ndugu Kambangwa, yeye ni Mkutubi Mkuu wa Maktaba ya *CCM* Makao Makuu. Karibu sana  Ndugu Kambangwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wengine, Maktaba mnazo?

Taarifa ya Kikao. Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anaomba Kikoa leo saa  7.00 cha Wajumbe wa Kamati hiyo, katika Ukumbi Namba 231, katika Jengo la Utawala la Bunge.

Mheshimiwa Abdulkarim  Shah, Makamu wa Mwenyekiti naona na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Daud  Lembeli yupo, saa  7.00 Mchana Wajumbe wote mnaombwa kukutana Ukumbi 231, katika  jengo la Utawala.

Mheshimiwa Anna Abdallah, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane saa 7.00 Ukumbi Namba 219. Saa 7.00, Ukumbi Namba 219, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Tunaomba kuwatangazia kutoka Ofisi yetu ya Utawala kwamba, Maafisa, kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* bado wapo Chumba 220. Kwa wale ambao hawajawaona au hawajakamilisha kujaza zile zile fomu, tunaombwa tufanye hivyo mara moja.

Haya, naomba kuchukua nafasi hii kuutambua uwepo wa Mheshimiwa Sabreena Sungura, kama Kiongozi wa Upande wa Kambi ya Upinzani, asubuhi ya leo. Jamaa zetu wa *CHADEMA,* wanaonesha kwamba, kumbe hata wao wanaweza wakawaamini watu wa Kigoma. Pia watani wetu. Kila la heri Mheshimiwa Sabreena. Wanamjibu Mheshimiwa Nahodha. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, juzi kule Dar-es-Salaam, kulikuwa na mechi kati ya Wabunge mashabiki na wapenzi wa timu ya Simba na Yanga, katika Uwanja wa Taifa kule. Sasa hapa, nimepata vijikaratasi vingi kweli kweli. Nianze na cha kutoka Yanga, kwa wachezaji wa Yanga kutoka Bungeni humu, wakiwakilishwa na Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis na Waheshimiwa Wabunge Wengine. *(Makofi)*

Yanga, wanasena bwana ile mechi irudiwe, haikuwa sawa. Kwamba, baada ya Simba, kuwa wamechoka na wanaanguka kila wakati, ikabidi wamrubuni refa. Kwa hiyo, wanaomba mechi irudiwe, wanakata rufaa kwangu. Mimi kama Jaji ambaye sina upendeleo upande wowote, nitatangaza hapa maamuzi yangu wakati muafaka. *(Makofi/Kicheko)*

Kwamba, taarifa ambazo nimezikusanya ni kwamba, baada ya kipigo cha bao 3 – 2, Simba kuwafunga Yanga kwa bao 3 – 2 za *penalt,* wachezaji wengi wa Yanga, bado wako njiani wanasuasua, hawajarudi hapa Ukumbini.

Kwa hiyo, Wabunge wote, tunawapongeza sana Timu zote mbili kwa burudani nzuri sana. Katika mchezo huo, nyota alikuwa ni Mheshimiwa Joshua Nassari, kwa kupangua *penalt tatu (*3) za Yanga. Nahodha wake alikuwa Mheshimiwa Amos Makalla, kwa upande wa Simba. *(Makofi/Kicheko)*

Uamuzi wa rufaa yangu ni kwamba kipigo hiki ni mwendelezo tu wa ule utaratibu wa kawaida wa dozi za mwaka 2012 tuvumiliane tu Waheshimiwa Wabunge. *(Kicheko/Makofi)*

Kipekee kwa kumalizia naomba nimtambulishe mgeni maalum kabisa nadhani atakuwa yuko *Speaker's Gallery* Mheshimiwa Martha Wejja, yupo wapi Mheshimiwa Martha Wejja, huyu ameshakuwa Mbunge katika Bunge hili kwa miaka kadhaa na ni katika Wabunge aliyekuwa maarufu kabisa na kwa

wadhifa wake yeye ndiyo aliyekuwa Miss Bunge. *(Makofi)*

Wadhifa ambao hivi sasa unashirikiwa na Mheshimiwa Maria Hewa. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo naomba sasa tuendelee na shughuli zinazoendelea Katibu, tuendelee na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 - Wizara ya Maji

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni Hoja za Serikali, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Waheshimiwa Wabunge naomba tuwe na utulivu kama tunavyojua Wizara hii inagusa Wapiga Kura wetu wengi sana, Mheshimiwa Profesa Maghembe.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Maji, sasa ikubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Maji, Wizara inayomgusa kila Mtanzania na yenye changamoto nyingi.

Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu kwamba, nitafanya kazi zangu kwa juhudi kubwa na ufanisi wa hali ya juu ili kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuwapatia wananchi wa Tanzania huduma ya maji safi, salama na ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2011/2012 na Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, yalizingatiwa wakati wa utayarishaji wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa na wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Wabunge hao ni Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu Jimbo la Igunga, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari Jimbo la Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed, Mbunge wa Baraza la

Wawakilishi (BLW) na Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, Viti Maalum (CHADEMA).

Wabunge wa kuteuliwa ni Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mheshimiwa Saada Salum Mkuya, Mheshimiwa James Francis Mbatia na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo. Naahidi kushirikiana nao katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu; Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Uhusiano na Uratibu, kwa hotuba zao ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa Bajeti, uchumi na utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2012/2013 na 2015. Nawapongeza pia, Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Hayati Regia Estelatus Mtema, Viti Maalum, Hayati Jeremiah Solomon Sumari, Jimbo la Arumeru Mashariki na Hayati Mussa Hamisi Silima, Jimbo la Msufini. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu na wananchi wa mkoa wa Morogoro, Jimbo la Arumeru Mashariki na Jimbo la Msufini. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Sekta ya Maji Nchini katika kutekeleza majukumu yake, Wizara yangu inazingatia ahadi zinazotolewa na Serikali, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II), Malengo ya Milenia, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sera ya Taifa ya Maji; Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji; Sheria za Maji na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rasilimali za Maji, kila mwaka Tanzania inakadiriwa kupata rasilimali ya maji juu ya ardhi yanayofaa kutumika kwa matumizi mbalimbali (annual renewable water resource) ya kiasi cha wastani wa kilomita za ujazo 89. Aidha, inakadiriwa kuwa hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi ni kilomita za ujazo 40. Hata hivyo, kutokana na tofauti ya hali ya hewa na jiolojia; mtawanyiko na upatikanaji wa rasilimali hizo nchini hauko sawa katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya nchi yetu yameendelea kuwa na uhaba wa maji kwa matumizi yaliyokusudiwa kutokana na maji hayo kutokuwa na ubora unaokubalika, uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi. Sababu nyingine ni pamoja na gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi rasilimali za maji, matumizi ya maji yasiyozingatia ufanisi, uchafuzi wa

vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli za kibinadamu na kasi kubwa ya ongezeko la watu. Inakadiriwa kuwa kiwango cha maji yaliyopo kwa sasa kwa kila mtu kwa mwaka ni wastani wa mita za ujazo 2,020 na ifikapo mwaka 2025 kiwango hicho kinatarajiwa kupungua hadi mita za ujazo 1,500. Hivyo, ni muhimu tuchukue hatua za kuhifadhi vyanzo vyetu vya maji ili kunusuru rasilimali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Maji Vijijini. Serikali imeendelea kuboresha huduma za maji vijijini kwa kujenga miradi mipya, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji. Uboreshaji huo unatekelezwa kwa kuwashirikisha wananchi katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga, kusanifu, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji.

Katika mwaka 2011, kulikuwa na ongezeko la watu 88,282 waliopata huduma ya maji katika vijiji mbalimbali. Katika baadhi ya maeneo, huduma hiyo imepungua kutokana na baadhi ya vyanzo vya maji kukauka. Miradi ya kuendeleza huduma ya maji vijijini inatekelezwa na Halmashauri za Wilaya chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Maji Mijini, huduma ya maji mijini inasimamiwa na kutekelezwa na Mamlaka 19 za majisafi na usafi mazingira katika miji mikuu ya mikoa, Mamlaka 109 katika ngazi za Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya Kitaifa. Katika kuimarisha usimamizi, Mamlaka hizo zimegawanywa katika Madaraja ya A, B na C kulingana na uwezo wa

kila Mamlaka kujitegemea. Mamlaka za miji mikuu ya mkoa zimegawanyika kama ifuatavyo; Mamlaka 13 za Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Tanga, Songea na Musoma zipo daraja ‘A’. Katika daraja hili, Mamlaka zina uwezo wa kujitegemea kwa kulipia gharama zote za uendeshaji na matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa daraja ‘B’ zipo Mamlaka nne za Bukoba, Kigoma, Singida na Sumbawanga ambazo bado zinapata ruzuku ya kulipia sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo. Mamlaka zilizo kwenye daraja ‘C’ ni Babati na Lindi ambazo bado zinapata ruzuku ya mishahara ya wafanyakazi wake pamoja na kulipia gharama za umeme wa kuendesha mitambo na uwekezaji. Aidha, Mamlaka zote za ngazi ya wilaya, miji midogo na miradi saba ya kitaifa nazo zipo katika daraja C. Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka hizo ili ziweze kujiendesha kibiashara na kuwahudumia wateja wake kwa ufanisi kwa lengo la kukidhi gharama zote za uendeshaji na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira mijini, Wizara kupitia Mamlaka za maji mijini imeendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi katika baadhi ya miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya maji ya kitaifa. Upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa ya daraja A unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 88 mwezi Desemba 2010 na kufikia wastani wa asilimia 89 mwezi Machi, 2012. Kwa Mamlaka za mikoa

za daraja B na C upatikanaji wa maji unakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 82 mwezi Machi, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Kibaha na Bagamoyo, huduma ya maji hutolewa na Shirika la usambazaji maji Dar es Salaam (DAWASCO) na kusimamiwa na DAWASA. Shirika la DAWASCO limekodishiwa miundombinu na DAWASA kwa mkataba wa miaka 10 kuanzia mwaka 2005. Kiwango cha utoaji wa huduma ya maji kwa sasa kinakadiriwa kuwa asilimia 67 kutoka asilimia 68 ya Desemba 2010. Hata hivyo kati ya hiyo asilimia 67, wakazi wanaopata huduma hiyo moja kwa moja kwenye makazi yao ni asilimia 55 na asilimia iliyobaki hupata maji kupitia magati (viosk) au kwa kuchota kwa majirani.

Hali ya ongezeko dogo au kupungua kwa huduma imesababishwa na ongezeko kubwa la watu wanaohamia mijini ikilinganishwa na kasi ya uwekezaji katika miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha utoaji wa huduma ya maji kwa sasa katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa ni wastani wa asilimia 52.5 ya wakazi wanaoishi maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa uondoaji majitaka mijini haujabadilika kulinganisha na miaka iliyopita kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Tabora, Tanga na

Songea. Katika miji mingine iliyobaki, hatuna miundombinu ya majitaka. Hali hiyo imetokana na kutokuwa na uwekezaji mpya katika kipindi hiki ambapo uwekezaji unategemewa kufanyika katika awamu ya pili ya *WSDP* inayotarajiwa kuanza mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa Hesabu, kama ilivyo ada, kila mwaka Wizara yangu hufanyiwa ukaguzi wa hesabu za mwaka *(Audited Annual Financial Statements)* kulingana na viwango vya ukaguzi vya kimataifa. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara imefanikiwa kupata hati safi (Unqualified Opinion) kufuatia ukaguzi wa hesabu uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu imepata hati safi kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2007/2008. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza watumishi wa Wizara yangu kwa kazi hii nzuri na kuwataka waendelee kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya 2011/2012 na Mpango wa 2012/2013, utekelezaji wa mpango wa mwaka 2011/2012 na malengo ya mwaka 2012/2013 kwa Sekta ya Maji katika maeneo ya rasilimali za maji, huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini, huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mijini, na masuala mtambuka umeainishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Naibu Spika, Rasilimali za Maji, kazi za Wizara yangu katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji ni pamoja na kuchunguza na kutathmini rasilimali za maji nchini; kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji; kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji ili zisimamie kikamilifu rasilimali hizo. Kazi nyingine ni kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele, yakiwemo mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Rasilimali za Maji, Wizara yangu ina jukumu la kuchunguza wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi. Uchunguzi huo hufanyika kwa kutumia takwimu kutoka kwenye mtandao wa vituo vya kupima mwenendo wa rasilimali hizo.

Katika kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi na kwa wakati, mwaka 2011/2012 jumla ya vifaa 126 vya utafiti wa vyanzo vya maji chini ya ardhi *(Geological hammers (72)* na *Geological compasses (54))* vilinunuliwa kwa ajili ya Ofisi za Mabonde ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya vifaa vipya vya utafiti wa vyanzo vya maji chini ya ardhi kwa watumishi 28 kutoka Ofisi za Mabonde na Wizara. Ujenzi na ukarabati wa vituo 20 vya kupima wingi wa maji na hali ya hewa katika mito na mabwawa katika Mabonde ya Ziwa Tanganyika (18), Wami/Ruvu (1) na Bonde la Ziwa Rukwa (1) ulifanyika. Vilevile, ukaguzi ulifanyika katika vituo vya

hali ya hewa kwenye mabonde ya Ziwa Victoria (13), Pangani (10) na katika vituo tisa vya upimaji wa wingi wa maji kwenye mito katika Bonde la Ziwa Rukwa ili kuhakikisha vinaendelea kutoa takwimu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, ukusanyaji wa takwimu ulifanyika katika vituo 104 vya kupimia wingi wa maji katika Mabonde ya Ziwa Nyasa (15), Ziwa Rukwa (18), Ruvuma (4), Wami/Ruvu (35), Ziwa Tanganyika (22) na Pangani (10). Ukusanyaji wa takwimu uliendelea katika vituo 79 vya kupimia hali ya hewa kwenye Mabonde ya Ziwa Nyasa (8), Ruvuma (4), Wami/Ruvu (45), Ziwa Rukwa (18) na Bonde la Kati (4). Pia, takwimu zilikusanywa kutoka vituo vitano vya kupimia maji chini ya ardhi katika Bonde la Wami/Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina jumla ya vituo 362 vya kupimia mwenendo wa rasilimali za maji juu ya ardhi. Kati ya vituo hivyo, 90 vipo katika hali nzuri na vinafanya kazi wakati vituo 272 haviko katika hali nzuri. Katika mwaka 2012/2013, vituo 32 vitajengwa upya na vituo 240 vitakarabatiwa. Pia, watumishi wa kada mbalimbali watapatiwa mafunzo ya jinsi ya kutumia vifaa katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Utafutaji wa Vyanzo Vipya vya Maji, maji chini ya ardhi ni moja ya vyanzo vya maji vinavyotumika hapa nchini hasa katika maeneo kame. Katika mwaka 2011/2012, utafiti wa kubaini maeneo yanayofaa kuchimba visima vya maji uliendelea katika maeneo 563 katika Mabonde ya: Ziwa Rukwa (22), Ziwa Tanganyika (14), Rufiji (7), Ziwa Victoria (63),

Ruvuma (80), Wami/Ruvu (68), Pangani (56), Ziwa Nyasa (8) na Bonde la Kati (245). Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuchunguza maeneo yanayofaa kuchimba visima virefu vya maji na kusimamia uchimbaji kwa maeneo 630 katika sehemu mbali mbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu wa uchimbaji wa visima vya maji ni jukumu la Wizara yangu. Uratibu huu unalenga kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zilizowekwa zinafuatwa ili kudhibiti uchimbaji holela wa visima unaoweza kusababisha athari za kiafya na uharibifu wa mazingira.

Kwa mwaka 2011/2012, Wizara ilihakiki uchimbaji na kusajili visima 561. Kati ya visima hivyo, 256 vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na 305 vilichimbwa na kampuni binafsi kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1 na 2. Kuna jumla ya kampuni binafsi 126 za uchimbaji wa visima vya maji nchini. Kati ya kampuni hizo, 10 zilisajiliwa mwaka 2011/2012.

Katika mwaka 2012/2013, uratibu wa uchimbaji wa visima vya maji utaendelea chini ya usimamizi na udhibiti wa Wizara yangu kupitia Ofisi za Mabonde ya Maji. Elimu itaendelea kutolewa kwa wadau kuhusu taratibu za kufuatwa katika uchimbaji wa visima, ikiwa ni pamoja na kuwa na vibali vya kuchimba na vibali vya kutumia maji. Wizara yangu inahimiza wamiliki wa visima kupima ubora wa maji ya visima vyao angalau mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya maandalizi ya mradi wa uchimbaji wa visima katika maeneo kame kwa kushirikiana na Serikali ya Misri. Mradi huo haukuweza kutekelezwa katika mwaka 2011/2012 kutokana na hali ya kisiasa iliyoikumba nchi ya Misri. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mradi huo utaanza kutekelezwa mwaka 2012/2013 kufuatia ziara ya wawakilishi toka Serikali ya Misri hapa nchini mwezi Mei, 2012. Pamoja na uchimbaji visima, Serikali ya Misri imekubali kutoa mafunzo kwa wataalam wa Wizara katika fani mbalimbali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo utahusisha maeneo kame ya Wilaya tisa za Maswa, Bariadi, Magu, Tarime, Same, Rorya, Bunda, Mwanga na Kiteto. Vijiji vitakavyohusika ni Shishiyu, Mwabulimbu, Mwang'honoli, Kadoto, Mwamanege, Mwabomba na Sangamwalugesha (Maswa); Sunzula, Kabale, Lagangabilili, Gambasingu, Mwanunui, Nanga, Bumela, Nkoma, Laini, Kilulu, Nkololo, Kidinda (Bariadi); Lutale, Kitumba, Shighala, Ng'hanya, Mwamigongwa, Lwangwe, Mwakiloba, Mwamgoba, Badugu na Kinango (Magu) na Nyasincha na Kibaso (Tarime).

Vingine ni Mwembe, Makanya, Mgwasi, Same mjini, Mvure, Kongei na Mheza (Same); Minigo, Omoche, Nyamasanda na Nyambori (Rorya); Karukekere, Buzimbwe, Buguma, Nyangere, Kitaramanka, Nyang'aranga, na Marambeka (Bunda); Lembeni, Mgagao, Pangaro, na Toloha (Mwanga) na Namelock, Ilera, Chapakazi, Kijungu, Loitepasi, Dongo, Engongangare na Katikati (Kiteto).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea na hatua za maandalizi ya ujenzi wa bwawa la Farkwa katika Bonde la Kati litakalokuwa chanzo cha maji kwa Manispaa ya Dodoma na miji ya wilaya za Kondoa, Chamwino na Bahi. Rasimu ya mkataba wa mtaalam mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni na rasimu ya mkataba wa kutathmini athari za kimazingira na kijamii kwa ajili mradi wa ujenzi wa bwawa hilo zimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia, itaendelea na maandalizi ya ujenzi wa bwawa la Ndembera katika Bonde la Mto Rufiji litakalotumika kwa ajili ya kusawazisha (balance) mtiririko wa maji katika kipindi cha mwaka mzima kwenye mto Ruaha Mkuu. Matumizi mengine ya bwawa hilo ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha umeme. Rasimu ya mkataba wa mtaalam mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa bwawa hilo imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio na ushauri. Aidha, taratibu za kumpata mtaalam mshauri wa kutathmini athari za kimazingira na kijamii kwa ajili ya mradi wa bwawa hilo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara imeendelea na taratibu za kuwapata wataalam washauri watakaokagua athari za kimazingira na kijamii (Environmental and Social Audit) kwa ajili ya ukarabati wa mabwawa ya Mchema lililopo Masasi;

Leken/ Elenywe, Enguikument I na Enguikument II yaliyopo wilaya ya Monduli, na Itobo, Uchama na Nkiniziwa yaliyopo wilaya ya Nzega. Kazi za kuwapata wataalam hao zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itafanya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni vya ujenzi wa mabwawa ya Farkwa na Ndembera na ukaguzi wa athari za mazingira kwa mabwawa ya Mchema; Leken/ Elenywe, Enguikument I, Enguikument II, Itobo, Uchama na Nkiniziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji nchini. Lengo ni kuimarisha matumizi endelevu na kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinagawanywa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Jumla ya vibali vya kutumia maji 605 vilitolewa na matoleo 171 ya maji yalikaguliwa katika mabonde ya Rufiji (144), Tanganyika (16) na Pangani (11) kulingana na masharti ya vibali vya kutumia maji.

Ukaguzi huo ulibaini matatizo ya ubovu wa mabanio unaopelekea upotevu wa maji kutoka katika vyanzo, uchepushaji wa maji usiozingatia sheria na uchafu wa matoleo na mifereji ya maji. Wahusika walielekezwa kukarabati mabanio na kusafisha mifereji na kuzingatia masharti ya vibali vya kutumia maji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kupitia Ofisi za Mabonde ya Maji itaendelea kutoa elimu kwa wadau

juu ya umuhimu wa kuwa na vibali vya kutumia maji na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utayarishaji wa Mipango Shirikishi, katika kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji, Wizara yangu iliendelea na utayarishaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa rasilimali hizo. Katika mwaka 2011/2012, kazi zilizofanyika ni pamoja na kutathmini wingi na ubora wa rasilimali za maji, kuainisha mahitaji ya maji ya sekta mbalimbali katika muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango hiyo imeendelea kutayarishwa katika Mabonde ya Rufiji, Wami/Ruvu na Bonde la Kati. Katika Bonde la Rufiji, taarifa ya pili ya uandaaji wa Mpango imekubaliwa na wadau. Utayarishaji wa mpango huo unaendelea. Kwa upande wa Bonde la Kati, mtaalam mshauri amekamilisha tathmini ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde zima. Kwa upande wa Bonde la Wami/Ruvu, baada ya taarifa ya pili ya uandaaji wa Mpango kukubaliwa na wadau, utayarishaji wa Mpango unaendelea kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA).* Wizara imekamilisha upatikanaji wa wataalam washauri wa kutayarisha Mipango Shirikishi katika Mabonde ya Pangani, Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa na Ruvuma na kazi ya kutayarisha mipango hiyo imeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu katika hotuba yangu ya mwaka jana, Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ziwa Victoria

ilipanga kuanza utayarishaji wa Mpango Shirikishi kwa Bonde la Ziwa Victoria. Taratibu za kumpata mtaalam mshauri atakayetayarisha Mpango huo zinaendelea na atapatikana mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itakamilisha utayarishaji wa Mipango Shirikishi kwa Mabonde ya Rufiji, Wami/Ruvu na Bonde la Kati, na kuanza utayarishaji wa Mpango Shirikishi katika Bonde la Ziwa Victoria. Aidha, Ofisi za Mabonde ya Maji zitaendelea kuanzisha na kuimarisha jumuiya za watumiaji maji kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009. Elimu kuhusu uanzishwaji wa kamati za mabonde madogo ya maji na jumuiya za watumiaji maji katika mabonde yote ya maji itaendelea kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kupitia timu za uwezeshaji *(District Facilitation Teams - DFTs)* imeendelea kutoa elimu ya uundaji wa jumuiya za watumiaji maji katika Mabonde yote tisa. Jumuiya tatu za watumiaji maji katika maeneo ya Lulindi, Likonde na Ndanda kwenye Bonde la Mto Ruvuma zilisajiliwa kwa kufuata Sheria ya Rasilimali za Maji. Hadi sasa kuna jumuiya 53 zilizosajiliwa nchini kote. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuunda jumuiya kumi za watumiaji maji katika Mabonde ili kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji unaolenga kupunguza migogoro miongoni mwa watumiaji wa maji na kurahisisha ukusanyaji wa ada za matumizi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji. Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Ofisi za Mabonde ya Maji kwa kutoa mafunzo kwa watumishi, ujenzi wa ofisi na ununuzi wa vitendea kazi. Katika mwaka 2011/2012, wataalam wa Ofisi za Mabonde ya Maji walipatiwa mafunzo katika fani za uandaaji wa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Matumizi ya taarifa za kijiografia kwa kutumia mfumo wa kompyuta na usimamizi wa takwimu.

Fani nyingine ni pamoja na usuluhishi wa migogoro katika matumizi ya maji na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, sheria za kazi, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, sheria mpya ya usimamizi wa rasilimali za maji, na matumizi ya programu mbalimbali za kompyuta. Elimu hiyo ilitolewa kwa wataalam 61 katika mabonde ya Pangani (4), Ziwa Nyasa (1), Ruvuma (1), Ziwa Rukwa (8), Rufiji (44) na Wami/Ruvu (3). Aidha, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa katika mji wa Tukuyu unaendelea, kwa sasa umefikia asilimia 80 na utakamilika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuziimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji kwa kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Mabonde ya Maji na Maabara za Maji na kuzipatia wataalam, vitendea kazi na mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makusanyo ya Maduhuli, moja ya majukumu ya Bodi za Mabonde ya Maji ni kuandaa mikakati ya ukusanyaji wa maduhuli

yatokanayo na ada za matumizi ya maji. Katika mwaka 2011/2012, maduhuli ya jumla ya shilingi 1,034,634,857.55 sawa na asilimia 88 ya lengo la shilingi 1,181,000,000 yalikusanywa hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012. Katika mwaka 2012/2013, Ofisi za Mabonde ya Maji zinakadiria kukusanya kiasi cha shilingi 1,300,000,000 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kudhibiti Migogoro Miongoni mwa Watumiaji wa Maji, Ofisi za Maji za Mabonde zimeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuunda kamati za pamoja za kusuluhisha migogoro katika matumizi ya maji katika maeneo yao, kuhamasisha uundaji wa Jumuiya za Watumiaji Maji na pale inapobidi, kutumia vyombo vya kisheria kutatua migogoro inayojitokeza. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya migogoro 27 ya watumiaji maji ilishughulikiwa na Wizara yangu. Kati ya hiyo, migogoro 25 ilipatiwa suluhisho katika Mabonde ya Maji ya Pangani (11), Wami/Ruvu (10), Rufiji (3) na Bonde la Kati (1). Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kudhibiti na kusuluhisha migogoro ya watumiaji maji kadri itakavyojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji. Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inatamka bayana kuwa miradi yote lazima ifanyiwe tathmini ya athari za mazingira katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake. Katika mwaka 2011/2012 miradi 164 ya maji ilifanyiwa uchunguzi wa awali wa athari za kimazingira na kubaini kwamba miradi 29 itahitaji kufanyiwa tathmini ya kina ili

kuchukua tahadhari katika ujenzi na kuhakikisha uendelevu wake. Kati ya miradi hiyo, tathmini ya miradi minne (Kimbiji/Mpera, Bwawa la Kidunda, bomba kuu la Ruvu Chini na Mradi wa maji Tanga mjini) imekamilika. Miradi 135 iliyobaki, ilibainika kutohitaji tathmini ya kina, bali inahitaji kuchukua tahadhari za msingi tu. Wizara yangu itazingatia mapendekezo yanayotokana na tathmini hizo, wakati wa ujenzi na uendelezaji wake.

Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kukamilisha tathmini ya miradi 25 ya maji katika miji mikuu ya mikoa na miradi ya kitaifa kwa ajili ya kuiwasilisha NEMC ili ihakikiwe na athari za kimazingira na kijamii zitakazobainika zishughulikiwe wakati wa ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kudhibiti Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji, Wizara yangu iliendelea na jitihada za kudhibiti na kuzuia uchafuzi wa vyanzo vya maji kwa kukagua viwanda, migodi na hoteli na kutoa maelekezo. Ukaguzi ulifanyika katika viwanda 17, migodi mitano ya dhahabu ya North Mara, Bulyanhulu, Geita na Kahama iliyopo katika Bonde la Ziwa Victoria, na mgodi wa Resolute Golden Pride uliopo katika Bonde la Kati. Ukaguzi wa Hoteli mbili ulifanyika katika Bonde la Maji la Rufiji. Machimbo ya chumvi yaliyopo Bonde la Ziwa Tanganyika pia yalikaguliwa. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha baadhi ya viwanda vilivyokaguliwa katika Bonde la Mto Rufiji vilikuwa vinatiririsha majitaka yasiyofikia viwango vinavyokubalika kwenye mazingira. Viwanda hivyo viliagizwa kuboresha mifumo ya ukusanyaji na uondoaji

wa majitaka kufikia viwango vinavyokubalika ili viweze kupewa kibali cha kutiririsha majitaka yaliyosafishwa katika mazingira. Migodi imeagizwa kuweka mfumo madhubuti wa kuzuia kuvuja maji yenye kemikali katika baadhi ya mabwawa. Jumla ya vibali sita vya kutiririsha majitaka yanayokidhi viwango kwenye vyanzo vya maji vilitolewa na Bodi za Maji za Mabonde ya Wami/Ruvu (2), Ziwa Victoria (2), Ziwa Rukwa (1) na Ruvuma (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria iliendelea kufuatilia ubora wa maji kwenye eneo la mgodi wa North Mara ili kubaini kama kuna uvujaji wa majitaka kutoka mgodini yanayoingia kwenye vyanzo vya maji vinavyotumiwa na wananchi. Ukaguzi uliofanyika umeonesha kuwa uvujaji huo umedhibitiwa. Vipimo vya kemikali kwenye sampuli za maji zinazokusanywa kila mwezi vinaonesha kuwa kiasi cha kemikali na madini tembo kiko ndani ya viwango vinavyokubalika. Mgodi umepewa maelekezo ya kuendelea kudhibiti uchafuzi kwa kuzuia uvujaji wa majitaka kutoka katika miundombinu ya mgodi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na *NEMC* itaendelea kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinatunzwa na kulindwa. Vilevile, Wizara itaendelea kubaini maeneo yanayofaa kutengwa ili kuyakinga dhidi ya uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi wa Rasilimali za Majishiriki, nchi yetu ina mabonde tisa ya maji na kati ya hayo mabonde saba yana rasilimali ya majishiriki inayokadiriwa kuwa asilimia 43 ya maji yote. Kutokana na hali hiyo, tunashirikiana na nchi 18 ambazo ni Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Eritrea.

Lengo la ushirikiano huo ni kuhakikisha inakuwepo mifumo ya uwazi katika usimamizi, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali za maji kwa njia endelevu na kwa manufaa ya nchi shiriki. Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi hizo kwa kuendelea kuunda vyombo vya pamoja na kuimarisha vilivyopo ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo. Utekelezaji katika eneo hilo umeainishwa kwa kifupi katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Nile, Bonde la Mto Nile linajumuisha nchi kumi za Burundi, Eritrea, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan/Sudan Kusini, Tanzania na Uganda. Nchi hizi zinashirikiana kupitia chombo cha mpito cha usimamizi wa rasilimali hiyo kinachojulikana kama Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Initiative (NBI).* Madhumuni ya ushirikiano huo ni kupata maendeleo ya kiuchumi na kijamii na faida zinazotokana na usimamizi wa pamoja na matumizi ya uwiano na endelevu wa rasilimali za maji za Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, NBI inaratibu utiaji saini wa Mkataba wa Kudumu wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde hilo utakaoanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Hadi kufikia Juni, 2012 nchi sita kati ya kumi za umoja huo ambazo ni Burundi, Ethiopia, Tanzania, Uganda, Rwanda na Kenya zimesaini Mkataba huo. Nchi ya Eritrea ni mtazamaji *(observer)* katika jumuiya hiyo. Nchi za Misri na Sudan bado hazijasaini kwa kutaka mkataba utambue matumizi ya maji ya Mto Nile na haki zao kama zilivyo katika mikataba ya kikoloni. Mikataba hiyo inazipa nchi hizo mbili karibu mgao wote wa maji na haki zaidi kuliko nchi nyingine wanachama, jambo ambalo halikubaliki kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, mazungumzo yataendelea kuzishawishi nchi za Misri na Sudan kuukubali na kusaini mkataba huo. Pia, jitihada zitaendelea kuishawishi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo ilionesha nia tangu awali ya kusaini mkataba huo iweze kufanya hivyo. Vilevile, Tanzania na nchi nyingine zilizosaini mkataba wa ushirikiano zitaendelea na juhudi za kuridhiwa na mabunge ya nchi hizo ili mkataba uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria awamu ya pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria ilianza rasmi tarehe 20 Agosti, 2009. Madhumuni ya mradi huo ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za Bonde la Ziwa Victoria na kupunguza uharibifu wa mazingira katika ziwa hilo. Kwa upande wa Tanzania, mradi huo unalenga kuimarisha taasisi

zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki; kukarabati mifumo ya kusafisha majitaka katika miji mikubwa iliyo kando kando ya ziwa ya Mwanza, Musoma na Bukoba. Walengwa wengine ni Halmashauri za Wilaya ya Maswa, Bariadi, Magu, Meatu, na Kwimba.

Jumla ya miradi midogo 37 ya kijamii yenye thamani ya Dola za Marekani 706,300 inatekelezwa. Jedwali Na. 4 linaonesha majina ya vijiji na miradi ya kijamii iliyobainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, zinatekeleza Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria *(LVEMP II).* Katika mwaka 2012/2013, tutaendelea kufuatilia na kusimamia ukamilishaji wa kazi zinazofanywa na wataalam washauri kuhusu uboreshaji wa Sera, Sheria, Kanuni na viwango vya utupaji majitaka katika Ziwa Victoria, mito na vyanzo vingine vya maji katika bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Zambezi, tarehe 8 Februari 2010, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission (ZAMCOM).* Mkataba huo kwa sasa unafanya kazi baada ya nchi sita kuridhia. Sekretarieti ya muda *(Interim ZAMCOM Secretariat)* itakayoendeleza shughuli za *ZAMCOM* ilianza kazi rasmi tarehe 6 Mei, 2011. Sekretarieti hiyo itafanya kazi kwa miaka mitatu na jukumu lake kubwa ni kushirikiana na nchi wanachama kutekeleza hatua za uundaji wa

chombo cha kudumu, wakati nchi nyingine wanachama zikiendelea kuridhia Mkataba huo. Jukumu jingine ni kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji kwa Bonde la Mto Zambezi uliokubaliwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri wa Maji wa *SADC* uliofanyika mwezi Novemba 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, mwezi Aprili 2012 Tanzania ilizindua rasmi Kamati ya Taifa ya wadau itakayoratibu shughuli za *ZAMCOM* hapa nchini chini ya Sekretarieti ya Muda. Kamati hiyo itakuwa na kazi ya kukusanya maoni, kujadili na kuwasilisha maoni ya nchi yetu kwenye vikao vya wadau wa *ZAMCOM.* Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea na uratibu wa shughuli za Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Ruvuma, Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini kupitia Mradi wa Majishirikishi unaoratibiwa na *SADC,* limetengewa Jumla ya Dola za Kimarekani 800,000 kwa ajili ya kutekeleza jumla ya miradi sita ya kijamii. Miradi hiyo imepangwa kutekelezwa katika wilaya tano za mikoa ya Mtwara na Ruvuma ambazo ni Songea, Tunduru, Tandahimba, Nanyumbu na Mbinga. Ujenzi wa miradi hiyo unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2012 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2012. Fedha za kutekeleza miradi hiyo ni msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia *SADC.* Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na *SADC* pamoja na Serikali ya Msumbiji kutekeleza miradi ya pamoja katika Bonde hilo. Jedwali

Na. 5 linaonesha orodha ya miradi itakayotekelezwa chini ya Bonde la Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Songwe, ushirikiano wa Tanzania na Malawi katika Programu ya Kuendeleza Rasilimali za Bonde la Mto Songwe ulianza mwaka 1976 ambapo utekelezaji wake ulipangwa kufanyika kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ilihusu upembuzi yakinifu na ilitekelezwa kati ya mwaka 2001 na 2003. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni utekelezaji wa awamu ya pili ambayo ni usanifu wa kina wa miundombinu ya rasilimali za maji itakayojengwa kwa ajili ya kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko ambayo huharibu mali na mashamba ya wananchi kila mara katika eneo la hekta zipatazo 15,000. Makao makuu ya Programu yako Kyela, Mbeya ambapo Meneja wa Mradi ni Mtanzania, na ameanza kazi tangu mwezi Machi 2012. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na nchi ya Malawi kuratibu utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika tatizo la kupungua kina cha maji katika Ziwa Tanganyika liliendelea kufanyiwa kazi mwaka 2011/2012. Kupitia *Common Market for Eastern and Southern Africa (COMESA,* Serikali ya Kidemokrasia ya Kongo, ilimwajiri mshauri mwelekezi mwaka 2011 ili afanye tafiti ya athari za Kijamii na Mazingira *(Environmental and Social Impact Assessment),* tafiti ya kihaidrolojia *(Hydrology Study)* na usanifu wa michoro ya kihandisi *(Engineering Designs)* ili kujenga Banio la Mto Lukuga ambalo lilikuwa limebomoka. Mshauri mwelekezi amewasilisha

taarifa za awali za utafiti huo katika kikao cha wataalam kutoka nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika mwezi Novemba 2011, chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Mamlaka ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, mshauri mwelekezi ataendelea na kazi na anatarajiwa kuikamilisha ifikapo mwezi Novemba, 2012. Aidha, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia pamoja na Washirika wa Maendeleo ili kuendeleza juhudi za hifadhi ya Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Chala, Jipe na Mto Umba. Mkutano wa tisa na wa kumi wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Maji wa nchi za Bonde la Ziwa Victoria ilifanyika Kisumu, Kenya tarehe 26 Agosti, 2011 na Kigali, Rwanda tarehe 4 Mei, 2012. Mikutano hiyo iliagiza Sekretarieti ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kushirikiana na nchi za Kenya na Tanzania kutoa msaada wa kitaalam pamoja na ushauri wa namna ya kutunza na kuendeleza ikolojia ya maziwa ya Chala na Jipe; na Mto Umba. Nchi za Kenya na Tanzania zitakamilisha na kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) kati yao mwaka 2012/2013 ili kuzipa nguvu hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huo unalenga kuweka misingi ya ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza rasilimali zilizopo katika Mabonde ya Mto Umba, Ziwa Jipe na Ziwa Chala ili matumizi yake yawe

endelevu ikiwa ni pamoja na kulinda mifumo ya ikolojia.

Chini ya makubaliano hayo, Ofisi ya Bonde la Mto Pangani, Halmashauri husika, jumuiya za watumiaji maji, na taasisi zisizo za kiserikali zilizopo katika mabonde hayo zitaimarishwa na taasisi mpya zitaanzishwa kulingana na mahitaji. Makubaliano hayo yataweka pia mfumo wa uongozi wa pamoja wa kusimamia rasilimali hizo. Kazi zitakazotekelezwa kwa pamoja zinajumuisha ufuatiliaji wa wingi na ubora wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubora na Usafi wa Maji, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuhakiki ubora na usafi wa maji katika vyanzo vya maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Katika kutimiza jukumu hilo mwaka 2011/2012, Wizara ilipanga kukagua vyanzo vya maji kwa kuchunguza sampuli 8,000 za maji ili kuhakiki ubora wake kwa kutumia mtandao wa maabara za maji zilizopo nchini. Vilevile, sampuli 1,000 za majitaka zilipangwa kukusanywa na kuchunguzwa ubora wake ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji unaosababishwa na majitaka kutoka viwandani na mabwawa ya kusafisha majitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Mei 2012, jumla ya sampuli za maji 5,107 zilikusanywa katika maeneo ya mijini na vijijini na kuchunguzwa viwango vinavyokubalika kwa matumizi mbalimbali. Kati ya sampuli hizo sampuli 3,866 sawa na asilimia 76 zilikuwa na ubora unaokubalika.

Sampuli zilizosalia zilikuwa na matatizo mbalimbali ambapo sampuli 309 zilikuwa na tatizo la uwepo wa vijidudu, sampuli 485 zilikuwa na kiasi kikubwa cha chumvichumvi na sampuli 447 zilionesha kuwepo kwa matope na virutubisho visivyokubalika.

Ushauri ulitolewa kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kutibu maji kufikia viwango vinavyotakiwa kabla ya kuyasambaza kwa watumiaji, kutafuta vyanzo mbadala na elimu kuhusu uhifadhi wa vyanzo vya maji dhidi ya uchafuzi inaendelea kutolewa. Jedwali Na. 6 linaonesha mtiririko wa sampuli za maji zilizokusanywa na kuchunguzwa ubora wake kuanzia mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya sampuli 612 za majitaka zilikusanywa toka miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Morogoro, Dodoma, Bukoba na Iringa. Sampuli 489 sawa na asilimia 80 zilikidhi viwango vya majitaka kurudishwa katika mazingira bila kuwa na athari na pia ushauri ulitolewa kuhusu majitaka ambayo hayakukidhi viwango.

Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa maji yanayosambazwa kwa wananchi ni safi na salama na kuwa dawa zinazotumika kutibu na kusafisha maji zina viwango vinavyokubalika. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya sampuli 52 za dawa za kutibu maji kutoka kwenye Mamlaka za Maji nchini na makampuni binafsi zilihakikiwa ubora wake. Sampuli hizo ni 19 aina ya shabu (Aluminium Sulphate) na 15 aina ya *Polyaluminium Chloride* ambazo hutumika kusafisha maji; na 18 aina ya *Calcium Hypochlorite* ambayo

hutumika kuua vijidudu. Matokeo yalionesha kuwa dawa hizo zilikuwa na viwango vinavyokubalika na ushauri ulitolewa kuhusu matumizi yake. Sampuli tano za dawa aina ya *Polyaluminium Chloride* zilionesha kuwa na uwezo mdogo wa kusafisha maji, hivyo Mamlaka husika ilishauriwa kutotumia dawa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Agosti, 2011 Maabara Kuu ya Maji iliyopo Dar es Salaam, ilishiriki katika zoezi la nane chini ya mpango wa Southern African *Development Community Measurement Traceability (SADCMET)* linaloratibiwa na Shirika la Maji la Namibia. Zoezi hilo linafanyika kila mwaka ili kupima uwezo wa kiutendaji wa maabara *(Laboratory Performance Evaluation or Proficiency Testing*).

Lengo ni kuhakikisha kuwa maabara zinatoa takwimu sahihi zenye kukidhi matakwa ya taratibu za maabara za maji ili kupata Ithibati *(Accreditation)* na kutambulika kimataifa. Matokeo ya zoezi hilo yalipokelewa mwezi Oktoba 2011 na yameonesha kuwa utendaji wa maabara yetu umefikia kiwango cha asilimia 68.4 ya ubora wa kimataifa. Kiwango hicho kimeongezeka kutoka asilimia 65 mwaka 2010. Kwa matokeo hayo, Maabara Kuu ya Maji inaweza sasa kuanza taratibu za kuomba kupata Ithibati. Jedwali Na.7 linaonesha vielelezo vilivyofuzu kulingana na viwango hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, vyanzo vya maji vitatathminiwa ubora wake ambapo jumla ya sampuli 8,000 za maji na sampuli 1,000 za majitaka zitapimwa ili kulinda afya za

wananchi na mazingira kwa ujumla. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuziimarisha Maabara Kuu na Maabara ya Maji Mwanza ili ziweze kupata Ithibati na maabara nyingine zitajengewa uwezo kwa kupatiwa wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kulingana na mipango na vipaumbele vya kila Halmashauri. Programu hii inatekelezwa kwa awamu nne za miaka mitano kwa kila awamu. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ulipangwa kuanza mwaka 2005/2006 na kukamilika mwaka 2010/2011, na ulikadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani milioni 292. Baada ya miaka miwili na nusu ya utekelezaji wa programu, mapitio *(mid term review)* yalifanyika kwa kuzingatia malengo na fedha zilizobakia, ambapo muda wa kukamilisha awamu ya kwanza uliongezwa hadi Juni 2014. Lengo ni kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini kutoka asilimia 55.7 mwaka 2006 hadi asilimia 65 mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Sera ya Maji na Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Sekta ya Maji, utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini unafanywa kwa kushirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta binafsi. Hivyo, wataalam washauri wanatumika katika usanifu wa miradi ya maji vijijini na kusimamia ujenzi wa miradi hiyo na wakandarasi wa ujenzi wanatumika kujenga miradi.

Halmashauri kupitia Kamati ya Maji na Usafi wa Mazingira ina jukumu la kusimamia sekta binafsi inapotekeleza wajibu wake kulingana na mikataba mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ulihusu kujenga miradi ya maji kwenye vijiji 10 kwa kila Halmashauri, kujenga uwezo kwa watekelezaji wa programu, kuhamasisha wananchi kuhusu usafi binafsi na usafi wa mazingira, kusimamia na kufuatilia miradi ya maji. Wakati taratibu za kuwapata wataalam washauri zikiendelea, Serikali ilianza kutekeleza programu kwa ujenzi na ukarabati wa miradi midogo yenye kuleta matokeo ya haraka (quick wins) katika hatua hiyo ya kwanza ya utekelezaji wa quick wins shilingi 96.4 bilioni zilitumika. Taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji kwenye vijiji kumi (10) kwa kila Halmashauri imezingatia mikoa na Halmashauri ambazo zimesaini mikataba na wataalam washauri na wakandarasi wa kujenga miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza miradi ya maji kwenye vijiji 10 katika kila Halmashauri, hadi Juni 2012, Halmashauri 131 kati ya Halmashauri 132 tayari zina wataalam washauri. Hii ni baada ya Halmashauri hizo kukamilisha taratibu zote za ununuzi na kupata ridhaa ya Benki ya Dunia. Wataalam hao wanafanya upimaji, usanifu wa miradi, kuandaa zabuni na watasimamia ujenzi wa miundombinu ya maji itakayojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Halmashauri ya Simanjiro haikupata wataalam washauri kutokana na wataalam hao kutojitokeza kuomba kazi. Katika mwaka 2011/2012, baada ya kuwasilisha orodha fupi ya wataalam washauri, Halmashauri ilipata kibali cha Benki ya Dunia cha kufungua mapendekezo ya kifedha na kufanya majadiliano na mtaalam mshauri aliyepata alama za juu. Taarifa ya tathmini ya mapendekezo ya kiufundi na kifedha pamoja na rasimu ya mkataba iliwasilishwa Benki ya Dunia ili kupata ridhaa ya kusaini mkataba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 28 Juni 2012, Halmashauri ilisaini mkataba kati yake na mtaalam mshauri aliyeshinda, ili kuanza kazi ya upimaji na usanifu wa miradi ya maji katika vijiji 10 vilivyoainishwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, usanifu na usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya maji unafanywa na mtaalam mshauri ambaye ameajiriwa na Mamlaka ya Maji mjini Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Halmashauri ya Morogoro, kampuni iliyoshinda kandarasi hii kwa mara ya kwanza gharama zake za kufanya kazi zilikuwa juu kuliko kiwango kinachokubalika. Halmashauri hiyo ilirudia zoezi hili kwa kuandaa orodha fupi (short list) ya wataalam washauri ambao waliombwa kuwasilisha mapendekezo yao kwenye Halmashauri.

Halmashauri ilipata ridhaa ya Benki ya Dunia ya kufungua mapendekezo ya kiufundi na ya kifedha na kufanya majadiliano na mtaalam mshauri aliyepata alama za juu. Halmashauri inaendelea na taratibu hizo na mtaalam mshauri anatarajiwa kupatikana katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye baadhi ya vijiji 10 vya kila Halmashauri, hadi kufikia mwezi Juni 2012, Halmashauri 62 zimetangaza zabuni na kupata vibali vyote vinavyohitajika ili kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji. Halmashauri hizo ni Kilolo na Manispaa ya Iringa (Iringa); Njombe, Ludewa na Makete (Njombe); Biharamulo, Bukoba, Karagwe na Manispaa ya Bukoba (Kagera); Hai, Mwanga na Same (Kilimanjaro); Kilwa, Manispaa ya Lindi, Liwale, Lindi, Nachingwea na Ruangwa (Lindi); Babati, Mji wa Babati na Mbulu (Manyara); Bunda na Serengeti (Mara); Mbarali, Mbozi, Chunya, Jiji la Mbeya, Kyela na Rungwe (Mbeya); Kilombero na Ulanga (Morogoro); Masasi, Mtwara, Newala, Nanyumbu, Manispaa ya Mtwara na Tandahimba (Mtwara); Kwimba, Sengerema, Misungwi na Ukerewe (Mwanza); Kibaha, Mji wa Kibaha na Rufiji (Pwani); Mpanda na Mji wa Mpanda (Katavi); Tunduru na Mbinga (Ruvuma); Bukombe (Geita); Kahama, Kishapu na Shinyanga (Shinyanga); Maswa na Meatu (Simiyu); Iramba, Manyoni na Singida (Singida); Manispaa ya Tabora na Nzega (Tabora); Kilindi, Mkinga na Pangani (Tanga). Halmashauri 25 kati ya hizo, tayari zimeanza ujenzi. Halmashauri hizo ni Kilolo (Iringa); Kilwa, Manispaa ya Lindi na Ruangwa (Lindi); Bukoba (Kagera); Mwanga (Kilimanjaro); Babati na Mbulu

(Manyara); Serengeti (Mara); Mbozi (Mbeya); Kilombero (Morogoro); Masasi, Newala na Mtwara (Mtwara); Kibaha na Mji wa Kibaha (Pwani); Mpanda (Katavi); Bukombe (Geita); Shinyanga, Kishapu na Kahama (Shinyanga); Meatu (Simiyu); Singida na Manyoni (Singida); na Mkinga (Tanga). Halmashauri 37 zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za kuanza ujenzi. Jedwali Na. 8 linaonesha Halmashauri 62 ambazo zimetangaza zabuni na kupata vibali vyote vinavyohitajika ili kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri 53 zimepata vibali vya kutangaza zabuni za ujenzi na ziko katika hatua mbalimbali za kupata vibali ili kuanza ujenzi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9. Kati ya hizo, Halmashauri 26 zitapata kibali cha kuanza kujenga wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, jumla ya Halmashauri 115 zilizoko katika Jedwali Namba 8 na 9, zinatarajiwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya maji kwa wastani wa vijiji vitatu kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa visima vya maji na usanifu wa miradi ya maji atika Halmashauri 14 upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji chini ya usimamizi wa wataalam washauri. Halmashauri nne zimekamilisha uchimbaji wa visima vya maji na zinafanya usanifu wa miundombinu ya maji. Aidha, Halmashauri tisa zimeajiri wakandarasi wa kuchimba visima vya maji na uchimbaji unaendelea. Katika Halmashauri moja, mtaalam mshauri anaandaa taarifa

itakayoainisha kazi zitakazofanyika (*scoping study).* Jedwali Na. 10 linaonesha Halmashauri 14 ambazo ziko katika hatua mbalimbali za uchimbaji wa visima na usanifu wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji kwa ajili ya miradi mbalimbali ni pamoja na visima, mito, maziwa, chemchemi na mabwawa. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Programu inaonesha kuwa wananchi kwenye vijiji vingi vinavyotekeleza mradi wa vijiji 10 katika kila Halmashauri wamechagua visima kama vyanzo vya kuwapatia maji. Jumla ya visima 1,159 vilipangwa kuchimbwa ambapo 1,129 vimechimbwa. Kati ya hivyo, visima 788 sawa na asilimia 70, vina maji. Kiwango hiki cha upatikanaji wa maji kinakubalika kitaifa, ambapo kiwango cha chini cha mafanikio ni asilimia 50. Jedwali Na. 11 linaonesha idadi ya visima vilivyopangwa kuchimbwa, vilivyochimbwa na vilivyofanikiwa kupata maji katika Halmashauri 101.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuzipatia fedha Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ambapo katika mwaka 2011/2012, jumla ya shilingi 47,025,481,007 zilipelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili kutekeleza miradi kwenye vijiji vilivyoainishwa kwenye Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Vilevile, jumla ya shilingi 1,088,250,000 zilitumwa kwenye Sekretarieti za Mkoa kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu. Jedwali Na. 12 linaonesha fedha zilizotumwa kwenye Halmashauri kuanzia mwezi Juni 2007 hadi Juni 2012. Kwa ujumla, sehemu kubwa ya fedha za kujenga miundombinu ya maji katika

Halmashauri tayari zimetumwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, kupitia Bajeti ya Serikali, shilingi bilioni 51.9 kutoka Mfuko wa Pamoja (*Water Sector Basket Fund*) zimepangwa kugharamia ujenzi wa miundombinu ya maji, kujenga uwezo wa watekelezaji wa programu, uhamasishaji, kutoa elimu ya usafi binafsi na mazingira, usimamizi, ufuatiliaji na kulipa wataalam washauri kwa ajili ya usimamizi wa wakandarasi wa ujenzi. Majedwali Na. 13 (a) na (b) linaonesha fedha zilizokasimiwa katika Mafungu mbalimbali kwa mwaka 2012/2013. Kiwango hicho cha fedha kilichotengwa ni sehemu ya shilingi bilioni 81.8 ya mchango wa Serikali na ahadi ya Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuziimarisha Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi kwa kutoa ushauri wa kitaalam na nyenzo za kufanyia kazi. Kuanzia mwaka 2010 hadi kufikia mwezi Mei 2012 Halmashauri zimepata magari 125, pikipiki 252, *printer* 124, kompyuta 111 na *scanner* 116. Sekretarieti za Mkoa zimepata magari 21, *printer* 21, kompyuta 20 na *scanner* 21. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushirikiana na kuziimarisha Halmashauri na Sekretarieti za mikoa ili kuharakisha utekelezaji wa Programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kuzisaidia baadhi ya Halmashauri kusanifu na kuandaa zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji vijijini. Katika mwaka wa 2012/2013 Wizara yangu

itazisaidia Halmashauri husika katika kutekeleza miradi ya Lugenge-Kisilo, Lukululu, Masoko, Mwakaleli, Kakonko, Chuo Kikuu cha Mandela - Arusha, Iwungilo, Mputwa, Milola, Matema, Michire, Ingri Juu, Kidete, Nyamongo, Oljoro-Muriet-Losinyai, Gabimori, Kongoto, Lifua Manda, Kabembe, Ilamba, Ngeleka, Chiwambo, Komuge, Masonga, Masuguru, Kawa, Sadani, Ujuni, Kilulu, Manyovu, Lutete, Haruzale, Bungu na Mbumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Wilaya za Moshi Vijijini na Hai. Mradi wa maji katika Wilaya ya Moshi Vijijini ulianza kutekelezwa mwezi Aprili 2007 ukiwa na lengo la kuwahudumia wakazi 100,000 katika vijiji 30. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*) iliendelea na utekelezaji wa mradi wa maji katika Wilaya ya Moshi na kuongeza vijiji viwili vyenye wakazi wapatao 10,000. Mradi huo umekamilika kwa vijiji 30 vya awali. Katika mwaka 2012/2013 ujenzi wa mradi utaendelea katika vijiji viwili vilivyoongezeka vya Kilototoni na *Rau River* na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)* na Umoja wa Ulaya *(EU)* iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa maji katika wilaya za Hai na Siha. Awamu ya nne ya Mradi wa maji katika wilaya za Hai na Siha inayoendelea, ilianza kutekelezwa mwezi Machi 2005 na ililenga kunufaisha watu 172,000 katika vijiji 21. Katika Wilaya ya Hai, ujenzi wa Skimu ya maji ya Mkalama inayohudumia vijiji vitano ulikamilika Desemba 2011. Katika Wilaya ya Siha,

utekelezaji ulijumuisha ukarabati wa skimu za mtiririko za *West Kilimanjaro* na *North West Kilimanjaro*. Ujenzi wa Skimu ya *West Kilimanjaro* umekamilika na ujenzi wa Skimu ya *North West Kilimanjaro* umefikia asilimia 40. Katika mwaka 2012/2013, ujenzi utaendelea katika Skimu ya *North West Kilimanjaro.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Same – Korogwe .Serikali imeendelea na maandalizi ya mradi wa maji wa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mtaalam mshauri ambaye atafanya mapitio ya usanifu na kusimamia kazi za ujenzi wa mradi amepatikana. Kinachosubiriwa ni kibali kutoka *BADEA* ili mkataba baina ya Wizara na mtaalam mshauri usainiwe. Mara baada ya mtaalam mshauri kusaini mkataba na kufanya mapitio ya usanifu, taratibu za kumpata mkandarasi zitafanyika na ujenzi utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Vijijini katika Mikoa ya Mwanza na Mara. .Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza mradi wa maji vijijini katika mikoa ya Mwanza na Mara. Mradi huo ulilenga kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama katika vijiji 44 vya mikoa ya Mwanza (26) na Mara (18). Jumla ya visima 177 vilichimbwa na kufungwa pampu za mkono. Aidha, mradi umejenga majukwaa (*platforms*) kwenye visima vitano vilivyokuwa vimechimbwa wakati wa majaribio na kujengea chemchemi moja, hivyo kufanya jumla ya visima 182 kujengwa. Hadi mwezi Machi 2011, chini ya awamu ya kwanza na ya pili ya utekelezaji wa mradi huo, jumla ya visima 114 vilikuwa vimechimbwa na kufungwa pampu za mkono. Kwa Mkoa wa Mwanza,

jumla ya visima 72 vilichimbwa katika wilaya za Kwimba (9), Misungwi (10), Sengerema (23) na Wilaya ya Geita (30) na chemchem moja kujengwa katika Kijiji cha Kasota. Kwa Mkoa wa Mara jumla ya visima 42 vilichimbwa katika wilaya za Musoma (5), Rorya (21), Tarime (3) na Serengeti (13).

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya tatu ya mradi huo iliyoanza kutekelezwa mwezi Aprili 2011 imehusisha uchimbaji wa visima 63 katika Mikoa ya Mwanza (36) na Mara (27). Visima vyote 63 tayari vimechimbwa na mradi ulikamilika mwezi Januari 2012 kama ilivyopangwa. Jedwali Na. 14 linaonesha vijiji ambapo uchimbaji wa visima ulifanyika katika mikoa ya Mwanza na Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Vijijini katika Mkoa wa Tabora. Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan ilipanga kutekeleza mradi wa maji vijijini katika mkoa wa Tabora. Mradi huo ulilenga kuwapatia huduma ya maji wananchi wapatao 44,977 katika vijiji 20 vya mkoa huo. Kutokana na maafa ya *Tsunami* yaliyoikumba nchi ya Japan mwezi Machi, 2011, utekelezaji wa mradi ulisimama kwa muda. Katika mwaka 2012/2013, utafiti na usanifu wa kina katika maeneo yaliyoonesha kuwa na maji ya kutosha utafanyika kwa kushirikiana na Serikali ya Japan na utekelezaji unatarajiwa kuchukua miaka mitatu.

Vijiji vilivyolengwa kupata maji kupitia mradi huu ni Busomeke na Kalemela (Igunga); Isanga, Kitangili, Makomelo na Wela (Nzega); Kasandalala, Usunga na Mpombwe (Sikonge); Mabama, Ufuluma na Mpumbuli (Tabora/Uyui); Kakola, Misha na Uyui (Manispaa ya

Tabora) na Imalamakoye, Kalembela, Kiloleli na Nsungwa (Urambo).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Mabwawa na Uchimbaji wa Visima. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kusimamia ujenzi wa mabwawa nchini. Hadi kufikia mwezi Mei, 2012 utekelezaji kwa kila bwawa ni kama ifuatavyo: Habiya (45%), Seke Ididi (73%), Wegero (100%), Iguluba (40%), Kawa (95%), Sasajila (75%), Matwiga (36%), na Mwanjoro (93%). Jedwali Na. 15 (b) linaonesha mabwawa yaliyoendelea kujengwa katika mwaka 2011/2012. Katika mwaka 2012/2013, mabwawa ambayo ujenzi wake haujakamilika utaendelea. Ujenzi wa mabwawa madogo utafanywa na Halmashauri kulingana na vipaumbele vyake, ambapo Wizara yangu itatoa ushauri wa kiufundi utakaohitajika katika ujenzi huo. Uchimbaji wa visima utafanywa kwa kuzisaidia baadhi ya Halmashauri katika kukabiliana na matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Miradi Mingine ya Maji Vijijini. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea na juhudi nyingine mbalimbali za ujenzi wa miradi ya maji vijijini. Juhudi hizo ni zile zinazofanyika kupitia vyanzo mbalimbali vya fedha. Vyanzo hivyo ni pamoja na Halmashauri, Ruzuku ya Maendeleo, *Devon Aid (DAK),* Mfuko wa Jimbo, *TANAPA, WVT, Aqua for all Women for Partnership, CRS, Rev Lief - Lutheran Church, SADC, CDCF, TASAF, Anglican Churches and Emmanuel International, TRR (Tanzania Rural Revival), Living Water of Tanzania,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, *SHIPO,* Serikali ya *Italy na ACRA*, *Lutheran Church Minessota – USA, Serengeti Breweries Ltd,*

Kanisa Katoliki Jimbo la Iringa, *Tanzania Rural Revival*, *Concern, SEDP, ACCORD, UN-HABITAT* na *World Vision Tanzania*. Juhudi hizo zinachangia katika kuinua kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini.

Jedwali Na. 16 linaonesha taasisi zilizochangia katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini katika mikoa mbalimbali kwa mwaka 2011/2012. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali katika ujenzi wa miradi ya maji vijijini ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuanisha Vituo vya Kuchotea Maji. Wizara yangu imeendelea na zoezi la kuainisha vituo vya kuchotea maji vijijini kwa lengo la kupata takwimu sahihi zinazohusiana na huduma ya maji vijijini kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Hadi kufikia mwezi Mei, 2012 takwimu za vituo vya kuchotea maji katika Halmashauri 63 zimekusanywa na kuwekwa kwenye mfumo husika. Katika mwaka 2012/2013, kazi hiyo itakamilishwa katika Halmashauri zilizobaki ili kujua idadi ya vituo hivyo na watu wanaohudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uundaji na Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji. Uuundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji ni mkakati wa kuisaidia miradi ya maji kuwa endelevu. Hadi kufikia mwezi Mei 2012, aina ya vyombo vya watumiaji maji vilivyoundwa na kusajiliwa, na idadi yake kwa ujumla, ni kama ifuatavyo:- Jumuiya za Watumiaji Maji 651 kwa mchanganuo ufuatao kimkoa: Arusha (34), Iringa (26), Mbeya (19), Dodoma (10), Ruvuma (12), Kilimanjaro (17), Kagera (71), Shinyanga (37), Lindi (16), Morogoro (20), Tabora (21), Manyara (12), Mara (85), Singida (51),

Kigoma (11), Dar es Salaam (68), Pwani (11), Tanga (27), Mtwara (34), Mwanza (18) na Rukwa (51). Kampuni 20; Morogoro (18) na Kilimanjaro (2); Bodi za Udhamini 6 za Arusha, Ushirika 2 za Arusha (1) na Mtwara (1); Shirika Dola *(Corporation Sole)* (1) ya Mtwara (Lulindi) na vikundi vya watumiaji maji 6,832: Arusha (4), Dar es Salaam (211), Dodoma (56), Kagera (855), Mwanza (967), Pwani (3), Rukwa (53), Shinyanga (4,653) na Tabora (30).

Mheshimiwa Naibu Spika.katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu ilitoa mwongozo wa uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji, kwa mujibu wa kanuni inayohusu Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji *[The Water Supply and Sanitation (Registration of Community Owned Water Supply Organisations) Regulations, 2009, GN. No. 21 of 22/01/2010].* Hadi sasa Halmashauri 110 zimeteua wasajili wa vyombo vya watumiaji maji. Napenda kuchukua fursa hii kushauri Halmashauri zilizobaki kuteua wasajili ili kuharakisha zoezi la uundaji na usajili wa vyombo huru vya kuendesha na kusimamia miradi ya maji. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu kwa kuwa itasimamiwa na kuendeshwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini. .katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini kwa kukarabati, kujenga na kupanua mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za maji za Dar es Salaam, miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya,

miji midogo, na miradi ya kitaifa ya maji ili kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dar es Salaam. Hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo inayohudumiwa na DAWASA kwa sasa unakadiriwa kufikia asilimia 67 kwa wastani wa muda wa upatikanaji wa huduma ya maji wa saa 8 kwa siku. Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na changamoto kubwa ya maji yanayopotea, ongezeko kubwa la watu la asilimia 6 kwa mwaka na kukua kwa shughuli za kiuchumi sambamba na ongezeko kubwa la viwanda na kupanuka kwa ujenzi wa makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo uliopo wa mitambo ya kuzalisha maji kwa jiji la Dar es Salaam ni mita za ujazo 300,000 kwa siku. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, uzalishaji wa maji ulikuwa ni wastani wa mita za ujazo 240,316 kwa siku. Upungufu huu unatokana na tatizo la kukatika mara kwa mara kwa umeme kwenye mitambo ya kuzalishia maji pamoja na matengenezo. Mahitaji ya maji kwa jiji la Dar es Salaam hivi sasa ni mita za ujazo 455,000 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, DAWASCO imeongeza makusanyo ya maduhuli kutoka wastani wa shilingi bilioni 2.15 kwa mwezi mwaka 2010/2011 hadi shilingi bilioni 2.63 (sawa na asilimia 22) kwa mwezi, mwaka 2011/2012. Kufikia mwezi Machi 2012, DAWASCO ilikuwa na wateja 129,672 ikilinganishwa na wateja 113,962 mwezi Juni 2011; kati ya hao, wateja 105,441

sawa na asilimia 81 wamefungiwa dira za maji. Kazi hiyo inaendelea na lengo ni kuwafungia wateja wote wa maji jijini ifikapo Desemba 2012. Upotevu wa maji umepungua kutoka asilimia 49.9 mwezi Juni 2011 hadi kufikia asilimia 41.8 mwezi Machi 2012. Lengo ni kufikia asilimia 30 ifikapo mwezi Juni 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika,Huduma ya Majisafi katika Miji Mikuu 19 ya Mikoa. Hali ya utoaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa miji mikuu ya mikoa 19 imeongezeka kwa Mamlaka za daraja A kutoka asilimia 88 mwaka 2011 na kufikia asilimia 89 kwa mwaka 2012 na kwa Mamlaka za daraja B na C wastani wa maeneo yanayopata maji ni asilimia 83. Mamlaka hizo zinakabiliwa na changamoto ya kusambaza maji kwenye maeneo mapya inayosababishwa na upanuzi wa maeneo ya miji yetu mikuu ya mikoa. Jedwali Na. 17 linaonesha hali ya utoaji wa huduma ya maji mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa majisafi kwa Mamlaka zote 19 za miji mikuu ya mikoa uliongezeka kutoka wastani wa mita za ujazo 320,904 kwa siku kwa mwezi Juni 2011 hadi kufikia wastani wa mita za ujazo 330,994 kwa siku mwezi Machi 2012. Ongezeko hili limetokana na ukarabati wa miundombinu ya maji iliyokamilika na inayoendelea katika miji mikuu ya mikoa mbalimbali nchini, hususan miji ya Mbeya na Iringa. Hata hivyo, kiwango hiki cha uzalishaji ni asilimia 65 tu ya kiwango kinachohitajika ili kukidhi mahitaji ya maji ya miji yetu mikuu ya mikoa. Makusanyo ya maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji katika Mamlaka za miji mikuu ya mikoa 19 kwa

mwezi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 3.02 mwaka 2010/2011 hadi kufikia shilingi bilioni 4.45 mwezi Machi, 2012, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 47.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia mwezi Machi 2012, ufungaji wa dira za maji kwenye miji mikuu ya mikoa 19 umeongezeka kutoka dira 246,373 mwezi Juni 2011 hadi kufikia dira 264,090 mwezi Machi 2012. Ongezeko hilo limefanya idadi ya wateja waliofungiwa dira katika miji hiyo kufika asilimia 93. Aidha, upotevu wa maji umepungua na kufikia asilimia 36.13. Lengo ni kupunguza upotevu huo hadi kufikia asilimia 20 (kiwango kinachokubalika kimataifa) ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, hatua mbalimbali zilichukuliwa katika kuboresha huduma ya maji mijini na baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na Mamlaka zote za maji ngazi ya miji mikuu ya mikoa zinaweza kugharamia gharama zote za uendeshaji na sehemu ya uwekezaji isipokuwa Mamlaka ya Lindi. Aidha, Mamlaka sasa zinatoa huduma kwa kiwango cha ufanisi wa kimataifa. Katika mwaka 2011/2012 Mamlaka ya Maji mjini Moshi imefanikiwa kuwa Mamlaka ya tatu baada ya Tanga na Arusha kupata cheti cha ubora wa huduma ya maji cha kimataifa cha *ISO Na 9001 2000;* na Mamlaka zilizobaki za daraja ‘A’ zinaendelea na taratibu za kupata cheti hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka, Mamlaka zote hufanyiwa ukaguzi wa hesabu za mwaka (*Audited Accounts*) kulingana na viwango vya kimataifa vya ukaguzi. Kwa mwaka wa fedha ulioishia 2010/2011,

Mamlaka zote zilipata hati safi isipokuwa Mamlaka za Mtwara, Musoma, Songea, DAWASA na DAWASCO. Mamlaka hizo zimeelekezwa kufanyia kazi maeneo yenye dosari katika hesabu zao. Huduma ya Majisafi katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Mahitaji ya maji katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo katika mwaka 2010/2011 ilikuwa mita za ujazo 243,165 kwa siku ambapo uzalishaji ulikuwa ni mita za ujazo 99,346 sawa na asilimia 40. Asilimia 47 ya wakazi wa miji hiyo wanapata huduma ya maji na asilimia 45 ya wateja 88,600 wamefungiwa dira za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miradi ya kitaifa mahitaji ya maji yalikuwa mita za ujazo 76,724 kwa siku ikilinganishwa na uzalishaji wa mita za ujazo 36,312 kwa siku, sawa na asilimia 47. Idadi ya wateja ni 10,733 na kati yao, 6,762 sawa na asilimia 63 wamefungiwa dira za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya maji na kuzijengea uwezo Mamlaka za maji za ngazi ya wilaya. miji midogo na miradi ya kitaifa ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi katika maeneo ya Mamlaka hizo. Kwa lengo la kuongeza ufanisi na miji kujiendesha kibiashara, Wizara yangu itaendelea na zoezi la kuunganisha miji midogo na mji mkubwa au miji midogo kwa midogo (*clustering*). Aidha, mawasiliano yanaendelea na TAMISEMI ili kuzitangaza kwenye Gazeti la Serikali, Mamlaka za Makambako, Ngara, Kahama, Kyela, Tukuyu, Kondoa, Itumba, Nzega, Liwale, Pangani, Kasulu, Kilwa-Masoko, Igunga, Njombe na Mpanda

kupanda daraja kutoka C kwenda B ambapo Mamlaka hizo zinaweza kulipia mishahara ya watumishi wake na sehemu ya gharama za uendeshaji. Jedwali Na. 18 linaonesha Mamlaka za maji za miji ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Uondoaji wa Majitaka Mijini. Kwa upande wa huduma ya uondoaji wa majitaka, malengo ya MKUKUTA II ni kuboresha huduma hadi kufikia asilimia 22 ifikapo 2015. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya majitaka katika miji ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa, na kupunguza au kuondoa kero iliyokuwepo hapo awali ya majitaka kutiririka ovyo katikati ya miji hiyo. Huduma ya uondoaji wa majitaka mijini imeendelea kuwa asilimia 18 ya wakazi wake. Hali hii imetokana na mwamko mdogo wa wananchi kuomba kuunganishwa kwenye mtandao, uchakavu wa miundombinu iliyopo, ongezeko kubwa la watu mijini pamoja na miji mingine kutokuwa na mitandao ya majitaka. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, jumla ya wateja wa majitaka mijini wamefikia 20,773 kutoka wateja 18,240 mwezi Machi 2011, hii ni sawa na ongezeko la wateja 2,533 (sawa na asilimia 14). Kuimarisha Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuboresha Mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa kwa kuzijengea uwezo ili ziongeze ufanisi katika utoaji wa huduma kwenye maeneo yao. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Babati ambao

umefikia asilimia 32 hadi mwezi Mei 2012. Wizara yangu itaendelea kuziimarisha mamlaka za ngazi ya mikoa, wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa kwa kuzitengenezea mazingira mazuri ya kazi, katika kipindi cha mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweka misingi ya kufuatilia utendaji kazi wa Mamlaka za Maji mijini, Wizara imesaini Mkataba wa Makubaliano wa miaka mitatu (*MoU 2011 – 2014*) na Mamlaka za Maji za miji mikuu ya mikoa. Mkataba huo umeainisha viwango na viashiria vya utendaji kazi vinavyozitaka Mamlaka hizo kuvifikia. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuzisimamia Mamlaka za Maji kwa kuzifanyia tathmini ya utendaji kila mwaka kwa kulinganisha na viashiria vya utendaji kazi vilivyokubalika katika *MoU* ili kupima uwezo wa Mamlaka hizo katika kutoa huduma bora na kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Mei 2012, Wizara yangu ilikuwa imechangia jumla ya shilingi bilioni 1.90 katika gharama za uendeshaji wa Miradi ya Kitaifa kwa kulipia sehemu ya ankara za umeme wa mitambo ya kuzalisha maji. Katika mwaka 2012/2013 Wizara yangu itaendelea kuijengea uwezo miradi ya kitaifa ili hatimaye iweze kujiendesha yenyewe na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kuchangia gharama za uendeshaji kwenye mamlaka zikiwemo gharama za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kukarabati, Kujenga na Kupanua Miundombinu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kutekeleza mpango unaolenga

kukidhi mahitaji ya maji ya muda mfupi kwa kujenga, kukarabati na kupanua vyanzo vya maji; kuchimba visima, kupanua mitandao ya usambazaji maji; na kujenga matanki ya maji katika miji ya Mtwara, Babati, Lindi na Sumbawanga.

Ujenzi wa miundombinu ya maji hadi Mei 2012, kwa mji wa Mtwara umefikia asilimia 80, Babati asilimia 76, Lindi asilimia 95 na Sumbawanga asilimia 54. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itakamilisha ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutekeleza mpango unaolenga kukidhi mahitaji ya maji ya muda wa kati na muda mrefu kwa miji saba ya Lindi, Mtwara, Musoma, Sumbawanga, Kigoma, Babati na Bukoba. Ili kukidhi malengo ya kipindi cha muda wa kati, kazi ya usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni za ujenzi wa miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji hiyo imekamilika. Aidha, kwa kipindi cha muda mrefu hadi mwaka 2030; kazi za upembuzi yakinifu kwa miji hiyo nao umekamilika.

Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani, Umoja wa Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD);* itaanza ujenzi wa miradi ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati katika miji mitano ya Bukoba, Musoma, Lindi, Kigoma na Sumbawanga. Miradi ya miji ya Bukoba na Musoma itaanza kujengwa kwa ufadhili wa AFD ya Ufaransa mwezi Septemba 2012. Kwa upande wa miji ya Lindi, Kigoma na Sumbawanga, taratibu za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi zinaendelea na ujenzi

unatarajiwa kuanza mwezi Januari 2013 kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya na Serikali ya Ujerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya *Lake Victoria Water and Sanitation (LVWATSAN II);* ikiwa ni mradi wa pamoja wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Utekelezaji wa Programu hiyo kwa upande wa nchi yetu ni pamoja na kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira katika miji ya Geita, Sengerema na Nansio ambapo msimamizi wa Programu hiyo ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira mjini Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, wahandisi washauri wamewasilisha mapendekezo ya makadirio ya gharama za kusimamia kazi za uwekezaji wa muda mfupi na usanifu wa mradi wa huduma ya maji katika miji ya Geita, Sengerema na Nansio ili kukidhi mahitaji ya maji kwa kipindi cha muda mrefu. Katika mwaka 2012/2013, mhandisi mshauri na mkandarasi wataajiriwa ili kujenga miundombinu ya maji itakayotoa matokeo ya muda mfupi. Aidha, mhandisi mshauri atafanya mapitio ya usanifu wa mradi wa maji ili kukidhi mahitaji ya muda mrefu katika miji hiyo. Katika mwaka 2011/2012, Halmashauri ya mji wa Geita kwa kushirikiana na mgodi wa madini wa Geita (*Geita Gold Mine – GGM*) ilianza kutekeleza kazi ya ujenzi wa chanzo, chujio la maji, bomba kuu na matanki mawili. Mradi unatarajiwa kuzalisha mita za ujazo 4,800 za maji kwa siku. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo (*SECO)*, inaendelea kutekeleza mradi wa kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi na majitaka ya miji ya Tabora na Dodoma. Kwa upande wa mji wa Tabora, katika mwaka 2011/2012 ukarabati wa bwawa la Igombe na upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi ulianza na hadi sasa umefikia asilimia 15. Wizara itaendelea kutekeleza mradi huo katika kipindi cha mwaka 2012/2013. Kukamilika kwa kazi hizo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 15,000 hadi kufikia mita za ujazo 30,000 kwa siku, wakati mahitaji kwa sasa ni mita za ujazo 23,500 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mji wa Dodoma, kazi zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi katika eneo la Kisasa kwa jumla ya kilomita 30. Mradi huu umegharimu jumla ya shilingi bilioni 3.4 na unatarajia kunufaisha kaya zaidi ya 3,000. Wizara itaendelea kukamilisha kazi zilizobaki katika kipindi cha mwaka 2012/2013.

Inaendelea kuboresha huduma ya majisafi na majitaka ili kukidhi mahitaji ya muda mfupi katika Chuo Kikuu cha Dodoma; Mradi huu unalenga kujenga mfumo wa uondoaji majitaka unaojumuisha mtandao wa kukusanyia majitaka wa umbali wa kilomita 32 na mabwawa ya kutibia majitaka pamoja na kituo cha kusukumia maji na matanki makubwa ya kuhifadhia maji (jumla mita za ujazo 12,000) katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika mwaka 2011/2012, visima virefu viwili

zaidi vilichimbwa na kufikia visima tisa na mabwawa manne ya majitaka yalijengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kujenga mfumo wa majisafi na majitaka chuoni hapo; ambapo mkandarasi ataanza kazi mwezi Oktoba, 2012. Ujenzi huo utajumuisha ulazaji wa bomba kuu kilomita 15.5, ulazaji wa mabomba ya kusambaza majisafi kilomita 7.5, ujenzi wa matanki matatu, ulazaji wa bomba kuu la majitaka kilomita 12 na ujenzi wa mabwawa mengine matano ya majitaka. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini inatekeleza mradi wa maji katika mji wa Dodoma ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati. Katika mwaka 2011/2012, mtaalam mshauri alifanya mapitio ya usanifu wa kina na aliandaa vitabu vya zabuni. Awamu ya kwanza ya mradi huu ambayo inahusisha usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni ilianza mwezi Juni, 2011 na kukamilika mwezi Machi, 2012.

Kwa sasa, DUWASA imepata kibali cha kutangaza zabuni ili kumpata Mkandarasi atakayeanza ujenzi wa mradi katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi itakayotekelezwa katika mradi huo ni kuongeza uwezo wa uzalishaji na usafirishaji maji kutoka wastani wa mita za ujazo 30,000 kwa siku hadi mita za ujazo 61,500 kwa siku, kwa kuchimba visima vya ziada na kulaza bomba kubwa lenye kipenyo cha mm 600 umbali wa kilomita 30

kutoka Mzakwe hadi mjini Dodoma. Hii itasaidia kuwa na uhakika wa maji mjini na katika Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho mahitaji yake yatafikia mita za ujazo 9,000 kwa siku.

Kazi nyingine ni ujenzi wa matanki yenye jumla ya mita za ujazo 12,500 katika maeneo mbalimbali ya mji, ujenzi wa vituo vya kusukumia maji na ukarabati wa vituo vya zamani, na ujenzi wa mtandao wa kusambaza majisafi katika maeneo mbalimbali ya mji. Ujenzi wa mradi huo utaanza kutekelezwa mwaka 2012/2013 na unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu *(BADEA)* pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID)* iliendelea na ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi mjini Singida. Hadi mwezi Mei 2012, ujenzi umefikia asilimia 62 ambapo visima virefu vitano vilichimbwa na visima virefu viwili kati ya vitano vimepata maji yatakayosukumwa hadi tanki la Mandewa (*Airport*) eneo la Mwankoko. Aidha, Mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 67 yamelazwa. Katika mwaka 2012/2013, ujenzi wa mradi na uchimbaji wa visima vitano vya eneo la Irao kwa ajili ya kupeleka maji tanki la Karakana utaendelea. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2012 na utaongeza uzalishaji wa maji kufikia mita za ujazo 17,760 kwa siku. Mahitaji ya maji ya mji wa Singida kwa sasa ni mita za ujazo 7,400 kwa siku

wakati uzalishaji ni mita za ujazo 4,301 tu kwa siku; sawa na asilimia 58 ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la *Millennium Challenge Corporation (MCC)*, iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kupanua na kuboresha upatikanaji wa maji safi katika Manispaa ya Morogoro kwa kukarabati matanki matatu na ulazaji wa bomba kuu la maji la urefu wa kilomita 1.8. Utekelezaji umefikia asilimia 35. Wizara katika mwaka 2012/2013 itaendelea kutekeleza mradi huo ikiwa ni pamoja na kupanua chujio la maji la Mafiga na kukarabati chujio la Mambogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na *KfW* na *EU* iliendelea kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya majisafi na majitaka katika miji ya Mwanza, Iringa na Mbeya.

Katika mji wa Mbeya, mradi ulikamilika tarehe 21/12/2011 na kwa sasa upo katika kipindi cha uangalizi (*defect liability period*). Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa kitekeo cha maji eneo la Imeta, Iyela Ivumwe na Halewa; ujenzi wa matanki eneo la Forest, Iwambi, Iganzo, *VETA,* Iganjo, Nsoho na Idunda yenye ujazo wa mita 6,900 ya kuhifadhia maji; ujenzi wa majengo kwa ajili ya mitambo ya kutibu maji maeneo ya Sisimba, Sawaya na Imeta; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 56.8 na mabomba ya usambazaji maji kilometa 280.15, ujenzi wa mfumo wa majitaka wa

urefu wa kilomita 38 na ujenzi wa mabwawa ya majitaka katika eneo la Kalobe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mji wa Iringa, katika mwaka 2011/2012, kazi ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ilikamilika. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa kitekeo (*intake*), matanki nane na mtambo wa kusafisha maji, ujenzi wa mfumo wa majitaka, ukarabati wa mabwawa ya majitaka, ukarabati wa mtambo wa zamani wa kusafisha maji, kulaza bomba za usambazaji majisafi na kumalizia mfumo wa majitaka, ulazaji wa bomba kuu la maji. Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22/03/2012 wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Maji kitaifa. Katika mwaka 2012/2013, kazi ya uunganishaji wateja katika mtandao wa majisafi na majitaka itaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ilikamilisha usanifu na utayarishaji wa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya maji kukidhi mahitaji ya maji mpaka mwaka 2025 kwa miji midogo ya Mbinga, Tunduru na Namtumbo chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea; miji ya Magu, Misungwi, Ngudu, Nansio, Geita na Sengerema chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza; miji midogo ya Rujewa, Vwawa, Chunya, Kyela, Kasumulu, Tunduma, Mbalizi, Itumba na Tukuyu chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya; na miji midogo ya Njombe, Kilolo, Ilula, Mafinga, Ludewa, Makete, Makambako na mradi

wa kitaifa wa Wanging'ombe chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekamilisha kazi ya usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni wa miradi ya majisafi na uondoaji wa majitaka katika miji ya Moshi, Tabora, Arusha, Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Tanga na Kigoma ili kuboresha huduma ya majisafi na majitaka katika miji hiyo. Katika mwaka 2012/2013, Serikali kupitia mamlaka hizo za maji itawahamasisha wananchi katika maeneo yao ili waelewe umuhimu wa usafi wa mazingira na kuunganisha wateja zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama – Shinyanga. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Wizara yangu imeendelea kusimamia mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji ya Shinyanga na Kahama na Vijiji 44 imezidi kuimarika ambapo kwa upande wa mji wa Shinyanga hali ya huduma imeongezeka na kwa sasa wakazi wanaopata huduma hiyo wamefikia wateja 13,827 ikilinganishwa na wateja 13,117 mwezi Machi 2011. Kwa upande wa mji wa Kahama, idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji ni asilimia 70 na idadi ya wateja imeongezeka kutoka wateja 8,308 mwezi Machi 2011 hadi kufikia wateja 8,856 mwezi Machi 2012. Katika mwaka 2012/2013, Mamlaka za majisafi katika miji hiyo zitaendelea na kazi ya kuunganisha wateja wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu iliendelea kuimarisha uendeshaji wa

mradi mkubwa wa maji wa Kahama-Shinyanga unaosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi KASHWASA kwa kuchangia shilingi milioni 332 kulipia sehemu ya ankara za umeme wa kuendesha mitambo. Katika mwaka 2012/2013 Wizara yangu itaendelea kuijengea uwezo mamlaka hiyo ili hatimaye iweze kujiendesha yenyewe na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kuchangia gharama za uendeshaji zikiwepo gharama za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji KASHWASA imeainisha jumla ya vijiji vipya 96 katika Wilaya za Misungwi, Kwimba, Shinyanga na Kahama vilivyopo umbali usiozidi kilomita 12 kutoka kwenye bomba kubwa la kusafirishia maji. Kati ya vijiji hivyo, 81 ni vipya na 15 ni vya awali. Vijiji hivyo vimepangwa kuunganishwa kwenye mtandao wa maji ya Ziwa Victoria kwa kutumia fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Ili kuharakisha utekelezaji, kazi ya kusanifu miundombinu ya kusambazia maji katika vijiji inafanywa na Wataalam wa Halmashauri za Wilaya husika na kuratibiwa na KASHWASA. Ujenzi utafanywa na wakandarasi watakaoajiriwa na KASHWASA. Kazi hiyo itafanywa hatua kwa hatua kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia mamlaka ya KASHWASA ilianza utekelezaji wa mpango wa kuunganisha vijiji hivyo 96 kwenye mradi wa maji wa Ziwa Victoria. Upimaji katika vijiji vya Mbalike, Igenge na Kisesa umekamilika. Vijiji vitatu vilivyopo Wilaya ya Kwimba, Tarafa ya Mwamashimba vitaunganishwa

katika mwaka 2012/2013 kupitia tanki la Mhalo. Kazi ya upimaji na usanifu imekamilika kwenye kijiji cha Nyang'homango kikiwemo kitongoji cha Ihelele ulipo mtambo wa uzalishaji maji. Wizara itaendelea kutekeleza ujenzi wa mradi huo mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kuwapata wahandisi washauri wa kufanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya ujenzi wa mradi wa kufikisha maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Nzega, Igunga na Tabora pamoja na mradi wa kupeleka maji katika miji midogo ya Kagongwa, Isaka hadi Tinde zinaendelea. Tangazo la kusudio la kushiriki (*expression of interest*) limetoka gazetini na uchambuzi wa maombi ulifanyika mwezi Juni 2012. Wahandisi washauri wanatarajiwa kupatikana mwezi Oktoba 2012 na kazi itaanza mwezi Novemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Bariadi na Mwanhuzi utafanyika. Aidha, upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kutoa maji kutoka Ziwa Victoria na kuyafikisha katika miji ya Magu hadi Ngudu na vijiji vilivyo jirani na bomba kuu utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Chalinze. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa maji wa Chalinze, unaojumuisha usambazaji wa majisafi katika vijiji 48 vilivyogawanywa katika makundi tisa ya utekelezaji. Mradi huo utakaonufaisha wilaya tatu za

Bagamoyo, Kibaha na Morogoro unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Maji. Hadi kufikia mwezi Juni 2012, utekelezaji katika vijiji vya Mdaula, Msolwa, Ubenazomozi, Kaloleni, Mwidu, Visakazi, Matuli na Tukamisasa umefikia asilimia 70; vijiji vya Kinonko, Sinyaulime, Kidugalo, Kizuka, Sangasanga na Ngerengere umefikia asilimia 75; na vijiji vya Mihuga, Masimbani, Kweikonje, Mandamazingara na Mkonge umefikia asilimia 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji katika vijiji vya Masuguru, Kiwangwa, Fukayosi, Kidomole, Msinune, Pongwe Msungura, Madesa na Makurunge umefikia asilimia 32; vijiji vya Kinzagu, Mindukeni, Makombe, Talawanda, Malivundo, Msigi na Kisanga umefikia asilimia 52; vijiji vya Chamakweza, Vigwaza, Buyuni na Visezi umefikia asilimia 48; vijiji vya Chahua, Gwata, Gumba, Magindu na Lukenge umefikia asilimia 35; na vijiji vya Kwang'andu, Kwaruhombo, Kifuleta na Pongwe Kione umefikia asilimia 60. Jedwali Na. 19 linaonesha viwango vya utekelezaji wa miradi hiyo. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mradi wa Chalinze Awamu ya Pili na mradi utakamilika mwaka 2013 na utahudumia wakazi 109,648.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji katika Mijo ya Ikwiriri, Kibaigwa, kilosa, Turiani, Mvomero, Kibiti na Gairo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu imeendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji saba ya Ikwiriri, Kibiti, Kibaigwa, Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo ili kukidhi mahitaji ya wakazi wa miji hiyo.

Ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kibiti umekamilika na kwa mji wa Ikwiriri umefikia asilimia 80. Hadi kufikia mwezi Mei 2012, ujenzi wa miradi ya maji katika miji ya Kibaigwa, Gairo, Turiani, Kilosa na Mvomero, unaendelea vizuri na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kukamilisha miradi katika miji hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji Masasi/Nachingwea, Bunda na Orkesumet. Katika mwaka 2011/2012, miradi ya kuboresha huduma za maji katika miji ya Masasi, Nachingwea, Bunda na Orkesumet imeendelea kutekelezwa. Utekelezaji upo katika hatua zifuatazo:-

Katika mradi wa maji wa Masasi-Nachingwea, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 110 mjini Masasi na kilomita 79 mjini Nachingwea umekamilika. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 70. Katika mwaka 2012/2013, ujenzi wa mradi huo utaendelea ambapo ulazaji wa bomba lenye urefu wa kilomita 50 kutoka Mbwinji hadi Masasi utafanyika; mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa maji wa Bunda, utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi inayohusisha ujenzi wa matanki mawili, nyumba ya mashine na nyumba ya mlinzi umekamilika. Awamu ya pili ambayo inahusisha ulazaji wa bomba lenye urefu wa kilomita 23.5 kutoka kwenye chanzo hadi kwenye matanki umeanza na unatarajiwa kukamilika mwaka 2012/2013. Hadi kufikia mwezi Mei 2012, Mkandarasi amekamilisha kuchimba mtaro umbali wa kilomita 1.8,

kununua mabomba na kuagiza pampu pamoja na kuanza maandalizi ya kujenga magati 10 katika mradi wa maji mjini Orkesumet. Serikali ilisaini mkataba na *BADEA* tarehe 23/09/2011 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Dharura kwa jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2011/2012, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Dharura wa Kuboresha Huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo. Utekelezaji wa Mpango huo unalenga kukabiliana na changamoto zinazolikabili Jiji la Dar es Salaam zikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya majisafi na majitaka; kupungua kwa maji ya Mto Ruvu hasa wakati wa kiangazi; ongezeko kubwa la idadi ya watu la asilimia 6 kwa mwaka ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.5 mijini kitaifa; ongezeko la makazi mapya katika maeneo yasiyopimwa; na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii kwa ujumla. Mpango huo unalenga kuongeza uwezo wa uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 300,000 kwa siku kwa sasa hadi mita za ujazo 710,000 kwa siku ifikapo mwaka 2014. Mradi wa kuongeza uwezo wa uondoshaji wa majitaka kutoka asilimia 10 za sasa hadi asilimia 25 utatekelezwa katika awamu ya pili ya *WSDP* itakayoanza mwaka 2014/2015.

Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango huo kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia (*MCC*), Serikali ya Norway, Serikali ya India na washirika wengine wa maendeleo kupitia Mfuko wa Pamoja wa Maji. Utekelezaji wa Mpango huo ulianza rasmi mwezi Februari 2011 na umepangwa kukamilika

mwezi Desemba 2014, na utagharimu jumla ya shilingi bilioni 653.9. Hadi sasa, kazi zinazoendelea kutekelezwa ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Usanifu wa bwawa ulianza mwaka 2010 na utakamilika mwezi Agosti 2012. Usanifu huo pia umejumuisha mtambo wa kuzalisha umeme wa MW 20 na njia kuu ya umeme hadi gridi ya Taifa; na upimaji wa maeneo mapya watakayohamishiwa wakazi watakaoathiriwa na ujenzi wa bwawa. Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetengwa kwa ajili ya ulipaji wa fidia katika mwaka 2012/2013. Aidha, usanifu wa barabara ya kuingilia eneo la bwawa unaendelea na utakamilika mwezi Agosti, 2012. Ujenzi utaanza baada ya kulipa fidia za mali za wananchi watakaoathiriwa na ujenzi wa bwawa hilo. Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera. Zoezi la kuchimba visima 20 katika maeneo ya Kimbiji na Mpera halikuanza kama lilivyopangwa mwaka jana kutokana na kuchelewa kwa taratibu za ununuzi. Kwa sasa zabuni za kuwapata wakandarasi wa kuchimba visima vinane vya majaribio na visima 20 vya uzalishaji maji katika maeneo hayo zimetangazwa. Mikataba ya uchimbaji itasainiwa Septemba, 2012 na kazi kuanza. Serikali inafanya tathmini ya mali katika eneo lote la Kimbiji na Mpera ili kulihifadhi kama chanzo cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaanza uchimbaji wa visima virefu 20 vya uzalishaji na kukamilisha tathmini ya mwenendo wa maji ardhini. Makisio ya awali ni kuweza kupata maji yenye ujazo wa mita 260,000 kwa siku kutoka katika visima hivyo ifikapo mwaka 2014. Fedha zilizotengwa

kwa ajili ya kazi zilizopangwa katika mwaka 2012/2013 ni shilingi bilioni 29.99.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu. Mhandisi mshauri ameanza kazi ya usanifu wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara mwezi Machi 2012. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu utaongeza uwezo wa mtambo kutoka mita za ujazo 82,000 kwa siku mpaka mita za ujazo 196,000 kwa siku ili kukabiliana na ukuaji wa kasi wa miji ya Mlandizi, Kibaha na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upanuzi wa Mradi wa Maji wa Ruvu Chini. Katika mwaka 2011/2012, Serikali kwa kushirikiana na *MCC*, iliendelea na upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini. Mkataba kati ya Serikali na Mkandarasi ulisainiwa tarehe 28/1/2011 na utekelezaji hadi mwezi Aprili 2012 umefikia asilimia 36. Taratibu za ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji yatakayoongezeka kutokana na upanuzi wa mtambo Ruvu Chini hadi jijini Dar es Salaam zimeanza ambapo uhakiki mali kwa wananchi watakoathirika na mradi huo umekamilika na fidia imeshalipwa. Aidha, taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi zitakamilika mwezi Julai 2012. Mhandisi mshauri wa kusimamia ujenzi amepatikana. Serikali imetenga shilingi bilioni 116.4 katika mwaka 2012/2013 kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo ambao utaanza mwezi Agosti 2012 na kukamilika baada ya miezi 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mingine ya Kuboresha Huduma ya Maji Jijini Dar es Salaam. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na

Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*) na Umoja wa Nchi za Ulaya ilitekeleza mradi wa kuboresha upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam kwa kuchimba visima 18 vya uzalishaji katika maeneo ya Mbagala Kuu, Makangarawe, Tandika, Mtoni Mashine ya Maji (Temeke); Tandale na Barafu (Kinondoni); na Tabata Kisiwani, Kiwalani na Kinyerezi (Ilala). Visima hivyo vinakadiriwa kuzalisha maji yenye mita za ujazo 3,500 kwa saa ambayo yatanufaisha jumla ya wakazi 170,000. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri husika itamuajiri mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mifumo ya usambazaji maji kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Mei, 2010, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitembelea maeneo yenye kero ya huduma ya maji jijini Dar es Salaam na kuiagiza Serikali kuchimba visima virefu 27 ili kupunguza adha ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo hayo. Uchimbaji huo unaenda sambamba na utekelezaji wa Mpango wa dharura wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2012, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (*DAWASA*) imechimba visima virefu 11 ambapo vitano vipo katika maeneo ya Mburahati National Housing, Shule ya Msingi Muungano, Kwa Shebe, Mavurunza na Kilungule katika Manispaa ya Kinondoni. Visima sita vipo katika maeneo ya Keko Magurumbasi,

Chang'ombe, Chang'ombe Toroli, Sandali, Sandali Mpogo na Sandali Mwembeladu katika Manispaa ya Temeke. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais na kukamilisha uchimbaji wa visima hivyo pamoja na kazi ya kuandaa upatikanaji wa maji hayo kwa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Sekta ya Maji. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) inatekeleza majukumu ya kudhibiti utoaji wa huduma kwenye sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, majisafi na majitaka nchini ikiwa chini ya Wizara yangu. Majukumu hayo ni pamoja na kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma, kusikiliza malalamiko na kutatua migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, *EWURA* imetekeleza kazi muhimu zifuatazo: kuanzisha utaratibu wa kurahisisha ukokotoaji na upitishaji bei za maji kwa Mamlaka za Maji za miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa ambazo hazina takwimu za kutosheleza. Kazi zingine zilizokamilika ni kuanzisha utaratibu wa ununuzi wa mafuta ya petroli kwa pamoja (*bulk procurement system*) na uwekaji vinasaba kwenye mafuta (fuel marking) ambazo ni hatua muhimu katika kudhibiti bei ya mafuta; kuongeza kiwango cha mafuta yanayolipiwa kodi, kuleta ushindani wa haki miongoni mwa wafanyabiashara ya mafuta, kudhibiti uchakachuaji wa mafuta na kudhibiti uuzaji nchini wa

mafuta yanayokusudiwa kupelekwa nchi jirani (*fuel dumping*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utafiti uliofanywa mwaka 2011 na taasisi iitwayo Application *Européenne de Technologies et de Services (AETS) Consortium* ya nchini Ufaransa, *EWURA* imeshika nafasi ya kwanza katika Mamlaka za Udhibiti barani Afrika. Utafiti huo ulifanywa kwa niaba ya *African Forum for Utility Regulators (AFUR)* na ulifadhiliwa na Jumuia ya Nchi za Ulaya. Aidha, katika uchunguzi wa mlinganisho wa utendaji wa Mamlaka za Udhibiti, jopo la wataalamu lililo-ongozwa na Chuo Kikuu cha *Cape Town* cha Afrika Kusini, pia lilitaja *EWURA* kuwa Mamlaka bora ya udhibiti kimuundo na kiutawala kwa mamlaka za nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara. Kutokana na mafaniko hayo, Mamlaka nyingi za Afrika zinakuja Tanzania kujifunza kuhusu masuala ya udhibiti katika nchi zao. Kwa niaba ya Serikali, napenda kuipongeza EWURA kwa mafanikio hayo makubwa. Ni mategemeo yangu kuwa hawatarudi nyuma bali wataendelea kufanya kazi yao kwa ufanisi wa juu na kuwa mfano bora wa udhibiti duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Maji, EWURA imeendelea na udhibiti wa huduma za maji zinazotolewa na Mamlaka za Maji 129. Kati ya Mamlaka hizo, 19 ni za miji mikuu ya mikoa, 102 za miji mikuu ya wilaya na miji midogo, *DAWASA, DAWASCO* na miradi saba ya kitaifa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, *EWURA* iliidhinisha bei mpya za maji kwa

Mamlaka za Maji 14, ambazo ni Arusha, Babati, Bukoba, Dodoma, Iringa, Kigoma, Lindi, Musoma, Mwanza, Singida, Tabora, Tanga, *DAWASA* na *DAWASCO*. Aidha, bei za maji kwa Mamlaka za Maji 82 za ngazi ya wilaya na miji midogo pamoja na miradi mitano ya kitaifa ya maji ziliidhinishwa kwa pamoja. Jedwali Na.20 linaonesha wastani wa bei za maji kwa Mamlaka za Maji za miji mikuu ya mikoa na miradi ya kitaifa zinazotumika hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, EWURA ilizipatia leseni za kudumu za kutoa huduma ya majisafi na majitaka Mamlaka za Maji zote 19 za miji mikuu ya mikoa. Leseni zilizotolewa kwa mamlaka hizo ni za daraja la tatu. Mamlaka nyingi zimeshindwa kupata leseni za daraja la pili au la kwanza kutokana na kutokuwa na hati miliki za maeneo ilipo miundombinu (*title deeds*) na kutofikia kiwango cha kuridhisha cha urejeshaji wa gharama za uendeshaji (*cost recovery*). Mamlaka za Maji zote ziko katika hatua mbalimbali za kupata miliki za maeneo yake. Leseni zilizotolewa zitakuwa halali kwa kipindi cha miaka 10 na kwa mujibu wa leseni hizo, kila Mamlaka ya Maji inatakiwa iboreshe huduma zake ili ipande daraja ndani ya kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012*, EWURA* ilitoa mwongozo wa kutengeneza mipango ya kibiashara (*Business Plans)* ambayo itatoa mwelekeo kwa kila Mamlaka ya Maji ili iweze kukidhi gharama zote za uendeshaji na uwekezaji kwa lengo la kuzifanya ziwe endelevu. Kwa sasa, *EWURA* inapitia

*Business Plans* za Mamlaka hizo kuona kama zimezingatia mwongozo uliotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, *EWURA* ilifanya uchambuzi wa utendaji kazi wa Mamlaka za Maji zote nchini kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 kulingana na malengo yaliyowekwa kati ya Mamlaka za Maji na *EWURA*. Uchambuzi huo ulibaini kuwa mamlaka za maji zimekuwa na mafanikio katika kuongeza uzalishaji maji, ukusanyaji wa mapato, ufungaji wa dira za maji na kuongeza ufanisi katika matumizi kutumia rasilimali watu. Pamoja na mafanikio hayo, mapungufu yaliobainika ni uzalishaji mdogo wa maji ukilinganishwa na mahitaji, upotevu wa maji unaozidi kiwango kinachokubalika kitaifa cha asilimia 20 na kutokuwepo kwa miundombinu ya majitaka katika miji mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji. Katika mwaka 2011/2012 Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji kiliendelea na jukumu lake la kujenga uwezo wa kitaalam wa fani za ufundi zinazohitajika katika utoaji wa huduma za maji na usimamizi wa rasilimali za maji. Chuo kilidahili wanafunzi 227 na kukifanya kiwe na jumla ya wanafunzi 474 wa Stashahada. Kati ya hao, wanafunzi 91 walihitimu mafunzo yao mwezi Mei 2012. Wanafunzi 47 walihitimu katika fani ya Uhandisi wa Mifumo ya ugavi wa Maji safi na Uondoaji taka (*Water Supply and Sanitation*); 13 katika utafutaji wa maji ardhini na uchimbaji visima vya maji (*Hydrogeology and Water Well Drilling*); wawili katika fani ya Haidrolojia; na 29 katika Teknolojia ya Maabara za Uchunguzi wa maji.

Mafundi stadi (*artisans*) 131 watahitimu mafunzo mwezi Novemba 2012 katika fani mbalimbali zinazohusiana na sekta ya maji. Utaratibu wa kuanzisha na kusajili mafunzo ya stashahada ya Umwagiliaji katika Baraza la Vyuo vya Ufundi (*NACTE*) ulikamilika, na wanafunzi 13 walidahiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu yake ya msingi, Chuo kwa kutumia wataalam wake, kilifanya utafiti wa maji aridhini na kutoa ushauri wakati wa uchimbaji na ujenzi wa visima mbalimbali nchini; vikiwemo vijiji 30 katika kata ya Isimani Wilaya ya Iringa vijijini. Pia, chuo kilifanya uchunguzi wa ubora wa maji katika maabara yake na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wateja 102 wakiwemo watu binafsi na makampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji kitaongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa mwaka kutoka 227 ya sasa na kufikia 300 wakiwemo wanafunzi wa stashahada ya umwagiliaji. Chuo kinatarajia kuanza kutoa mafunzo ngazi ya shahada ya kwanza ya Maji na Umwagiliaji kwa kudahili wanafunzi 50; mafundi stadi 150 katika ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Pia, Chuo kinaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwenye fani mbalimbali zinazohusiana na sekta ya maji. Matarajio kwa mwaka 2012/2013 ni kudahili washiriki 500 wa mafunzo ya muda mfupi ikilinganishwa na washiriki 280 katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Chuo kitaendelea kutekeleza mpango mkakati wa uendeshaji wa Chuo wa kuanzia mwaka

2011 mpaka 2014, ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa jengo jipya la gorofa sita, ambapo zabuni ya kumtafuta Mtaalam Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo imeshatangazwa na tathmini imefanyika; kununua samani na jenereta; kuboresha mifumo ya TEHAMA; na kuendelea kuboresha mitaala ya cheti na stashahada katika fani zote zinazotolewa kwenye Chuo ili iendane na mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuujengea uwezo Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) kwa kuupatia malori sita kwa ajili ya shughuli za uchimbaji visima na mabwawa. Wakala ilichimba visima virefu na ujenzi wa mabwawa ambapo jumla ya visima virefu 256 vilichimbwa nchini kote. Aidha, ujenzi wa Bwawa la Misozwe lililopo katika Wilaya ya Muheza umekamilika kwa asilimia 85. Uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya uchimbaji visima virefu katika maeneo 262 na usanifu wa maeneo sita kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ulifanyika. Maeneo hayo ni Matundasi huko Chunya, Mkomazi huko Same na Msoga huko Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu yake ya msingi, Wakala pia ulifanya uchunguzi wa udongo katika miradi saba kwa ajili ya ujenzi ambayo ni mradi wa daraja la Mto Malagarasi, Kigoma; Skimu ya umwagiliaji ya Kitere, Mtwara; bwawa la Matundasi, Chunya na bwawa la Mkomazi, Same. Aidha, Wakala ulijenga mfumo mmoja wa usambazaji maji katika Hospitali ya *St. Francis* iliyopo Ifakara, Morogoro.

Wakala utaendelea kufanya uchunguzi kwa kuangalia maeneo yanayoweza kujengwa mabwawa katika Wilaya kame.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013 Wizara itaendelea kuimarisha Wakala huu kwa kununua mitambo minne na vifaa vyake *(Drilling rigs and accessories)* kwa ajili ya uchimbaji wa visima na uchunguzi wa maji chini ya ardhi; ambavyo havikununuliwa mwaka 2011/2012 kutokana na kuchelewa kusainiwa kwa mkataba wa fedha kati ya Serikali ya Tanzania na *NORAD.* Kupitia mpango huo, Wakala utakuwa na uwezo wa kuchimba visima virefu 450 kwa mwaka katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bohari Kuu ya Maji, Katika mwaka 2011/2012 Bohari Kuu ya Maji iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kununua, kuhifadhi na kusambaza vifaa na dawa za kusafisha na kutibu maji. Bohari Kuu ya Maji kwa sasa imehamisha Ofisi zake na maghala kutoka Kurasini kwenda Boko, eneo ambalo ni kubwa zaidi. Mpango huu unalenga kuwezesha upanuzi wa shughuli za ugavi wa vifaa na nyenzo za ujenzi wa miradi ya maji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea na taratibu za kuibadili Bohari hiyo kuwa Wakala wa Serikali. Lengo ni kuiboresha ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika upatikanaji na usambazaji wa vifaa vya miradi ya maji.

Masuala Mtambuka: Sheria. Wizara yangu imeendelea kutoa elimu ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009. Elimu kuhusu sheria hizo imetolewa

kwenye Halmashauri, Ofisi za Mabonde ya Maji, Mamlaka za maji na wadau wengine wa sekta ya maji pamoja na jamii kwa ujumla kupitia warsha, mikutano na makongamano. Mtaalam mshauri atakayetafsiri sheria za maji kwa lugha ya Kiswahili amekwishapatikana. Wizara inaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria na hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara imekamilisha kuandaa notisi mbili za kisheria zinazohusiana na kubadilisha majina ya mamlaka za maji *(Change of Names of Water Authorities Notice, Government Notice (GN), No. 24 of 13/01/2012)* ili yaendane na Sheria Na. 12 ya 2009 na notisi ya kutangaza Wajumbe wa Bodi ya Maji ya Taifa *(Appointment of National Water Board Members Notice, GN, No. 22 of 2012)* hivyo kufanya jumla ya kanuni zilizokamilika hadi sasa kuwa nane kama ifuatavyo:-

(i) Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji, *(Registration of Water Users Association) Regulations 2010, GN, No.22 of 22/01/2010);*

(ii) Uteuzi wa wajumbe wa Bodi (*Water Resources Management (Procedure for Nomination of Board Members) Regulations, 2010, GN. No 187 of 21/05/2010);*

(iii) Kuchukua maji kwenye vyanzo na kutiririsha majitaka yanayokidhi viwango kwenye vyanzo (*the Water Resources Management (Water Abstraction Use*

*and Discharge) Regulations 2010, GN. No. 190 of 21/ 05/2010);*

(iv) Notisi ya tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria namba 11/2009 *(Commencement Notice), GN, No. 235 of 10/07/2009);*

(v) Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji *(Community Owned Water Supply Organisations) Regulations 2010, GN.21 of 22/01/2010);*

(vi) Notisi ya tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria namba 12/2009 *(Commencement Notice GN, No. 234 of 10/07/2009);*

(vii) Notisi ya Kubadilisha Majina ya Mamlaka za Maji*(Change of Names for Water Authorities)Notice, 2012,GN, No.23 of 13/01/2012); na*

(viii) Notisi ya kutangaza Wajumbe wa Bodi ya Maji ya Taifa *(Appointment of National Water Board Members), Notice, 2012,GN , No. 22 of 2012.*

Katika mwaka 2011/2012, maoni ya wadau kuhusu kanuni za Usalama wa Mabwawa (*Dam Safety Regulations*) na Usambazaji wa Maji *(Water Supply Regulations),* yalifanyiwa kazi na rasimu zimekamilika kwa ajili ya hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Rasimu za kanuni zinazohusu uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji wa Maji *(National Water Investment Fund Regulations),* Usimamizi wa Maji chini ya Ardhi *(Ground Water Regulations),* kuratibu kazi za mafundi stadi na sanifu *(Codes of Workmanship Regulations)* pamoja na uunganishaji wa mamlaka za maji *(Clustering of Water Utilities Regulations)*

zimetayarishwa na maoni ya wadau yanaendelea kupokelewa. Notisi za kuitangaza Miradi ya Kitaifa ya Maji ya Chalinze na Wanging'ombe kuwa Mamlaka za Maji *(Establishment of Water Supply and Sanitation Authorities Notice, 2012)*, zimeandaliwa na zipo katika hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria, kukamilisha tafsiri ya sheria kwa lugha ya Kiswahili na kuendelea kutayarisha kanuni za sheria za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Habari, Elimu na Mawasiliano. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa wananchi kupitia tovuti yake na vyombo vya habari. Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru Kitaifa, yaliyofanyika kwenye viwanja vya michezo vya Chuo cha Usimamizi na Maendeleo ya Maji mwezi Oktoba 2011; na kilele chake kwenye uwanja wa Maonesho ya Biashara wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere jijini Dar es Salaam mwezi Desemba 2011. Katika kufanikisha maadhimisho hayo, jumla ya vipeperushi 30,000, vijitabu 10,000 vinavyohusu Sekta ya Maji; nakala 75,000 za gazeti maalum la mafanikio ya miaka 50 ya Uhuru katika Sekta ya Maji ziliandaliwa na kusambazwa kwa wananchi. Aidha, vipindi 16 vilirushwa kwenye redio na luninga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipeperushi na machapisho mengine yalitolewa katika maadhimisho ya Wiki ya Maji ambayo kwa mwaka huu yalifanyika kitaifa mkoani Iringa. Vipindi vinane vya televisheni na

redio ambavyo vilifafanua na kuelimisha masuala mbalimbali ya sekta ya maji vilirushwa. Makala ya filamu (*documentary film*) ya mafanikio ya Sekta ya Maji ilitengenezwa na kurushwa. Kwa ujumla, makala 21 ziliandikwa na kutolewa magazetini na kwenye mitandao ya kijamii ya mawasiliano. Pia, Wizara yangu ilishiriki katika maonesho ya Kilimo ya Nanenane mwaka 2011 yaliyofanyika Nzuguni mjini Dodoma. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuelimisha wananchi na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta ya Maji kwa kuiboresha tovuti ya Wizara ili wananchi wengi zaidi waitumie; kuandaa na kutangaza vipindi katika luninga na redio pamoja na utoaji wa taarifa za uwazi katika Sekta ya Maji kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Serikali Ubia (*Open Government Partnership OGP*). Lengo kuu likiwa ni kuongeza uelewa na kuboresha mawasiliano kati ya wadau wa Sekta ya Maji na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuimarisha utekelezaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Takwimu na Taarifa za Sekta ya Maji (*Water Sector Management Information System*) kwa kutoa mafunzo zaidi na kupanua matumizi yake hadi kwenye ngazi zote za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo mfumo huo unatumika. Jumla ya watumishi 424 walipata mafunzo kuhusu Mfumo huo katika ngazi zote. Mfumo unawezesha watekelezaji wa Programu kuwasilisha takwimu na taarifa za mipango, mikataba na matumizi ya fedha za Programu kwa njia ya mtandao wa kompyuta. Katika mwaka 2012/2013,

Wizara yangu itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu. Hii ni pamoja na kupanua Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Takwimu wa Taarifa za Sekta ya Maji ili uunganishwe na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (*Monitoring and Evaluation*).

Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya TEHAMA, Wizara itaandaa Sera ya Usalama wa Habari *(Information Security Policy and Disaster Recovery Plan)* kwa lengo la kulinda na kudhibiti taarifa na takwimu za wizara dhidi ya uhalifu wa mitandao. Aidha, Wizara itanunua vifaa na vitendea kazi vya kisasa vya TEHAMA kwa lengo la kuboresha ufanisi wa utendaji na huduma kwa wananchi. Wizara itaimarisha miundombinu ya mtandao kwenye Ofisi za Wizara Ubungo, Dar es Salaam kwa kuweka mkonga wa mawasiliano ambao utaunganishwa katika Mkonga wa Mawasiliano wa Taifa (*National Fibre Optic Cable).* Hadidu rejea za kazi hiyo zimeandaliwa na kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali cha ununuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jinsia. .Wizara yangu imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria za Maji za mwaka 2009 kwa kuhamasisha uwepo wa uwiano wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume kwenye vyombo vya kusimamia Sekta ya Maji. Vyombo hivyo vina maamuzi makubwa katika usimamizi na matumizi ya maji katika maeneo yao. Asilimia ya wanawake katika vyombo hivyo ni kama ifuatavyo: Bodi ya Taifa ya Maji (33%), Bodi za Mabonde ya Maji (35%), Bodi za Mamlaka za Maji (33%), Bodi za Wakala (43%) na Jumuiya za

Watumiaji Maji (33%). Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kutoa fursa za uwiano kwa jinsia zote katika ngazi za maamuzi na uongozi. Aidha, jamii itaendelea kuhamasishwa kusajili jumuiya za watumiaji maji na kupewa mafunzo ya usimamizi wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, ambayo yatawashirikisha wanaume na wanawake katika jumuiya zao. Vita dhidi ya Rushwa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa kukiwezesha kufanya ukaguzi wa masuala ya uongozi na utawala na kutoa taarifa. Taarifa hizo zimesaidia kuwakumbusha watumishi kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Aidha, Kamati ya Uadilifu iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia maadili katika utumishi.

Ili kuboresha huduma zake, Wizara imezindua Mkataba wa Huduma Bora kwa Mteja, baada ya kuufanyia mapitio na marekebisho. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitoa mafunzo ya maadili ya viongozi kwa wajumbe wote wa menejimenti na maafisa wakuu wa Wizara yaliyolenga kusisitiza umuhimu wa watumishi kuzingatia maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetoa mafunzo kwa wajumbe wa menejimenti ya Wizara kuhusu namna bora ya kushughulikia malalamiko ya wananchi. Mafunzo hayo yataiwezesha Wizara kushughulikia malalamiko yanayotolewa na wananchi kwa haraka na uwazi zaidi. Wizara pia

itakuwa na takwimu za malalamiko yaliyopokelewa na kupatiwa ufumbuzi hivyo kuboresha maeneo yenye mapungufu kiutendaji. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeanzisha dawati la malalamiko na kuunda timu ya kuboresha huduma kwa mteja. Wizara itaendelea kuwakumbusha watendaji na watumishi wote kwa ujumla kufanya kazi kwa bidii wakizingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaanza kutekeleza Mpango wa Serikali wa kuwa wazi zaidi katika utekelezaji wa majukumu *(Open Government Partnership - OGP)*. Mpango huo unatoa fursa kwa Wizara kuhimiza, kukuza na kuboresha utawala bora, uitikiaji pamoja na kuwa na Serikali inayowajibika. Mpango wa *'OGP'* utakuwa chombo chenye manufaa kwa wananchi, jumuiya za kiraia, Sekta Binafsi na vyombo vya habari, katika kudai uwazi zaidi kwenye uendeshaji wa shughuli za Serikali. Mpango huo una manufaa makubwa kwa Wizara kwa kuwa utawezesha zaidi kukuza uadilifu na uwazi kwa umma, kuhimiza usimamizi bora wa rasilimali za taifa na kupambana na rushwa na kuimarisha taratibu za kushirikisha wananchi katika kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma za jamii katika maeneo yao. Kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Nchi na wa Wizara, upatikanaji zaidi wa habari na taarifa zinazohusu Sekta ya Maji utakuwa wazi na rahisi, na hivyo kuchangia kupunguza vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukimwi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu imeendelea kutoa posho kwa watumishi tisa waliojitambulisha kuwa wanaishi na Virusi

vya Ukimwi. Posho hiyo ni kwa ajili ya kununulia lishe bora na mahitaji mengine muhimu kwa afya. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi kwa watumishi wa Sekta ya Maji. Pia itaendelea kutoa posho ya kununulia lishe bora kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya Ukimwi; na itaendelea kutumia utaratibu wa kuzialika Taasisi zinazotoa huduma ya kuelimisha umma kuhusu Ukimwi, kuwepo katika mabanda ya Wiki ya Maji na mikusanyiko mingine ya sekta ili kutoa elimu kwa wadau kuhusu Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu iliendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi na usimamizi wa mipango ya kisekta. Aidha, watumishi 77 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo katika nafasi mbalimbali na watumishi wapya saba wameajiriwa katika Idara ya Ubora wa Maji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 47 ili kukidhi Ikama ya watumishi 1,723 wanaohitajika na kuwapandisha vyeo watumishi 64. Wizara kwa sasa ina jumla ya watumishi 1,676.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji; inaendelea kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo watumishi *(Capacity Development Plan).* Katika utekelezaji wa mpango huo, watumishi wamepatiwa mafunzo mbali mbali yaliyoainishwa katika mpango. Watumishi 318 kutoka Mamlaka 99 za Majisafi na Usafi

wa Mazingira za miji ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa ya maji na Mamlaka saba za miji mikuu ya mikoa wamepatiwa mafunzo yanayohusu masuala ya menejimenti, biashara na ufundi (hususan uzalishaji maji, upotevu wa maji na kuongeza makusanyo ya maduhuli). Mafunzo pia yalihusu uandaaji wa maombi ya fedha za uwekezaji, utumiaji wa TEHAMA katika kutayarisha ankara, Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (*GIS*) na masuala ya kuhudumia wateja. Wizara pia ilitoa mafunzo kwa wajumbe wa Bodi na Menejimenti za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wapatao 270 katika Mikoa 19, kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo mengine yalitolewa kwa watumishi 212 kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji nchini. Kati ya hao, 156 walipata mafunzo katika Sera na Miongozo inayotumika katika uhifadhi wa mazingira, namna ya kuzuia uchafuzi na usimamizi wa vibali vya matumizi ya rasilimali za maji na 56 walipata mafunzo katika usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji, matumizi ya vifaa vya kupima maji chini ya ardhi na utatuzi wa migogoro kwa watumiaji maji. Pia, watumishi 22 walipatiwa mafunzo juu ya viwango vya ubora wa maji *(ISO 17025 - Quality Assurance)* ikiwa ni maandalizi ya Maabara za Maji kupata ithibati (*Accreditation*). Watumishi 18 wanaendelea kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada na Shahada ya Uzamili. Mtumishi mmoja anapata mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*Ph.D.*) kuhusu masuala ya TEHAMA. Vilevile, watumishi 98 wamepata mafunzo ya muda mfupi katika ngazi ya cheti na Stashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi wa kujenga uwezo wa sekta unaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*); watendaji 13 wa Timu za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika mikoa ya Singida, Tabora na Mwanza walipewa mafunzo. Aidha, watumishi 68 wa Timu za Maji na Usafi wa Mazingira katika Halmashauri sita za Sikonge, Uyui, Singida, Manyoni, Kwimba na Sengerema wamepatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo watumishi na wadau wengi zaidi kwa kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo watumishi (*Capacity Development Plans*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto na Hatua zinazochukuliwa. Katika kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2011/2012, Wizara ilikabiliana na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuongezeka kwa Idadi ya Watu na shughuli za kiuchumi na kijamii nchini. Utoaji wa huduma ya maji unakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa idadi ya watu kusikoendana na uwekezaji. Hali hiyo ni dhahiri katika maeneo yote ya vijijini na mijini. Kiwango cha ongezeko la watu kwa mwaka kitaifa ni asilimia 2.3 vijijini, asilimia 4.5 mijini, na asilimia 6 katika Jiji la Dar es Salaam. Ongezeko lingine ni kukua kwa shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la viwanda na kupanuka kwa ujenzi wa makazi. Kutokana na ukuaji huo wa kasi, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kushirikisha wananchi hususan katika maeneo ya vijijini katika hatua zote za miradi katika kubuni, kujenga, kusimamia, kuendesha na kuchangia gharama za uendeshaji;

(ii) Kukarabati na kujenga miradi ya kipaumbele ambayo inatoa huduma kwa wananchi wengi katika ujenzi wa mradi wa maji wa vijiji 10 kwa kila Halmashauri; Ujenzi wa miradi ya maji ya miji ya Mbeya, Songea, Iringa na Mwanza; mradi wa maji wa Mwanga-Same-Korogwe, kujenga bwawa la Farkwa kwa ajili ya mji wa Dodoma, Wilaya za Kondoa, Chamwino na Bahi na kutekeleza mradi wa maji wa Masasi-Nachingwea; na

(iii) Mradi wa maji Jijini Dar es Salaam unaojumuisha upanuzi wa chanzo cha maji Ruvu Chini na Ruvu Juu, kuchimba visima vya maji vya Mpera na Kimbiji; na ujenzi wa bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma kwenye Miundombinu ya Maji. Biashara ya vyuma chakavu imechangia kwa kiasi kikubwa uharibufu kwenye miundombinu ya maji hali inayoathiri upatikanaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka kwa jamii. Hatua zinazochukuliwa ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa ulinzi shirikishi katika kulinda miundombinu ya maji kupitia maonesho na sherehe mbalimbali za kitaifa kupitia Wiki ya Maji na maigizo kwenye luninga na redio pamoja na usambazaji wa vipeperushi. Aidha, Mamlaka za Majisafi mijini zimeendelea kushirikiana na uongozi wa mikoa, Jeshi la Polisi na Wananchi ili kubaini wanaojihusisha na hujuma hizo ikiwa ni pamoja na kutoa zawadi ya fedha kwa

watoa taarifa. Vilevile, Wizara imetoa Waraka kwa Mamlaka zote nchini kutokununua vifaa vya maji vilivyotumika kama vile mita za maji, mabomba na vipuli vya mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha kutokutabirika kwa misimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu, mafuriko ya mara kwa mara hali inayoathiri ujenzi wa miundombinu ya maji na upatikanaji wa rasilimali za maji. Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na:-

(i) Kujenga mabwawa madogo na makubwa kwa ajili ya hifadhi ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

(ii) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wataalam ili kuongeza weledi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kutumia utaalam asilia (*Indigenous knowledge*) katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(v) Kuendeleza matumizi ya teknolojia sahihi zinazotumia maji kwa ufanisi; na

(vi) Kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa lengo la

kubaini namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Kupungua kwa raslimali za maji. Maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali yanaendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutokana uharibifu mkubwa wa mazingira hasa kwa kuchoma misitu, ukataji wa miti holela kwa kuchoma mkaa, kupasua mbao, kulima kandokando mwa vyanzo vya maji na ufugaji holela. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali inaendelea kusimamia na kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa dhidi ya uharibifu na uchafuzi. Wizara imeendelea kushirikisha wadau mbalimbali katika kutunza vyanzo vya maji kwa kuvitambua na kuviwekea mipaka, kupanda miti, kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo oevu, maeneo ya milimani na katika chemichemi. Hatua nyingine ni kudhibiti matumizi holela ya maji kwa kutoa kibali cha kutumia maji na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na uharibifu wa mazingira kwa kutumia Sheria za Maji na Mazingira na pia kwa kutumia sheria ndogo ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taifa letu limekuwa na utajiri mkubwa sana wa gesi asilia, napenda kulishauri taifa lianze kuandaa mpango utakaowafanya Watanzania walio wengi kutumia nishati ya gesi kwa kupikia na matumizi mengine ya nyumbani ili kupunguza na hatimaye kuacha kabisa matumizi ya mkaa majumbani. Lengo likiwa ni kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji na kupunguza mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine wa kukabiliana na uhaba wa maji ni kuendelea kuimarisha muundo bora wa kitaasisi kwa ajili ya usimamizi endelevu wa raslimali za maji katika mabonde ya maji kwa kuhakikisha uwepo wa mgawanyo yakinifu na matumizi bora ya maji kwa ajili ya mahitaji ya kijamii na kiuchumi. Vilevile, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2011/2012 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha. Napenda kuzishukuru Serikali za Ujerumani, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea ya Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India na Misri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW*),* Benki ya Maendeleo ya Ufaransa *(AFD),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB),* Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID),* Umoja wa Ulaya

(*EU*), Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia *(MCC),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Norway *(NORAD),* Taasisi ya Maendeleo ya Uingereza *(DFID),* Shirika la Kiufundi la Ujerumani (GIZ*),* Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo *(UNDP),* Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(*JICA*)*, Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani *(UN Habitat)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden *(SIDA),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Canada *(CIDA),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Denmark *(DANIDA),* na Shirika la Misaada la Marekani *(USAID)* kwa misaada ya fedha na michango yao ya kitaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayashukuru pia, mashirika ya kidini ya *World Islamic League,* Shirika la Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania*, Islamic Foundation,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, Baraza Kuu la Waislam Tanzania, Kanisa Katoliki Tanzania, Kanisa la Kianglikana Tanzania, *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Norwegian Church Aid* na *Livingwater International*. Nashukuru pia, taasisi zisizo za kiserikali za *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET),* Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(*WAMMA), *Southern Highlands Participatory Organizasition (SHIPO)*, *WaterAid*, *World Vision*, *Plan International*, *Concern Worldwide*, *Netherlands Volunteers Services (SNV)*, Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (*IUCN*), *Adventist Development Relief Agency (ADRA), World*

*Wide Fund for Nature (WWF*), *African Medical Research Foundation (AMREF), Clinton HIV Aids Initiative (CHAI)* na *Bill and Melinda Gates Foundation,* na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wameendelea kuisaidia Sekta ya Maji kufanikisha malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika; nitumie fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Professa Mark James Mwandosya (Mb) kwa kazi nzuri aliyoifanya akiwa Waziri wa Maji. Juhudi na maarifa yake zimenifanya niwe na mahali pazuri pa kuanzia katika kuwapatia wananchi wa Tanzania huduma ya majisafi na usafi wa mazingira karibu na makazi yao. Kwa namna ya pekee, nachukua nafasi hii kumpa pole nyingi wakati huu ambapo bado anaendelea na matibabu; tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu ampe nafuu apone haraka. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi Gerson Lwenge (Mb) kwa kazi yake nzuri aliyoifanya akiwa Naibu Waziri wa Maji. Nawatakia kila la kheri na mafanikio katika majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa njia ya pekee nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mhandisi Dr. Binilith Saatano Mahenge (Mb), Naibu Waziri wa Maji, kwa msaada na ushirikiano anaonipatia tangu tulipopewa majukumu ya kuiongoza Wizara ya Maji. Naomba pia, nitoe shukrani zangu kwa Mhandisi Christopher Nestory Sayi, Katibu Mkuu, Mhandisi Bashir Juma Mrindoko, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Wakuu wa Vitengo, Maafisa na Watendaji Wakuu wa Mashirika, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara

yangu, wataalam na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kuishukuru familia yangu kwa upendo kunipa kila aina ya misaada ili niweze kumudu majukumu yangu. Napenda kumshukuru sana mke wangu Kudra Maghembe na watoto wetu Dkt. Ngwalu Maghembe, Dkt. Mwanamkuu Maghembe na Mcheja na Namvumo Maghembe na kwa njia ya pekee napenda niwashukuru wananchi wa jimbo langu la Mwanga kwa kuniunga mkono na kufanikisha kwa ufanisi mkubwa uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi unaoendelea hivi sasa. Nawapongeza sana na kuwaahidi kuendelea kushirikiana nao katika kuiletea Wilaya yetu maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013. Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 485,898,613,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 20,142,275,000 ambapo shilingi 14,273,856,000 ni Mishahara ya Watumishi *(PE),* na shilingi 5,868,419,000 ni fedha za Matumizi Mengine *(OC).* Jumla ya Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 465,756,338,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 140,015,967,000 ni fedha za ndani na shilingi 325,740,371,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwako wewe mwenyewe na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa

kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anwani: *www.maji.go.tz .*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:**Ahsante sana Mheshimiwa Professa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maji kwa kupitia hotuba yako kwa ufundi mkubwa sana na imeungwa mkono. Hoja iliyotolewa na kwa kumalizia Waheshimiwa Wabunge kama mlisikiliza vizuri katika familia ya Mheshimiwa Dkt. Jumanne Maghembe kuna Madaktari wawili, Dkt. Ngwaru na Dkt. Mwanamkuu. Kwa hiyo katika familia hii kuna Madaktari watatu, inataka kufanana kidogo na familia ya Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambayo ina Profesa, ina Daktari na Daktari.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati niwaandae wachangiaji watakaofuata baadaye ili waendelee kujijua Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Halima Mdee, Selemani Zedi na Sylvester Kasulumbayi. Utaratibu utakaokuwepo hapa kama zamu yako ikifika haupo basi itakuwa imejifuta yenyewe.

Naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na masuala ya maji. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA M. HAMID - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla sijaanza kusoma taarifa ya Kamati naomba nianze kuwapongeza Wabunge wa Simba kwa kuwapa kipigo cha mabao 3 kwa 2 Wabunge wa Yanga. Nawapongeza wachezaji wa Wabunge wa Simba waliopachika mikwaju hiyo kwa *penalty* nikianzia na Mheshimiwa Amos Makalla ambaye aliwapatia ubingwa Wabunge wa Simba. Mheshimiwa Amos Makalla ni nahodha lakini huyu ndio *boban* wetu wa Simba. Lakini pia nimpongeze Yona Kirumbi *tourist* wetu wa Simba. Nimpongeze Kikula huyu ni f*abrigoes* wa Simba, Simba Oyee*!!! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maji tarehe 01Juni na tarehe 4 Juni, 2012 katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam ili kuchambua taarifa ya utekelezaji wa maoni ya Kamati, utekelezaji wa bajeti na changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2011/2012 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Wakati wa kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imeyafanyia kazi maoni ya Kamati. Napenda kutaja baadhi ya maeneo ambayo utekelezaji wake unaridhisha ikiwa ni pamoja na:-

(a) Visima virefu 15 vimechimbwa katika eneo la Sanya Juu (Hai) kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na umwagiliaji.

(b) Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi: - Serikali imeendelea na juhudi za kutafuta fedha zaidi zitakazowezesha mradi huu kuendelezwa katika vijiji zaidi. Kamati ilifahamishwa kwamba *DFID* wameahidi kutoa *EURO* milioni 15 na *ADB* dola za Marekani milioni 100 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

(c) Upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu: - DAWASA imefunga mabomba mapya na kufanya ukarabati wa mabomba yenye urefu wa Kilomita 1,550. Aidha, wananchi wamepewa elimu na wanaendelea kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kila mteja kufungiwa dira kama njia mojawapo ya kudhibiti upotevu wa maji.

(d) Uvunaji wa maji, Wizara imeendelea kuhamasisha utumiaji wa teknolojia ya kuvuna maji ya mvua; hadi sasa matangi 313 yamejengwa katika Halmashauri mbali mbali nchini. Aidha, Wizara ina mpango wa kutoa mafunzo kwa mafundi wawili kutoka kila kijiji kilicho katika program ya vijiji kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inakumbana na changamoto mbali mbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika kufikia malengo iliyojiwekea. Baadhi ya changamoto ni kama ifuatavyo:-

(a) Kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa, lakini pia kuchelewa kutolewa fedha zamaendeleo na hivyo kuathiri kasi ya utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Wizara;

(b) Kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi na kijamii nchini hususan katika maeneo ya mijini wakati miundombinu ya maji bado ni ya zamani. Hii husababisha wananchi wengi kutofikiwa na huduma ya maji;

(c) Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha kutotabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu katika baadhi ya maeneo, kukauka kwa vyanzo vya maji na mafuriko; athari hizi zimeleta uharibifu mkubwa wa miundombinu ya maji na umwagiliaji;

(d) Uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya kemikali katika maeneo ya uchimbaji wa madini; na

(e) Ugumu wa kupata kwa wakati takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji kutokana na programu kushirikisha taasisi mbalimbali ambazo Wizara ya Maji haina mamlaka juu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, ili kuweza kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Maji na Umwagiliaji chini ya Fungu 49 inaomba jumla ya shilingi 485,898,613,000/=.

Kati ya fedha hizo, shilingi 20,142,275,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 465,756,338,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 140,015,967,000/= ni fedha za ndani na shilingi 325,740,371,000/= ni fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinazoombwa zitaiwezesha Wizara kutekeleza kazi mbali mbali. Baadhi ya kazi hizo ni pamoja na:-

(a) Kuimarisha Bodi za maji za mabonde kwa kujenga au kukarabati majengo ya ofisi, kununua vitendea kama kompyuta na vifaa;

(b) Kuhifadhi vyanzo muhimu vya maji vya Maisaka, Makutupora na Mawanya dhidi ya uchafuzi na kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya migodi na maeneo ya viwanda;

(c) Kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea ya maji vijijini ikiwa ni pamoja na Lukululu, Masoko, Mwakaleli, Pawga, Usangi, Mgagao, Taroha, Butu, Lolwe, Kisanjuni, Vuaga, Lomwe, Ng'onde, Kikungula, Makuuranga na Mbalate;

(d) Kutekeleza mradi ya vijiji 10 kila Halmashauri,

(e) Kuendelea na upanuzi wa chanzo cha maji cha Ruvu Chini,

(f) Kuchimba visima virefu eneo la Mpera kwa ajili ya kuongeza kiasi cha maji katika jiji la Dar es Salaam;

(g) Kuimarisha Chuo cha Maji kwa kukarabati na kupanua majengo ya madarasa na mabweni ya wanafunzi;

(h) Kuendelea na mradi wa kuvipatia maji vijiji 76 na miji ya Kagongwa,Isaka na Tinde kutokana na mradi wa maji wa Kahama/Shinyanga;

(i) Kupanua chanzo cha maji cha Ruvu Juu na miundombinu ya kusambaza maji kutoka Kibaha hadi Kimara; na

(j) Kuratibu na kufuatilia utunzaji na udhibiti wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Baada ya kuelezea utekelezaji wa maoni ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Mlheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Jumla:-

(i) Bajeti ya Wizara Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya maji mwaka hadi mwaka toka shilingi bilioni 30.7 mwaka 2010/2011, shilingi bilioni 41.5 mwaka 2011/2012 na shilingi bilioni 140 mwaka 20012/2013. Pamoja na pongezi hizi, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuongeza bajeti ya maji kwa pesa za ndani ili kupunguza utegemezi wa fedha za wahisani.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Mtiririko wa utoaji wa fedha za Maendeleo. Miradi mingi ya maendeleo inashindwa kukamilika kwa wakati kutokana na utoaji wa fedha kutozingatia muda. Kamati inaishauri Serikali ifanye jitihada kuhakikisha kuwa fedha za maendeleo zinatolewa kwa wakati ili ziweze kufanya kazi kwa kasi iliyokusudiwa. Aidha, utoaji wa fedha za maendeleo uzingatie misimu ili utekelezaji wa baadhi ya shughuli za maendeleo ufanyike kwa kuzingatia hali ya hewa, mfano kipindi cha masika na kipindi cha kiangazi.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, Kodi ya madawa ya maji. Kamati inaishauri Serikali kuondoa kodi za ongezeko la thamani kwenye dawa za kutibia maji kwa nchi nzima ili kupunguza bei ya dawa hizo ambazo hatima yake mtumiaji wa mwisho wa maji ndiye anayeumia na bei kubwa ya maji. Cha kushangaza Serikali imeweza kusamehe kodi hiyo kwa baadhi ya Halmashauri tu na nyingine bado zinalipa kodi hiyo.

Kamati inashauri na kusisitiza kuwa tozo za ongezeko la thamani (VAT) kwenye dawa za maji iondolewe ili kumpa unafuu mtumiaji wa maji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maji. Maji ni hitaji la msingi la maisha na uhai wa viumbe vyote. Aidha shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme na bidhaa za viwandani, matumizi ya majumbani na usafi wa mazingira zinategemea uwepo wa maji ya kutosha.

Katika nchi yetu huduma ya maji bado haijatosheleza mahitaji ndiyo maana maeneo mengi wananchi wanataja ukosefu wa huduma za maji kuwa ndiyo tatizo kubwa linalowasumbua. Kutokana na umuhimu huu, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, Vyanzo vya maji. Kwa kuwa mahitaji ya maji yanaongezeka siku hadi siku kulingana na ongezeko la watu, mifugo, pamoja na shughuli za kilimo, na kwa kuwa mito mingi nchini imeanza kupungua maji kwa kasi kutokana na

mabadiliko ya tabianchi na kuvamiwa na wafugaji wanaohamahama kutafuta malisho na shughuli nyingine za binadamu, Kamati inaitaka Serikali kuweka na kuisimamia mikakati endelevu ya kutunza vyanzo vyake vya maji.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Uvunaji wa maji. Kwa kuwa uhaba wa maji ni tatizo kubwa kwa nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuhimiza na kuhamasisha jamii kwa kutoa elimu juu ya namna ya kuvuna maji ya mvua badala ya kutegemea maji ya visima au ya bomba ambayo hayatoshelezi. Aidha, inashauriwa kwamba mfumo wa kuvuna maji uwe sehemu ya michoro yote ya nyumba zinazotarajiwa kujengwa.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Mradi wa Vijiji Kumi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni mradi huu ambao unalenga kupunguza tatizo la maji vijijini. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Maeneo yenye madini kama chumvi na *chloride,* iangaliwe namna ya kupata maji kwa njia nyingine kama mabwawa ili kupunguza athari zinazoweza kutokana na matumizi ya maji yenye madini hayo kwa viumbe hai;

(b) Kwa miaka ijayo, bajeti ya mradi iongezwe na ipanue wigo wa mradi kwa vijiji vingi zaidi nchini;

(c) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi ya utunzaji mzuri wa pampu za maji ili kuepuka

uharibifu unaotokana na matumizi yasiyo sahihi ya pampu hizo; na

(d) Badala ya kutegemea fedha za wahisani kwa asilimia 100 kutekeleza mradi wa vijiji kumi, Serikali inashauriwa itenge fedha za ndani kwa ajili ya mradi huu.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kwamba, Miradi ya Maji imekuwa ikitekelezwa katika maeneo kadhaa na kusababisha maeneo mengine kusahaulika. Jambo hili limeleta maswali mengi na kuonekana kuna upendeleo kwa baadhi ya maeneo. Kamati inaishauri Serikali iwe na ugawaji sawa wa Miradi ya Maji na kuyaangalia maeneo yanayoonekana kusahaulika kwa muda mrefu na kuyapatia huduma ya maji.

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa biashara ya vyuma chakavu imeharibu miundombinu ya maji kwa kiasi kikubwa. Kamati inaishauri Serikali kusitisha biashara ya chuma chakavu ili kuokoa miundombinu ya maji inayotokana na wizi wa mifuniko ya maji machafu na vifaa vingine. Aidha, kama biashara hii ni lazima ifanyike, basi utafutwe utaratibu mzuri na wa wazi ambao utaratibiwa na vyombo vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, uvumilivu na

michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua kwa kina Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdulsalaam S. Amer, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Sylvester M. Kasulumbayi, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Seleman Said Bungara, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani na Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Binilith Satano Mahenge (Mb), Katibu Mkuu, Eng. Christopher Sayi na Wataalam wote wa Wizara, kwa ushirikiano na juhudi wanazofanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Elieka Saanya, kwa kuihudumia vyema Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, jumla ya shilingi 485,898,613,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Makamu Mwenyekiti, kwa uwasilisho huo kwa niaba ya Kamati inayohusika na masuala ya maji. Naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai na kuweza kusimama hapa mbele yenu hivi sasa na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Viongozi wetu; Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa imani

kubwa kwetu na kututeua kuwa Wasemaji wa Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu; aidha, namshukuru Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe (Mb), Naibu Kiongozi wa Upinzani na Mheshimiwa Tundu Lissu (Mb), Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Tunawashukuru kwa kutuongoza vyema kutimiza majukumu yetu kwa wananchi wetu wote. Pia nawashukuru wote waliotoa mchango wao katika kuandaa hotuba hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nawashukuru Wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwa ujumla, kwa ushirikiano wanaotupatia katika kutimiza majukumu yetu sisi Wabunge tutokao Mkoani humo. Nasema ahsanteni sana na ninawaahidi kuendelea kuwasemea juu ya kero zenu kwa kipindi chote nitakachokuwa Bungeni. Pia naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa kwa kipindi chote cha majukumu yangu na kwa wakati huu ambapo nafanya shughuli za uwakilishi wa wananchi Bungeni. Nawakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, nakupongeza wewe binafsi, kwa kuliongoza vyema Bunge hili la Kumi lenye changamoto nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Maji ni kuwa wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama ni asilimia 86 katika Miji Mikuu ya Mikoa na asilimia 57.8 vijijini. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, upatikanaji wa maji safi ni asilimia 55 tu. Taarifa hizi zinatia wasiwasi kwani nchi yetu ina

rasilimali za maji za kutosha ila tatizo ni vipaumbele vyetu katika kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Dar es Salaam, hali hii haikubaliki kwani vyanzo vya maji kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam vimepatikana na maji mengi chini ya ardhi yamegunduliwa kwenye maeneo ya Kimbiji na Mpera. Ila mpaka leo hii vyanzo hivi havijatumika kikamilifu katika kuliwezesha Jiji la Dar es Salaam kuweza kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge liliidhinisha fedha za ndani kwa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kiasi cha shilingi bilioni 41.6 fedha za ndani na fedha za nje shilingi bilioni 387.1. Kwa hali hii, ni dhahiri kuwa Serikali imeamua kuachia jukumu la kutoa huduma ya maji kwa wananchi wake kwa kutegemea fedha za wafadhili na wahisani wa nje badala ya kutenga fedha za ndani za kutosha ili kuweza kuokoa wananchi ambao wanaathirika kutokana na kukosa maji safi na salama kutokana na miradi hii ya wafadhili kutokutekelezwa kwa wakati na mfano ni Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia kila Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kutoa huduma za kijamii duniani kote ni ya Serikali inayokusanya kodi. Kitendo cha Serikali kutegemea mashirika ya nje kugharamia huduma za kijamii kama maji kwa wananchi wetu si sahihi kwa sababu ama mashirika hayo huchelewesha misaada hiyo au misaada haiji kabisa. Kwa mwaka 2011/2012, fedha za nje zilikuwa shilingi bilioni 387.1 wakati za ndani zilikuwa shilingi

bilioni 41.6, mwaka huu wa 2012/2013 fedha za nje ni shilingi bilioni 325.7 za ndani ni shilingi bilioni 140.

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iondokane na utaratibu huu wa kutegemea wafadhili kwenye huduma muhimu kama ya maji, badala yake zitengwe fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanapata maji safi na salama na hasa ikizingatiwa kuwa kwa mujibu wa tafiti mbalimbali maji ndiyo yameonekana kuwa kero kuu kwa wananchi wetu .

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa Mradi wa Programu ya Maji Vijijini kwa mwaka 2011/2012 ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 50.8 wakati Programu ya Maji Safi na Maji Taka Mijini ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 313.55.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka huu wa Fedha (2012/2013), Programu ya Maji Vijijini imetengewa fedha za ndani jumla ya shilingi bilioni 9.6 na fedha za nje shilingi bilioni 27.2 na Programu ya Maji Safi na Maji Taka ni shilingi bilioni 126.8 za ndani na shilingi bilioni 245.2 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, upangaji mipango na ugawaji wa rasilimali fedha usiozingatia uwiano wa hali halisi ya mahitaji ni kosa kubwa ambalo litaendelea kukandamiza jamii ziishizo vijijini. Takwimu zinatuonesha kuwa, asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini (31,809,808) na ndiyo wenye shida kubwa ya maji ikilinganishwa na wale waishio mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tatizo kubwa la maji mijini, hali ni mbaya zaidi vijijini na hili linathibitishwa na kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Juma Nkamia kuwa, kwa sasa wananchi kwenye moja ya vijiji vilivyopo jimboni mwake wanabadilishana kati ya debe la mahindi na ndoo ya maji. Hali hii haikubaliki kwa Taifa ambalo lina vyanzo vya kutosha vya maji kama vile mito, maziwa na chemchemi nyingi za asili na za kutosha.

Kwa sababu hiyo basi, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuanzia bajeti hii, ianze kuangalia ugawaji wa fedha kwa uwiano kati ya Programu ya Maji Vijijini na Programu ya Maji Safi na Maji Taka Mijini ili kuwawezesha wananchi wa vijijini kupata huduma ya maji, kwani kwa hali ilivyo ni kuwa uwiano wa mgawanyo wa fedha za Miradi ya Maendeleo baina ya mijini na vijijini ni 1:10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo ni kuwa Wataalamu wa Maji waliopo wengi ni wale ambao walisomeshwa miaka ya 70 wakati wa kutekeleza Mpango Kabambe wa Maji wa Miaka 20, kwani Julai 1974, Chuo cha Maji kilianzishwa rasmi kikiwa na wanafunzi 30 na wakafuatiwa na wanafunzi wengine 60 mwezi Machi 1975.

Mheshimiwa Naibu Spika, kozi za wanafunzi zilikuwa ni *Hydrolojia, Hydrojiolojia* na *Ujenzi* na zilikuwa ni za miaka mitatu kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Nne. Kila aliyemaliza alipata stashahada ya *Water Resources Engineering* kwa fani hizo. Ilitarajiwa kuwa, Chuo kingedahili wanafunzi 250 kila mwaka, lakini

kiwango cha juu kilichofikiwa ni wanafunzi 128 tu waliodahiliwa mwaka 1983.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi 129 walipelekwa Nchini India kwa mafunzo ya Shahada ya Uhandisi wa Maji katika Chuo Kikuu cha Roorkee, chini ya ufadhili wa Serikali ya Sweden ikishirikiana na Serikali za India na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maji imekuwa ikikabiliana na changamoto ya upatikanaji wa wataalam wa kutosha katika fani mbalimbali za masuala ya maji. Kwa sasa kwa mujibu wa taarifa za Wizara ni kuwa mahitaji ya wataalam hao ni: Sekretariati ya Mikoa zinahitaji wataalam 63, wanatakiwa wahandisi 560 na mafundi sanifu katika fani za maji zaidi ya 1,700 katika ngazi za Halmashauri ya Wilaya. Kwa upande wa usimamizi wa rasilimali za maji, changamoto kubwa iliyopo ni kukosa wataalamu wa ngazi ya juu kutokana na wengi wao kumaliza kipindi chao cha utumishi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ni kwa nini Serikali iliamua kuachana na utaratibu wa kusomesha vijana wetu kwa kuwapa ufadhili haswa kwenye Sekta ya Maji ili kuweza kukabiliana na changamoto hii. Aidha, tunataka kujua mwaka huu wa fedha Wizara inajiandaa kusomesha vijana wangapi ili kuweza kukabiliana na changamoto ya upungufu wa wataalamu hawa? Kwani taarifa zilizopo ni kuwa wengi wamestaafu na hakuna waliokuwa wameandaliwa kuchukua nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na vyanzo vya kutosha vya maji kuweza kutosheleza mahitaji ya Watanzania wote kwa kipindi chote cha mwaka; vyanzo hivyo ni maji yaliyo juu ya uso wa ardhi na yaliyo chini ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya maji kwa nchi yetu kwa takwimu za mwaka 2002 yalikadiriwa kuwa ni mita za ujazo milioni 5,142. Kati ya hizo, kilimo kilitumia mita za ujazo milioni 4,624 (karibu asilimia 90 ya maji yote), kati ya ujazo huo, mita za ujazo milioni 4,417 zilitumika kwa umwagiliaji na mita za ujazo milioni 207 kwa ajili ya mifugo, kiasi kilichobaki cha mita za ujazo milioni 493 ndicho kilitumika kwa matumizi ya viwandani na majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa maji umefikia mita za ujazo 304,443 kwa siku kwa mwaka 2011, japokuwa mahitaji ya maji ni mita za ujazo 468,051 kwa siku. Hii maana yake ni kuwa kuna upungufu wa uzalishaji wa maji kulingana na mahitaji ya kiasi kinachohitajika kwa matumizi kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Sekta ya Maji katika Pato la Taifa kwa mwaka 2011 ulipungua na kuwa asilimia 0.3 kulinganisha na asilimia 0.4 kwa mwaka 2010. Hii maana yake ni kwamba, shughuli nyingi za uzalishaji zinazotegemea maji ili kutoa tija, zilishindwa kuzalisha kwa kadiri ya uwezo wake kutokana na sababu mbalimbali nyingine zikiwa ni ukosefu wa mipango na mikakati thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa fedha za ndani katika Bajeti ya Maendeleo kwenye Sekta ya Maji kwa kipindi cha miaka minne (2007 hadi 2011), takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2005/2006 mchango wa fedha za ndani kwenye Bajeti ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ilikuwa asilimia 57 na mwaka 2008/2009 ikawa asilimia 33 na kwa bajeti ya 2011/2012 ilikuwa ni asilimia kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka huku kwa mchango wa Serikali kwenye fedha za maendeleo ya miradi ya maji maana yake ni kuwa jukumu la msingi la Serikali kuwahudumia wananchi wake katika kupata huduma za msingi na hasa maji linaelekea kuishinda Serikali kadiri siku zinavyozidi kwenda. Jambo hili linapelekea Serikali kukosa uhalali wa kuendelea kuongoza nchi hii kama inashindwa kutekeleza wajibu wake wa msingi kama huu ilhali wakijua kuwa maji ni uhai na kama hakuna maji hakuna maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali itoe sababu za kina na za kimsingi ni kwa nini haitilii maanani upatikanaji wa maji na hasa kwa kutenga fedha zetu za ndani za kutosha kwa ajili ya kuhudumia wananchi wetu na kuondoa tatizo la akina mama kuhangaika usiku na mchana kutafuta maji na kuacha kufanya shughuli nyingine za kuongeza uzalishaji. Aidha, tunaitaka Serikali kuwasilisha mpango mahususi wa kutatua kero ya maji hasa vijijini ili tuweze kupunguza umaskini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa hata fedha zinazotolewa na wadau wa

maendeleo toka nje katika kutekeleza Programu ya Maendelelo ya Sekta ya Maji *(WSDP),* kwa mwaka 2011 hadi Juni, takriban asilimia 62 ya fedha zote walizoahidi zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kutoa usawia wa Miradi ya Maji nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti mbalimbali zinaonesha kutokuwepo kwa usawa kwa Serikali katika ugawaji wa fedha hizo kwa Miradi ya Maji Safi na Salama kati ya maeneo ya mijini na vijijini. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mgawo kwa maeneo ya vijijini ni asilimia 36 ya fedha zote na maeneo ya mijini ni asilimia 64 ya fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake ni kuwa, kila shilingi mia moja zilizotolewa na wafadhili kwa ajili ya Miradi ya Maji maeneo ya vijijini, yalipata mgawo wa shilingi 36 ilhali maeneo ya mijini walipewa mgawo wa shilingi 64. Hii ni pamoja na ukweli kwamba, katika nchi yetu Watanzania waishio vijijini ni takriban asilimia 77.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi kuhusiana na fedha zilizotengwa siyo njema na hasa kutokana na ukweli kuwa, Wananchi wengi waishio katika mikoa yenye ukame ni wafugaji na asilimia kubwa ya mifugo ipo vijijini. Mifugo hiyo inahitaji maji ya kunywa ya wastani wa lita 25 kwa ng’ombe wa kawaida kwa siku. Ili kuhakikisha kuwa mifugo inapata maji ipasavyo, Sera ya Maji inaelekeza kujenga mabwawa makubwa na madogo au kuchimba visima virefu na vifupi katika maeneo ya wafugaji na usanifu wa Miradi yote ya Maji Vijijini uzingatie mahitaji ya mifugo. Kambi ya Upinzani

tunahoji kutokana na mgawo wa aina hii ni lini tatizo la maji vijijini litamalizika? Kuna mkakati gani wa kumaliza tatizo la maji vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sheria inayolinda rasilimali za maji, inayohusu Usimamizi wa Rasilimali za Maji *(The Water Resources Management Act* Na. 11 ya Mwaka 2009), inahusika na usimamizi wa rasilimali za maji; vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi. Imetungwa na Bunge tarehe 28 Aprili 2009, imesainiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 12 Mei 2009 na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Agosti 2009 baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (*GN 235* la tarehe 10 Julai 2009).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria ya Utunzaji wa Rasilimali za Maji, Matumizi ya Maji Chini ya Ardhi kinasema kuwa: *"Endapo katika ardhi anayoishi mtu kihalali yatapatikana maji chini ya ardhi, ataruhusiwa kujenga kisima cha mkono kwa ajili ya kutumia maji kwa matumizi ya nyumbani bila kuwa na kibali cha kutumia maji kwa viwango vya uchimbaji vitakavyotangazwa katika Kanuni zinazoidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya Maji."*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu cha 54 (1) kinasema kuwa: *"Mtu yeyote anayetarajia kujenga, kuchimba, kuongeza ukubwa au kina cha kisima katika eneo lililotangazwa kuwa la hifadhi ya maji chini ya ardhi, anapaswa aombe kibali cha maji chini ya ardhi. Maombi ya kibali cha maji ya chini ya ardhi yatachukuliwa kama ni maombi ya matumizi ya maji*

*yatakayochukuliwa kutoka kwenye kisima husika na kwamba Bodi ya Maji ya Bonde ina mamlaka ya kufanya ukaguzi, kifungu cha 54(2) na (3).”*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa vipo viwanda na makampuni mbalimbali ambao wameamua kuchimba visima virefu na vifupi kwa ajili ya kupata maji kwa matumizi ya shughuli mbalimbali kwenye viwanda na makampuni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni kwa vipi inadhibiti matumizi ya maji ya chini ya ardhi na kupata mapato stahiki kutoka kwenye viwanda vikubwa kama vile kiwanda cha bia, kiwanda cha sigara, kiwanda cha kibuku, kiwanda cha cement, kiwanda cha mafuta ya kupikia, viwanda vya nguo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyote tajwa hapo juu vimechimba visima vya maji kwa ajili ya matumizi ya viwanda vyao na wachimbaji wa visima binafsi wanaongezeka kwa kadiri mahitaji ya maji kwa matumizi ya majumbani na viwandani yanavyozidi kuwa shida hasa maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuatilia kwa makini uchimbaji huu wa visima na kuhakikisha kuwa fedha ambazo wamiliki binafsi wa visima wanatakiwa kulipa walipe na visima hivyo viwe chini ya uangalizi wa mamlaka husika, kwa lengo la kuzia usababishwaji visima hivyo vya maji safi na salama kutokubadilika na kuwa na maji yasiyokuwa

na ubora kwa mujibu wa Sheria na Viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yatokayo ardhini kwa matumizi ya nyumbani kwa maeneo yote ya mijini na vijijini yanakadiriwa kuwa mita za ujazo 755,000 kwa siku (asilimia 60 ya matumizi yote), wakati mahitaji ni ni mita za ujazo milioni 0.8 hadi 3.4 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, umwagiliaji kwenye mashamba ya miwa, maua, matunda, hutumia mita za ujazo 130,000 kwa siku (asilimia kumi), wakati matumizi ya viwandani na migodini hutumia takriban mita za ujazo 30,000 kwa siku (asilimia mbili). Mifugo na matumizi mengine kama vile ufugaji wa samaki kwenye maeneo yasiyo na maji hutumia mita za ujazo 350,000 kwa siku (asilimia 28). Matumizi ya jumla kwa maji yatokayo ardhini yanakadiriwa kuwa mita za ujazo milioni 1.265 kwa siku, ambayo ni sawa na asilimia 12 ya rasilimali yote ya maji ya ardhini ya mita za ujazo milioni 11 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya maji ya ardhini kwa uzalishaji viwandani yamejikita zaidi kwa maeneo ya mijini hasa Dar es Salaam, ambapo takriban asilimia 80 ya viwanda vyote nchini vipo. Matumizi haya ya maji ya ardhini kwa viwanda yanatokana na kushindwa kwa mamlaka inayotoa huduma hiyo kwa Mkoa wa Dar es Salaam kutoa maji ya kutosha kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kiasi gani cha fedha

kinashindwa kukusanywa kutokana na viwanda kuchimba visima vyao binafsi na hivyo kuacha kutumia maji ya *DAWASCO?* Je, matumizi ya maji haya yanayofanywa na viwanda ni endelevu kwa Sekta ya Maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2011 sekta ya maji ilishuka kwa kiwango cha asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2010. Hata hivyo, mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 0.4 mwaka 2010 hadi asilimia 0.3 mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011, Sura ya 18, ukurasa wa 245, inaonesha kuwa uzalishaji wa maji mijini kwa mwaka 2011 ulipungua hadi kufikia mita za ujazo milioni 116.45 kutoka mita za ujazo milioni 116.55 kwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, upungufu huu unasababishwa na kuwepo kwa miundombinu chakavu kwa ajili ya usambazaji wa maji mijini na hasa kutokana na kukaa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au ukarabati na hivyo kusababisha upotevu mwingi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa za Serikali ni kuwa, Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika Miji Mikuu ya Mikoa hutoa huduma ya maji bila gharama kwa kaya zisizokuwa na uwezo kwa kuzisaidia lita 160 kwa siku, sawa na lita 5,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Maji kwenye Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru inaonesha kuwa hadi sasa jumla ya kaya 1,466 zinapata huduma ya maji bure kutoka Mamlaka za Maji katika miji mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka ipate majibu kuhusiana na maswali yafuatayo:-

(i) Je, ni katika Miji gani huduma hii hutolewa na ni utaratibu gani unaotumika katika kuzitambua kaya hizo?

(ii) Je, ni utaratibu gani unaopaswa kufuatwa na kaya husika ili wananchi waweze kufuatilia na kupata huduma hii?

(iii) Je, ni kwa nini kaya maskini za vijijini zinasahaulika kutokana na kukosekana kwa utaratibu kama huu na ikizingatiwa kuwa kiwango cha umaskini ni kikubwa zaidi vijijini kuliko mijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Visima Virefu Kimbiji na Mpera: Kwa mwaka uliopita Serikali ililieleza Bunge kuwa tayari imekwishatoa fidia kwa wananchi kwa maeneo ya kuchimba visima virefu 20 vya uzalishaji wa maji wa kutoa mita za ujazo 260,000 kwa siku, kwenye maeneo ya Kimbiji na Mpera kwa ajili ya kusambaza maji Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kwa Mwaka wa Fedha uliopita (2011/2012) Mpango huo ulitakiwa

kutengewa kiasi cha shilingi bilioni 22.4 na Mwaka huu wa Fedha (2012/2013) Mradi huo ulitakiwa kutengewa kiasi cha shilingi bilioni 39.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizopo kwenye randama zinaonesha kuwa bajeti iliyopangwa kwa Mradi huo kwa mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni moja kama fedha za ndani na shilingi bilioni 29.992 kama fedha za nje. Tofauti ya fedha zilizopangwa katika Mpango wa Miaka Mitano kwa Mradi huo na Bajeti iliyotengwa ni shilingi bilioni 9.208.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa tofauti hiyo ni kubwa kiasi kwamba inaweza kukwamisha utekelezaji wa mradi huu na ni kinyume cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na hivyo wananchi watachelewa kupata huduma ya maji safi katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, fedha nyingi zilizotengwa ni za nje na kwa uzoefu wetu katika Miradi mbalimbali iliyokuwa inategemea fedha kutoka nje imekwama kukamilika kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Bwawa la Kidunda: Serikali haioneshi kuwa ina nia ya dhati ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliopitishwa na Bunge hili, kwani Mpango wa Maendeleo unaelekeza kuwa kwa mwaka huu wa fedha, zitengwe shilingi billioni 46 kwa ajili ya Mradi huu lakini kwa mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 3.398 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.824 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani tunataka maelezo ya kina kuhusiana na Mradi huu na hasa ikizingatiwa kuwa fedha zinazopaswa kutengwa ni nyingi ila zilizotengwa ni kidogo sana na ni dhahiri kuwa Serikali haina nia ya dhati ya kuutekeleza Mradi huu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, jumla ya mabwawa 568 tu yalijengwa sehemu mbalimbali nchini tangu Uhuru mpaka mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dar es Salaam unapata maji kutoka mito na visima kwa matumizi ya nyumbani, viwandani, bustanini, mifugo, usafi na mazingira. Eneo kubwa linalopata maji linahudumiwa na Kampuni ya *Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Company (DAWASCO).* Maeneo yasiyo na mtandao wa *DAWASA* hupata maji kutoka visima vinavyoendeshwa na vyombo vya watumia maji, taasisi na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vikuu vya maji ni mitambo ya Ruvu Juu, Ruvu Chini, Mtoni na visima virefu 1,100 na vifupi 238 vilivyopo katika Mkoa. Vyanzo vyote hivi huzalisha lita milioni 353 kwa siku wakati Jiji lina mahitaji ya lita milioni 469.3 kwa siku, ambapo ni sawa na upungufu wa lita milioni 116 kwa siku. Aidha, kuna maji ambayo yanapotea wakati wa usambazaji yakiwa njiani kutokana na uchakavu wa mitambo na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazoathiri utoaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ni pamoja na uzalishaji mdogo wa maji ukilinganisha na mahitaji, uhaba wa vyanzo vya maji, ubadhirifu, uwezo

mdogo wa watumia maji kulipia gharama na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji maji ambayo husababisha upotevu mkubwa sana wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo, Jiji huwa na ukosefu mkubwa wa maji na Kitaifa ni Jiji la mwisho kwa upatikanaji wa maji hapa nchini, kwani ni asilimia 55 tu ya Wakazi wa Jiji ambao wanapata maji ikilinganishwa na Majiji na Miji mingine nchini ambayo wastani wake ni asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2003 mpaka 2010, Serikali ilitekeleza Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka Jijini Dar es Salaam na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha *(Dar es salaam Water Supply and Sanitation Project - DWSSP*), uliotumia dola milioni 164.6. Hata hivyo, mpaka sasa katika maeneo mengi mtandao wake maarufu kama Mabomba ya Wachina hautoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya utoaji wa huduma ya maji Jijini Dar es Salaam yanahusu pia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka *(DAWASA),* ambayo ni mmiliki, mkodishaji na msimamizi wa utoaji wa huduma ya majisafi na majitaka katika Jiji la Dar es Salaam kwenye wajibu wa kupanga na kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu, kuiendeleza na kugharamia matengenezo ya dharura na makubwa.

Kambi ya Upinzani, tunaitaka serikali itoe majibu kuhusiana na mambo yafuatayo:-

(i) Kuna mkakati gani wa kuhakikisha kuwa maji yanapatikana kwa Wananchi wa Jiji la Dar es Salaam na hasa kwenye maeneo ya ujenzi wa makazi mapya kama vile Kimara, Changanyikeni, Msakuzi, Mbezi, Kigamboni, Kilungule, Tabata, Kinyerezi na kwingineko?

(ii) Kuna mpango gani wa kuhakikisha kuwa maji yanayozalishwa hayapotei yakiwa njiani na hasa kutokana na uchakavu wa miundombinu ya maji?

(iii) Wizara itakamilisha lini Miradi ya Maji iliyopangwa kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa maji Jijini?

(iv) Serikali iwasilishe Bungeni Mpango Maalum wa kuboresha huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam uliopitishwa mwezi Machi 2011 kwa ajili ya kuidhinishwa, kutengewa bajeti ya utekelezaji wa haraka katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na kusimamiwa.

(v) Mpango wa dharura wa kupunguza kero ya maji ulianza kutekelezwa na Wizara ya Maji kwa kushirikiana na *DAWASA* kuanzia Juni 2010, unaohusisha uchimbaji wa visima 24, uliopaswa kukamilika Oktoba 2011, uwekewe muda wa ukomo wa kukamilika kuwa Oktoba 2012 katika maeneo ambayo Miradi haijakamilika mpaka hivi sasa.

(vi) Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* afanye ukaguzi wa thamani ukilinganisha na ufanisi *(Value for Money)* wa Mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya Majisafi na Majitaka Jijini Dar es

Salaam na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha (*Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Project - DWSSP)* kwa kurejea ukaguzi wa kiufundi *(Technical Audit)* uliofanywa na Kampuni ya *Howard Humphreys.*

(vii) *EWURA* ifanye ukaguzi wa kiufanisi *(Performance Audit)* wa Miradi ya Visima vya Maji takriban 200 ambavyo vilichimbwa na Serikali na kukabidhiwa kwa *DAWASCO,* Jumuiya za Wananchi na Taasisi mbalimbali lakini haitoi huduma inavyostahili kwa kadiri ya malengo ya awali. Aidha, *EWURA* iharakishe kutunga kanuni za udhibiti wa ubora na bei ya huduma ya maji kwa upande wa Sekta Binafsi katika Jiji la Dar es Salaam.

(viii) Serikali ieleze imefikia hatua gani katika kutekeleza mapendekezo ya taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu usimamizi wa usambazaji wa maji katika maeneo ya mijini *(Performance Audit Report on the Management of Water Distribution in Urban Areas)* ya Januari 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jiji la Dar es Salaam miaka ya hivi karibuni kumejitokeza na kushamiri tabia ya wananchi kuharibu na kuiba miundombinu ya Miradi ya Maji na kuiuza kama chuma chakavu. Vifaa vinavyoibwa sana ni mifuniko ya mashimo ya maji taka, mabomba ya maji, mita za maji na vifaa vinginevyo.

Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa Serikali inafahamu kunakouzwa vyuma hivi chakavu kwa kuwa ndiyo imetoa leseni kwa biashara hii. Tunataka

kuwachukulia hatua wale wote ambao wanafanya biashara hii ya kuhujumu miundombinu yetu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya uondoaji wa majitaka Jijjini Dar es Salaam si ya kuridhisha kutokana na uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali katika eneo hili. Hadi sasa ni asilimia 18 tu ya wakazi mijini ndiyo wameunganishwa kwenye huduma hii. Jambo hili limewafanya wakazi wengi wa mijini kutumia vyoo vya mashimo, makaro *(septic tanks)* na vyoo vya shimo ambavyo huchangia uchafuzi wa maji yaliyoko chini ya ardhi. Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali ihakikishe kuwa inawekeza vya kutosha ili kuweza kukabiliana na hali hii na hasa ikizingatiwa kuwa kama hatua zitachelewa kuchukuliwa, uchafuzi huu utaendelea kuathiri wananchi kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa majisafi na majitaka katika Jiji la Dar es Salaam,uchakavu wa miundombinu kutokana na mabomba kutokarabatiwa ipasavyo pamoja na uharibifu katika mitandao ya maji wa kujiunganishia kinyemela na kiholela, umesababisha ongezeko kubwa la upotevu wa maji mpaka kufikia kati ya asilimia 40 hadi 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imesababisha ongezeko kubwa la bei ya maji kwa wananchi wa kipato cha chini wanaotegemea kupata maji kutoka sekta binafsi ambapo wanaonunua maji kwa madumu hununua bei ambayo ni takriban mara 15 ya bei ya mteja anayepata huduma ya maji ya bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa uondoaji wa maji taka ni chini ya asilimia kumi tu ya makazi ndiyo yaliyounganishwa na hivyo kuleta uchafuzi wa mazingira hususan katika maeneo yasiyopimwa. Hata katika maeneo yaliyopimwa Jijini Dar es Salaam, mitandao ya majitaka haijakarabatiwa na kupanuliwa licha ya ongezeko kubwa la watu. Kampuni ya Majisafi na Majitaka *(DAWASCO)* ambayo ni mwendeshaji mwenye wajibu wa kuendesha shughuli za kutoa huduma ya maji, kutoa ankara kwa wateja, kukusanya maduhuli, kutekeleza matengenezo makubwa yanayogharamiwa na *DAWASA* na kutekeleza uunganishaji wa maji kwa wateja wapya kwa kutumia mfuko wa maji. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iongeze mtandao wa majisafi na majitaka hasa kwa maeneo mapya kama tulivyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Miradi inayochangiwa na nchi wahisani iliyotolewa Juni 2011, Sura ya 3, ukurasa wa 13 - 15 inaonesha fedha zilizotolewa na Serikali pamoja na Nchi Washirika wa Maendeleo zilikuwa jumla ya shilingi 226,913,350,139 kwa ajili ya Miradi ya Maji. Aidha, katika Programu hiyo ilikuwa na bakaa ya shilingi 68,332,741,760 na hivyo kufanya mwaka huo wa fedha kuwa na jumla ya shilingi 295,246,091,899 na hadi kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha kulikuwa na fedha zisizotumika kiasi cha shilingi 72,582,156,680.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 vitabu vya Halmashauri mbalimbali vilikuwa vinaonesha kuwa kiasi cha shilingi 32,240,623,989.47

zilikuwa kama bakaa ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 58 ya fedha za Miradi ya Maji. Kwa maoni ya Mkaguzi, kiasi hiki kikubwa ni kutokana na kushindwa kwa Halimashauri kutekeleza Miradi ya Maji kwa mujibu wa mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kwa nini fedha hizi zinashindwa kutumika wakati tatizo la maji ni kubwa mno kwa wananchi. Mfano ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, ambayo miaka yote toka enzi za *(Mhe Simpasa, Luka Siyamena sasa Mhe.Godfrey Zambi na Mhe. David Silinde),* imekuwa na tatizo kubwa la maji, lakini takwimu zinaonesha kuwa Halmashauri ilishindwa kutekeleza mpango wake wa miradi ya maji na mwisho wa mwaka wa fedha ilibakiza fedha za miradi ya maji kiasi cha shilingi milioni 865.7. Hizi ni fedha nyingi kwa wananchi ambao wana tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kama hili lilizikumba Halmashauri za Wilaya ya Karagwe, Kondoa, Musoma, Mbeya Vijijini, Ngorongoro, Iringa, Meatu, Temeke na Ilala, ambazo ziliacha kiasi kikubwa sana cha fedha bila kutumika. Aidha, Halimashauri ya Wilaya ya Iramba ilishindwa kutekeleza Miradi ya Maji kwa kipindi hicho na kubakiza fedha kiasi cha shilingi 894,376,237.15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa hizi ni dhahiri kuwa Miradi mingi ya Maji imekuwa ikishindwa kutekelezwa na fedha nyingi kubakia bila kutumika ilhali wananchi wetu wakiteseka kutafuta huduma za maji.

Kambi ya Upinzani, tunataka maelezo ya kina kuhusiana na fedha hizi kutokutumika ni sababu gani zilipelekea hali hiyo kujitokeza? Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa Miradi hii inatekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na taarifa mbalimbali za migogoro baina ya wananchi na wakala mbalimbali wa usambazaji maji kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini na hali hiyo imetokana na ama wananchi kutokuhusishwa kwenye kupanga bei mpya za maji au huduma kuwa chini ya kiwango ilhali wananchi wakiwa wanapaswa kulipia huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 29 Oktoba 2011, Wananchi wa Mbalizi walifunga Ofisi za Mamlaka ya Majisafi Mbalizi kutokana na huduma wanayopata kuwa duni. Vilevile Mradi wa Maji ni wao na hivyo walipaswa kuuendesha Mradi wao wenyewe, bei ya maji ya shilingi 10,000 kwa mwezi ni kubwa na walitaka ipungue hadi shilingi 7,000 kwa mwezi na Meneja wa Mamlaka na Mafundi hawatakiwi kuonekana ofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na madai ya wananchi hawa kuwa sahihi, Mkuu wa Wilaya aliitisha mkutano wa hadhara mnamo tarehe 9 Novemba 2011 na kuzungumza na wananchi hao lakini walimweleza wazi kuwa hawatakuwa tayari kufungua ofisi kama madai yao ya msingi hayatapata ufumbuzi na hadi anaondoka kwenye mkutano huo walikuwa hawajakubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walikubali kufungua ofisi hizo mnamo tarehe 17 Novemba 2011 na hii ni baada ya madai yao kukubaliwa ikiwemo Meneja wa Mamlaka aliyekuwepo kuhamishiwa Kituo chake cha awali cha kazi Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri na baadhi ya mafundi waliokuwa wanalalamikiwa kusimamishwa kazi na Bodi Mpya ya Mamlaka kuundwa ikiwa na Wajumbe saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mtafaruku huu, uliipelekea Mamlaka ya Maji Mbeya kuzuia huduma ya maji kwa Wananchi wa Mbalizi na hivyo kuwafanya Wananchi kukosa huduma ya maji kwa muda mrefu tangu mwezi Oktoba 2011 hadi mwezi Juni mwaka huu ilikuwa haijarejeshwa. Aidha, tunataka kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya Meneja na Mafundi wote ambao walikuwa wanalalamikiwa na wananchi na ni lini huduma hii ya maji itarejeshwa katika Mji wa Mbalizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma unatoa huduma ya maji kwa kutumia teknolojia mbalimbali, kwa mfano, kusukuma maji kwa mashine, chemchemi, skimu za maji ya mtiririko, visima vifupi na virefu vyenye pampu za mkono, pamoja na uvunaji maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosekanaji wa mita hususan kwa Wakazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji: Mamlaka ya Maji Mkoani Kigoma imeshindwa kutekeleza kabisa maagizo ya *EWURA* ya kutaka wananchi wapewe mita ili waweze kujua wanatumia

maji kiasi gani na kulipa kulingana na kiasi cha maji wanayotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameshindwa kujibu barua aliyoandikiwa na Manispaa baada ya kumteua Diwani mmoja ili awe Mjumbe wa Bodi ya Maji na Mwakilishi wa Wananchi katika Bodi hiyo lakini mpaka dakika hii Waziri hajajibu. Kwa hiyo, Idara ya Maji inapanga gharama za maji inavyotaka, ilianza na shilingi 5,200 ikaenda shilingi 17,500 hadi shilingi 19,500 na sasa wanataka kupandisha ankara hadi shilingi 23,000 kwa mwezi. Huku ni kuwakomoa Watu wa Kigoma. Huu ni udhalilishaji na dharau kwa Wananchi na Wakazi wa Mkoa wa Kigoma. Mpaka sasa hatua zilizochukuliwa ni kwamba, Wenyeviti wa Mitaa 68 wamechanga pesa kwa ajili ya kuishtaki Bodi ya Maji ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina juu ya utaratibu wa kupandisha bei za maji bila kuwashirikisha wadau ambao ni wananchi, kwani huku ni kwenda kinyume na Sera ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro katika Miradi ya Maji ya Wananchi haipo tu maeneo ya vijijini bali pia katika maeneo ya mijini ikiwemo katika Jiji la Dar es Salaam. Mfano wa migogoro hiyo ni wa Mradi wa Wananchi wanaotumia maji katika Kata ya Goba uliodumu kwa zaidi ya miaka mitano na kusababisha wananchi kukosa huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya matatizo hayo ni pamoja na uendeshaji mbovu wa Mradi wa Maji chini ya Kamati za Maji unaosababisha kuibuka kwa tuhuma za mara kwa mara za ufisadi, malimbikizo ya madeni na kuharibika kwa miundombinu. Aidha, chanzo kingine kikubwa ni uwezo mdogo wa Miradi hiyo ya Maji ukilinganisha na ongezeko la idadi ya watu katika Mitaa ya Kata hiyo ambayo awali ilikuwa vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kushughulikia kasoro hizo, tarehe 24 Oktoba 2011, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni aliandikiwa barua ili achukue hatua za dharura kutatua mgogoro huo na kuwezesha wananchi kupata huduma ya maji. Taarifa ya suala hilo ilifikishwa Wizara ya Maji, hata hivyo, mgogoro huo umedumu mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Maji kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni kuchukua hatua za haraka kufuatilia kwa dharura kuhakikisha maji yanarejeshwa Goba. Hatua hii iende sambamba na kupanua wigo wa maji Goba kwa kutekeleza kwa haraka upatikanaji wa maji kutoka pia Mradi wa Maji toka Madale Kisauke. Wizara ya Maji ishirikiane na Manispaa kuhakikisha matatizo yaliyopo yanatatuliwa kwenye Miradi ya Maji inayoendeshwa na Manispaa pamoja na Kamati za Wananchi au Vyama vya Watumia Maji katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina vyanzo vikuu vya maji ambavyo ni mito mikubwa, maziwa, chemchemi na maji chini ya ardhi. Maji ya vyanzo

hivyo ndiyo yatumikayo majumbani, viwandani, mashambani na kwa ajili ya mifugo. Maji yanayotumika toka Ziwa Viktoria kwa kiasi kikubwa yanachafuka kutokana na viwanda kama vya kusindika kahawa, pamba, mafuta ya kula na viwanda vya sabuni na manukato, bila kusahau viwanda vya samaki, ambapo uchafu toka viwanda hivyo huelekezwa ziwani au kwenye mito ambayo inaingiza maji yake ziwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya madawa ya kuchenjulia dhahabu yanayotumiwa na wachimbaji wadogo kwenye mito ambayo wakati wa masika maji hutiririka hadi Ziwa Viktoria na mahali pengine kwenye mito mikubwa ambayo ni vyanzo vya maji ambayo maji yake yanatumika kwa matumizi ya majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha matumizi ya mbolea na madawa ya viwandani kinachoendeshwa katika maeneo yaliyo karibu na vyanzo vikuu vya maji ni mojawapo ya vyanzo vya uchafuzi mkubwa wa vyanzo vyetu muhimu vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uvamizi wa vyanzo vya maji na uharibifu wa mazingira, vipo vyanzo vya maji ambavyo vilikauka, kupungua maji na vingine kuchafuka na kutokufaa kama vile Ziwa Chala, Ziwa Jipe, Mto Umba na Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali katika hili la matumizi ya mbolea za viwandani, katika uchafuzi wa vyanzo vya maji, suluhu ya hilo ni kuingia katika matumizi ya mbolea za asili

kama vile mboji au mbolea za marejea na mimea kama hiyo hasa kwa wakulima ambao wanafanya shughuli zao karibu na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunaitaka Serikali iweke mkakati mahususi wa kuhakikisha kuwa vyanzo vya maji vinalindwa kikamilifu dhidi ya uchafuzi wowote na kama ikitokea viwanda vinahusika basi Sheria ya Mazingira itumike ili wahusika wawajibishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni hayo, kwa niaba Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ninashukuru sana. Wachangiaji niliokuwa nimewaorodhesha mwanzo siwaoni. Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyogera na Mheshimiwa Sylvester Kasulambayi ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuweza kusimama hapa kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Bukene na mimi nitoe mchango wangu katika Hotuba hii ya Wizara ya Maji. Maji nchini kwetu bado ni tatizo, nichukue fursa hii ya kwanza, niipongeze Serikali kwa kutambua umuhimu wa maji na kuhakikisha kwamba, wameweka katika vipaumbele vikubwa vitano. Ukiangalia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika vipaumbele vikubwa vitano maji ni kimojawapo; kwa hiyo, hii ni ishara kwamba, Serikali imetambua umuhimu wa maji katika mchango wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, ukisoma Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Hotuba ya Wizara ya Maji, takwimu zinaonesha kwamba, upatikanaji wa maji safi katika maeneo ya vijijini ni asilimia 57. Mimi kwa mtazamo wangu asilimia hii ni wastani wa jumla sana, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo upatikanaji wa maji safi, kwa mfano Jimboni kwangu Bukene, asilimia kubwa ya Jimbo langu ni maeneo ya vijijini, karibu asilimia 100 ni vijiji, ukienda kule ukaangalia upatikanaji wa maji safi katika Vijiji vya Jimbo la Bukene na ukisema kwamba upatikanaji wa maji vijiji ni asilimia 57, kwa kweli asilimia haioneshi hali halisi ya upatikanaji wa maji katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Bukene ukienda katika maeneo ya Kata ya Semembela, kwa mfano, maji ni tatizo kwa sababu asilimia 57 ni zaidi ya nusu, yaani maana yake katika kila watu 100 watu 57 wanapata maji safi. Hali ilivyo katika maeneo mengi ya Vijiji vya Jimbo la Bukene siyo kweli kwamba, katika kila watu 100 watu 57 wanapata maji safi. Kwa hiyo, kusema kwamba asilimia 57 ya watu ndiyo wanaopata maji safi katika maeneo ya vijiji ni ya jumla mno. Rai yangu ni kwamba, tufike mahali sasa tuanze kwenda kutoa asilimia kwa maeneo husika; kwamba, kwa kuwa ninafahamu hii ni wastani wa jumla lakini wakati mwingine inaweza isitoe picha halisi na ikaifanya Serikali isielekeze nguvu mahususi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kuna maeneo mengine ambayo upatikanaji wa maji uko juu

ya asilimia 57 lakini maeneo mengine kama Jimbo langu la Bukene ni chini ya hapo, pengine hata asilimia 30 au asilimia 20. Tukilitambua hilo, tutaiwezesha Serikali kuelekeza nguvu nyingi za maji katika maeneo ambayo kweli yana shida ya maji na kwamba maji bado ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie visima vya maji ambavyo vinafadhiliwa na Benki ya Dunia. Visima hivi vimeanza kuzungumzwa miaka kadhaa kiasi kwamba wananchi wengi maeneo mengi ikiwemo Wilaya ya Nzega, ukizungumzia visima hivi, kwa sababu vimezungumzwa miaka kadhaa, wanaanza kuona ni hadithi zilezile. Niseme tu kwamba, mwaka jana ilifanyika kazi ya awali ya kuvichimba ili kuona kama maji yapo katika vijiji kumi ambavyo vilikuwa vimeainishwa. Katika vijiji kumi vya Wilaya ya Nzega, karibu vijiji tisa vilionekana kwamba maji yapo na yanatosha kuchimbwa na kusambazwa kwa watu ili wayatumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika Vitabu hivi vya Bajeti vilivyotolewa leo katika Hotuba ya Waziri wa Maji kwamba, katika vile vijiji kumi, vijiji vitano mwaka huu kwa sababu vimeshachimbwa na kuonekana maji yapo, sasa kazi ya kuanza kujenga miundombinu kwa maana ya kujenga matanki, kwa maana ya kulaza mabomba na kujenga magati kwa ajili ya kutolea maji, sasa katika bajeti hii kazi hiyo inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwamba kazi hiyo itafanyika katika Wilaya ya Nzega katika Kisima

cha Sigili ambako tanki litajengwa, mifereji italazwa na magati yatajengwa. Katika Kisima cha Ikindwa, tanki litajengwa, mabomba yatalazwa na magati yatajengwa. Katika Kisima cha Mahene na Buhondo ambavyo vyote vipo katika Kata ya Mwamala ndani ya Jimbo la Bukene, matanki yatajengwa, mabomba yatalazwa na magati yatajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kwamba, kazi hizi safari hii zifanyike zifike mwisho, watu katika maeneo haya waanze kunywa maji haya ambayo yanafadhiliwa na Benki ya Dunia, ambayo kwa kipindi kirefu imekuwa ni kama hadithi na watu wameanza kupoteza matumaini. Kwa hiyo, sasa ifike mwisho na watu waanze kuyanywa haya maji na waone Serikali ya CCM ilichokuwa inaahidi kweli imekitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia Mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyafikisha Tabora Mjini. Hii ni ahadi ya Rais. Rais wakati anapita kuomba kura za wananchi hasa katika Mkoa wa Tabora, moja ya ahadi zake kubwa ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, ifikapo mwaka 2015, wakati kipindi chake cha Uongozi kinaisha, watu wa Tabora Mjini wanywe maji ya kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika Mpango huu kwamba, Wizara ya Maji imepanga fedha ambazo sasa upembuzi yakinifu utafanyika, lakini tumebakiza miaka miwili tu hadi kufikia mwaka 2015.  Kwa hiyo, ili hili litendeke kweli ni lazima hiyo kazi ya upembuzi yakinifu mwaka huu ifanyike kikamilifu ili mwaka 2013/2014 uwe mwaka wa kujenga.  Tukifika mwisho

wa mwaka tukaambiwa fedha hazikupatikana kwa hiyo upembuzi haukufanyika, maana yake 2014 ndiyo utafanyika, utakapofanyika ni mwaka hakutakuwa na muda wa kujenga tena. Kwa hiyo, tutajikuta mwaka 2015 tumefika Tabora Mjini hawajanywa maji na ahadi ya Rais haijatekelezeka. Mimi kama Mbunge wa CCM, sitaki ahadi ya Rais wangu wa CCM ishindwe kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Maji kwamba, katika mambo muhimu ni hii ya kuhakikisha Mradi huo mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Viktoria kufika Tabora Mjini unatekelezeka na Wananchi wa Tabora kweli wanakunywa maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Selemani Zedi. Mheshimiwa Kamishna Agripina Buyogera, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti kwa Taifa letu, Wizara ya Maji. Tumefundishwa tangu darasa la kwanza tukiwa watoto kwamba maji ni uhai na maji kweli ni uhai, ndiyo maana hata binadamu yeyote akiugua ni afadhali upungukiwe damu kuliko kupungukiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Watanzania walio wengi, tatizo la maji la Mradi wa Benki ya Dunia ni kero kubwa sana kwa Watanzania hususan sisi tulio vijijini. Ninaiomba Serikali kupitia Wizara ya Maji, wakati wa majumuisho ituambie ni lini Mradi huu utakamilika, pamoja na kutupa mchanganuo mzuri wa kutuonesha kila Mkoa na kila Wilaya imefikia hatua gani. Ni vizuri Serikali itamke ni lini tatizo hili la maji ya kupitia Mradi wa Benki ya Dunia utakamilika na iwe mwisho wa Wabunge kuendelea kuchangia vijiji hivi kumi kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika mchanganuo huu, ninaomba kutoka moyoni nimpongeze Injinia wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, amefanya kazi nzuri sana lakini mpaka leo tunaambiwa bado kuna tatizo la kibali. Hivi hiki kibali kinatoka nchi gani? Ninaomba Wizara ilichukue hili. Tumekwama mambo muhimu sana kwa sababu ya kukosa maji. Leo hii kuna vijiji ambavyo vilishakamilisha, vilichanga fedha hizi miaka mingi mpaka leo havijapata maji. Tuna Kijiji cha Kasangezi ambacho kilishakamilisha taratibu zote na pale katika Jimbo langu la Kasulu Vijijini, katika Kata 19, hatuna *high school* hata moja. Nina shule za sekondari 15, Kijiji cha Kasangezi tumekwama kufungua *High School* kwa kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri katika majumuisho yako baadaye mtujali mtupe fedha katika hivi vijiji tuweze kukamilisha huu Mradi ili Watanzania wa Kasulu waweze kupata mahitaji mbalimbali hususan yaliyokwamishwa kwa kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia tatizo la maji nimesema ni la Taifa zima, lakini ni kwa nini wataalam wetu hawawezi kufanya upembuzi yakinifu wa kulinganisha Mkoa hadi Mkoa ili pale ambapo pametofautiana kwa ukosefu wa maji, waweze kuangalia kwa kina kumaliza tatizo angalau mkoa mmoja baada ya mwingine tuweze kupunguza kelele za maji. Mfano, Mkoa wa Kigoma, tuna vyanzo vingi sana vya maji ikiwemo Ziwa Tanganyika, leo Ziwa Tanganyika liko pale, Ziwa la kwanza Afrika lenye kina kirefu cha maji, lakini Mkoa wa Kigoma hauna maji. Ukienda Kigoma Mjini yenyewe wananchi wanalilia maji kila siku; haiingii akilini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kasulu, Kibondo, Mto Malagarasi ni mkubwa sana kiasi ambacho mngeweza kuwekeza katika Mto ule kuandaa vile vyanzo kwa ajili ya kutuwezesha kupata maji, leo sisi tusingekuwa tunasimama hapa tunalia maji. Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine Viongozi wetu bado hawajawa na utashi wa kumaliza matatizo mengine ambayo yanawezekana kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaongea kwa sababu kama maji yaliweza kutoka Ziwa Victoria yakavutwa na Serikali yetu mpaka kwenda Kahama; inashindwaje kutafuta maji Ziwa Tanganyika kufika Kigoma Mjini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kasulu Vijijini, Mto Malagarasi tumepakana na Burundi. Mimi nikiwa nahutubia, Warundi wanakuja kunisikiliza hiyo

haipingiki. Pamoja na kwamba Mto Malagarasi upo katika Kijiji ambacho mimi Mbunge naenda kuhutubia na hakina maji, lakini Burundi ukivuka Warundi wanafua Mto Malagarasi, Watanzania wanafua Mto Malagarasi, Burundi kuna maji ya kutosha na Jimbo la Kasulu Vijijini hakuna maji ya kutosha; haiingii akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali yetu, hii ni Serikali ya Watanzania wote, siyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi wala nini, hii ni ninaomba ifike wakati sasa Viongozi wetu wawe na utashi kwa dhamira ya moyoni kabisa kusikiliza kero za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Tanzania tuna wataalam wazuri sana, leo namsifia Injinia wangu wa Kasulu ni mtaalam mzuri sana, lakini anafanya nini? Wizara haijamwezesha kupata fedha ili aweze kumaliza matatizo haya. Ninyi wenyewe mkiangalia kwenye mchanganuo mliotuletea hapa Kasulu imefanya vizuri, kwenye utafiti wa maji ya Vijiji kumi, lakini mpaka leo kibali tu hakuna; nitamlaumu Injinia?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba katika suala hili Viongozi tubadilike, tuwasimamie vizuri Watendaji wetu, tukubaliane na ushauri wao. Ninarudia tena kwamba, Tanzania tuna wataalam wazuri, wakati mwingine sisi wanasiasa ndiyo tunawachanganya. Wanapokaa kuratibu mambo yao vizuri, tunaleta mambo ya kisiasa, mambo ya itikadi za vyama, haiwezekani! Tuwatumie wataalam wetu vizuri kwa maslahi ya Watanzania wote bila kujali itikadi za vyama. Tufike mahali pale tunapopata dhamana, mimi

najua leo ni Mbunge ninawaongoza watu kesho nitaongozwa kwa sababu Taifa ni hili moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua muda hautoshi, lakini sipo tayari kugongewa kengele, naomba nisisitize tena kwamba Waziri wa Maji Bajeti hii uhakikishe vijiji hivyo vitano ulivyovipitisha Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu vinakamilika hususan Kijiji cha Kasangenzi ambacho tunategemea kufungua *high school* katika Jimbo langu la Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na Mungu akubariki sana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Agripina Buyogera. Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kaika Telele.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia mawazo yangu juu ya Bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 77 ya Watanzania wanaishi vijijini, hawa wanafikia karibu milioni thelathini na moja laki nane na tisa mia nane na nane. Ukiangalia watu hawa ambao ni wengi, wanajikuta wanapata asilimia ndogo sana ya huduma ya maji ukilinganisha na wenzao wanaoishi mjini ambao wapo asilimia 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linawapa tabu sana Watanzania hasa wanaoishi Vijijini ambao ndiyo wazalishaji na ndiyo tunaowategemea sana. Katika hali halisi nilitegemea kwamba, Wizara ingeweza kubadilisha mfumo iliouzoea wa kuendelea kuwaneemesha watu wa mijini na kuwafanya mafukara watu wa vijijini na matokeo yake vijana wetu vijijini wameamua nao kubanana kukaa mjini na hapo hapo Serikali inaanza kulalamika vijana hawazalishi, vijana wanang'ang'ania mijini na matokeo yake Serikali hii inaamua kuwahamisha na kuwaambia warudi kwao. Watarudi kwao wapi wakati mjini wanakula keki nzuri na kijijini watu wanaishi maisha mabaya? Unapotenga asilimia ndogo ya maji wakati ukijua maji ni uhai maana yake unataka kuwaambia vijana wetu wa vijijini waondoke vijijini waende mijini ambako kumeboreshwa.

Hii imesababisha pia wafugaji vijijini waweze kuamua kuhama kwenye maeneo kame hasa kwenye Mikoa ya Shinyanga, Maswa ikiwa sehemu mojawapo. Maeneo haya hayajarutubishwa vizuri na Serikali ambayo ndiyo inatakiwa ikusanye mapato lakini itoe huduma, matokeo yake wafugaji hawa imewaacha kama walivyo na matokeo yake wameamua kufuata maeneo ambayo yana maji na leo wafugaji hao wanaitwa wahamiaji haramu, lakini kumbe kilichosababisha ni huduma duni kwenye maeneo yao.

Kwa Serikali inayojiita sikivu ya Chama cha Mapinduzi, nilitarajia usikivu huo ungeelekezwa kwa wananchi hawa wanaoishi miaka hamsini na moja iliyopita katika maisha duni. Cha ajabu bajeti ya leo

imeonesha tena pia ina ubaguzi mkubwa; katika mazingira haya unatarajia nini? Tutapata wapi maendeleo? Kilimo kitaibuka lini kiongeze Pato la Taifa kama maji hayapatikani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano; Wasukuma ni watu wanaojituma sana katika kulima, hawahitaji kupigiwa kampeni, ukiwakuta wakati wa masika wakilima wanatumia hata ngoma utafikiri wanamuziki kumbe wanashughulika na kulima. Tatizo linalowakabili hawa ni maji yanapokosekana, mvua zinapogoma, matokeo yake wanajikuta wameingiwa na umaskini ambao wengine wanatafsiri kwamba watu hawa hawajitumi katika kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia Serikali yako inayojiita sikivu itaongeza bajeti ya maji kwenye Wizara ili wakulima hawa waweze kuneemeka na waweze kuondokana na umaskini. Mategemeo yangu yalikuwa ni hayo, cha ajabu Serikali imekuwa inajisifia ni sikivu, inawathamini wananchi, lakini matokeo yake inaenda kinyume. Labda ndiyo maana inaitwa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ukifikiria sana ndiyo umapinduzi wenyewe, kwa sababu kama kweli ingekuwa na lengo basi watu hawa wangekuwa wameshatoka kwenye umaskini.

Ninaomba sasa ufike wakati tuache mzaha, tuwafikirie hawa watu wanaoishi vijijini ambao ndiyo walio wengi. Asilimia 77 ni watu wengi, mkate unatakiwa upelekwe mkubwa, tuache mazoea ya kuendelea kuwatengea watu wa mjini na kuwasahau walio wengi; hali hii haikubaliki. Itabidi watu wote sasa

ambao wanaona haki inatendeka upande mmoja na wao wakabanane mjini tuone nani atazalisha, jambo ambalo litakuwa ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupitia nafasi hii, Bajeti ijayo Wizara ya Maji itengewe fedha za kutosha ili watu wetu ambao sasa ni maskini wa kutupwa, waweze kuondoka kwenye hali hiyo. Ukiweka maji kwenye mashamba yao, kilimo kitapanda na watu wataondoka kwenye ufukara huu uliopo. Tunayo maji mengi, Mungu ametujalia, kama kuna nchi iliyojaliwa ni Tanzania, kama kuna ubaguzi basi Mungu aliwabagua wengine sisi tukapendelewa tukapewa utitiri wa maji, kila unakogeuka ni maji, lakini namna gani sasa yafike kwa wananchi ni jambo ambalo linatakiwa lifanywe na Serikali. Serikali ambayo ina wajibu, Serikali inayokusanya kodi kutoka kwa wananchi, ihakikishe hizo kodi za wananchi sasa zinaenda kuwapa manufaa wananchi hawa.

Mchango wangu kwa leo ninaomba Serikali ione haja ya lazima kabisa kama inavyowajibika ihakikishe watu wetu inawatengea bajeti nzuri ya maji na ikifanya hivyo kwa miaka mingine, sasa kama mtaanza kujigamba mnavyopenda basi itaonekana kweli kuna maana. Kwa sasa hamstahili kuchukua hiyo sifa mnayopenda kuipata, kwa sababu wananchi wetu hasa akina mama wanahangaika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Maswa kwa mfano, kila kukicha Serikali hii inayojiita sikivu, imeendelea kuwanyima huduma yao muhimu ambayo ni ya lazima. Maji yanakatika sasa ni miezi minne, maji

hayapatikani kwenye Mji wa Nyalikungu Maswa na sababu ya kutokupatikana haielezwi vizuri. Wana bwawa lililokuwa na maji mengi, lakini Serikali imeshindwa kulipia umeme na matokeo yake watu wa Maswa wanaadhibiwa kwa kosa la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini mnawatesa walipa kodi wa Maswa wakati wao wanatimiza majukumu kwa Serikali? Kwa nini wana miezi minne hawapati maji safi na salama kwa wakati unaotakiwa? Naomba Serikali inipe jibu wakati Waziri anahitimisha kwa nini tangu mwezi Machi mpaka leo Wananchi wa Maswa wanahangaika kupata maji wakati bwawa wanalo? Jukumu la kuvuta maji ni la Serikali je imeshindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niambiwe ni kwa sababu gani mnawaadhibu Wananchi wa Maswa bila ya kosa lolote. Katika hilo naomba nielezwe sababu kubwa; vinginevyo, Watu wa Maswa nao wajitangazie kwamba imefika wakati nao waamue kuwa na Serikali yao itakayokuwa inawapa huduma hizi. Miezi minne mtu hapati maji maana yake nini? Haiwezekani na siwezi kukubali, lazima nipate majibu ya msingi; vinginevyo, tutaona namna gani sasa na sisi tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie

hotuba ya Waziri wa Maji. Kwa kweli maji ni uhai na maji ni muhimu sana kwa binadamu, kwa mifugo, kwa wanyamapori, kwa mazao, kwa viumbe vyote na kwa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, niligusia jambo la maji lakini nafurahi kwamba leo ni siku yake hasa mambo ya maji. Niende moja kwa moja kwenye mradi vijiji kumi. Huu mradi ni maarufu pia kama mradi wa *World Bank* hata kama pengine unafadhiliwa na benki zingine kama *African Development Bank*. Mradi huu unasuasua sana utadhani kama kuna mkono wa mganga wa kienyeji katika kutekeleza mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu, hawa Wabunge wote walipomaliza Ubunge mwaka 2005 kuingia mwaka 2006, Serikali ilikuja na mradi huu, tukapeleka maelezo kwa wananchi wetu kwamba kaeni mkao wa kupokea mradi huu lakini mpaka leo karibu tunaingia kwenye uchaguzi mwingine mambo hayajaenda sawasawa. Kule kwangu Ngorongoro wamechimba visima 10 kama ambavyo iliainishwa lakini ni visima viwili tu tunapata maji, visima vingine 8 ni *dry* kabisa, hakuna kitu chochote. Sasa tatizo ni nini? Je, ni teknolojia duni, tunatumia teknolojia ambayo imepitwa na wakati au hata hao washauri nao ni wa ngazi za chini au pengine hata mabadiliko ya tabianchi yameathiri upatikanaji wa maji chini ya ardhi, ndio maana maji hayapatikani? Haya ni maswali ambayo Wizara lazima itujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mfanyabiashara mmoja, mdau muhimu sana wa uchimbaji wa visima anaitwa Sabodo, tulielezwa na Wizara naye anafanya kazi hii ya kuwachimbia Watanzania visima. Je, yeye anaathirika, anakosa maji anapochimba hivi visima? Au ni sisi tu kwa sababu huu ni mradi wa Serikali kupitia Benki ya Dunia ambapo pengine kuna ujanja, kuna uchakachuaji, kuna kila kitu? Tuelezwe na Wizara, huyu mwenzetu yeye anafanikiwa ili tuweze kujua kama maji ndio sasa hayapatikani chini ya ardhi au kuna matatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufanye nini? Napendekeza mambo matatu. Moja, Serikali itumie watalaam wake, tuna *hydrologists* wazuri sana katika mabonde yetu, wafanye utafiti kabla ya uchimbaji na baadaye wanaweza waka-*contract* kazi hiyo ya uchimbaji sasa kwa kampuni binafsi. Hilo la kwanza. Pili, Chuo Kikuu cha Mandela kilichoko Arusha tumeelezwa kwamba ni watalaam juu jambo hili. Pengine hawa wapewe kazi hii. Jambo la tatu ninalopendekeza ni kwamba Serikali itafute fedha ndani na tuingie awamu ya pili ya mradi huu kwa sababu hakuna kurudi nyuma. Watanzania tulishawaeleza Serikali ya CCM itawaletea maji, maji hayo lazima yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji Waso na Loliondo. Kwanza kabla sijasahau, nimefurahi kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji yuko hapa Christopher Sayi, ni mtu mwema, mtaratibu sana na mpole lakini sijui kwa nini hajajibu barua yangu ya tangu mwaka 2010. Naomba baada ya kikao, anitafute, tuonane nimkabidhi barua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeanzishwa mwaka 1979 na Makao Makuu ni Loliondo, ni kilomita zaidi ya 400 kutoka Arusha Mjini ambako ni Makao Makuu ya Mkoa lakini Mji wa Loliondo na Mji wa Waso ni miji ambayo inakua sana kwa sasa kwa matumaini, kwanza, Serikali ya CCM tunaishukuru sana wametuletea umeme lakini pili, tunazungukwa na hoteli za kitalii nyingi tu, ziko maeneo yale, hali ya hewa ni nzuri, tuna matumaini ya barabara ya lami ya kutoka Mto wa Mbu kwenda mpaka Musoma upande wa pili. Kwa hiyo, tuna biashara kubwa na nchi jirani maana tuko mpakani, kwa hiyo, Mji huu wa Loliondo na Mji wa Waso unakua kwa kasi sana. Tatizo la miji hii, tuna chanzo cha maji Ng'arwa ambacho miundombinu yake iliwekwa tangu mwaka 1989, sasa ni miaka 23 miundombinu hiyo kwa kweli imeshindwa kazi kwa sababu ilikuwa inahudumia watu siyo zaidi 500, sasa hivi watu wa Loliondo na Mji wa Waso ni watu 10,000. Kwa hiyo, miundombinu haitoshelezi ndio maana Katibu Mkuu tulikuomba tangu mwaka jana shilingi milioni 200 ya kurekebisha miundombinu hiyo tuweze kupata maji mengi zaidi lakini kwa sababu umeshindwa kujibu barua yetu, tumeongeza maombi, tumekuja na ombi maalum la shilingi milioni 400. Naomba hiyo fedha Wizara itutafutie tuweze kuwasaidia hawa watu maji kwa sababu Loliondo na Waso wanapata sasa mgao wa maji, maji ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kule ambako tumepata maji katika Kijiji cha Enduleni na Kitongoji cha Njoroi, naomba Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa Enduleni iko ndani ya eneo lake na ni

wadau pia wa maendeleo, kwa upande wa Tarafa ya Ngorongoro ambayo ni hifadhi, naomba sasa hayo maji yaliyopatikana Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itusaidie kusambaza katika vijiji na vitongoji vya jirani badala ya kuendelea kuisubiri Serikali kwa sababu hilo nalo ni Shirika la Umma. Watusaidie kusambaza maji huko Enduleni, Madukani katika kijiji cha Ndiani, Rajanwa, Mekeke na Sipoorioni, Losilale, Esilya, Embalwai na Esere.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata zangu tatu zina matatizo pia makubwa ya maji Olbalubalu, Bulati, Naiyobi, Kakeswe na Osnoni. Naomba haya maeneo tupate maji kwa sababu Olbalubalu kwa mfano tulikuwa na njozi ya kujenga Sekondari ya Wasichana tulishindwa kwa sababu ya ukame. Hapa Bulati wana tatizo kubwa la maji, naomba Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wakishirikiana na Baraza la Mazingira kukamilisha *environment impact assessment* ili tuweze kupata maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nawashukuru *World Food Program* wametusaidia matanki mawili katika kijiji cha Bulati, Shule ya Msingi na kila *tank* moja lina *capacity* ya kuchukua lita 30,000, kwa hiyo wametusaidia sasa wanavuna maji ya mvua. Lakini siyo hilo tu, wamesaidia katika shule 20 katika Wilaya nzima ya Ngorongoro. Nawashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Majina ya Vijiji vile sijui kama Mheshimiwa Waziri amevipata vizuri.

Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar wanasema urudie tena. *(Kicheko)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikushukuru kupata nafasi ya kuchangia kwenye hoja ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kama kutakuweko na vita kuu ya tatu duniani itasababishwa na maji. Kwa hiyo, lazima kama nchi tulinde sana vyanzo vyetu vya maji na tuyalinde maji yetu. Kuvilinda vyanzo vya maji kwa kweli lazima tutunze mazingira kwa gharama yoyote ile. Ukiangalia hali tunavyozidi kwenda unaanza kuona tatizo la kutolinda vyanzo vya maji inazidi kuwa tatizo. Pia lazima tuanze *culture* ya kuvuna maji. Wakati wa masika maji mengi sana yanapotolea baharini, yanapotolea kwenye maziwa. Kwa hiyo, naomba sana Serikali waje na mkakati wa kuhakikisha tunavuna maji ya mvua. Tukiwapa Watanzania maji safi na salama, tutapunguza magonjwa kwa asilimia 50. Yako magonjwa mengi sana Tanzania yanasababishwa na watu kutokuwa na maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuzungumzia Kigoma. Manispaa ya Kigoma ina matatizo makubwa sana ya maji lakini ndio Manispaa peke yake imezungukwa na Ziwa Tanganyika chini ya kilomita moja. Mimi nataka leo nimuulize Waziri, hivi sasa tungekuwa mbali na Ziwa lile hali ingekuwaje? Maana chanzo kiko hapo karibu halafu watu wa Kigoma hawana maji. Toka nimeingia Bunge hili naambiwa yafuatayo; *KFW* wanaleta mradi,

kuna *EU Water Facility*, kuna *Lake Tanganyika Integrated Project,* leo ni mwaka wa nane hakuna kilichotokea, shida ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu ambacho ni kibaya zaidi wakati hakuna maji tumepandishiwa ankara ya maji na bili yenyewe mmeipandisha, kila mtu alipe kiasi fulani, watu wote *flat rate,* kuna watu wengine maeneo yao hayana maji kabisa, kuna wengine wanapata maji kwa wiki, kuna wengine wanapata maji mara tano kwa wiki, kuna wengine wanapata mara mbili kwa wiki lakini wote wanalipa sawa, wapi hii iko duniani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo kwa mara ya kwanza sitaunga mkono hoja ya maji mpaka niambiwe hizi ankara za maji kwa nini watu wasitozwe kulingana na wanavyotumia? Mimi sina shida kupandisha bei ya maji, lakini tutozwe kulingana na tunavyotumia, anayetumia maji mengi alipe fedha nyingi. Haiwezekani mtu wa Ujiji kule anapata maji mara moja unamtoza sawa na mtu wa Mji Mwema anayepata maji mara tano. Haiwezekani! Ningeomba Waziri aniambie ni kigezo kilitumika kuamua kwamba sasa Kigoma watu wote walipe *flat rate* na wakati wote hawapati maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua miradi ya maji ya Mkoa wa Kigoma itaanza lini? Mwaka jana tuliambiwa itaanza mwaka huu, mwaka 2010 naliambiwa itaanza mwaka 2011, sasa Waziri ananiambia itaanza 2013 Januari, lugha hii Waziri nimeichoka. Kwa sababu lugha hii nimeambiwa toka

naingia Bunge hili leo mwaka wa nane. Kuna maeneo pale Kigoma, maeneo yote ya Kagera hakuna maji, Buhanda hakuna maji, Mwasenga hakuna maji, Businde hakuna maji, Kahabu hakuna maji, Bulonge hakuna maji, Mlole hakuna maji, Bushabani hakuna maji, Kibirizi hakuna maji, Burega hakuna maji na maeneo mengine ambayo sijatamka hakuna maji. Maana yake ni nini? Yote haya hayako zaidi ya kilomita tano na maji yalipo. Kibirizi ni mita 100, maji haya hapa kijiji cha Kibirizi hiki hapa, hakuna maji. Jamani na sisi nao ni Watanzania tunalipa kodi. Nataka Waziri aje aniambie miradi hii ya maji itaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, yako maeneo ya Hospitali, yako maeneo ya Makanisa, yako maeneo ya Misikiti, watu wetu wanasali sana, mara tano, hakuna maji na watu hao wanahitaji maji. Basi kama yako maji machache basi tuyapange kwa vipaumbele. Maeneo yote ya Misikiti, maeneo ya Makanisa, maeneo ya hospitali angalau yapewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yanayoendelea kwenye Manispaa ya Kigoma kuhusu maji ni matatizo makubwa sana. Watu wa Idara ya Maji hawajui kama tuna tatizo. Ukienda vibomba vilivyopo viliwekwa mwaka 1972, ni vibomba vidogo wakati Mji ulikuwa ni sehemu ndogo, leo mji umekuwa zaidi ya mara tano ya miaka hiyo, lakini bado vinatumika hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kuchukulia maji kwa maana ya *catchments area* imekuwa hiyohiyo toka tumepata uhuru. Mimi naomba leo Waziri aniambie tunatatuaje tatizo la maji la Mji wa Kigoma. Mimi naamini akiamua tunaweza kwa sababu sisi *investment* ya maji Kigoma huhitaji fedha nyingi kwa sababu maji yako pale. Kigoma unachohitaji ni kutandika mabomba, unachohitaji ni kujenga, unaweka *reserve* zaidi ya nne, tano kwa ile milima umemaliza tatizo la Kigoma, ni ku-*pump*. Mwanzoni mlikuwa mnasema tatizo la Kigoma la maji linasababishwa na umeme, Serikali yetu ya CCM ikaleta umeme lakini tatizo la maji bado lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba sana tatizo la Kigoma, Kigoma hatujawekeza ndio maana kuna tatizo la maji. Ninaomba sana Waziri anapokuja kujibu kesho aniambie yafuatayo: miradi hii ya maji ya Kigoma inaanza lini, habari ya maneno nimechoka, nimeyasikiliza maneno matamu haya ya *KFW, EU Water Facility*, *ADB* sijui nani kila lugha nzuri imeandikwa kwenye vitabu vyote. Nimekuja na vitabu vyote vitano vinaongea lugha moja lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba aniambie bei ya Ankara hizi za maji, leo naomba nimwambie Waziri, wananchi wa Mkoa wa Kigoma wameamua kwenda Mahakamani kupinga ankara za maji kwa sababu wamesema hatuwezi kupata haki, haki yetu tukaitafute Mahakamani kwa sababu walivyoweka ankara za maji sivyo kinachotakiwa kufanyika. Haiwezekani mtu anapata maji siku moja alipe sawa

na mtu anayepata siku tano. Tunachoomba, waweke mita, wachaji kulingana na mita hakuna atakayepiga kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa vile ambavyo tumeshaanza mjadala huu vizuri na tutaendelea na uchangiaji jioni ya leo ambapo Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba ataanza, atuatiwa na Mheshimiwa Said Mtanda na wengine watafuatia. Nitaomba wale ambao watakuwa wameomba kuchangia wawepo katika viti vyao inanirahisishia kujua upo au hupo. Kama haupo kwenye kiti chako ni rahisi sana kukuruka kwenye orodha. Nilitaka kumwambia rafiki yangu Kusulumbayi kwamba tumethubutu, tumeweza na tunasonga mbele. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.56 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, nilikuwa nimesema kwamba Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba angeanza, karibu uendelee na Mheshimiwa Bernadetha Mushashu ajiandae. Mheshimiwa Ntabaliba!

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kujadili bajeti muhimu kabisa ya Wizara ya Maji kama ilivyowasilishwa vizuri na Profesa Maghembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwanza naomba nitoe masikitiko yangu makubwa kwa Wizara hii. Wizara hii kwa kweli sisi haijatutendea haki kwa sababu katika uwakilishi wake wote hakuna mahali Kigoma imetajwa kama kuna mradi, sasa sijui wao kama Wizara hawaoni kama kuna matatizo ya maji kule au Mkoa wa Kigoma hauko kwenye *desk* lake pale kwenye Wizara yake au huenda nafikiri hana hata simu ya Meneja wa Mradi wa Maji wa Kigoma. Kwa hiyo, hilo naomba tu niwe-*registered* kwamba Obama hajafurahia kwa sababu haoni tatizo la maji likitatuliwa katika Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiona miradi mingi ambayo inafadhiliwa na watu wengi, tunaona miradi ya maji Wilaya za Moshi, Hai, Same, naiona mingine Mwanza, Mara na Tabora. Vilevile ukienda kwenye jedwali lake la wafadhili wanaofadhili maji nchini Tanzania, kwenye jedwali namba 16, kwenye ambatanisho lake, hakuna mahali unaona kwamba kuna mfadhili yeyote ambaye anafadhili Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, nilitaka tujue kama sisi hatuna haki hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda ukurasa wa 106, kwenye jedwali lake huoni mradi wowote anaofadhiliwa na nchi za nje kwenye Mkoa wa

Kigoma. Kama Mkoa wa Kigoma una maji, naomba usimame uwaambie Watanzania ili utupongeze kwamba Kigoma tuna maji. Kutupa miradi hutupi, kutupongeza hutupongezi, sasa hatukuelewi uko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukija kwenye bajeti yako uliyoiwasilisha hapa, fedha nyingi najua zinashughulikia Mjini, najua Vijijini nako kunahitaji maji, lakini utaona bilioni shilingi 36.8 ndiyo tu unapeleka miradi ya maji Vijijini ambapo kunakaa watu wengi lakini naona shilingi bilioni 372 inajikita Mjini, sasa sijui unataka kuipeleka wapi nchi hii? Nikiangalia kwenye hotuba yako, unasema mpaka 2015, Vijiji viwe vimefikiwa kwa asilimia 65, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inatuambia asilimia 75 Vijijini. Kwa hiyo, kwanza unaenda kinyume na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inakuelekeza. Kwa hiyo, umeshatupoteza kwa asilimia 10. Kwa hiyo, ni vizuri uweze ku-*adjust figure* zako ili ziweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine, sijaona mikakati ndani ya Wizara yako, hasa upimaji wa maji Vijijini. Wananchi wengi wanatumia maji aidha ya Mto, ya chemchem, lakini sioni umakini wa Wizara yako kupitia Halmashauri kwamba yale maji yanaenda kupimwa kujua wananchi kama wanakunywa maji salama au hawanywi maji salama. Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba Kitengo chako uweze kukiimarisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye Jimbo langu la Manyovu na naomba kwa sababu wewe ni Waziri mpya kupitia Naibu Spika uweze kuya-*note* haya

ili uweze kuyafanyia kazi kwa sababu hujafanya chochote na kwenye bajeti yako Obama hayumo. Kwa hiyo, ni sawa tu mimi ningeenda nyumbani kupumzika kwa sababu mawazo ya wananchi wangu hujayaweka. Pale Jimbo la Manyovu, tulikuwa na mradi wa Mnanila. Mnanila pale kulikuwa na mradi ambao ulikuwa una-*supply* maji kwenye Vijiji sita, Vijiji sita hivyo ni Mkatanga, Nyakimue, Kitambuka, Kibigwa, Mwayaya na Mnanila na sasa hivi Vijiji hivi vyote vina takribani watu laki moja, sasa maji pale ni tatizo. Kwa hiyo, naomba Wizara yako na TAMISEMI mfike pale muweze ku-*assess* ili watu wale waweze kupata maji. Kulikuwa zamani kuna *pump*, mifumo ya maji na matenki yote yapo, kilichobaki ni dhamira ya Serikali kuweka fedha kidogo tu pale na watu waweze kupata maji na vyanzo vya maji viko hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye mradi wa Vijiji Kumi, huu wa Benki ya Dunia, sasa ifike mahali Serikali, naomba niishauri kama Serikali haina fedha na Benki ya Dunia haijatoa, mtuambie ukweli, sio mnakaa mnatuyumbisha Vijiji Kumi. Hivi Vijiji kumi ni nyie kama Serikali mlisema Halmashauri zi-*identify* Vijiji hivyo. Sasa hivi kwenye Vijiji vyangu, nina Vijiji sita kwenye hii programu, Vijiji vya Munzeze, Kibogwe, Mbanga, kirungu, Bulimani na Nyamugali. Nashukuru Kijiji kimoja cha Mbanga ndicho ameweza kuwepo *Engineer* ambapo sasa ujenzi utaanza, kwa hiyo, Vijiji vitano bado ni *pending*. Kwa hiyo, naomba kwa kweli pale napo mtufikirie na hii Mikoa ya pembezoni Mheshimiwa Waziri, hebu iangalie sasa, usiangalie tu pale unapoambiwa kila wakati, usisaidie wale wanaoshinda kugongagonga milango kwenye ofisi yako, Obama

hata kama hakuja ofisini kwako, basi mfikirie sio lazima nije ofisini kugongagonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunayo Wilaya mpya ambayo tumepewa, Wilaya ya Buhigwe, hatuoni programu kwenye Wizara yako, ndani ya Wilaya mpya maji yakoje. Tunapewa Wilaya nyingi ambapo zimeanzishwa Wilaya 19, zote nazisemea kwa ujumla, lakini hatuoni mipango inayoonyesha kwamba unapeleka maji pale, labda tu kupitia fedha niliyoiona kwenye bajeti ya Serikali Kuu, labda kama hicho kifungu kitakuwa kiko kule Obama atakuwa hana matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilikuwa nataka kusema ni utunzaji vyanzo vya maji, hasa vya Vijijini. Kwa Mjini, naona mnajitahidi, mnaenda kukagua viwanda, vingine mnatoza hela, mnapata na hela hukohuko, sawa, lakini Vijijini vile vyanzo vya maji ya Mito ambavyo nilifikiri bajeti ile ingeweza kutumika kuwapa fedha kidogo ili na vile vyanzo vya Vijijini viweze kulindwa. Kule kwetu kuna miti ambayo sio rafiki wa maji, lakini watu wa maji hawawezi kufanya chochote kwa sababu hawawezi kulipa *compensation* kwa wale watu wenye mashamba. Kwa hiyo, naomba sana muweze kuwapa fedha pale ili vyanzo vitunzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitaka kujua, kwa kutokupima, sisi kwetu Manyovu tunalima kahawa na sehemu nyingine za milima na ndizi na nini na zile kahawa, tunaweka mbolea, tunaweka mbolea kwenye mahindi na maji yanatiririka kwenye vyanzo

vya maji. Tulitaka kujua je, kuna usalama? Kama hawaji kutupimia maji, itakuwa watu wetu wanaumwa kila wakati kumbe tatizo huenda inatokana na uchafuzi wa mbolea tunayoitumia kwenye mashamba yetu. Kwa hiyo, naomba Wizara mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningine, nilikuwa napenda nishauri *EWURA, EWURA* wanafanya kazi nzuri ku-*regulate* bei, sina matatizo nao, lakini naomba waende mbele zaidi, wasukume zile Halmahsauri ambazo zimezembea kusambaza maji, badala ya kuendelea kukaba tu bei iwe ndogo huku maji hayapo kwenye Mamlaka za Maji. Kwa hiyo, naishauri *EWURA* iende mbele zaidi, isikabe tu bei, ikashinda pale bila kuzihimiza zile Mamlaka za Maji ili ziweze kuzalisha maji ya kutosha kwa wananchi wetu. Naomba kuwe na mashindano na zile Mamlaka ambazo zinafanya vizuri, ziwe zinapewa taji.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima, Tanzania kuna watu wengi wamechimba visima mbalimbali na sioni hotuba yako ikiwapongeza hata kuwapongeza kwamba wanaisaidia Serikali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nipewe majibu.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri yetu ya Wilaya ya Lindi, Ndugu Abdul Makwita kwa kuchaguliwa tena kuendelea na wadhifa wake huo. Pia nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali kwa kutambua kilio cha wananchi hasa wa Kitongoji cha Ruvu ambao walikuwa wameandamwa na kero kubwa tatu; moja ikiwa ni upatikanaji wa Serikali ya Kijiji pale na Serikali sasa tarehe 14 tutatangaza Kitongoji kile kuwa Kijiji jambo ambalo litatoa tija na furaha kubwa kwa wananchi wa Kitongoji cha Ruvu. Kazi kubwa iliyobaki sasa katika Kijiji hicho, ni upatikanaji wa maji baada ya kero hizo mbili ya Kijiji na ile ya barabara kutoka pale Mchinga kwenda Ruvu kuwa imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nitumie fursa hii kwanza kumshukuru sana Profesa Maghembe kwa kazi kubwa na Dokta Benilithi Mahenge, Naibu Waziri kwa kuchaguliwa kushika wadhifa huo. Mimi binafsi nina imani kubwa na watendaji na viongozi hawa na nina imani tutashirikiana nao katika kutatua changamoto ya maji inayotukabili katika maeneo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Lindi ina Vijiji visivyopungua 154, lakini inao wakazi 274,000 lakini kwa masikitiko makubwa napenda Wizara itambue kwamba kati ya wananchi 274,000 ni wananchi 82,114

pekee ndiyo ambao wana uwezo wa kupata maji na hapo sizungumzii maji safi na salama. Wale wenye uwezo wa kupata maji ni elfu 82 kati ya wananchi 274,000. Kwa hivyo, bado tunayo changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji katika Wilaya yetu ya Lindi. Naiomba Serikali na kupitia bajeti hii, kuelekeza nguzu zake katika utaoji na upatikanaji wa maji maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu Obama amesema fedha iliyotengwa haitoshi kutatua matatizo ya maji hasa maeneo ya Vijijini. Tunaelekeza nguvu kubwa maeneo ya Mijini, lakini tunahitaji kuboresha miundombinu hasa ya maji Vijijini ili wananchi wetu, vijana wetu wakae maeneo ya Vijijini na kufanya shughuli za uchumi maeneo hayo ya Vijijini badala ya kukimbilia Mijini. Kwa tathmini hiyo basi ni asilimia 33 tu ya wakazi wa Wilaya ya Lindi wanao uwezo wa kupata maji. Kati ya asilimia 100 ni asilimia 33, jambo hili linasikitisha na naiomba Wizara hii kuchukua hatua za makusudi ili kuboresha huduma za maji katika Wilaya ya Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji kama vya Namkongo, tumekuwa tukipiga kelele hapa na tukaahidiwa na Wizara kupitia Mradi wa Vijiji Kumi, nashukuru jedwali ambalo tumepewa inaonekana hatua zote nne tayari tumeshazifikia kwa hivyo Mkandarasi yule ataanza kazi ya kujenga miundombinu ile ya maji katika Vijiji vya Namkongo, Likwaya na maeneo mengine katika Jimbo langu. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba Serikali sasa, mradi huu umechosha Waheshimiwa Wabunge,

wananchi, tunachohitaji sasa ni kuona hatua za makusudi na za dhati zikichukuliwa ili kuboresha Miradi hii ya Vijiji Kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Mnang'ole, Kilola Mbwani, Lihimilo ni maeneo ambayo yana ukame mkubwa na yanahitaji huduma ya maji kwa haraka. Vitongoji vya Kitohavi ambavyo kupitia mradi wa maji wa Sabodo tulifanikiwa kuchimba kisima, lakini kisima kile hakitoi maji. Kwa hiyo, naomba Serikali na juzi tumeagiza pale Wahandisi wa Halmashauri kwenda kufanya *survey* ili kujiridhisha na wapi kisima kikitobolewa tunaweza kupata maji. Kwa hivyo, tunaomba Serikali nayo ihakikishe wananchi wa maeneo ya Kitohavi, Kipunga, Uleka, lakini pia Likonde na Kingulungundwa wanapata maji. Hayo ni maeneo ambayo yanakabiliwa na upungufu mkubwa wa maji katika Jimbo langu la Mchinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuzungumzia pia mradi wa maji wa Kijiji cha Mipingo. Toka tarehe 28/7/2011, mota inayoendesha umeme katika mradi wa maji pale Mipingo iliungua, ikasababisha waya zile pale kuungua, kwa hivyo wananchi wale wamekosa huduma ya maji toka tarehe 28/7/2011na wataalamu wetu, Ma-*engineer* wetu wa Wilaya pale, wamefanya kazi kubwa sana wakiongozwa na *Engineer* Boniface, ninawapongeza kweli kweli, lakini wameshindwa kutatua, kinachohitajika ni mtaalamu wa *mechanical* na *electrical engineer* kuweza kufika pale kutoka Wizarani. Kwa hivyo, namwomba Profesa anihakikishie mara baada ya mchango huu anawasiliana na

*Engineer* Goyagoya ambaye amekuwa ni msaada mkubwa katika utengenezaji wa pampu hizi maeneo mbalimbali nchini. Kama ambavyo walivyofanya kutengeneza pampu pale Kilangala na leo huduma ya maji iko vizuri, naomba pia Profesa amuelekeze huyu *Engineer* Goyagoya kwenda pale Kijiji cha Mipingo ili shida hii ambayo sasa takribani mwaka mmoja inawapata wananchi wa Mipingo iweze kumalizwa na sisi tutatoa ushirikiano mkubwa ili mambo yaende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiachana na mradi huo wa maji pale Mipingo, liko tatizo lingine kule Milola. Lakini tunaishukuru Serikali kwa sababu kule Milola tumepata fedha ambayo itatuwezesha kutoa maji kutoka Milola B kupeleka Shule ya Sekondari ya Milola na mimi kama Mbunge nimefanya juhudi kubwa kuweka umeme wa jua pale Shule ya Sekondari Milola kwa thamani ya shilingi milioni 15. Kwa hivyo, upatikanaji wa maji ambayo ilikuwa ni huduma ya msingi pale Milola Sekondari ni jambo la msingi. Kwa hivyo, naomba Serikali iharakishe sasa wale wafadhili wetu wa Chuo Kikuu cha Michigan na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitengo cha *IRA* waweze kufanya kazi ile kwa haraka kutoa maji pale Milola B na kupeleka maji kwenye Shule ya Sekondari Milola.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tunalo tatizo kwa sababu maji ya Milola yanatoka kwenye chanzo cha maporomoko ya Mto Chipwapwa, lakini wale wananchi wa Namtamba ambao mashamba yao yamevurugwa ili kupisha mabomba ya maji, kutoka kule Chipwapwa kwenda

Milola ila maji yale yaende mpaka Kinyope, wao wenyewe hawana maji na Serikali inasema tuwachimbie kisima. Unachimba kisima cha nini wakati maji yako kilomita mbili kutoka kwenye chanzo cha maji yaani Chipwapwa kufika pale Namtamba. Kwa hiyo, naishauri Serikali ione umuhimu wa kuwasaidia na kuwahudumia wananchi wa Namtamba kwa kuweka mtandao wa mabomba kutoka pale chanzo cha Chipwapwa kufika pale Namtamba, kilometa mbili tu. Tuweke pale mtandao wa mabomba, tenki, virula vile ili wananchi wa maeneo yale na wao waweze kufaidi maji badala ya kuwa na mawazo ya kuchimba kisima ilihali wao chanzo cha maji kiko maeneo yao. Kwa kufanya hivyo, kwa kuwashirikisha wananchi hawa, ndipo wanapoweza kutoa ulinzi shirikishi kwa mabomba yale yanayotoka Namtamba kwenda hadi Milola. Tusipofanya hivyo, tunatengeneza mazingira magumu na wananchi wale hawataweza kutuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo lingine pale Kilangara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, samahani, habari za Kilangara zimeshindikania hapo. Sasa Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Herbert James Mntangi. Mheshimiwa Kakoso!

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Maji. Tatizo la maji katika Mkoa wa Katavi, ni tatizo kubwa sana. Mkoa wa Katavi katika Tarafa zote zilizopo katika Mkoa huo bado kuna uhaba wa maji mkubwa mno. Kwa hiyo, naiomba Serikali ielekeze nguvu kubwa sana katika maeneo ya Mkoa huu ikizingatiwa kwamba Mkoa huu ni Mkoa mpya na ni miongoni mwa Mikoa iliyokuwa imesahaulika, Mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililoko katika Mkoa huu, ni tatizo ambalo hata maelezo hayawezi kufikia kiwango ambacho kipo kule. Mkoa huu una Mradi wa Vijiji Kumi vya *World Bank,* lakini katika mradi huo, bado havijapata fedha, ni vijiji vitatu tu ambavyo ndio vimepata fedha za mradi huo lakini vijiji vingine vyote zimekuwa ni ngonjera za kudumu na miradi hii imeanza toka mwaka 2005/2006, lakini mpaka sasa hivi, mradi huu umetekelezwa kwa vijiji vitatu tu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa majibu, atueleze ni lini huduma ya maji katika vijiji vile vya mradi wa maji, itapatikana? Vijiji hivyo ni Mamba katika Tarafa ya Mpimbwe, Majimoto, Mwenge, Mtakumbuka, Isinde, Sungamila, Ngomalusambo, Kalema na Ikola.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ungekamilika, ungetatua matatizo ya wananchi ambao wana dhiki kubwa sana. Imefikia hatua wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao za uzalishaji na za ujenzi wa Taifa, muda mwingi wakitumia kwa ajili ya kutafuta maji.

Akina mama walio wengi ndio wanaopata usumbufu kwa sababu wao ndio wanaoenda kutafuta maji na ndio wazalishaji wakubwa katika Taifa letu. Pia ukizingatia Mikoa hii inategemea zaidi miradi ya kilimo; kwa hiyo, Taifa linapoteza nguvu kazi kubwa kwa ajili ya muda mwingi unaotumika kutafuta maji. Naiomba Serikali, izingatie hili na itoe kipaumbele cha aina yake kwa ajili ya kuwapelekea huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna tatizo lingine katika Vijiji ambavyo haviko katika mradi wa maji wa Vijiji Kumi. Vijiji hivyo, vingine toka nchi ipate uhuru, havijawahi kupata huduma ya maji, huduma inayotolewa na Serikali. Walikuwa wakitegemea sana maji yanayotoka, yanayotiririka kwenye mito, bahati mbaya baada ya tabianchi na kuharibika kwa mazingira, mito ile imeacha kutiririsha maji kiasi kwamba, wananchi sasa hawana huduma kabisa. Katika Tarafa ya Mwese, tunavyo vijiji vya Rugonesi, Katuma, Mwese Namba 1, Mwese Namba 2, Mwese Namba 3, wote wana shida ya maji. Pindi mito ile inapoacha kutiririsha maji, wananchi wanatembea zaidi ya kilometa kadhaa kwenda kutafuta maji. Naomba maeneo hayo nayo yaangaliwe ili yapewe uzito na wao waweze kufaidi matunda ya uhuru wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vijiji ambavyo havijawahi kupata kabisa mradi wa maji na huwa wanasikia tu kwenye redio ni vijiji vya Igagala, Vikonge, Kamsanga, Kasinde, Iloba, Kungwi, Sibwesa na vinginevyo vingi ambavyo havijapata huduma ya maji. Huko kuna matatizo makubwa sana. Naiomba Serikali,

kupitia Wizara ya Maji ihakikishe inapeleka nguvu katika maeneo ambayo yalisahaulika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maeneo ya vijiji ambavyo vilibahatika kupata huduma ya maji lakini mpaka sasa huwa wanapata huduma hiyo kwa muda wa miezi mitano tu, kipindi cha mvua, mvua zinapokata, maji hayapatikani tena. Vijiji hivyo ni Mchakamchakam, Ifukutwa, Milala na Majalila, vijiji hivi vina visima vifupi. Tunaomba Serikali, ifikirie haraka kuweza kuwasaidia wananchi wa vijiji hivi, ili viweze kusaidiwa kufanyiwa ukarabati wa kutengeneza miundombinu iliyoharibika ili wananchi waweze kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo Serikali imejisahau ni maeneo ya taasisi, kama vile shule, shule za msingi, shule za sekondari na zahanati. Katika maeneo haya, huduma ya maji haipo. Vijana wetu walioko shule, wanachukua muda mwingi, badala ya kujisomea, wanaenda kutafuta maji katika maeneo ambayo yanatoa huduma hiyo. Naomba Serikali, iangalie kwa kina, ili iweze kutoa kipaumbele katika taasisi zile za umma, hasa zahanati, shule za sekondari na shule za msingi, zipate huduma ya maji ambayo ninaamini itaweza kuwasaidia na kuweza kuwapa fursa pekee ya kujisomea na kupata huduma nzuri mahali pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mkubwa wa maji ulioko kule Ukanda wa Ziwa Tanganyika, Kijiji cha Ikola; mradi huu umefadhiliwa na wafadhili, lakini bado huduma yake haijaelekezwa kwa nguvu zote. Naomba

Wizara, ihakikishe mradi ule unasimamiwa ili uweze kutoa huduma kwa wananchi ambapo utakuwa umetatua tatizo la mlipuko wa kipindupindu kule. Maeneo haya ni maeneo ya ukanda wa Ziwa na kila masika, tunakuwa na tatizo kubwa sana la mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu kwa sababu ya kunywa maji machafu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, mradi ule iusimamie na ihakikishe unakamilika na uende sambamba mpaka kijiji cha jirani kile cha Mchangani, uhusishe na Kijiji kingine kilichopo jirani, Kijiji cha Isengule; utakuwa umewasaidia sana wananchi wa eneo hili ili waweze kunufaika na mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali, kuhakikisha Wizara inapokuwa inapanga bajeti, iangalie umuhimu wa kupeleka huduma hizi vijijini. Wakazi wengi wa nchi hii, wanaishi vijijini lakini Serikali, kupitia Wizara hii, tumeona ilivyoelekeza nguvu zake kwa ajili ya wananchi wa mijini tu. Hatuwatendei haki Watanzania walio wengi. Watanzania walio wengi takribani karibu milioni 35 hivi, wanaishi maeneo ya vijijini lakini huduma au ukiangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imejikita sana katika maeneo ya mijini na Dar-es-Salaam peke yake, ina shilingi bilioni 100. Hii sio kitu sahihi, tunahitaji kuwe na uwiano wa kusaidia maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono endapo Mheshimiwa Waziri atajibu hoja zangu, ili niweze kuangalia maeneo yale kama yamewekewa uzito wa aina yake, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nitoe tu pongezi kwa viongozi wote wa Wizara, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na Watendaji wake, kwa maandalizi mazuri ya hotuba iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwa kusema yafuatayo; kwanza katika Wilaya ya Muheza, zipo ahadi mbili za Mheshimiwa Rais, za kuhusu maji. Ya kwanza, ni maji kutoka katika chanzo cha Mto Zigi, kuja katika Mji wa Muheza lakini ahadi ya pili ya Rais, ni maji katika mradi unaoitwa Mbambara. Sasa ukiuliza Wataalam katika Wizara hii, wanaukumbuka mradi huo mmoja wa Zigi, huu mwingine hawaukumbuki. Ndio maana nimekuwa nikisema mara kwa mara kwamba, ni vizuri katika Ofisi ya Rais, Wizara, kukawa na Chombo kinachoratibu utekelezaji wa ahadi za Rais. Washirikishe watu wa Mipango na wataalam wa Idara ya Fedha, waweze ku-*monitor* na kukumbusha Wizara zote, hizi ahadi za Mheshimiwa Rais. Hii ahadi ya pili ilikuwepo na aliyekuwepo siku hiyo, ni aliyekuwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Profesa Mwandosya, alikuwepo wakati Mheshimiwa Rais anatoa ahadi hiyo ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kusema hayo, niseme kwamba, katika programu yote iliyopo hapa, Muheza haijaguswa, licha ya matatizo makubwa tuliyokuwa nayo. Lakini, nimshukuru aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, nilipozungumza naye kuhusu matatizo makubwa ya hali ya Muheza, sasa hivi amehamia Wizara nyingine ya Ujenzi, lakini waliopo nina uhakika wana habari hizo.

Alileta wataalamu, kuja kunisaidia Muheza, kuangalia kuna matatizo gani yanayotufanya Muheza tukose maji kwa kiwango hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Mto Zigi, umekwenda kilometa 70 kupeleka maji Tanga Mjini, sisi wenyewe ambao mto ule upo ndani ya Muheza, hatuna maji, kilometa 15 tu kutoka kwenye chanzo, lakini kilometa 70, wamepata. Sasa, imeandaliwa Taarifa ambayo ni ya Mpango wa Dharura wa kuwezesha kuondoa tatizo la maji katika Mji wa Muheza na Wilaya ya Muheza. Mpango huu wa Dharura, umeandaliwa na wataalamu walioletwa na Wizara yako ya Maji. Kwa hiyo, ni taarifa ambayo nina imani kabisa, japokuwa sikuona katika Taarifa ya Mheshimiwa Waziri, lakini Mheshimiwa Waziri, atakuwa na Mpango wa Dharura wa Utekelezaji wa Mpango huo wa Dharura ulioandaliwa na Wizara yake ili kuondoa matatizo ya maji katika Mji wa Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, walichoandika pale ni utekelezaji wa mambo makubwa matatu. Moja ni, kwanza hicho ambacho sisi tunakipa kipaumbele, ni kisima kirefu ambacho tayari kimeshachimbwa, kipo; kisima kina uwezo wa kutoa lita 40,000 kwa saa. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, mkijenga miundombinu, tutaweza kupata lita 960,000 kwa siku; kiwango hiki ni kizuri na kikubwa na kinaweza kusaidia sana kupunguza matatizo ya maji katika Wilaya ya Muheza. Hicho ndio kipaumbele chetu cha kwanza katika utekelezaji, ambapo ninaamini Wizara itakuja na Mpango wa namna ya kutusaidia katika utekelezaji wake. Lakini cha pili ni kisima cha Polisi, ambacho kina

uwezo wa kutoa lita 5,000 kwa saa, ni lita 60,000 hizo kwa siku. Si haba ukilinganisha na sifuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, Rais alikuja Mkoa wa Tanga mwezi Mei mwaka huu na alipofika Tanga, alipouliza habari za Muheza kuhusu maji, Mheshimiwa Rais, akatoa tena Kauli ya kutaka Wizara yako, Wizara ya Maji, iisaidie Muheza katika utekelezaji wa Mpango huu wa Dharura. Nimeleta barua inayotoka kwa Mkuu wa Mkoa, kwenda kwa Mheshimiwa Waziri, inayozungumzia ahadi hiyo mpya ya Mheshimiwa Rais, mwezi Mei, mwaka huu wa 2012. Nina imani kabisa Mpango huo utatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jedwali Namba 16, katika Hotuba hii na Kitabu cha Mheshimiwa Waziri, imeonesha maeneo ambayo wapo watu wamesaidia katika kupeleka maji katika maeneo mbalimbali ya vijiji. Katika Wilaya ya Muheza, naomba niweke wazi kwamba, kuna Mhisani ambaye anatusaidia sana ni *World Vision,* hayupo katika jedwali lako, inawezekana watu wa Muheza hawakuleta taarifa. Lakini si vizuri tukaacha kumtaja, mwaka uliopita nilimtaja na nikamwomba Waziri Mkuu na kweli akawaandikia barua ya kuwashukuru, *World Vision* wanatusaidia sana katika maji vijijini kwenye Tarafa moja inayoitwa Tarafa ya Bwembwera.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika Mpango pia jedwali linalofuatia, hili ni jedwali namba 10, visima vile 10, katika Wilaya ya Muheza mmeandika visima 10 na vimechimbwa visima 10. Wilaya ya Muheza *World Bank*

*Project,* visima vilivyochimbwa ni tisa (9) na hiki kisima cha 10, kiligeuzwa katika Mpango wa *Water Gravity,* mpango ambao leo hii nimezungumza na wenzangu kule, tumeshafikia hatua ya kumpata Mkandarasi wa kujenga huo mpango wa maji ya mtiririko kutoka katika chanzo kinachoitwa Ubembe-Kwemhosi. Kwa hiyo, visima virefu ni tisa (9), kisima hicho cha 10, tumekigeuza katika mpango huo ambao utaelekeza maji katika Vijiji vya Ubembe, Kwemhosi na katika maeneo mengi yaliyopo chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri chanzo kile cha maji hayo ya Ubembe-Kwemhosi, tulishakijenga. Kwa hiyo, Mkandarasi anayekwenda pale, ni kuchimba mitaro na kufukia mabomba, kushusha maji, kuelekea kwenye Vijiji zaidi ya saba (7) ambavyo nina uhakika watafurahi kuona mpango huo unatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipouliza swali hapa kuhusu utekelezaji wa visima hivi vya *World Bank,* kuna eneo tulipata matatizo katika Wilaya yetu ya Muheza. Mkandarasi amekwenda kuchimba kisima katika eneo ambalo silo lililokuwa limefanyiwa tathmini. Sasa amechimba, wataalam wetu wamemuachia, ameondoka na amechukua fedha; tumefanya jitihada, amekwishaitwa. Namshukuru sana kwanza, Mkuu wangu mpya wa Wilaya ya Muheza na *DED* wa Wilaya ya Muheza, ambao wote ni wageni, lakini wamekuja na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Amekwishaitwa Mkandarasi na ametakiwa aeleze ni kwa nini amechimba nje ya eneo? Dhamira yetu ni

kama hatutakuwa tumeelewana, tutakwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Wizara itusaidie. Muheza, tunaye Mwanasheria mzuri, lakini tunahitaji pia nguvu za ziada kwa sababu, hela hizi sio za Muheza tu, hela hizi ni za Taifa. Haiwezekani Mkandarasi akazichukua, akaondoka na tukabaki bila kupata maji. Kwa hiyo, nitaomba msaada wenu, msaidie pia Halmashauri kuhakikisha Mkandarasi huyu anachukua jukumu la kuchimba tena katika eneo ambalo ni dhahiri, tuna imani kubwa maji yanaweza yakapatikana. Kwa hiyo, tunaomba sana msaada kutoka kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee tu kwa kusema Wilaya yetu inahitaji msaada mkubwa wa maji. Tumewavumilia ndugu zetu wa Tanga na tunawavumilia kwa sababu, awali Wilaya ya Muheza ilikuwa ndani ya Wilaya ya Tanga. Kwa hiyo, wametoa maji kutoka Muheza na sisi hatuna maji lakini tunavyo visima vingine, hivyo nilivyovitaja ni viwili tu, tunavyo vingine tumekwishachimba na taarifa zinaonesha kwamba, vina maji mengi. Kuna kisima cha Mpapayu, kinatoa zaidi ya lita 9,000 kwa saa. Tuna kisima kingine Mkuzi, kinatoa zaidi ya lita 16,000 kwa saa. Tuna kisima kingine pia kinatoa zaidi ya lita 9,000 kwa saa. Tatizo ni nini, ni usimamizi na utekelezaji wa miradi ya namna bora ya kutumia visima hivi vikubwa ambavyo tayari tumeshaingia gharama ya kuvichimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe jambo moja, nimeona hapa kuna fedha kwenye Jedwali

Namba 13, fedha za Mfuko wa Pamoja, ambapo Programu hii, fedha hizi zinapelekwa katika Halmashauri. Zimeanza kupelekwa fedha hizo tangu mwaka 2007 na mpaka leo, Wilaya yangu ya Muheza imepata zaidi ya shilingi bilioni 1.3, lakini hakuna hata mara moja ndani ya Baraza la Madiwani tumepewa taarifa ya ujio wa fedha hizo na jinsi fedha hizo zilivyokuwa zinatumika. Vilevile, kama fedha hizo zinatoka Wizara ya Maji, zinakwenda TAMISEMI, matarajio yetu ni kwamba, sasa tutakuwa tunapewa taarifa ya ujio wa fedha hizo, ili tuweze kuzifuatilia. Vinginevyo, wenzetu wajanja wanaendelea kutumia fedha hizo wakati sisi tunaendelea kukosa maji, fedha zimekuja ambazo zipo katika mpango huo wa mfuko, wao wanajengea maofisi ya kifahari badala ya kuhakikisha wananchi wanapata maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji. Kabla sijaanza kuchangia, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa kuteuliwa kushika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa heshima kubwa sana, naomba nimpongeze aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji katika Wizara hii, Mheshimiwa Lwenge, kwa jinsi ambavyo alinipa ushirikiano. Alijali kusikiliza matatizo ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Masasi na aliweza kwenda Masasi, kwenda kujionea jinsi tatizo la maji lilivyo kubwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo wameanza kuutekeleza mradi wa maji wa Mbwinji, kama nilivyoshukuru wakati wa Wizara ya Maji nilipokuwa nachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu wa maji Mbwinji, bado kuna tatizo la watu kutolipwa fidia. Wananchi wa Jimbo la Masasi kwa kutambua tatizo kubwa la maji walilonalo, walipohamasishwa waweze kuondoa majengo yao, kuna watu walibomoa nyumba zao, wengine walifyeka mikorosho yao ili kuweza kupitisha mradi huu wakiwa na imani kwamba maji yatakayoletwa katika Mji wa Masasi itakuwa ni kwa faida ya wananchi wa Masasi. Lakini hadi leo wananchi hawa, huruma ile yote waliyoifanya kwa Serikali ya kuruhusu mradi ule upite, hawajalipwa fidia zao hadi leo. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri afanye haraka sana aweze kuwalipa wananchi hawa fidia zao kwa sababu ni muda mrefu umepita, na mimi ninaporudi Jimboni, napata usumbufu mkubwa sana wa wapiga kura kuniuliza fidia zao watalipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Masasi, kuna Kata 19; lakini katika Kata hizi 19, ni Vijiji viwili tu ndivyo ambavyo vina vyanzo vya maji vya kudumu kwa maana kuna mito. Lakini vijiji vingine vyote, Kata nyingine zote, hatuna mto hata mmoja wa kudumu, na hatuna vyanzo vya maji vya kudumu. Kwa hiyo, Jimbo la Masasi naweza nikasema kwamba kwa asilimia 95 wananchi wangu hawana maji, wanakunywa maji ya kuokota, wanakesha visimani, lakini tatizo hili lingeweza kutatuka kama Serikali ingeanza kuangalia kwanza historia ya huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Jimbo la Masasi, ni kukame, lakini Wamisionari walipoingia Masasi walilitambua tatizo hili kubwa la maji na ndiyo maana walianza kuchimba mabwawa. Walichimba bwawa Lukuredi, walichimba bwawa Mchema, na walianza kuchimba tena bwawa kwenye Vijiji vya Nambawala. Hii yote ilikuwa wanatambua kwamba Jimbo lile kwa visima virefu hatuwezi tukapata maji. Kwa kuthibitisha hivyo, katika mradi wa visima hivi vya *World Bank,* kwenye Jimbo langu la Masasi tulipata visima, lakini hata kisima kimoja kilichotoa maji hakuna. Kwa hiyo, naiomba Serikali, hebu irudi nyuma na kuangalia kwanini Wakoloni waliamua kuchimba mabwawa? Hii inaelekea kwamba walishajua kwamba hata wakichimba visima hawatapata maji huku chini. Kwa hiyo, kwa kuwa tuna bwawa pale Lukuledi, tuna bwawa ambalo halikukamilika pale Mihima, tuna bwawa ambalo lilikamilika lakini likapasuka pale Chiwale, tuna bwawa pale Chingulungulu, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kutoa fedha na kwenda kufufua mabwawa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa lililopo Lukuledi lina maji, lakini bwawa lilichimbwa mwaka 1956, tokea hapo, bwawa hili halijawahi kukarabatiwa hata siku moja. Kwa hiyo, hivi sasa kina cha maji ni kifupi kiasi kwamba maji yanayoingia pale hayatoshelezi kwa mahitaji kwa mwaka mzima. Unapofika mwezi wa Kumi, maji yanakuwa yameshakauka. Kwa sababu Bwawa hili linategemewa na Vijiji saba, vikiwemo na vijiji vya Wilaya ya Nachingwea, wanakuja kuchota maji. Uwezo wa Halmashauri ni mdogo kukarabati hili bwawa, kwa sababu hatuna vifaa na vilevile hatuna fedha za kutosha. Ningeiomba Serikali, tafadhali sana wafanye kila litakalowezekana itafakapofika mwezi tisa au mwezi wa kumi mtufanyie utaratibu wa kupeleka wataalam na vifaa kwa ajili ya kwenda kuongeza kina kwenye bwawa hili la Lukuledi. Wananchi wa Lukuledi wanapata shida sana. Kumekuwa na magonjwa ya milipuko mara kwa mara kwa sababu ya maji wanayokunywa siyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu la Masasi, kama tukitegemea kuchimba visima, tutakuwa tunapoteza fedha za Serikali kila mwaka. Sasa naomba, haya mabwawa ambayo nimeyataja katika vijiji husika, Serikali ingefanya jitihada za kuweza kuhakikisha kwamba mabwawa haya yanafufuliwa ili kuwaondolea kero wapiga kura wangu na wananchi wa Jimbo la Masasi. Vinginevyo tutakuwa hatutekelezi ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo tuliahidi kwamba tukishika madaraka, tutajitahidi kuondoa kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu la Masasi, hata ukienda usiku wa manane ukamkuta mtoto ukamwuliza kero ya Jimbo la Masasi ni nini? Atakwambia ni maji. Kwa hiyo, naiomba Serikali iliangalie Jimbo la Masasi kwa ukaribu kabisa kwa ajili ya kutatua tatizo la maji. Mradi wa maji Mbwinji, hautasaidia sana katika Vijiji vyangu vyote, kwa sababu huu mradi unafika katika Mji wa Masasi na hakuna utaratibu wowote wa kupeleka maji Vijijini. Sasa hivi Masasi imeshakuwa Mji. Naiomba Serikali, maji haya ya Mbwinji yatakapofika Masasi, basi ufanyike utaratibu wa kusambaza maji haya katika Vijiji vyote; Mji, kwa maana ya Temeke, Sululu, Marika, Chisegu, pamoja na Mtandi. Kwa ujumla vijiji vyote ambavyo vinazunguka Mji ningeshukuru sana kama maji haya yatafika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Mbunge atakayesimama hapa tumekuwa na kilio kikubwa kuhusu tatizo la maji. Lakini kama tungekuwa tunapima ukubwa wa tatizo, inawezekana Jimbo langu la Masasi linaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hadithi, wananchi wangu wa Vijiji vya Nambawala, ukifika mwezi wa Tisa ni wakulima wazuri sana wa mahindi, wanavuna sana, lakini kila mwaka wanakuwa na upungufu mkubwa wa chakula kwa sababu wamekuwa wakitumia chakula kubadilisha kwa maji. Katika kipindi cha ukame, ukipeleka *plastic* la maji kule, unapata *plastic* la mahindi. Kwa hiyo*,* utaona tatizo hili limekuwa kubwa sana, havina hata uwiano! Unapeleka *plastic* la maji, unapata *plastic* la mahindi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri anifikirie katika Jimbo la Masasi,

niweze kutatua angalau katika Kata nne. Katika kipindi hiki ukichimba mabwawa, vijiji vingine vitaweza kuwafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye ilani ya Uchaguzi, Serikali iliahidi kuchimba tena bwawa lingine katika mto Myesi. Nataka kujua utaratibu huu ambao tumeahidi sisi wenyewe kwenye ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Bwawa hili la Mchema litakarabatiwa lini na hili bwawa ambalo tuliahidi tutachimba kwenye mto Myesi kazi hii ya kuchimba itaanza lini? Kwa sababu nimesikiliza katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri, sikuona ukitaja na wakati bajeti ya mwaka 2011 tuliahidiwa kwamba fedha zitatengwa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. Utakapokuwa unafanya majumuisho Mheshimiwa Waziri, ningependa kujua kazi hizo zitaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri vilevile aniambie, mabwawa haya niliyoyataja, ni lini Serikali itakuwa tayari kwa ajili ya kufufua visima ili tuondokane na kero ya maji? Lakini la mwisho, naomba kwa makusudi Mheshimiwa Waziri afanye ziara ya kuja kwenye Jimbo langu la Masasi, azunguke kwenye Kata zote ili aweze kujionea jinsi wananchi wanavyopata shida ya maji. Kwa kuzungumza tu hapa, hutaweza kuelewa tatizo la maji lilivyo katika Jimbo langu la Masasi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, afike azuke na mabwawa haya, aweze kujionea mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naishukuru sana Serikali kwa mradi huo ulioonyeshwa

hapo wa maji Mbwinji, ninaamini hizo tu ni mvua za mwanzo, mtaweza kunitekelezea maombi haya yote niliyoyazungumza hapa. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Kasembe. Mimi ni shahidi yako kwa Mheshimiwa Waziri kwamba mradi wa Mbwinji, umesemewa sana.

Sasa baada ya Mheshimiwa Kasembe, kama nilivyosema, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Ally Keissy baadaye kidogo, atafuata Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nfasi. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Sub-hanah-wa-tallah, kunijalia afya njema na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nataka niwapongeze Mawaziri wapya wa Wazara hii kwa kazi ambazo wanaonyesha kuzifanya, lakini Wizara moja sugu ina matatizo mengi. Naamini kwa jitihada zao, wanaweza kufika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kusema, tungeshirikishana. Nilipofika hapa jioni, nilikuta karatasi hii nataka niisome ili huyu aliyeandika karatasi hii ajitokeza hapa. Karatasi inasema hivi: “Mmethubutu, mmeweza kuwanyima Watanzania maji safi na salama ndani ya miaka 50 ya uhuru na mnasonga mbele kufanya hayo hayo wakati mnajua kuwa maji ni uhai.” *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Rudia, rudia!

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni moja ya vitu vyenye thamani kubwa sana katika uso wa dunia hii. Ndiyo maana maji yako ardhini, yako hewani, kwa njia ya mawingu na yanatengeneza bahari. Robo tatu ya uso wa dunia umefunikwa kwa maji, lakini kama unataka kujua thamani halisi ya maji, mwulize zaidi wale ambao hawana maji. Waulizeni watu walioishi katika majangwa na watu ambao wanaishi katika sehemu kame ya nchi yetu wanajua thamani kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upatikanaji wa maji umeendelea kushuka siku hadi siku, kutokana na kuongezeka kwa binadamu, watu na shughuli za kibinadamu kama kilimo, umwagiliaji, mifugo viwanda na kadhalika. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali sasa kuhakikisha kwamba maji haya hayaendelei kupungua na wanayatunza haya yaliyokuwepo kwa kuyapatia bajeti ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili tumelikabidhi Wizara ya Maji, ingawa kuna Wizara ya Mazingira ambayo inafanya kazi kama hii, lakini maji nayo imehusika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoangalia bajeti ya maji kwa miaka sita iliyopita, ukiacha mwaka huu, utakuta kwamba bajeti hii ni ndogo mno, haitoshi hata kidogo. Kwa hiyo, ilikuwa haikidhi haja. Kwa mfano, toka Awamu ya Nne ya Serikali ya Kikwete ilipoanza, bajeti ya maji ilikuwa Shilingi bilioni 77.9 ikaongezeka kidogo ikawa Shilingi bilioni 70, ikaanza kushuka Shilingi

bilioni 46.5, Shilingi bilioni 50.5 ikashuka sana mwaka 2010/2011 ikawa Shilingi bilioni 30.7 na katika mwaka ulipita ilikuwa Shilingi bilioni 41.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari kweli kwa Wizara kama hii ambayo inasema maji ni muhimu, maji ni uhai. Sababu kubwa ya bajeti ndogo kama hii ni kwamba, Serikali haina vyanzo vya mapato ya ndani. Lakini Serikali inasema kwamba sungura mdogo, na kwa kawaida sungura huwa hakui, kimo chake ni kile kile. Kwa hiyo, hatutegemei mabadiliko yoyote. Tunaomba Wizara au Serikali kwa ujumla ihakikishe inaongeza bajeti ya maji. Lakini ukiangalia bajeti ya mwaka huu, kwa mfano, mimi nimeshtuka kidogo nilipoona bajeti mwaka huu ni Shilingi bilioni 485.8, nilisema labda ndiyo wameanza kuthubutu, wanaweza. Lakini la hasha*! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipoangalia bajeti hii ya mwaka huu Shilingi bilioni 485.8, kwanza nilishutka kwa sababu bajeti ya maendeleo ni Shilingi bilioni 465. Katika bajeti hii, mchango wa Serikali ni Shilingi bilioni 140 tu. Kwa hiyo, Shilingi bilioni 325 ni za wahisani au wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hali mbaya sana, kwa sababu tunaendelea kuwategemea wahisani kwa mambo yetu ya msingi. Nchi yetu ni nchi ya kijamaa na kujitegemea. Ingawa ujamaa hauonekani, lakini katika Katiba, ibara ya (9) inasema hivyo, kwamba Tanzania imefuata siasa ya ujamaa na kujitegemea. Tukianza kutegemea wahisani kwa miradi yetu ya maendeleo, basi tunauza uhuru wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la utegemezi limekuwa sasa hivi katika bajeti hii inayoonekana kuwa kubwa, lakini utegemezi ni mkubwa sana. Lakini siyo utegemezi tu, lakini hata utoaji wa fedha zenyewe hauzingatii muda. Kwa mfano, unaweza ukapata hayo makisio yaliyowekwa mwisho wa mwaka. Ninao mfano hapa, bajeti iliyopita hadi 30 Aprili, 2012, mchango wa Serikali kwa bajeti hii ilikuwa asilimi 37.9 tu wakati mchango wa hao tunaowaita wadau wa maendeleo, wenzetu, ni asilimia 14 tu. Sasa utakuta inaonekana kwamba haya makisio yanafanywa, lakini utekelezaji wenyewe hamna. Kwa sababu ikiwa *by* Aprili, mchango ni huu wa asilimia 37 za Serikali na wahisani asilimia 14, tutafika wapi? Tunayo miradi mingi ya maendeleo, haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mnaandaa bajeti hizi, mnasema mnazingatia malengo ya Millennia, malengo ya MKUKUTA, lakini suala hili vile vile lina matatizo yake kwa sababu Serikali haichangii fedha katika malengo ya *millennium*, imelenga MKUKUTA. Kwa mfano, katika malengo ya MKUKUTA imesema ifikapo mwaka 2015, vijiji vyote vya Tanzania viwe vimepata maji kwa asilimia 15 wakati Miji Mikuu ya Wilaya na Mikoa imepata maji kwa asilimia 95 na Dar es Salaam Mji Mkuu umefikia asilimia 75. Lakini katika hili Serikali ina mchango wake na katika MKUKUTA Serikali ilitakiwa itoe Shilingi bilioni 95 kila mwaka, fedha ambayo haipatikani. Utakuta hata hayo malengo ya *millennium* na malengo ya MKUKUTA ambayo

mnayafanya, kwa hakika bado hayatekelezwi kwa sababu Serikali haina fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna program nyingine inaitwa *WSDP,* yaani *Water Sector for Development Program,* ni mradi wa maendeleo ya Sekta ya Maji ya miaka 18, ambayo imeanza mwaka 2007/2008 na itashia mwaka 2025 kwa miaka mitano mitano. Lakini katika mpango huu vile vile, programu kama hii ambayo thamani yake ni Dola za Kimarekani 951, Serikali ilitakiwa kuchangia Shilingi bilioni 75 kwa mwaka, lakini hadi juzi Machi, 2012 imechangia asilimia 51 tu ya fedha hii ambayo inatakiwa kuchangiwa. Kwa hiyo, ni kusema kwamba, hata hii miradi ambayo mnaizungumza katika bajeti zetu ya *millennium* au ya MKUKUTA haitekelezwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwajibikaji, katika matatizo makubwa ya nchi hii na hasa Halmashauri zetu ni kuwajibika. Nafikiri tumeliona sote na katika ripoti ya *CAG* iliyotolewa mwaka huu katika Wizara hii, haikusema kwamba kuna ubadhirifu mkubwa sana wa fedha za umma isipokuwa imeorodhesha mambo matatu ambayo yako katika Halmashauri. Kwanza, usimamizi usioridhisha katika Sekta ya Maji; pili, kukosena kwa baadhi ya nyaraka muhimu; na tatu, kutumia bidhaa au fedha kinyume na maelekezo ya *Memorandum of Understanding.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama hakuna wizi wa fedha wa moja kwa moja, lakini hili suala la kutosimamia vizuri miradi, basi ni ubadhirifu na wizi, kwa sababu wale wanalipwa kama hawafanyi kazi, maana

yake ni kwamba wanaiibia Serikali. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kupitia hizi Halmashauri ambazo kwa kweli…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Sasa namwita Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi na Mheshimiwa Dkt. Dalali Kafumu ajiandae.

**MHE. CHACHA N. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili kuweza kuchangia hoja ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo nataka nijiulize na kama Taifa, tujiulize; kwamba nchi ya Tanzania tumebahatika kupata mito mingi sana. Katika dunia, ni nchi ya 11 kuwa na mito mingi sana, lakini vilevile tuna maziwa makubwa sana kama Ziwa Victoria na maziwa mengi sana na ndiyo maana tunaitwa ‘nchi ya Maziwa Makuu.’ Wanaposema Nchi ya Maziwa Makuu ni Tanzania, na pia tuna Bahari ya Hindi. Kwa nini mpaka sasa hivi tunalalamika kuhusu tatizo la maji? Ina maana uwezo wa kufikiri ndiyo hatuna au tatizo lipo wapi? Naomba kwa kweli nipate majibu kuhusu suala hili.

Pili, nakumbuka mwaka 2009 Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya kuanzishwa kwa mfuko wa maji, yaani *National Water Fund*. Mpaka sasa hivi sijaona utekelezaji wake kama mfuko huu umeanza kufanya kazi na sijui kwa nini. Naomba Waziri atakapokuwa anajibu, awaambie Watanzania, ni kwa nini *National Water Fund* haijaanza kufanya kazi na ilipitishwa mwaka 2009?

Vilevile naomba niishauri Serikali, kwa sababu maji ni sekta nyeti sana, inamgusa kila mtu, badala ya kukimbilia kusimamia barabara na kutengea bajeti kubwa. Barabara ni jambo zuri, lakini vilevile bajeti ya maji inatakiwa iongezeke hata mara tatu zaidi. Pia nashauri tuanzishe kitu kitakachoitwa *TANWATER* kama ilivyo *TANROAD* kwenye barabara, kwani hii itaweza kusaidia sana kusimamia maji katika Wilaya na Mikoa yetu badala ya kutegemea Wizara. Kwa kweli tukifanya mambo kama hayo, naamini tutakuwa tumewataendea haki Watanzania, hasa wale wa Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamka hadharani kwamba suingi mkono hoja na sitaunga daima kwa sababu zifuatazo:-

Moja, mwaka 1985 nikiwa nasoma Darasa la Kwanza, mpaka sasa hivi, Marais waliopita wote, yaani Rais Mwinyi…

**MBUNGE FULANI:** Nyerere!

**MHE. CHACHA N. M. NYANGWINE:** Hapana, Nyerere hakuwepo! Hao wote wametoa ahadi ya maji Tarime, lakini mpaka sasa hivi hakuna utekelezaji wowote ule uliofanyika. Inasikitisha na inashangaza sana na wananchi wa Tarime wamenituma kwa kweli kwamba nisiunge mkono bajeti hii. Mwaka 2011 wananchi wa Tarime walinituma nisiunge mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, nikawaambia hata ikiwezekana tutachukua mapanga, lakini wale wawekezaji walianza kutekeleza. Sasa kama Taifa na Serikali tutachukua nini ili muweze kuleta maji Tarime? Kwa kweli nashangaa sana, na hilo naomba nipate majibu halali na ambayo yatawaridhisha Wanatarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Mkoa wa Mara jina lake linatokana na Mto Mara. Huo mto Mara unapita katika Wilaya ya Serengeti, Rorya, Tarime na Musoma Vijijini, yaani Wilaya zote nne, na tunaotumia maji ya Mto Mara kwa kweli Wilaya ya Tarime na Mkoa wa Mara mzima haungetakiwa kuwa na tatizo la maji. Lakini cha ajabu na cha kushangaza, namshangaa hata Waziri anaposema kuna mpango maalum na mpango mkakati. Kwa nini asigusie mto Mara kwamba maji ya mto Mara kueneza maji vijijini? Kwa mfano, katika Wilaya ya Tarime kuna sehemu inaitwa Nyamwara, pale tungeweza kuweka tanki kubwa sana tukachukua maji kutoka mto Mara na yangeweza kusambaa Tarime nzima na wala msingesikia tunazungumzia maji na ahadi zote zilizotolewa katika awamu ya pili, ya tatu na ya nne.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie ni namna gani tutatumia wataalamu wetu ili tuweze

kutumia maji ya mto Mara kuwanufaisha watu wa Tarime.

La pili, kuna Ziwa Victoria. Unajua Mheshimiwa Waziri haiingii akilini kwamba Ziwa Victoria lipo kilomita 20 kutoka Tarime, lipo kilomita *zero* kutoka Rorya, kilomita *zero* kutoka Musoma Vijijini, kilomita 15 kutoka Bunda, lakini mimi nashangaa kwamba kuna mkakati wa kuchukua maji kutoka mto Mara kuyapeleka Shinyanga, Tabora, Kahama na kadhalika. Kwa nini msitumie maji ya Ziwa Victoria kuwanufaisha watu wa Tarime na wananchi wa Mkoa wa Mara kwa ujumla? Kwa kweli hii haiingii akilini kwamba unaacha maji ya Ziwa Victoria kilomita *zero*, unapeleka huko kilomita 700. Ni akili au ni uwezo wa kufikiri ndiyo hatuna?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hilo nasema ukweli na kwa dhati kwamba sitaungana nalo. Mheshimiwa Waziri nakuomba, wewe ni mpya katika Wizara hii, basi utakapokuja utuletee mkakati maalum wa kuwaambia wananchi wa Mkoa wa Mara na Mwanza na vilevile Mkoa wa Kagera kwamba watanufaikaje na maji ya Ziwa Victoria. Hiyo ndiyo itakuwa akili ya kufikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba tuangalie wananchi wa Tarime, kwa kweli wamenituma na hapa ninayoyasema ni mawazo yao kwamba hawaridhiki na wamechoka na ahadi ambazo hazitekelezeki. Tuangalie namna gani tutatekeleza hizo ahadi. Wananchi wa Tarime bado wana imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hata watakaosema watasema, ndiyo maana walishindwa

na Upinzani, wakaamua kukipatia Chama cha Mapinduzi na wakanichagua mimi. Lakini wananiambia, kwa kweli sasa hivi tujitahidi na tutekeleze...

**MBUNGE FULANI:** Hali mbaya!

**MHE. CHACHA N. M. NYANGWINE:** Hakuna cha hali mbaya! Maana wanafahamu kabisa kwamba Upinzani haukufanya chochote na hautafanya chochote, kwani bado wana imani na ndiyo maana waliamini Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba kupitia kwako mbele ya Bunge hili tuangalie ni namna gani tutawasaidia wananchi wa Tarime. Haiingii akilini kwamba Wilaya ya Tarime ina vijiji 150 na vijiji hivyo 150 hakuna kijiji cha kujivunia kwamba kina maji. Inashangaza kwa kweli! Kama jirani yangu anavyosema kwamba ni kama Ukonga, hatukubaliani na hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengine ambayo ni vizuri tukajiuliza, kwamba, hivi nchi kama Tanzania sasa hivi kwa nini tutegemee kila kitu kutoka kwa wafadhili? Kwenye maji tutegemee wafadhili, kwenye barabara tutegemee wafadhili, tutajivunia nini? Kwa kweli naomba hilo tukae kwa makini tulitafakari. Ni kwa nini fedha za migodi, utalii na kodi zetu tusizielekeze kwenye maji? Tuseme kwamba, basi tutumie sasa fedha hizo kutatua tatizo la maji katika makusanyo yetu yote tunayokusanya, tutatue tatizo la maji vijijini kuliko kukimbilia mijini. Mngelijua shida na

taabu wanazozipata wanawake wa vijijini, kwa kweli hapa wote siyo wageni, wote tunatoka vijijini tunafahamu, tusikimbilie mijini kutatua tatizo la maji Dar es Salaam. Watu wanakimbia wanasema tukae tujadili, kwa nini tusijadili watu wa vijijini ambao wanaangamia kila siku? Kwa kweli naomba hilo tukae na tutafakari kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimesikia Wabunge wa Mkoa wa Kigoma wakilalamika, waliopata kuchangia kuhusu malipo ya maji. Kwa kweli hata siyo Dar es Salaam, tu wala Mara. Unaweza ...

*(Hapa Kengele ililia Kuashiria muda wa Mzungumzaji Kwisha)*

**MHE. CHACHA N. M. NYANGWINGE:** Muda umekwisha?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. CHACHA N. M. NYANGWINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja na ninaomba majibu ya uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine. Sasa namwita Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dalali Kafumu na Mheshimiwa Salum Barwany ajiandae.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mezani kwetu leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze na kusema kwamba maji ni chakula, maji ni uhai, maji ni kila kitu na wote mnalifahamu hilo. Sasa hivi maji imekuwa ni siasa, yaani ni nyongeza ya hayo. Kwa nini nasema hayo? Nasema hayo kwa sababu kila mtu na kila jamii inahitaji maji na maji imekuwa ni tatizo kubwa nchini, aidha kwa sababu ya upungufu wa mvua zinazonyesha, au matatizo ya kutokuwa na maziwa labda au mito. Lakini maji imekuwa ni tatizo kubwa sana nchini. Kila Mjumbe anayesimama kuzungumza, anasema matatizo ya maji. Mimi nasema, pamoja na jitihada za Serikali za kuibua miradi mbalimbali nchini, lakini bado maji ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kwamba kuna miradi ya Uswisi, *JTZ* na ninaomba ninukuu: "Kuna miradi ya *World Bank*, miradi ya Ziwa Victoria ambayo inakwenda Nzega mpaka Kahama, kuna miradi ya *JICA, Quick Wins* na Mbwinji ambayo imezungumzwa hapa, pia kuna kuvuna maji, kuna miradi ya *TASAF* na hata miradi ya *Global Funds*." Miradi hii yote kila mtu anasimama analalamika anasema haifanyi kazi. Kulikoni? Mimi naona sasa hivi imefika wakati Wizara ikae itathmini hii miradi yote pamoja na mingine ambayo sikuitaja ione tatizo ni nini mpaka huu mradi wa mwisho ambao umeletwa siku hizi hizi wa Mzee Sabodo umetajwa hapa, haufanyi kazi, imekuwaje? Wizara ikae itathmini miradi yote nchini na ione tatizo ni nini na ilifanyie kazi ili wananchi wajue tatizo ni nini au

tatizo ni fedha badala tu ya kusikia miradi mingi inatamkwa lakini haifanyi kazi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji Lindi, yaani wote waliozungumza hapa ni Maji Lindi. Maji Lindi ilianza mwaka 1950, nakumbuka ilikuwa ni kwa ajili ya wafanyakazi wa Mkonge wa Lindi na ukakarabatiwa mwaka 1990. Lakini hivi ninavyozungumza, maji hayatoki, mabomba yote yameziba kwa ajili ya chumvi, kwa sababu Mji wa Lindi umezungukwa na bahari, Lindi Mjini huwezi kuchimba kisima kikawa maji, yatakuwa ni maji chumvi, ni lazima yatoke mbali. Kwa hiyo, tunapata shida, tunanunua maji kutoka Masasi ndoo Sh 1,500/=. Naomba tafadhali sana, Wizara ituonee huruma, ije Lindi ione matatizo ya Lindi yakoje.

Waheshimiwa Wabunge, hapa mtasimama, lakini Lindi kumezidi tatizo la maji. Hivyo, tunaomba sana Wizara ije Lindi itazame matatizo ya maji yakoje hapo Lindi mjini, ili basi angalau kisima kimoja kimoja kila Kata, yaani kisima kirefu, basi wangechimba wakati wanasubiri mradi wa *World Bank* ambao upo. Basi hata watumie za Tanzania, yaani *African Bank*, afadhali! Lakini *World Bank* inatusumbua sana. Watuchimbie visima vichache angalau kila Kata ili tuweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wangechimba katika Vijiji vya Mitoro, Kineng'ene, Kitumbikoa, Mtanda, Ndoro, Mikumbi, Rahaleo, Wailes, Gitandi, Msinjaili, Matopeni na Makonde angalau sehemu hizo tu kwa Lindi Mjini. Kulikoni watu kwenda Masasi kuchota maji?

**MBUNGE FULANI:** Aah!

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Ndiyo tunachota Masasi! Kwa hiyo, Lindi Mjini kuna matatizo makubwa sana ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la maji Nachingwea. Nachingwea tulikuwa tupate mradi wa Mbwinji. Mradi wa Mbwinji una miaka 15 na zaidi unazungumziwa. Wabunge waliopita, wa sasa, na watakaokuja watausikia huu mradi wa Mbwinji unatoka Masasi unakwenda Nachingwe. Masasi watapata na sisi tutapata, lakini sasa lini utakwisha? Tunaomba tafadhali Wizara itusaidie, Nachingwea ni jangwa tu, hakuna maji wala mto na hakuna chochote mpaka maji yatoke huko huko Masasi yaende Nachingwea. Kule kumejaa migodi ya dhahabu tu, ni jangwa. Kwa hiyo, tunaomba huu mradi wa Mbwinji basi uishe tupate maji Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusu Maji Rongwa, Liwale na Mchinga, lakini pia Mbunge wa Mchinga amesimama na amezungumza kuhusu Kilolambwani na kadhalika, kwamba hakuna maji. Sasa tatizo la maji nasema ni la nchi nzima, kwa sababu watu tumeongezeka. Tunaomba sana mtusaidie maeneo ya Kusini, tusikose kila kitu basi, angalau maji mtusaidie, tafadhali Wizara mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala la mwisho ambalo Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga

amesimama na kuzungumza kwa uchungu mkubwa kuhusu Jimbo la Mchinga. Wenzetu walipata mradi wa Sabodo na miradi mingine mingine, lakini miradi ile bado haijatoa maji. Yusaidieni, ni mpaka lini? Tunapata shida sana na jamii ya Jimbo la Mchinga inapata shida sana. Mheshimiwa Mtanda mmemsikia hapa anasema. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ije hasa kwa makusudi katika Mkoa wa Lindi ili ifanye tathmini ya miradi yote ya maji, kwa nini maji hayatoki, na vipi mtusaidie maji katika Mkoa wa Lindi kwa ujumla pamoja na Lindi Mjini na Nachingwe ambao ni waathirika wakubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatuma Mikidadi. Kama nilivyokwishaeleza, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Dalali Kafumu na Mheshimiwa Salum Barwanyi ajiandae.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, nampongeza pamoja na wataalamu wake kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuanza kujenga daraja la Mbutu ambalo lilikuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Igunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Igunga kama nilivyowahi kusema awali ni Wilaya kame labda kuliko Wilaya zote katika nchi ya Tanzania. Hii inatokana na jiolojia yake kwamba iko kwenye bonde la Manonga na bonde la Wembele. Mabonde haya ni ziwa la zamani la Victoria lililokauka. Kwa hiyo, miambatabaka yake haina maji chini hata ukichimba huwezi kupata maji. Kwa hiyo, kati ya Kata 26 za Wilaya ya Igunga, ni Kata 16 zipo kwenye bonde hili. Kwa mfano, Kata za Kininginila, Vijiji vya Mwanyagula, hakuna maji kabisa.

Mheshimiwa Wasira tulivyokuwa kwenye kampeni na Wabunge wengine, kwa kweli mliona. Nitamwalika Waziri tukimaliza hapa akatembelee Igunga Kata ya Mwamashimba, Kinungu, Mbutu, Itumba, Chomachankora vyote hivi vipo katika bonde la Manonga na bonde la Wembele, hakuna maji. Hata tukichimba visima hatuwezi kupata maji. Kwa hiyo, suluhisho kubwa la maji katika Wilaya ya Igunga katika mabonde hayo ni kuchimba mabwawa. Bahati mbaya tuna mabwawa mawili tu tangu Uhuru, tunahitaji tupate mengine mawili katika miaka mitano mitano ijayo. Pamoja na kwamba kwenye bajeti yako hakuna, naomba utafakari juu ya jambo hili kwa sababu sisi hatuna maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuchimba mabwawa, ni suala la msingi, na ninaomba labda bajeti ijayo kama siyo bajeti hii muweze ku-*reallocate* tupate hata bwawa moja. Ukiangalia hii *speech,* Wilaya ya Igunga tuna miradi ya Vijiji viwili tu, yaani Ilemela katika Kata ya Mwisi na Busomeke. Ni vijiji viwili tu. Lakini pia kuna ile miradi ya kuchimba visima,

tumechimbiwa visima 13, visima sita tu ndiyo vina maji na hali yetu ni mbaya na hii ni kwenye maeneo ya juu ambayo siyo ya Bondeni. Kwa hiyo, tunahitaji mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mito kwa mfano, Manonga, Mbutu, Ulugubu na mito mingine tunaweza tukatengenezewa mabwawa mawili makubwa na tukapunguza matatizo ya maji Igunga. Bajeti haijatupendelea. Wenzangu angalau kuna miradi unaweza ukaona isipokuwa Kigoma. Lakini Igunga nayo tunafanana na Kigoma. Mheshimiwa Waziri naomba utakapokuwa unahitimisha, basi ufikirie kuitazama Igunga kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda unakimbia sijui kama nini, nizungumzie ukurasa wa 33 wa kitabu cha hotuba ya Waziri. Kama nilivyosema, hotuba inataja Vijiji vya Busomeke na Kalemela Kata ya Mwisu tu. Ukiangalia Ukurasa wa 93 pia utaona ile miradi ya maji tumepata visima sita tu sijui kwa muda gani, maana sijaangalia. Sijui ni mwaka mmoja! Hivi havitoshi kabisa. Naomba juhudi za aina ya pekee zichukuliwe kwa ajili ya Igunga ili tuweze kupata visima vya kutosha, lakini pia tupate mabwawa makubwa na siyo madogo kwa sababu sisi hatuna Ziwa. Wenzetu wanazungumzia ziwa Kilomita *zero*, sisi hakuna Ziwa. Wenzetu wanazungumzia mito kilomita *zero*, sisi hakuna mto ambao una maji kwa kipindi cha mwaka mzima.

Kwa hiyo, tuna matatizo makubwa sana na ndiyo maana Wasukuma wengi ilibidi tuhame kwa sababu maji hamna, wale tuliobaki sasa ndiyo tunahangaika.

Unakwenda kuchukua maji kilomita; akina mama inabidi waamke usiku sana. Kwa mfano, ukienda Kijiji cha Mwanyagula, utakuta akina mama wanaamka usiku kwenda kwenye bonde la mto Manonga huko wakachimbe bondeni. Ni taabu kubwa kweli kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie, itengeneze mkakati mzuri kwenye Wilaya kama hizi ambazo hazina maji kabisa, basi na sisi tupate angalau kidogo. Vinginevyo, kwa kweli ni kazi kubwa, kwani maji ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo maji katika Mji wa Igunga. Mji wa Igunga unapata maji kutoka bwawa la Igogo, wengine wanaita Bulenya. Maji haya yanakuja kama yalivyo. Kwa hiyo, wananchi wa Igunga wanakunywa maji ya tope ambayo ni ya ajabu kweli kweli. Tulikuwa na mradi wa kujenga chujio kwa ajili ya mji huu. Mradi huu umesuasua kweli na hadi ninavyooongea sasa hivi, ukiwauliza watendaji, wanasema wiki ijayo tayari. Sasa hivi nimepiga simu chujio halijaanza kutumika. Kwa hiyo, wananchi wanapata maji ya ajabu kweli kweli. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri ashughulikie jambo hili angalau basi Mji wa Igunga upate maji hata mazuri basi, na siyo tope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine ni huu wa Benki ya Dunia ambao Waheshimiwa Wabunge wengi wameuzungumzia, na kwa Igunga hakuna tofauti. Tuna mradi wa kupeleka maji katika vijiji vya Mbutu, Isakamaliwa, Ibutamisuzi, pamoja na vijiji jirani

vya Hindishi na kadhalika. Mradi huu mabomba yametandazwa, lakini ulifanya kazi siku moja tu. Inaonekana kuna tatizo la kiufundi mahali fulani na ndiyo maana haujaanza kufanya kazi. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri basi atusaidie kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema tena kwamba, Wilaya ya Igunga ni kati ya Wilaya kame katika nchi yetu na tuhitaji kutazamwa kwa jicho la huruma na tofauti. Wenzetu wenye maziwa na mito karibu, hawana matatizo, lakini sisi tuna taabu kubwa. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kupitia Waziri, atakapokuwa anahitimisha, basi angalau afikirie hata ku-*reallocate* fedha kwa sababu kwenye bajeti hii sijaona kabisa mahali ambapo ninasaidiwa. Afanye *reallocation* kidogo na sisi tupate hata mradi mmoja mdogo, na hasa bwawa moja kubwa katika kipindi cha miaka mitatu hii, kufikia mwaka 2015, tutakuwa tumefanya jambo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kumaliza muda wangu wote kwa sababu niliyotaka kuyasema nimeyamaliza. Namwalika tu Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake, Mheshimiwa Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, nawakaribisha Igunga waje waone jiolojia yetu na waone jinsi tulivyo na matatizo na labda watatutengenezea mradi unaofaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja nikiomba nipatiwe mradi mmoja angalau wa bwana katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi hii na mimi nipate kuchangia jioni ya leo katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niseme umuhimu wa utawala bora katika nchi yoyote ambayo inafuata misingi ya demokrasia, ni kuhakikisha kwamba, utawala ulio ndani ya Taifa hilo unawawezesha wananchi kunufaika kwa kuhakikisha huduma za jamii ambazo ndiyo lengo kubwa la kuwepo utawala huo zinapatikana katika nchi hiyo. Hatuna maana ya bora utawala. Lakini katika mambo muhimu ambayo yanapatikana katika utawala bora ni hizo huduma za jamii kama vile maji, barabara na hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo sisi Wabunge tupo hapa kama tunampigia Mbuzi gitaa. Ni kauli za muda mrefu za Wabunge juu ya kilio chao cha maji, na siyo kilio cha Wabunge tu, bali ni kilio pia cha wapiga kura wetu walio Majimboni ambao wanatutuma tuje tuseme. Lakini bado Serikali haijatoa jawabu la tatizo la maji katika nchi hii, leo ikiwa ni takribani miaka 50 na hakuna jibu. Bajeti zimepita nyingi tu, lakini bado hazijaweza kutoa jawabu juu ya tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa bajeti ya safari ya 2012/2013 ni Shilingi bilioni 485, lakini imeonekana kwamba, hapa mahitaji yote ya bajeti hii yanategemea wahisani ili tuweze kupata maji katika maeneo yetu. Hii inatukatisha tamaa. Shilingi bilioni 325

ni fedha ambazo zinahitajika kutoka kwa wahisani ambao sasa wana masharti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahisani wana masharti ambayo tumeshindwa kuyakamilisha ndani ya kipindi cha miaka 50. Wahisani wanahakikisha kwamba, hawatoi misaada yao kama bado hatujawa na utawala wa demokrasia katika nchi zetu; hawawezi kutoa misaada yao kama hatujawa na utawala bora na pia utawala wa sheria katika mataifa yetu. Sisi tunajua hayo na tumeshindwa kukidhi haja ya wahisani kutupa misaada. Hivyo, kwa hii Shilingi bilioni 325 kama haya hatujayatekeleza, ni ndoto kwa wahisani kutusaidia kututoa katika janga la maji katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Serikali iseme wazi kwamba tatizo la maji katika nchi hii litaisha lini. Hatuna tatizo la maji kama maji, maji tunayo katika nchi nzima; kuna maziwa makubwa, na mito inayotiririsha maji kila siku kwenda huko katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo duniani kuna nchi nyingine ambazo wanatumia maji ya bahari kupata maji katika nchi zao. Kuna majangwa huko, lakini hawana tatizo la maji. Ni aibu kwa Taifa la 50 Wabunge tunapoteza fedha za wananchi kuja hapa kuomba maji. Watanzania hawaombi maji, wanataka maji. Maana yake nasikia Wabunge wenzangu hapa wanaomba maji, mimi watu wa Lindi wameniambia usiende kuomba maji, kawaambie tunataka maji. Ni

jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya *World Bank* ambayo imzeungumziwa kwa kiasi kikubwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni kilio cha muda mrefu. Lakini iwe wazi kwamba, miradi ya *World Bank* imeshindwa kukamilisha majukumu yake. Wananchi wamechangishwa fedha katika maeneo mengi, na sasa wanadai fedha zao zirudishwe. Wananchi wanataka zile fedha ambazo walichangia katika miradi ya *World Bank* zirudishwe na tuna hakika kabisa katika akaunti nyingine, fedha hizo hazipo. Fedha zimeshatumika, wananchi hawajapata maji na fedha zao leo hazijulikani zipo wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la mpango wa *World Bank* katika maji ni vitu ambavyo vinawakatisha tamaa wananchi ambao wamechangia na hawana matumaini tena kwamba, wanaweza kupata maji kupitia miradi ya *World Bank*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu nizungumzie kidogo kuhusu Jimbo langu la Lindi. Kuna vyanzo vitatu vya maji katika Mji wa Lindi, Kitunda, ambapo sasa hivi Serikali inakarabati mabomba ya mjini pale ili kupata maji. Lakini kinachosikisha sasa hivi, ni kwamba, Serikali ilikurupuka katika mradi ule wa chanzo cha maji cha Kitunda. Imeonekana kwamba pale hakuna maji ya kutosha, na ndipo Serikali sasa inaandaa mradi

mwingine wa kupata maji kutoka katika kijiji cha Ng'aka. Mnaona ni jinsi gani Serikali inapoteza fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wataalam wa kutosha ambao wanafanya *research, survey* lakini baada ya siku tunaambiwa kwamba pale hakuna maji. Fedha nyingi zinapotezwa katika kufanya *survey* kwa lengo la kutafuta maji katika maeneo mbalimbali, lakini mwisho wa siku wanapokwenda wataalamu kuchimba katika maeneo yale, maji hayapatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nini hapa? Hatuna wataalam wa kutosha? Hatujasomesha wataalam katika sekta hii? Hiyo inaonesha kwamba, kila tunachojaribu bado ni matatizo. Hatuna uhakika wa mambo yetu. Kuna nini hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri aje atupe ufafanuzi kwamba, kwanini *survey* wanafanya *research* katika maeneo, lakini mwisho wa siku maji hayapatikani katika maeneo yale?

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha maji kilichopo Lindi leo ni chanzo cha Wakoloni. Wakoloni tayari walikuwa na mashamba ya mkonge kule na hivyo wakawa na vyanzo vya maji kwa ajili ya mashamba yao. Sisi kwa kushindwa tukaenda kuchukua maji yale ili kuuboresha mji wetu wa Lindi, lakini hata hivyo bado maji hayajatosheleza katika Mji wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie ahadi za Rais. Tumezungumza mara nyingi katika

Bunge hili kwamba, ahadi za Rais ni kama sheria katika nchi. Ahadi za Rais ni kitu cha kukienzi, lakini leo ahadi za Mheshimiwa Rais zimekuwa ni jambo la kawaida tu. Mheshimiwa Rais anakuja anapata hamasa katika mapokezi yake, watu wanamshangilia na anaahidi jambo pale, lakini mwisho wa siku hakuna utekelezaji wake. Mheshimiwa Rais ameahidi mambo mengi, ameahidi katika Vijiji vya Kineng'ene, Chikonji na maeneo mengine ya Manispaa ya Lindi kwamba atatoa Shilingi milioni 328 kwa ajili ya Mradi wa Maji katika eneo la Mtange. Fedha hizi zimetoka hazina, taarifa tunazo, lakini mpaka leo hatujui zimekwenda wapi. Hazina inasema fedha zimekwenda kwa *RAS, RAS* anasema hebu mwulize Mkurugenzi wako wa Halmashauri ya Mji wa Lindi, wanapigiana mpira tu. Sasa tupo katika kizungumkuti. Ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kitu cha kukienzi, lakini matokeo yake ahadi hizo hazitekelezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Mamlaka za Maji za Miji. Hapa kuna mkinzano mkubwa kati ya Halmashauri zetu na hizi mamlaka. Nani ana mamlaka kamili katika hili? Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi. Leo Lindi kuna mgogoro mkubwa kati ya *LOWASA* Mamlaka ya Mji wa Lindi pamoja na Manispaa ya Mji wa Lindi. Kuna mgongano wa maslahi hapa. Kuna Kijiji cha Mingoyo ambacho kuna mradi wa maji pale, mradi ule tayari wanasema *LOWASA* wanataka kuushughulikia, wautengeneze na waweke pampu, lakini Halmashauri ya Manispaa wanasema hapana mradi huu utashughulikiwa na Halmashauri. Sasa hii ni hoja ya muda mrefu, hakuna maji Mingoyo. Tatizo ni kupata mashine na *LOWASA* wanasema

uwezo wa kupata mashinde tunao, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi wanasema hapana, sisi tutamiliki mradi huo. Hapa kunaonekana kuna mgongano mkubwa wa maslahi katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie ulinzi wa mazingira. Wazee wetu wa zamani walikuwa na hekima kubwa kabisa. Walikuwa wanatunza mazingira kwa hekima na busara zao. Walikuwa wanaweza kuwaambia kwamba, bwana msitu ule pale msiingie unatisha, una wadudu wabaya, majini na mashetani, hapafai kuingia. Ile ilikuwa ni hekima katika kutunza mazingira yao. Lakini leo mazingira yetu yanaharibika kwa makusudi kabisa. Tuna maprofesa, tuna wataalam, lakini wameshindwa kuwashauri wananchi kwamba mazingira yanaweza kuboresha maisha yetu. Leo vyanzo vyetu vya maji vinaharibika kwa sababu maeneo ambayo maji yalikuwa yanatunzwa yameharibika. Hebu tuangalie wazee wetu walikuwa na hekima ya namna gani. Watu walikuwa hawawezi kuingia katika msitu ovyo ovyo. Walikuwa na hekima kubwa na kweli maji yalidhibitiwa na sisi tumekuta katika nchi hii maji yanapatikana kwa uhakika, hata kama mabomba yenu haya wakati huo yalikuwa bado hayajapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni maisha. Tunashughulika leo bilioni za fedha zinapekelwa katika majeshi huko, lakini bado maji hayajapatikana. Watanzania wanataka maji; Watanzania hawaombi maji kutoka Serikalini, wanataka wapatiwe maji ili wayatumie kuboresha maisha yao na pia katika Kilimo. Hatutaki kutegemea mvua leo, hivyo tunategemea

tupate maji ili tuweze kuendesha kilimo chetu ambacho leo kinahitaji kiboreshwe kupitia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kumaliza muda wako, kwa hayo machache, nasema siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya tatizo la muda mrefu, nimetoa mchango wangu kwa maandishi, lakini nitaongea pia machache kadri muda utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba maji siyo kama umeme, kwa sababu ukikosa umeme unaweza ukawasha kibatari au mshumaa na ukaendelea kuishi, lakini ukikosa maji huwezi kuishi. Ukikosa dawa hospitalini wakati mwingine unaweza ukatumia dawa za miti shamba, na ukapona, lakini ukikosa maji huwezi kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitakwenda moja kwa moja kwenye Jimbo langu la Arumeru Mashariki kwa sababu nafahamu kwamba miongoni mwa maeneo ya nchi hii ambayo yana vyanzo vingi sana vya maji ni Wilaya yangu ya Arumeru. Lakini miongoni mwa Wilaya nyingi nchi hii ambazo zina matatizo makubwa ya maji, nafikiri Arumeru tunaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiingia kwenye *website* ya Serikali inatuonesha wazi kabisa kwamba, tuna

vyanzo vingi vya maji nchi hii kuliko hata matumizi ambayo wananchi wanahitaji. Kwa hiyo, tuna *source* kubwa ya maji ambayo inazidi mahitaji ya wananchi, lakini cha ajabu leo hii tunajadili matatizo makubwa ya maji kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa sababu najua Waziri ananisikiliza, sijui ni hujuma au nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 80 ya magonjwa vijijini yanatokana na ukosefu wa maji safi na hii ni kwa mujibu wa *website* ya Serikali. Lakini vilevile ukiangalia sera ya maji inayotumika mpaka leo hii ni ya mwaka 1991 muda ambao uhitaji wa maji ulikuwa ni tofauti sana na leo hii. Kwenye *Website* hiyo ya Serikali inasema kwamba, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji kwa umbali usiozidi mita 400. Lakini leo hii kwenye Jimbo langu, kwa mfano, kumekuwa na maafa makubwa kwa sababu ya tatizo la maji. Moja, kumekuwa na vifo kwa sababu ya maji. Kwa mfano, kuna wananchi kwenye baadhi ya Kata ambao wamepata ajali wakigongwa na magari usiku wakiwa wanasomba maji kwa baiskeli. Wananchi hao wameacha yatima na wajane kwa sababu ya tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo peke yake, kwenye Jimbo langu kuna watoto ambao wamekosa masomo kwa sababu ya kuhangaika na maji. Kuna akina mama ambao wanashindwa kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa sababu ya kuhangaika na maji. Nitaongelea Kata kadhaa kati ya 17 zilizopo katika Jimbo langu. Kati ya hizo, Kata 10 hazina maji. Kata ya

King'ori na vijiji vyake na juzi tu ndiyo tumetoka kwenye kampeni Arumeru na hivyo nafahamu kwamba, wote tuliona wawe wa CHADEMA. Chama cha Mapinduzi na baadhi ya Mawaziri walikuwepo na waliona. Kata ya King'ori kuna tatizo kubwa la maji. Kata ya Leguruki wananchi wanalazimika kusafiri mpaka kilomita 13 kwenda kwenye Majimbo jirani ya Hai na Siha kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hapo pekee, Kata ya Engaranyuki na vijiji vyake na ninaamini kwamba, Mheshimiwa Waziri ana-*note* ili baadaye atupe majibu mazuri hapa. Kata ya Kikatiti na vijiji vyake, Kata ya Maji ya Chai na vijiji vyake, Kata ya Kikwe, Kata ya Makiba, Kata ya Akeri, Kata ya Mbuguni na hata Kata ya *Usa River* ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya yetu, na siyo maeneo yote. Lakini kwa mfano kwenye hii Kata ya *User River* ambayo ni Mamlaka ya Mji Mdogo kumekuwa na tatizo kubwa la maji. Kwanza, wananchi hawapati maji, halafu vilevile maji siyo ya uhakika, lakini bado wananchi wanadaiwa maji kwa *flat rate*. Yaani ankara zinakuja kwa watu, mtu mwingine amepata maji mara moja kwa wiki na mwingine hajapata kabisa, lakini ankara zinapokuja, wote wanadaiwa gharama za maji kwa kiwango sawa. Nitaomba Mheshimiwa Waziri atupatie majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kwenye Jimbo hili tuna vyanzo vingi vya maji kama nilivyosema; tuna Ziwa Duruti ambalo *volcanic labe* lina maji mengi ambayo yanatokea chini ardhini, lakini cha ajabu ni kwamba, Serikali imeshindhwa ku-*invest* nguvu zozote kuhakikisha kwamba, pengine tunavuna haya maji na

tunaweka mtambo wa kuyasafisha kama ilivyofanyika kule Iringa ili wananchi wa Arumeru na Majimbo yote mawili ya Mashariki na Magharibi na pengine hata Arusha Mjini waweze kutumia maji haya.

Vilevile tuna chemchemi nyingi sana, tuna *slopes* za Mlima Meru ambazo zinatoa maji, tuna chemchemi za maji katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha *(Arusha National Parks),* maeneo ya Patandi Tengeru, Vijiji vya katikati ya Magadirisho na Teema, lakini cha ajabu ni kwamba wananchi hawafikiwi na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena cha kushangaza ni kwamba tuna mashamba ya maua ya wawekezaji wakubwa ambao yale mashamba hayajawahi kukosa maji. Tuna hoteli nyingi za kitalii ambazo hazijawahi kukosa maji, tuna viwanja vya gofu ambapo Wazungu wanacheza gofu Arumeru hawajawahi kukosa maji na nyasi zinanyweshwewa kwa maji haya haya. Tuna viwanja vya michezo ya Farasi *(Polo Clubs)* Wazungu wanakuja kuendesha farasi kwenye viwanja vinavyonyweshewewa maji lakini wananchi wetu wanakosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha atatupa majibu stahiki ni kwa nini hizi *efforts* zote Serikali hazijazifanya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji. Lakini vile vile ningependa kufahamishwa kwamba ni kwa nini wawekezaji hawa wamechukua maji ya wananchi halafu wameyapeleka kwenye *investments* zao na wananchi wanakosa maji. Hivi ni kweli kwamba tunawathamini sana wawekezaji kuliko wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani tupate wawekezaji, ndio, watuletee ajira na kadhalika, lakini sioni sababu ya wananchi wangu kupata ajali na kugongwa na kufariki na kuacha yatima na wajane eti kwa sababu mwekezaji wa Shamba la Maua Hoteli, sioni sababu ya wanafunzi kukosa masomo shuleni kwa sababu wakitumia muda mrefu kwenda kutafuta maji kwa sababu ya wawekezaji, sioni sababu ya akinamama na wazee kushindwa kufanya kazi za kilimo kwa sababu ya kwenda kutafuta maji kilomita 13 mpaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mambo ambayo wananchi wa Arumeru Mashariki wangetamani kupata majibu stahiki na niseme tu kwamba, sitakuwa tayari kuunga mkono hoja mpaka nipatiwe majibu ya masuala haya ya msingi kabisa kwa sababu kama nilivyotangulia kusema maji ni uhai na maji nafikiri kabla hatujazungumzia masuala ya daraja la Kigamboni, *flyovers* au barabara sita au tano kwenye nchi yetu tunapaswa kuzungumzia kwanza maji, kabla hatujazungumzia sijui masuala ya daraja la Mbutu tunatamani kusikia wananchi wanakunywa vipi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kugongewa kengele naomba niishie hapo, lakini naamini kabisa kwamba wasomi hao wawili Profesa na Daktari watakuja na majibu mazuri wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti ya Wizara yao. Naomba kumaliza kusema siungi mkono hoja mpaka nipate majibu stahiki

na wananchi wa Arumeru wakiniambia wameridhika, nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Livingstone Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed kutoka Namanyere.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kama ilivyo kawaida yangu nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kupata fursa ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu sana, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyokuwa tukisema mwanzo kwamba, kwenye nyanja fulani nchi yetu imeendelea kiasi ambacho siku hizi unaweza ukagundua kwamba mtu anataka kukuua kwa macho tu, nchi ina maendeleo makubwa sana. Kwa hiyo, kwenye nyanja zingine mngetuwekea vitu vizuri nako tungenufaika sana. Maana hata leo mimi kuna mtu alikuwa ananifuata fuata nyuma simjui nadhani yule naye anataka kuniua. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, nataka nizungumze mambo machache kuhusu maji. Jimbo la Mtera ni miongoni mwa Majimbo yenye matatizo makubwa sana ya maji. Kuna vitu ambavyo lazima tuvizungumze ili Serikali isikie iweze kushughulikia matatizo ili watu wapate maji. Wabunge waliotangulia wamesema vizuri sana kuhusu hali ya

uchumi kwamba unadorora, akinamama wanachelewa kwa sababu ya kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme kwamba, wakati mwingine akinababa wanalalamika sana, muda ule wa kutengeneza Watanzania wapya, mama anainuka kwenda kutafuta maji. Katika mazingira kama hayo hatutendi haki kwenye ndoa za watu, hatutendi haki kwenye maisha ya watu na tunakosea wakati mwingine hata kuruhusu uvunaji wa Watanzania wapya hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipita katika Kijiji cha Mvumi Makulu mahali alipozaliwa Chifu wa Wagogo Mtemi Mazengo pana foleni kubwa sana ya maji, ndoo zinakaribia hata kufikia 2,000 watu wanasubiri maji. Lakini hebu tujiulize kitu kimoja, hivi tunawezaje kuitegemea *World Bank* katika kila jambo. Vile visima 10 wamechimba, lakini wameviacha kama vilivyo. Watu waliona maji siku wanachimba, eti sasa tunawangojea mpaka watufungie mashine, hivi jamani ni hali gani hiyo? Mtu umuombe unga, mboga na kila kitu kama chumvi halafu baadaye watoto wanakuuliza mbona hujapika unasema nasubiri wanipe na sufuria, haiwezekani. Mradi wameshachimba na kuna baadhi kuna maji, sisi wenyewe hatuwezi kuchukua hatua yale maji tukayatumia, mpaka tusubiri *World Bank* waje watuletee? Jambo hili haliwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo kama Mvumi *Mission* sasa hivi sio Kijiji tena pale limekuwa Jiji, kuna wakazi karibu 23,000. Ukienda pale unakuta kisima cha maji kilichotengenezwa na Mzungu Biliges mwaka 1030

haiwezekani. Hebu ndugu zangu tuangalie kwani watu wana matatizo makubwa ya maji. Hawa akinamama ambao ndio tunawategemea wazalishe wanashinda kutwa nzima wanasubiria maji. Nenda kaangalie kama Kijiji cha Chinoje, utakuta matatizo ya maji, Kijiji cha Naguloo mabwawa yaliyochimbwa wakati wa Mwalimu Nyerere yamefukiwa. Hivi tunashindwa hata kuvifukua, hivi imekuwaje jamani! Ndiyo maana kuna siku nimeuliza tumelogwa na ndio maana naamini matatizo mengine yanayotupata Dodoma yanasababishwa na jela hii ya kunyonga watu na hospitali ya vichaa, nyie hamtaki kuamini, mngeviondoa hivi mngetukumbuka kwenye baadhi ya mambo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kuna vitu vinatusumbua mno. Leo hii tunataka kurudisha eti JKT. Hivi hawa watoto wa shule watakwenda JKT mara ngapi. Sasa hivi shule ya msingi ni kama JKT, asubuhi mtoto anadamka na kuni, anadamka na dumu la maji, na mfuko wa daftari, ni kama yuko jeshi tayari. Hivi tunataka kuwapeleka jeshi mara ngapi, ni vitu ambavyo haviwezekani, hebu tuboreshe huduma za msingi. Leo hii mzazi akienda kujifungua aende na dumu la maji, aende na mafuta ya taa, hivi hatuoni taabu, tuzingatie baadhi ya huduma za msingi, watu wetu wapate maji ya kunywa, wapate maji safi na salama. Tunazungumza maji karne hii ndio maana mnaona watu wengine wanapigapiga kelele, watu ambao wasingekuwa na hoja lakini wanapiga kelele. Juzi hapa tumeona Wizara ya Ujenzi, wanasema sasa lami, wanageukia upande mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dodoma hauna mto hata mmoja unaotiririsha maji mwaka mzima, wenzetu wenye mito, wenzetu waliopata lami, waliopata maji kidogo mngewaacha nao mkageukia wengine, kwani hii inasumbua nini mbona sehemu nyingine mmefanya hivyo. Kwenye barabara mmefanya hivyo, sehemu zingine mmefanya hivyo, watu wana mito inatiririka maji miaka yote na hatutaki kufanya hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siasa za kusema labda tunataka kuchimbana, hapana mmewasikia hata Wabunge wengine wanasema wanachota maji sehemu fulani, sasa kwa kuwa wanapo wanakochota, msingewapa, muwape wale ambao hawana na mwaka mwingine mtawapa wengine. Haiwezekani ukienda kwenye Jimbo la Mtera, Vijiji karibu vyote havina maji. Kuna Kijiji cha Ng'wenda tangu uhuru hawajaona maji, haiwezekani! Kuna vijiji kama Mlowa bwawani pale liko bwawa Mheshimiwa Daktari Shein aliahidi kulichimba pale, kila nikienda wanasema Makamu wa Rais aliahidi, nani anayezuia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie fursa hii kuwaambia maji ni tatizo kubwa mno katika Mkoa wa Dodoma. Mkoa wetu ni mkame, kwa hiyo, tunataka mtusaidie, Serikali wekeni nguvu kubwa katika maji tumekosa vitu vyote. Tumekosa hata stendi ya mabasi mnaona kuna ki-*corner* tu kile pale, tukose na maji ya kunywa jamani. Chondechonde kuweni na huruma. Ndiyo maana labda hamtaki kuja lakini Mungu anatusaidia, sasa hivi mtahamia tu huku maana juzi nilisikia mlikimbiakimbia tu mkaogopa lile tufani la maji

pale, iko siku mtakuja tu hapa Dodoma. Kwa hiyo, hili suala la kuhamia Dodoma sisi hatutaki kulizungumza tena. Tunajua tu kwamba maji yakiwatisha kule mtakuja tu huku Dodoma muwe mnataka au hamtaki. Kwa sababu sasa tumeona imekuwa hadithi ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nichukue fursa hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri atembelee Jimbo la Mtera, liko karibu na hata kama huna mafuta basi mimi nikuwekee twende hapo Jimboni kwangu uende ukaone watu wanavyopata tabu kutafuta maji. Watu wanafuata maji mpaka kilomita 16 au 17. Akinamama mpaka wameota misuli (vigimbi) kwa ajili ya kutafuta maji, kwa nini jamani tunawatesa watu wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mingapi tangu tumepata uhuru mabwawa ya maji yamechimbwa, yapo yamejaa tope kufukua tunashindwa? Hivi jamani hatuoni kwa macho hata kupapasa tunashindwa. Nataka niseme kwa uchungu mkubwa sana tuhakikishe watu wetu wanapata maji. Zahanati zetu hazina maji, shule hazina maji. Siku hizi eti ni zamu mtoto kwenda na dumu la maji shuleni wapi na wapi. Tuboreshe huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza maji kwa nini, nenda katembelee katika Jimbo langu kila Kijiji utakuta shida kubwa inayowakabili wanakijiji ni maji na nimewaambia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu sijakusikia ukitaja hata bwawa lile la Sasajila, Serikali imepoteza pale karibu shilingi milioni 700 na bwawa

lenyewe halina maji. Siku hizi tuna wakandarasi sijui nao wa Kichina maana yake inaonekana kila kitu cha Kichina hata kuchimba bwawa likajaa maji inashindikana. Kuna Wanabloo pale wanataka bwawa kuziba tu ili waweze kupata maji ya kutosha mwaka mzima na ukiwatumbukizia samaki pale wala hawana haja ya kwenda Mtera tena kwenda kuvutana na watu kule. Tuangalie nguzo za umeme zinapita na hata maji tukose jamani, chondechonde hebu tazameni haya mambo kwa huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwenye bajeti hii nimeipitia sijaona mahali popote na naogopa kuunga mkono kwa sababu watu wangu kukosa maji ndiyo ninachoogopa. Maana nikisema naunga mkono wakati maji hawapati ninachounga mkono nini sasa, ndicho ninachokiogopa. Siwezi kusimama hapa nikamwambia Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja wakati sina hakika kama Jimbo la Mtera linapata maji. Sasa nitakuwa naunga mkono nini, si nitakuwa nafanya vichekesho hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe atakapokuwa akijibu aseme Jimbo la Mtera tunapata wapi maji ili nitakapounga mkono wale waseme *swadakta* ameunga mkono, tunapata maji. Kwa hiyo, sitaki kufanya kazi hapa ya maigizo, tunataka kuhakikisha Serikali mnatuletea huduma ya maji. Ikifika saa tisa usiku ndio muda mzuri wa kuanza kulala, pale mama anainuka anakwenda kutafuta maji, wapi na wapi hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tunawanyima wananchi wetu raha, tunawanyima wananchi wetu utulivu, leo hii ndoa zinavunjika mnauliza kwa nini zinavunjika, zinavunjika kwa sababu ya maji. Tuhakikishe kwamba watu wanapata maji tuone kama ndoa zitavunjika, tuhakikishe watu wanapata huduma bora za maji, magonjwa yatapungua, tuhakikishe watu wanapata huduma bora za maji uchumi utakua, muda mrefu mtu kutwa nzima anakwenda kukaa anasubiria maji, haiwezekani. Nendeni mzunguke katika Vijiji Makang'wa na kadhalika, kote kuna tabu ya maji. Kuna visima tulivyochimbiwa na Wakoloni zamani hata wakija alama zake wanazijua. Tumewapeleka pale Profesa na huko *Engineer,* tena Jimbo langu apita Manzase na Sasajila watu wanakunywa maji pamoja na mifugo, kitu ambacho hakiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuunga mkono hoja kwa sababu sina hakika kama tutapata maji, mkituambia tutapata maji nitaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde kwa mchango wako na ni kweli taratibu zetu za Bunge lazima ku-*declare interest*. Hata mimi na-*declare interest* jamani Vijiji vya Kongwa maji hakuna. Kwenye kitabu hiki hakuna Kongwa hata mahali pamoja. Kwa hiyo, msione nimekaa hapa nimenyamaza. Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby. (*Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa niseme nisije nikasahau siungi mkono hoja kwa vyovyote vile. Nashauri na nimesikia Wabunge wengi sana hapa, ni kitu cha ajabu sana Naibu Spika anazungumza kuwa kwake pia hakuna maji, halafu anasema naunga mkono hoja ni kichekesho. Tushirikiane wote kama wakati ule wa Nishati na Madini, hii Wizara naishauri ivunjwe, iunganishwe pamoja na Nishati na Madini iwe Wizara moja, maana yake haina faida. Hakuna maji kabisa na hii Wizara ivunjwe. Sio kuchekesha maana kila mtu akisema hapa hakuna maji mwishoni anasema naunga mkono hoja ni vichekesho. Kwa hiyo ndugu wasikilizaji huko wananchi wote hao wanaosema wanaunga hoja kwao wana maji wanatudanganya hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema Wilaya yangu ndio inayoongoza, haina maji anaunga mkono hoja, sio kweli ana maji huyo. Nimezungumza nilipoingia Bungeni kuhusu Namanyere, hakuna maji, ni kweli hakuna maji. Mwaka 2010 nimezungumza, 2011 nimezungumza na 2012 nazungumza Namanyere hakuna maji na siungi mkono hoja na katika kitabu chake sikuona. Kila siku ananiambia lete makadirio namtuma Mhandisi wa Maji lete makaratasi anakuja hapa ananichezea mchezo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja na hii Wizara tushauriane ivunjwe, tumshauri Rais aivunje haina faida kwa wananchi. Tuna maji katika Afrika nzima tunaongoza kwa maji, lakini haina faida yoyote hii Wizara. Kwa hiyo, wapanguliwe tu, waunganishwe

kama wakati wa zamani wa Awamu ya Kwanza ilikuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini na tulikuwa na maji, leo imebaki Wizara moja, maji hakuna. Kwa hiyo, ivunjwe. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anasimama Mbunge kabisa ametumwa na wananchi wake anazungumza hakuna maji, halafu mwisho anasema naunga mkono hoja, ni kichekesho! Wabunge wa namna hii ndugu zangu wananchi mnaowasikiliza huko hao sio Wabunge wamekuja kupiga makofi hapa muwaone, hawafai na hawafai kuitwa Wabunge wa kuwatetea wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwe wasaliti ndugu zangu cha ukweli kisemeke maji hakuna na bila maji hakuna uhai, hakuna kujenga nyumba, utaishije bila maji, huwezi kufanya chochote bila maji. Namanyere haikui kwa sababu hamna maji. Cha ajabu mnapeleka maji kule kule. Dar es Salaam juzi maji ya bomba yamekatika Waziri mwenyewe amekwenda kusimamia, yeye mwenyewe kule Dar es Salaam kwa sababu ndio wako binadamu kule, kwetu sisi hakuna binadamu, sitakubali kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kijiji cha kule Wampembe mradi wa maji umekwenda, vijiji vinne maji ya kutega tu. Lakini ni ajabu wamekwenda kununua *pipe* za kunyonyea maji, zinapasuka ovyo ovyo, vijiji vile vinakosa maji, maji ya kutega tu. Hakuna maji yoyote. Awamu ya kwanza Kirando kulikuwa na maji na matenki mawili, maji yanamwagika. Namanyere maji, Chala maji, Kabwe maji leo hakuna maji. Awamu ya nne, maji yalikuwepo na leo maji

hakuna na ni Wizara moja zamani kulikuwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini Waziri wake Al-Noor Kassam maji yalimwagika. Sasa tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ziko Uswiss kule shilingi bilioni 300 kazichukueni ziende kwenye maji. Mheshimiwa Mpina amesema shilingi trilioni 11 wameiba leteni. Hapa tumezungumzia fedha za rada, mimi nilikuwa wa kwanza, nipeni fedha za rada kwa ajili ya maji Namanyere, leo wanachakachua hata kwenye vitabu watulazimishe, fedha zetu wakanunue vitabu wakati tuna shida ya maji, ndugu zangu tutafika wapi. Mpaka tushikiane fimbo. Nimefika Karema, Kaparamsenga na Ikola kuna mabomba kule ndugu zangu ya mabilioni yametupwa mradi wa kilomita 15 wakati wa awamu ya kwanza mabomba yale ya chuma, leo watu wanajengea majumba wanajengea masoko, ahaa imekaa kama hamna mwenyewe, mali ya yatima na wananchi hawana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa M.A.J. Sabodo wamegawana wakubwa wakubwa tu hapa. Tuliujua huo mradi wa Sabodo si wamegawana wajanja wajanja tu hapa hakuna cha tathmini. Hii Wizara ya Maji inasaidiwa na nchi 16, Mashirika 41 lakini hakuna maji. Nchi 16 ameandika katika kitabu chake hiki hapa. Nawashukuru hizo nchi 16 na wafadhili Mashirika mbalimbali ya Ulimwengu 41, nimehesabu lakini maji wananchi hawana sasa unasema hii ni Wizara. Hii ibanguliwe tu. Huu mradi wa *World Bank* anatuambia visima viko tayari Wilaya ya Nkasi vitano, lakini hata kimoja hakitoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu hawa wamekuwa kama Waganga wa Kienyeji wanachimba sehemu maji hakuna. Tafuteni basi kama mnawataka kwa sababu waganga wa kienyeji wanapiga ramli waone wapi kuna maji wachimbe, msione aibu. Kuna waganga wanaweza wakapiga ramli wakakuambia hapa kuna maji utachimba, utapata maji si ajabu. Unachimba hamna maji, unachimba hamna maji mabomba yanapotea chini. Tutafute waganga wa kienyeji tusione aibu. Kule kwetu mnaweza mkawapata, msione ajabu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Wachina Sinza. Sinza yalipita mabomba ya Kichina mpaka leo hamna maji. Mnakalia hapa miongozo, taarifa, Sinza haina maji. Mabomba Wachina walichimba mji mzima, lakini leo Sinza haina maji, mnakalia miongozo, taarifa wakati Jimbo lako halina maji, Sinza haina maji. Kwa hiyo bila ya kuniambia uhakika wa maji Namanyere sitaunga mkono hoja na ndugu Wabunge wote mliosimama hapa nnasema kwamba hamna maji Majimboni, msiunge hoja mkono. Kwa hiyo, isipite hii Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii isipite kwa mbinde yoyote na Mbunge kama atapitisha hii Wizara amewasaliti wananchi wake, ndugu zangu mumkatae kwenye Jimbo. Wananchi mnasikia huko mliko Mbunge atakayepitisha Wizara hii labda kwake kuna maji, lakini kama hakuna maji, tunaamka saa kumi za usiku na niliwaambia, mimi ni Mbunge, nimekaa Namanyere siku tatu sijakoga. Sasa fikiri kama mke wako hajakoga siku tatu hana hali gani? Wewe

mwanaume siku tatu mwanamke atakuwa hali gani, hatutakubali sisi kwenda kwenye visima na mikuki. Wanawake wamekuwa kama masanza kwa kupigania ndoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maneno mengi, wewe umesema Jimbo lako la Kongwa halina maji na wewe usiunge mkono hoja. Kama utaunga mkono hoja na wewe utakuwa umewasaliti wananchi wako wa Kongwa. Hapa hapa kura ipigwe, hii Wizara ibanguliwe, iunganishwe pamoja na Wizara nyingine, wale wote ambao wameshindwa kutupatia maji, waende kule wakatafute maji na wakatuchimbie maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na siungi mkono hoja kabisa mia kwa mia mbili. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Huyu ni Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed kutoka Namanyere. Mheshimiwa Ahmed Shabiby atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa ni mmoja wa wachangiaji katika Wizara ya Maji. Kwanza nianze na hii *paper* ya taarifa ya utekelezaji ya programu ya maji vijiji, miradi katika vijiji 10. Nimeingia Bungeni toka mwaka 2005 na kila mwaka katika kipindi cha bajeti lazima hii taarifa iletwe. Hii yote ni kwa ajili ya kuwaweka sawa Wabunge kukubaliana na kuipitisha bajeti pasipo utekelezaji. Wabunge wote waliopo katika kipindi cha kwanza cha Awamu ya Nne wameshuhudia, kitu cha kwanza lazima hii ripoti iletwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi sielewi kuna matatizo gani? Ukiangalia katika Wilaya yangu ya Kilosa ambayo sasa hivi tumegawanyika na kuwa na Wilaya ya Gairo. Huu Mradi wa Vijiji kumi vya *World Bank* bado uko pale pale kwenye usanifu wa miradi. Maana bado tuko namba moja hatujafika namba nne. Kuanzia 2006 mpaka sasa hivi tupo namba moja, usanifu wa mradi. Jana ndiyo limekuja lile gari la kisima kwenye Kijiji cha Kibedya na kuchimba kisima kimoja, jana na mpaka sasa hivi ninavyozungumza maji yamepatikana, lakini najua hiyo itakuwa ni hadithi tu inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niulize kitu kimoja, hii Wizara kama kila siku kwenye hii miradi ambayo Wabunge wengi tunalalamika haitekelezeki na kila siku haiendelei basi ni bora ifutwe tufahamu kwamba hii miradi haipo. Kuliko kwenda vijijini kuwadanganya watu halafu miradi yenyewe haitekelezeki. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kuna mradi wa maji wa Gairo. Naishukuru Serikali imenipa mradi wa maji wa shilingi bilioni 6.664 katika Mji Mdogo wa Gairo. Huu Mji Mdogo wa Gairo ni moja ya miji saba iliyopata huu mradi na mradi huu ulitakiwa tangu Mkandarasi anasaini hadi kwisha kwa mradi huu ni miezi 18. Lakini tunavyozungumza mpaka sasa hivi tayari ni miezi 24, miaka miwili na ndani ya miezi 24 bado hapa Hotuba ya Waziri katika hii miji saba anazungumzia mji mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimnukuu, anasema: "Mji wa Ikwiriri umefikia asilimia 80 ya mradi huu na Miji ya Gairo Kibaigwa, Turiani, Kilosa na Mvomero inaendelea vizuri na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji." Lakini hajazungumzia imefikia asilimia ngapi? Sasa hii naona ni propaganda. Kwa sababu ina maana hapa hata haelewi miradi hii imefikia wapi. Kwa nini katika miji saba azungumzie asilimilia 80 ya Mji wa Ikwiriri. Kwa nini anazungumza hivi, kuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie kwamba katika mradi wa Gairo, mradi huu umesimama na hauendelei kama alivyoandika hapa. Mkandarasi yupo pale matanki yote yamejengwa kuna tanki la lita milioni moja limekwisha, kuna matanki mawili ya lita laki tatu tatu yameshakwisha, lakini kwenye kuchimba kisima, kilichimbwa kimoja kikapatikana maji, viwili havina maji. Baadaye wakaja wataalam wa kutoka Wami Ruvu, wakatoa ushauri kwamba kile kisima kilichochimbwa badala ya inchi nane sasa kipanuliwe kiende inchi kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule mkandarasi ameleta lile gari la kuchimbia visima pale limekaa siku kumi. Mkandarasi ameandika barua kwa Mtaalam Mshauri, Mtaalam Mshauri akaandika *MORUWASA* Mkoani, *MORUWASA* wamekaa hawatoi majibu kwamba yule Mkandarasi aendelee na kipimo cha mwanzo au na hiki ambacho amepewa ushauri na Ruvu *one*. Mpaka leo ule mradi umesimama tu, hauendelei na Mkandarasi naye amekaa tu haendelei. Sasa sijui tunafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongea na Mheshimiwa Waziri mwenyewe ananiambia tu tayari, tayari. Majibu yale ya haraka haraka, yaani yale anakufurahisha. Mimi sitaki kufurahishwa na mtu, nataka kufurahishwa wananchi wa Jimbo la Gairo tu. Sasa ukiangalia kwa mfano, kama *MORUWASA* pale, wanachelewesha huu mradi. Huyo Mkurugenzi mwenyewe wa *MORUWASA* ameajiriwa toka mwaka 1993 mpaka leo. Amestaafu, kaongezewa muda, amestaafu tena ameongezewa muda na mabadiliko hakuna Mkoa mzima wa Morogoro hauna maji. Kwa vile tu anakula na wakubwa kule Wizarani bado yupo mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa mzima wa Morogoro una matatizo ya maji tu na amestaafu kwa ajili ya uzee. Sasa kama tunaendelea hivi, hivi hawa wataalam ni hawa wazee tu, hivyo Vyuo Vikuu vyote wanavyosoma hawawezi kuwataalam au hizi ajira za ukoo sasa? Maana umri wake unaweza ukamzaa Kapuya, lakini mpaka leo bado yupo palepale na hii miradi haiendelei. Sasa sio kwamba tu siungi hoja mkono kwa sababu ya kumwogopa Mheshimiwa Keissy, hapana, isipokuwa siungi mkono hoja kwa sababu nataka maelezo ya kutosha. Kwamba huu mradi utaisha lini kwa sababu muda wake wa kuisha umeshakwisha tangu miezi sita iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale pale maji inatakiwa maji yakishatoka kwenye kisima, iletwe mashine ya kuchuja maji, lakini mpaka leo, hiyo mashine haikuagizwa. Kwa hiyo, mradi ule bado utachukua

muda wa mwaka mzima tena. Sasa nikikaa hapa naunga hoja mkono itakuwa haina maana yoyote na Mheshimiwa Waziri kama watu wanakuficha hapa, wakati Baraza limevunjwa na sisi tulijua na wewe ni mmoja wa wasiorudi. Lakini kwa vile umerudi, tunajua Mheshimiwa Rais ana imani na wewe na ufanye mambo mazuri kwenye Wizara ya Maji kuonesha wananchi kwamba wewe kweli unamudu hii Wizara na unamudu Uwaziri. Kwa hiyo, nategemea kwamba na ukabila uliopo *MORUWASA* kwa Waziri wetu mpya na hutaongeza tena muda kwa Mkurugenzi anayefuata kwa sababu mwezi huu muda wake unakwisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa ahmed Shabiby, Mbunge wa Gairo. Sasa namwita Mheshimiwa Jerome Bwanausi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi. Mheshimiwa Bwanausi!

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii ya Wizara ya Maji. Lakini pili, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ambayo ameitoa leo ambayo inatarajiwa kuwa na matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba inaonesha kwamba kwa kweli bado hatupo

*serious* katika suala zima la kuondoa tatizo la maji hapa nchini kwa sababu tatizo ambalo linawakabili Watanzania kwa sasa ni maji. Lakini kama hatutengi fedha za kutosha kwenye maji maana yale hatujalipa umuhimu tatizo ambalo Watanzania wanalo. Naendelea kuishauri Serikali kwamba lazima tuweke mkakati wa kuhakikisha tunapata fedha za kutosha ili kuhakikisha miradi ya maji inapatiwa fedha na kuondoa tatizo la maji ambalo linawakabili Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Lulindi wana tatizo kubwa sana la upatikanaji wa maji. Katika Jimbo hili kama walivyoeleza Waheshimiwa Wabunge wengine, tatizo si maji. Tatizo ni jinsi ya kuyaondoa yale maji kutoka kwenye chanzo na kuyafikisha walipo wananchi. Chanzo cha maji cha Chiwambo ambacho ni kikubwa kabisa ambacho kina uwezo wa kuweza kulisha ama kuweza kuwapatia wananchi wa Kata tisa bila tatizo kimekuwa kikisuasua katika suala zima la kurekebisha miundombinu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo hiki kilianzishwa na mkoloni mwaka 1955 na maeneo ya Kata tisa yalikuwa yanahudumiwa na maji kuanzia miaka hiyo nayo ni Kata ya Ululindi, Namalenga, Mbuyuni, Chungutwa, Nanjota, Lipumbulu, Luwakala, Uchauru pamoja na Malele. Lakini kutokana na kutoiangalia vizuri miundombinu ile, imechakaa na kutokana na ongezeko la watu mabomba yale yaliyoko ambayo yalikuwa ya inchi nne na inchi tatu yalipaswa kubadilishwa ili kuwezesha wananchi wote waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishafanya tathmini ya kufanya ukarabati ya miundombinu hii karibu miaka kumi iliyopita, lakini kwa tathmini ya gharama ya mradi ule ya mwaka jana inatakiwa milioni 385, lakini Wizara mpaka sasa imepeleka milioni 50 tu na mradi huu ni kama umetelekezwa kwa kuwa hatupatiwi fedha za kutosha ili mradi huu uweze kuboresha maisha ya wakazi walioko katika Jimbo la Lulindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara na namwomba sana ndugu yangu Profesa Maghembe atakapokuwa anafanya majumuisho awaambie wananchi wa Jimbo la Lulindi ni lini utekelezaji ule wa mradi utafanyika kiuhakika. Maana kupeleka milioni 50 kwenye eneo lililotakiwa milioni 385 ni kutotekeleza huo mradi. Kwa hiyo, naiomba Wizara itakapofanya majumuisho yake inishawishi kama walivyonituma wananchi wa Lulindi, kuunga mkono baada ya kupata uhakika wa kupeleka fedha kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalokabili Wizara ya Maji ni kutokuwa makini katika utaratibu wa kupanga miradi, lakini pia katika utekelezaji wa miradi yenyewe, fedha nyingi sana hata katika huu mradi wa *World Bank* utakuta fedha nyingi sana zimelipwa kwa ma-*consultant*, fedha nyingi sana zimelipwa kwa wakandarasi baada ya kufanya *geophysical survey*. Lakini unashangaa fedha amelipwa Mkandarasi ya kufanya *geophysical survey,* lakini matokeo yake kisima kinachimbwa maji hayapatikani. Kwa mfano, katika Wilaya ya Masasi tulipangiwa kupata visima 12.

Nimeshangaa kidogo taarifa ya Hotuba ya Waziri inayosema kwamba katika visima 12 visima 10 vina maji. Taarifa hizi alizopewa labda na watendaji nadhani zina kasoro kwa sababu ni kisima kimoja tu ndicho kilichopatikana na maji na ndicho kitakachowekewa miundombinu. Visima vingine 11 haviwezi kufungwa pampu kwa sababu visima hivyo havina maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ni kwamba kwa nini kwenye maeneo haya ya mradi huu wa *World Bank* maeneo ambayo hayakupata maji kwa maana ya visima fedha zile ambazo zipo basi zielekezwe katika kuchimbwa mabwawa na katika maeneo ambayo yanahitajika mabomba yapelekewe mabomba ili wananchi waweze kupata maji pale. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho yake atoe ufafanuzi juu ya makubaliano na wenzetu wa *World Bank* kwenye yale maeneo ambayo yameonekana maji hayawezi kupatikana kwa kuchimba visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara pamoja na kwamba inapeleka fedha kwenye Halmashauri zetu, lakini lazima kuwe na kitengo cha Wizara kitakachokuwa kinasimamia utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Halmashauri zetu. Baadhi ya Halmashauri zetu hazina wataalam wa kutosha, kwa hiyo, bado Wizara inahitajika kutoa *support* ili kuhakikisha kwamba miradi ile ambayo inapangwa iweze kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema suluhisho la miradi hii ya maji ni kupatiwa fedha. *Priority* ni maji, hivi kwanini tusitafute hata vyanzo vingine tukaiongezea Wizara ya Maji ili tatizo la maji lianze kuondoka, tunabaki kulalamika. Tuondokane na kulalamika sasa tuthubutu kutekeleza. Hii Wizara ya Maji ambayo wengine wanailalamikia ivunjwe, Waziri yoyote atakayekaa pale kama fedha hazipo huyo Waziri ataonekana hafai. Kwa hiyo, suluhisho hapa ni kuhakikisha fedha zinapatikana ili Mawaziri na Watendaji waweze ku-*perfom* na kuweza kutekeleza miradi hii. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuhakikishe kwamba, kama tulivyofanya kwenye Wizara ya Nishati na Madini tuliahirisha kupitisha ili kutafutwe aina nyingine ya upatikanaji wa fedha ili Wizara iweze kutekeleza miradi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya namsubiri Mheshimiwa Waziri atoe maelezo yatakayowaridhisha wananchi wa Jimbo la Lulindi juu ya ukamilishaji wa miradi hasa mradi wa Chiwambo ambao ni ukombozi kwenye Jimbo la Lulindi. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo katika sekta hii ya maji. Awali ya yote, naomba niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru sana Mungu aliyetuwezesha kukutana jioni ya leo tayari kwa kazi iliyo mbele yetu ya kupitisha Bajeti ya Maji kwa sababu maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Mikoa niliyotembelea kwa mapokezi na heshima kubwa waliyonipatia na kuniwezesha kwenda mpaka Karagwe, Ngara, Kishapu na maeneo mengine yote niliyotembelea. Naomba niwahakikishie kwamba, nimefurahishwa sana na maandalizi ya ziara yenu na naomba niwaambie nimefika salama, ahsanteni sana endeleeni kutekeleza kazi ambayo tumekubaliana bila wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, nianze sasa kuchangia hotuba hii kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa sababu Bajeti hii kwa kweli imelenga kumkomboa Mtanzania na hasa wanawake. Natofautiana na Wabunge wenzangu ambao hawaungi mkono kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita nilisimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu nikaiomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kwenye kitabu hiki cha Bajeti nimeona Serikali yetu hii sikivu imeweza kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi ya miundombinu ya Ruvu, Mpiji, Mpera na bwawa la Kidunda. Kusema ukweli kama fedha zitapelekwa kwa wakati na mradi ukatekelezwa kama ulivyopangwa. Mwaka 2014 utekelezaji wa Ilani ya CCM utakuwa umefanyika kama ambavyo tumekubaliana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba niishukuru Serikali, nimshukuru Waziri na watu wake kwa

kazi nzuri sana kwa kuona kwamba Jiji la Dar es Salaam lazima lipate fedha nyingi za kutosha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu iliyopangwa. Lakini naomba nitoe ushauri kwa mambo machache yafuatayo:-

Naomba kuishauri sana Serikali pamoja na mipango mizuri iliyowekwa ya kutenga fedha kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine naomba sasa Serikali ijitahidi kuhakikisha fedha hizi zilizotengwa zinapelekwa kwa wakati katika mamlaka inayohusika ili miradi hii iweze kutekelezwa kwa wakati. Lakini vilevile naomba sana katika Mamlaka zinazohusika zijitahidi kusimamia fedha hizi zilizotengwa zote ili miradi hii itekelezwe bila ubabaishaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie Mradi wa Maji Mgango, Kyabakari na Butiama. Mradi huu tuliupokea kutoka kwa wakoloni miaka zaidi ya 90 iliyopita. Mpaka hivi sasa mradi huu unasuasua.

Kwanza pale kilipo chanzo cha maji, Kata ya Mgango, wananchi wanaozunguka chanzo kile cha maji Kata ya Mgango, Kata ya Kiriba na Kata ya Tegeruka na mpaka hata vijiji vinavyozunguka Kata ya Kyabakari na hata Butiama yenyewe ambapo ndiko liliko kaburi la Baba wa Taifa, kusema ukweli mradi huu bado una suasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iendelee kumuenzi Mheshimiwa Baba wa Taifa aliyetangulia mbele ya haki ili mradi huu uweze

kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya Mgango, Kyabakari na Butiama ambayo imechoka. Lipo tatizo pia la wafanyakazi ambao wako pale wana zaidi ya miaka ishirini na nne hata mshahara bado hawajaupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala la Mradi wa Maji Vijijini. Kwanza naomba niipongeze sana Serikali kwa jitihada zake kubwa za kuhakikisha wananchi walio vijijini wanapata maji safi na salama na ikiwezekana kufikia zaidi ya 65%. Mimi niko katika Kamati ya Maji. Katika Kamati tulizungumza vya kutosha na pia tuliona lipo tatizo katika kutenga fedha kwa ajili ya kupeleka maji vijijini. Kabla sijaja hapa nilikuwa vijijini na kuona wanawake wanavyotembea kilomita zaidi ya 10 kwenda kutafuta maji, naiomba Serikali katika mwaka ujao wa fedha 2013/2014, tujitahidi sana kufanya sekta ya maji kuwa namba moja katika kutenga fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wananchi hawapati maji ya kutosha, hasa wanawake ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa nchi hii, wanashinda wakitembea masafa marefu kutafuta maji bila mafanikio hata hiki tunachosema Kilimo Kwanza na hapa tunaposema kuimarisha uchumi wa nchi yetu hatutaufikia. Mwaka huu nitaunga mkono bajeti hii, lakini mwaka kesho kama sikuona fedha zimetengwa kwa ajili ya kupeleka maji vijijini itabidi niushike mshahara wa Waziri ili Serikali iongeze fedha kwa ajili ya Miradi ya Maji Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie kuhusu kupeleka fedha katika ujenzi wa miundombinu iliyochakaa katika baadhi ya miji yetu na majiji yetu. Naupongeza huu mpango wa Dar es Salaam, naishauri sana Serikali kuwa, huu mpango wa kuimarisha miundombinu na kuboresha miundombinu usiishie Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri Mkuu anawasilisha bajeti alitueleza kabisa ni jinsi gani ambavyo Serikali imepiga hatua katika kukarabati miundombinu katika baadhi ya miji na taarifa ilionesha kwamba iko baadhi ya miji zaidi ya 19 ambayo miundombinu imeboreshwa na wananchi wanapata maji safi na salama kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba sasa imefika wakati Serikali itenge fedha za kutosha ipeleke katika mamlaka za miji ambako miundombinu ni ya siku nyingi, imechakaa na matokeo yake sasa maji badala ya kuwafikia watumiaji yanapotea na wananchi hawapati maji kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie Mradi wa Vijiji Kumi ambavyo Wabunge wengi wamekuwa wakichangia na walio wengi wamekuwa wakionesha masikitiko yao juu ya utekelezaji wa mradi huo. Katika Kamati yetu na sisi tulitoa masikitiko makubwa sana chini ya Mwenyekiti wetu Mwakyusa, tuliishauri Serikali na tuliiambia kwamba sasa ifike wakati tujue moja kama shida ni Benki ya Dunia watuambie, kama shida ni wananchi wameshindwa kuchangia, tujue, kama hatuna

wataalam wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza mradi huo tufahamu, maana kusema ukweli baadhi ya vijiji wamechanga fedha zao, wamejitolea kwa hali na mali, wamejenga miundombinu, lakini unakuta pale kwenye kijiji pampu tu inafanya mradi usianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba sasa ifike wakati Waziri anapofanya majumuisho atuambie na awaambie Watanzania huu Mradi wa Vijiji Kumi upo au haupo ili tujue moja. Lakini wakati wa Kamati Waziri alileta mpango mzuri sana na hapa leo nimeuona ameuwasilisha kwamba sasa Serikali inakuja na mpango mwingine wa kupeleka kila vijiji vitano tunaimarisha miundombinu ya maji. Naomba mpango huu pia tuupe kipaumbele cha pekee na fedha zitafutwe popote pale na najua inawezekana, siyo lazima tutegemee bajeti hii, Serikali ijikite hata kutafuta fedha za dharura ili tuimarishe maji katika maeneo yetu ya vijijini, inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kwa kuwa wakati fulani nchi yetu ilipata mafuriko, miundombinu yote ya barabara ikaharibika na ya maji pia ikaharibika. Serikali ilipeleka fedha miundombinu ile ikarudi, kwa nini Serikali isiweze kutafuta fedha za dharura ili iweze kuimarisha masuala haya ya maji katika vijiji vyetu ili wananchi na wanawake waepukane na adha hii? Naiomba Serikali ijitahidi sana kufuta kodi za madawa ya maji kwani katika baadhi ya maeneo tunapata matatizo kutokana na kodi za madawa ya maji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa*

*muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Ooh ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini bajeti hii iangaliwe upya ili iweze kuongezwa. *(Makofi)*

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naanza kusema hivi, siungi mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Naungana na Mheshimiwa Keissy aliyesema kuwa Mbunge anayeunga bajeti hii mkono hafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabomba yanawekwa ardhini miaka na miaka, Serikali inakusanya pesa tu kwa walala hoi, maji yatoke yasitoke wananchi wanatoa pesa huku wanazidi kuneemeka maofisini. Naweza kusema mengi sana, lakini nataka kuanza kusema hivi mimi ni mkazi wa Kizwite Mjini Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa Mtakatifu wa Mungu, Padri Luka alipoona Wanarukwa hawana maji alikwenda akachimba kisima mwenyewe, akaweka mabomba, akasambaza kwa wananchi mwenyewe kwa pesa yake na siyo pesa ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikaona uchu ikaanza na yenyewe kwenda kupachika mabomba pale, ikaanza kuwauzia wananchi, yale maji yalikuwa yanatoa vyura, yalikuwa yanatoa samaki na matope ili huyu Padri awasaidie watu wa Mungu Serikali ikaanza kukusanya pesa, tunakunywa maji yana vyura yanatoka kwenye bomba, yananuka, ukimwita fundi unakuta chura ameshakufa miguu imeshanyooka au samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wanasema tumeboresha miundombinu tena maji yana siku hayatoki, maji yanatoka machafu, kuna watu wamekuja kwangu ni mashahidi, maji ya Rukwa hata kuoga ni shida, yanatia kinyaa. Lakini leo nitashangaa Mbunge wa Rukwa atakayeunga mkono bajeti hii. Visima vyote havifai, vilishakufa na Serikali hii ndiyo iliyosema kwamba Watanzania wote mkae pamoja tuwape huduma wanashindwa nini sasa kutupa huduma. Kuna watu wako Kasesya kule, kule kuna Uhamiaji, kuna Forodha, kuna *TRA*, kuna sijui Afya, yaani watu wamekaa kule kama shimoni. Jamani ukienda wanakunywa maji ya njano, ya kuchota mtoni, wana visima viwili lakini havikarabatiwi, watu wamekata tamaa na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuliwawajibisha Wizara ya Nishati na Madini kwa nini hawa wasiwajibike? Inaonekana kuna kasoro, kuna utendaji mbovu, ni lazima tuseme ukweli. Serikali hii ilikiri wazi nilipouliza swali wakasema wananchi wa Rukwa tunawapa maji machafu wakati wa kiangazi kwa sababu maji hayatoshelezi, huwa tunapachika bomba kule halafu linasambaza maji kwa wananchi. Tunaendelea kununua maji machafu na mita zinazunguka, matope yanazunguka kwenye mita, nikaomba basi mtutolee mita ili mtukisie tu kwamba tutalipa kama zamani shilingi elfu tano kila Kaya. Sasa maji ni machafu huwezi kupikia wala huwezi kuoga, nafikiri Wanarukwa watatuunga mkono Mheshimiwa Keissy wala usihofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niseme kwa kuwa shida kubwa kwa Watanzania wengi ni maji naamini Wabunge wote mtaniunga mkono. Tarehe 12/1/2012, Rais Barack Obama wa Marekani alisimama mbele aliomba Bunge lake Tukufu liidhinishe Dola za Kimarekani Trillioni 1.2 kwa ajili ya kutimiza ahadi mbalimbali. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu atawaambia nini Watanzania ambao wamepoteza watoto wao wapendwa, waume zao wapendwa na wake zao kwa ajili ya kunywa maji machafu, watu wanapata milipuko ya magonjwa *typhoid,* sijui nini kila siku hospitalini hawafanyi kazi za maendeleo, matokeo yake ni kuugua kila siku. *( Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Waziri asimame hapa kama hawezi kuiwajibisha Wizara yake asimame na atuahidi kwamba Serikali itatenga fedha kwa sababu ili sisi Wabunge tuidhinishe, watu wetu wanywe maji safi na salama, tumechoka kuona vilio vinavyotokea kila siku. Watu wa Rukwa tuna masikitiko makubwa, wenzetu wa Longido, Monduli na Ngorongoro walipofiwa ng'ombe walilipwa ng'ombe, lakini sisi watu wa Rukwa hata kupewa maji safi na salama imeshindikana. Katika Serikali hii ni kitu ambacho hakiwezekaniki, tunaona maji ya kijani yanatoka, hii Wizara ndugu zangu muiangalie kwa undani, hatuwezi kuunga mkono hoja bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kusema mengi, nasema siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa safari hii namwita Mheshimiwa Lucy Nkya, mzungumzaji wetu wa mwisho kwa jioni hii ya leo.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maji ambayo naamini kuwa ni mojawapo ya huduma nyeti sana kwa Watanzania. Nichukue fursa hii kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawaombea Mwenyezi Mungu awapelekee roho wake na awape nguvu ya kuweza kufanya kazi hii vizuri kwa sababu ndiyo imekuwa *center* ya maendeleo ya nchi hii, watu wanaharisha hawawezi kulima shambani, watu wasipokunywa maji hawawezi kufanya kazi, kwa hiyo, naomba Mwenyezi Mungu awasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na wataalam wao na naamini wataendelea kuwapa ushirikiano wa kuwa wawazi na kufanya kazi vizuri ili yote haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameahidi leo yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi naomba nizungumze machache kwa nia ya kuboresha. Niishukuru Serikali kwa kujenga bwawa la Kidunda katika Jimbo letu au katika Wilaya yetu ya Morogoro Vijijini. Katika kitabu hiki kwenye ukurasa wa 56, Mheshimiwa Waziri anasema kuwa zimetengwa bilioni 3.4 kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa ajili ya mwaka 2012/2013, ninapoona kuwa inaahidiwa tu kwamba,

zimetengwa sijui kwa uhakika hawa wananchi wangu ambao wanatusumbua kila siku mimi na Mbunge mwenzangu wakitaka kujua wanalipwa lini au watalipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nikienda kusoma kwenye *paragraph* hiyo nakuta kuwa kwenye ujenzi wa barabara ya kutoka Ngerengere mpaka Kidunda ambao ulitakiwa kujengwa na *DAWASA* unategemea na ulipaji wa hii. Ile barabara ni mbaya haipitiki wananchi wanasubiri *DAWASA* ijenge ile barabara na ndiyo sababu sisi kama Halmashauri kile kidogo ambacho tulikuwa nacho kwa ajili ya ile barabara tumepeleka kwingine. Namwomba Mheshimiwa Waziri leo anihakikishie kuwa hii barabara inaanza kujengwa lini kwa sababu mvua ikinyesha tena ndiyo mwanzo wa matatizo na tabu kwa wananchi wa Kata ya Matuli na Kata ya Mkunazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wananchi wangu wamekubali bila matatizo yoyote wakiishi kwa matumaini kwamba watalipwa, lakini naomba Serikali itangulize fedha za kutengeneza miundombinu ambayo itawawezesha hao wananchi waweze kuishi na kwenda kujenga nyumba, wapimiwe viwanja kwenye eneo jipya. Shule ambayo inavunjwa ijengwe upya kwa sababu watahama na watoto wanaosoma, *dispensary* inavunjwa nazo zijengwe kusudi watakapokwenda wakute kuna miumdombinu ambayo ni muhimu na tusisahau kwamba watahitaji kupelekewa maji kwa sababu walizoea kuchota maji katika Mto Ruvu kwa kuwa wataishi mbali na mto watatembea zaidi ya kilomita saba mpaka kumi kwenda kuchota maji mtoni. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu Mradi wa Maji wa Wami, Chalinze awamu ya pili ambao unafanyiwa *extension* kwenda katika Vijiji vya Mkoa wa Pwani kwenye Wilaya ya Kibaha eneo la Chalinze na maeneo kidogo tu ambayo yanaingia kwenye Jimbo langu Morogoro vijijini. Wananchi wangu wanatoa masikitiko yao kuona kwamba huu mradi wa maji unaotokea Chalinze kuelekea Magindu wakati hatua chache kutoka pale kuna binadamu ambao hawana hata tone la maji. Je, ni *criteria* gani ilitumika kupeleka maji Magindu na kuacha Kijiji cha Serengeti (a) na Serengeti (b) na hapo katikati kuna Kitongoji cha Morogoro Vijijini kinaitwa Kitongoji cha Kuyu, watu wanakunywa maji yanayonuka, hakuna aliyewafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamejisikia kwamba wao ni yatima kwa sababu wako Morogoro, naomba waangaliwe. Pamoja na hilo nashukuru kwamba maji yanakwenda mpaka Ngerengere Mjini na hiyo bahati tumeipata kwa sababu kuna kambi za majeshi. Pamoja na kwamba yanafika Kidugalo lakini kabla hayajafika Kidugalo hapo katikati kuna Kijiji cha Kisemu na hakiko mbali na maji yale, naomba Wizara iangalie namna ya kuwafikishia maji pamoja na *settlement* ya Wamasai inayoitwa Kijiji cha Ekenywa na wao wangepata maji naamini kuwa hata ng'ombe wao wangetulia ili kijiji kile watu waweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maji yanayofika Ngerengere, Mheshimiwa Rais kwa mara

mbili zote ambazo amekuja Ngerengere, kwanza alikuja kwenye awamu ya kampeni mwaka 2005, akaja kuzindua Mradi wa Maji tulioletewa pale Ngorongoro Mjini na *World Vision.* Akaja tena kwenye kampeni 2010 ameahidi kwamba tutapata maji katika Tarafa ya Ngerengere. Sasa maji yanaishia Ngerengere Mjini na yatoka kidogo tu na kwenda katika Kijiji cha Sinyaulimi, kuna wananchi ambao wanatembea kilomita 17 kutafuta maji na hawako mbali na Ngerengere wako Kiwege, Matuli na wengine wako Kwaba, wanahitaji maji na siyo mbali Mheshimiwa Waziri naomba wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nilichangie hapa ni kwamba, Wahenga walisema hivi, nikune na mimi nikukune. Serikali inategemea Mto Ruvu ndiyo sababu wanajenga Bwawa la Kidunda, ndiyo sababu wana-*expand Upper Ruvu* na *Lower Ruvu* wanasahau kuwa yale maji yanatoka kwenye Jimbo langu na Jimbo la Mheshimiwa Kalogeris.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wananchi kila siku tunawapigia kelele, tunawakamata na mbao, tunamkamata hata kama ana kidole kimoja kwa sababu tunataka wasiharibu mazingira ili chanzo cha mto Ruvu kisije kikakauka. Sasa hawa wananchi wake zao wanatembea kilomita mbili mpaka tatu wakiteremka mabonde na milima kwenda kuchota maji, wakati wa mvua wanaserereka na ndoo mpaka wengine wanavunjika shingo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri kama anataka maji ya mto Ruvu yaendelee kutiririka atavyosaidia Kijiji cha Amini, Kijiji cha Kanundwa, Kijiji cha Tandai pamoja na eneo la Mkuyuni na Kiroka waweze kupata maji yanayotoka katika chanzo cha Mto Ruvu, maji ya bomba, ili hawa akinamama hasa akinamama wajawazito wanaoporomoka na ndoo za maji kwenye ile miinuko na milima na wao waweze kufaidi matunda ya Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, matunda ya Uhuru wasifaidi watu wa Mkoa wa Pwani na watu wa Dar es Salaam. Sisi tunalinda vile vyanzo vya maji, sisi tukilegeza kamba yetu ni kwamba, mazingira yataharibika na Mto Ruvu utakauka Pwani pamoja na Dar es salaam watapata wapi maji? Tunaomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vijiji Kumi, Mheshimiwa Waziri *Proposal* ya *Consultant* ambayo tumem-*shortlist* kutoka Morogoro iko mezani kwako. Nimesikitika kuona kwamba, nimeangalia kwenye jedwali hatumo, namwomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha atuhakikishie anapokwenda ku-*sign* ili na sisi tuweze kufaidi huo msaada kwa sababu tumechangisha fedha, tuna milioni 450 kwenye akaunti yetu. Mheshimiwa Waziri kama atachelewa basi hizo pesa tutatumia kwa matumizi mengine ya kuchimba visima ili wanawake wapate maji pamoja na kurekebisha visima vingine. Kwa hiyo, nakuomba utakapotoka hapa tunatumaini kwamba kikao kijacho cha Kamati ya Uchumi na Fedha tutakuwa tumepata

pendekezo lako kwamba *consultant* wetu wa Morogoro Vijijini ni nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika sana kuona kwamba Morogoro Vijijini tumepangiwa milioni 142 tu, tumekuwa wa mwisho kabisa katika Mkoa wa Morogoro katika *allocation* kwenye jedwali, sikumbuki namba yake kwenye kitabu hiki. Namwomba Mheshimiwa Waziri aone kwamba na sisi watu wa milimani ni binadamu na sisi watu wa mabondeni kule Morogoro Vijijini tunaokufa kila siku kwa *cholera* kwa Kiingereza tunasema iko *endemic*, atuongezee fedha ili na sisi tuweze kufaidi matunda ya uhuru, kila kitu tuko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, kama Mheshimiwa Waziri atafanya hivyo, nitaunga mkono kwa matumaini. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lucy Nkya kwa mchango wako na pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa vile ambavyo tumeweza kushirikiana kutwa nzima ya leo. Tumepata wachangiaji 18 kwa jioni hii ya leo peke yake, ukiacha wale ambao walianza asubuhi, mtaona ambavyo Wizara hii inachangamkiwa na Wabunge wengi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa orodha yangu bado kesho tutajitahidi tuwapate kama 16 ambao wamebakia kama wakati utaruhusu, hilo la kwanza na kwa maana hiyo, kesho asubuhi watakaoanza kuchangia watakuwa Mheshimiwa Vicent Nyerere,

Mheshimiwa Moza Abeid na wengine watafuata, naomba waendelee kujiandaa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tatizo la maji ni tatizo kubwa, maji ni uhai kama nilivyosema na ni ukweli usiopingika kabisa kuwa vijijini hili ni tatizo namba moja. Tatizo kubwa Mheshimiwa Waziri kwanza ni wataalam wa maji katika Halmashauri za Wilaya kama kuna idara mbili hazina wataalam; moja ni Maji na nyingine ni Ardhi, hizi idara mbili zina shida kubwa sana ya wataalam. Lakini vilevile Serikali ina nia njema kupitia mradi huu wa Benki ya Dunia, inaweza kutoa hela vijiji vingine vinapata mpaka milioni 300 kwa kijiji kimoja. Milioni 200 ni mradi mkubwa, lakini siku Serikali ikiondoka, mradi wa milioni 200 hawa watu wanaweza kukarabati kweli?

Hapa watu wanachohitaji hasa sisi wa Dodoma kwa mfano, tunahitaji pampu, kisima chenyewe, mashine na tanki. Lakini habari ya usambazaji matanki yako kilomita 10, kilomita ngapi, mabomba ya plastiki, mamilioni ya pesa ambayo tungeweza kupata vijiji vitatu, vinne au vitano katika fedha zile zile, kwa hiyo, *design* ya mradi wa Benki ya Dunia kama inaweza kuja kutazamwa huko mbele, kwa kweli iko haja ya kuangalia. Tunatumia hela nyingi sana mahali pamoja ambapo tungeweza kuzitumia vizuri zikasambaa, lakini Wilayani pale hatuna mamlaka ya kufanya chochote kwa sababu *design* tayari imeshakubalika tangu huko, kwa Wahandisi Washauri kila dakika mbili mshauri, hela yote wanachukua Washauri, hili ni jambo la kulitazama sana. *(Makofi)*

Kwa kweli jambo la maji ni kero kubwa sana ambayo ni vizuri tukaiangalia. Lakini vile vile kwa kumalizia ni suala la vipaumbele, pale tulipopanga vipaumbele maji tulipanga kipaumbele cha ngapi? Sasa leo hii tukimgomea Waziri hapa tunamtendea haki? Kwa hiyo, mwakani tuangalie ikiwezekana tuisogeze mbele katika vipaumbele ili tumpe fedha zaidi, Waziri mwenyewe bado mgeni.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuruni sana kwa michango yenu na tutaendelea tena kesho, baada ya ratiba ya leo kuwa *almost* imekamilika. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1. 44 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 10 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*